# Kufanya Wanafunzi 1

# Kudumu Katika Neno Lake

*"Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru."* Yohana 8:31-32

## *Theolojia ya Kimfumo*

www.Theolojia.org

Jina langu:

Jina la mwalimu wangu:

Toleo la 2023.03.30

*"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli." 2 Timotheo 2:15*

## Kufanya Wanafunzi 1 - Kudumu Katika Neno Lake

# DIBAJI

*Kufanya Wanafunzi 1 - Kudumu katika Neno Lake*, inahusika tu na maudhui ya vitabu 66 vya Agano la Kale na Agano Jipya. Haiwasilishi wala haihamasishi ufuataji wa mila, desturi, au mambo yoyote ya kibinadamu yasiotajwa katika Biblia. Ikiwa hukubaliani na chochote katika kozi hii, kuwa Mberoya. Mtume Paulo alipowafundisha Waumini wa Beroya waliokuwa wenye busara, *"Walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo,"* Matendo 17:11. Chunguza Biblia kila siku ili upate ukweli. Kuwa Mberoya!

*Kufanya Wanafunzi 1 - Kudumu katika Neno Lake* inapatikana bila malipo kama kozi kamili au kama masomo binafsi kutoka katika www.Theolojia.org. Kwenye tovuti hiyo, unaweza kusoma mtandaoni, kufundishwa kupitia kusikiliza, na kuchapisha nakala zako mwenyewe bila malipo. Tafsiri inaweza kuruhusiwa kwa kuwasilisha ombi la maandishi kupitia barua pepe kwa John@Theolojia.org kwa msingi wa masharti kwamba tafsiri itafanywa katika kiwango cha hali ya juu, kwamba mafundisho hayatabadilishwa, kwamba hakuna kitu chochote kitakachoongezwa au kuondoloewa, kwamba nukuu za Biblia zitatolewa kutoka kwenye Biblia inayoheshimiwa inayofuata tafisiri ya neno kwa neno, kwamba chanzo asili kilichotumiwa kufanya tafsiri ya kozi hii kinatambuliwa kama www.Theolojia.org ikijumuisha taarifa ya chanzo iliyo hapa chini kwenye ukurasa huu, na kwamba nakala ya bila malipo ya kidijitali ya kozi iliyotafsiriwa iweze kupatikana bila vikwazo au masharti na kutumwa kwa John@Theolojia.org. Usambazaji upya wa kozi hii yote au sehemu yake yoyote, ikijumuisha tafsiri, lazima utolewe bila malipo au kwa gharama isiyozidi gharama ya wastani ya utayarishaji na usambazaji.

Theolojia ya Kikristo ilifafanuliwa na Thomas Aquinas (mwanatheolojia na mwanafalsafa Mkristo, 1225-1274 BK) kama somo la yale yanayofundishwa na Mungu, yanayofundisha kuhusu Mungu, na yanayoongoza kwa Mungu … kimahususi Mungu wa Biblia. Neno *theolojia* linatokana na neno la Kigiriki *theologia* ambayo inachanganya maneno ya Kigiriki *theos* [Mungu] na *logia* [neno]. Theolojia ni uchunguzi wa Neno la Mungu. *Kozi ya Msingi ya Kufanya Wanafunzi 1 - Kudumu katika Neno Lake* ni theolojia ya kimfumo iliyofupishwa na kurahisishwa ... aina mahususi na yenye malengo mahususi ya kuchunguza na kufundisha Neno la Mungu. Kozi hii imepanga kweli na mafundisho makuu ya Biblia katika mfumo unaoshikamana, ulio wazi, na unaoeleweka na inaweka msingi wa kujifunza zaidi. Inajumuisha muhtasari wa historia, kronolojia, wahusika wakuu, na jografia kuu ya Agano la Kale na Jipya.

Acts One Eight [Matendo Moja Nane]huchapisha tafsiri hii ya Kiswahili ya kozi ya lugha ya Kiingereza ya *Disciplemaking 1 … Abiding in His Word*. Unaweza kunakili kozi hii au sehemu yake yoyote bila malipo au kwa gharama ya usambazaji pekee, bila kubadilisha maudhui yake na ukiwa umeambatanisha kauli hii ya chanzo. Kozi hii inapatikana bila malipo katika lugha ya Kiswahili kutoka katika www.Theolojia.org au katika lugha ya Kiingereza kutoka katika www.VIrtualBibleAcademy.org. Kwenye tovuti hizi, unaweza kusoma mtandaoni, kufundishwa, kupakua, au kuchapisha nakala zako mwenyewe. Nukuu za Biblia ya Kiswahili zimetoka katika Biblia ya Swahili Union Version (SUV) ya 1997.

# JINSI YA KUSOMA KOZI HII

**Njia za Kusoma.** Omba kisha uchague njia unayotaka.
Soma peke yako. Ni sawa kusoma kozi hii kibinafsi.
Soma na mshirika wa masomo. Chagua kwa busara. Chuma hunoa chuma, Mithali 27:17.
Someni kama kikundi. Chagua wanafunzi waaminifu, 2 Timotheo 2:2.

**Kujiandikisha.** Huhitaji kujiandikisha ili usome kozi hii. Hata hivyo, tungependa kujua wewe ni nani, unaishi wapi (nchi na jiji … si anwani ya mtaani), na anwani yako ya baruapepe. Anwani yako ya baruapepe itatumiwa tu kwa ajili ya masasisho na matangazo ya nyenzo zingine za bila malipo za mafundisho ya Biblia na uinjilisti, video, na kozi.

**Uchapishaji wa nyenzo za kozi.** Kozi hii ina kurasa 160 za PDF. Na unaweza kuichapisha bila malipo. Nakala iliyochapishwa inapendekezwa kwa ajili ya kusoma. Chapisha kozi nzima au somo moja moja kutoka kwenye kurasa zilizoonyeshwa katika Jedwali la Yaliyomo … au kutoka kwenye viungo vya uchapishaji vilivyo katika www.Theolojia.org.

**Kupakua nyenzo za kozi**. PDF na faili za sauti zinaweza kupakuliwa bila malipo kwenye kifaa chako au kompyuta yako. PDF za kozi hufanya kazi vizuri zaidi kwenye kompyuta kubwa au ndogo. Matini ya kozi yamkini ni magumu sana kusomwa kwenye simu.

**Mafundisho kupitia sauti**. Mafundisho ya kozi hii kupitia sauti ya mwandishi yanapatikana bila malipo katika www.Theolojia.org. Unaweza kuyasikiliza mafundisho hayo mtandaoni ... au kuyapakua ili uyasome nje ya mtandao.

**Vyeti.** Omba taarifa kuhusu vyeti kwa kutuma barua pepe kwa John@Theolojia.org.

**Maswali na maombi**. Tuma maswali, maoni, na maombi yako ya maelezo zaidi kupitia barua pepe kwa John@Theolojia.org. Tutafanya kila tuwezalo kujibu maswali yako yote na kukusaidia kadiri ya uwezo wetu.

**Tafsiri**. Tafsiri inaweza kuruhusiwa kwa kuwasilisha ombi la maandishi kupitia barua pepe yenye maelezo ya kina kwa John@Theolojia.org kwa msingi wa masharti kwamba tafsiri itafanywa katika kiwango cha hali ya juu, kwamba mafundisho hayatabadilishwa, kwamba hakuna kitu chochote kitakachoongezwa au kuondoloewa, kwamba nukuu za Biblia zitatolewa kutoka kwenye Biblia yenye tafsiri sahihi, hasa inayofuata tafisiri ya neno kwa neno, kwamba chanzo asili kilichotumiwa kufanya tafsiri ya kozi hii yote au sehemu yake kinatambuliwa kama VirtualBibleAcademy.org ikijumuisha taarifa ya chanzo iliyo hapa chini kwenye ukurasa huu, na kwamba nakala ya bila malipo ya kidijitali ya kozi iliyotafsiriwa iweze kupatikana bila vikwazo au masharti na kutumwa kwa John@Theolojia.org.

**Vikwazo**. Usambazaji upya wa kozi hii yote au sehemu yake yoyote, ikijumuisha nyenzo zilizochapishwa na kupakuliwa, mafundisho ya sauti na video, na tafsiri, lazima utolewe bila malipo au kwa gharama ya wastani ya utayarishaji na usambazaji.

Acts One Eight [Matendo Moja Nane] huchapisha tafsiri hii ya Kiswahili ya kozi ya lugha ya Kiingereza ya *Disciplemaking 1 … Abiding in His Wor*d. Unaweza kunakili kozi hii au sehemu yake yoyote bila malipo au kwa gharama ya usambazaji pekee, bila kubadilisha maudhui yake na ukiwa umeambatanisha kauli hii ya chanzo. Kozi hii inapatikana bila malipo katika lugha ya Kiswahili kutoka katika www.Theolojia.org au katika lugha ya Kiingereza kutoka katika www.VIrtualBibleAcademy.org. Kwenye tovuti hizi, unaweza kusoma mtandaoni, kufundishwa, kupakua, au kuchapisha nakala zako mwenyewe. Nukuu za Biblia ya Kiswahili zimetoka katika Biblia [ya Swahili Union Version (SUV) ya 1997].

## KUTANA NA MWANDISHI

Ndugu wapendwa katika Kristo,

Nimekuwa muumini wa kweli wa Yesu Kristo tangu nilipokuwa na umri wa miaka 10. Nimekuwa katika huduma ya wakati wote tangu 1974. Na nimekuwa katika ndoa na mke wa ujana wangu kwa miongo mingi. Yeye, watoto wetu, na wajukuu wetu wote ni Waumini. Mimi ni mfuasi wa kanisa … lakini siendelezi kanisa maalum au dhehebu.Naamini kwamba vitabu 66 vya Biblia, kama vilivyoandikwa awali, ni Neno la Mungu lisilo na makosa, lililo sahihi, lisilofifia, na lililo kamili. Naamini Biblia nzima inamaanisha kile inachosema. Ina mamlaka kuu zaidi katika maisha na mafundisho.

Huduma yangu ya ana kwa ana nimeifanya Marekani, Uingereza, Poland, na Urusi. Huduma yangu ya ana kwa ana, kupitia nyenzo zilizochapishwa na kupitia mtandao, imegusa kila bara isipokuwa Antaktika na imejumuisha mafundisho ya Biblia, uinjilisti, kutetea imani ya Kikristo, na kuhubiri. Nimefanya huduma yangu katika makanisa, vyuo, nyumba, vituo vya mapumziko, ofisi, mikahawa ... na juu ya mlima, kwenye redio, kwenye video, na kwa kiwango kikubwa mtandaoni. Naamini kwamba mwalimu mzuri huishi kulingana na kile anachofundisha ... akiwaelekeza watu kwenye mambo ambayo tayari ameshayafanya. Kwa neema na rehema zake, Mungu amefanikisha huduma hii na ameniruhusu kuwa sehemu yake. Utukufu ni kwake Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu pekee.

*Kufanya Wanafunzi 1 - Kudumu Katika Neno Lake* ni kozi iliyoandikwa katika miaka ya 1980. Baada ya kuifundisha mara nyingi, imesasishwa na kupanuliwa mara kadhaa ikijumuisha sasisho kuu mnamo 2021. Mabadiliko yalifanywa kwenye maudhui yake ili kujibu maswali na mahitaji ya wanafunzi yaliyojitokeza wakati wa kufundisha. Mchakato wa asili wa kuandika na kusasisha kozi hii ulitekelezwa kwa maombi mengi na ulijumuisha utafiti wa kina, lakini usio wa kawaida. Baada ya kuamua mada nitakazojumuisha katika kozi hii, nilikusanya vitabu *vingi* kuhusu kila mada. Lakini, sikuzisoma. Nilipitia kila kitabu ili kupata kila kifungu cha Biblia kilichotajwa. Kisha vifungu hivyo vilipangwa kwa mpangilio wa kimantiki, vikasomwa, na kupangwa katika mfumo wa kozi hii. Tafsiri mbalimbali za Biblia za neno kwa neno, kamusi za Biblia, kamusi za Kigiriki na Kiebrania, konkodansi, maelezo yanayoheshimiwa, ramani, na nyenzo nyinginezo mbalimbali zilitumiwa. *Kufanya Uanafunzi 1 - Kudumu Katika Neno Lake* si ufafanuzi wa maandishi ya wengine. Kwa kadiri usomi mzuri unavyoruhusu, ni kazi asili ... mojawapo ya kazi kuu za maisha yangu.

Kuandika kozi hii kulibadilisha maisha yangu na kozi yenyewe imebadilisha maisha ya wengine ambao wameisoma ... na inaweza kubadilisha maisha yako. Yesu aliwaambia Waumini, "*Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru,*" Yohana 8:31-32. Kozi hii inaweza kukusaidia kudumu katika Neno la Mungu. Inaweza kukuandaa kwa ajili ya maisha na huduma yako. Kile unachojifunza kutoka kwenye Biblia kitakupa msingi imara katika ukweli wa Mungu ambao Neno lake pekee ndio linaloweza kukupa.

Ndugu yako katika Kristo,

*John D. Morris III*

John D. Morris III
Mwanzilishi na Rais, Acts One Eight
John@Theolojia.org

## YALIYOMO ...

**Dibaji** .................................... **2** [ chapisha ukurusa wa 2 ]

**Jinsi ya Kusoma Kozi Hii** ....... **3** [ chapisha ukurasa wa 3 ]

**Kutana na Mwandishi** ........... **4** [ chapisha ukurasa wa 4 ]

**Utangulizi** ............................. **6** [ chapisha ukurasa wa 6 - 11 ]

**1. Wokovu** ........................... **12** [ chapisha ukurasa wa 12 - 22 ]

**2. Sala** ................................ **23** [ chapisha ukurasa wa 23 - 30 ]

**3. Kujifunza Biblia** ............... **31** [ chapisha ukurasa wa 31 - 41 ]

**4. Agano la Kale** .................. **42** [ chapisha ukurasa wa 42 - 61 ]

**5. Maisha ya Yesu** ................ **62** [ chapisha ukurasa wa 62 - 80 ]

**6. Agano Jipya** .................... **81** [ chapisha ukurasa wa 81 - 97 ]

**7. Kumjua Mungu** ................ **98** [ chapisha ukurasa wa 98 - 109 ]

**8. Mapenzi ya Mungu** ......... **110** [ chapisha ukurasa wa 110 - 117 ]

**9. Katika Mwili** ................... **118** [ chapisha ukurasa wa 118 - 135 ]

**10. Katika Vita** ................... **136** [ chapisha ukurasa wa 136 - 154 ]

**Kiambatisho:**
**Kuwafundisha Wengine** ..... **155** [ chapisha ukurasa wa 155 - 159 ]

**Mahimizo ya Mwisho** ......... **160** [ chapisha ukurasa wa 160 ]

**Kumbuka:** Maswali ya marudio na majibu yako katika kurasa nne za mwisho za Utangulizi na kurasa nne za mwisho za kila moja ya masomo kumi. Kwa mfano: maswali ya *Somo la 8 - Mapenzi ya Mungu* yako katika ukurasa wa 114-117.

## Kufanya Wanafunzi 1 - Kudumu Katika Neno Lake

# UTANGULIZI

*“Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.”* Mathayo 28:18-20

### AMRI YA KUFANYA WANAFUNZI

Baada ya Yesu kusulubiwa, aliwatokea wanafunzi wake mara nyingi kabla ya kupaa Mbinguni [akiwa nje kidogo ya Yerusalemu]. Katika mojawapo ya matukio hayo ya kujitokeza kwake [siku kadhaa kabla ya kupaa kwake] kwenye mlima huko Galilaya, Yesu aliwapa wanafunzi wake amri ya Mathayo 28:18-20 ambayo imenukuliwa hapo juu. Amri hiyo muhimu sana inajulikana kama Agizo Kuu. Zao la mtu binafsi la kutii Agizo Kuu ni mwanafunzi. Mchakato wa kutii Agizo Kuu ni mchakato wa kuzidisha.

### UFAFANUZI WA MWANAFUNZI

Mwanafunzi ni mwanafunzi na mfuasi wa Yesu Kristo ... mtu anayeishi kulingana na mafundisho ya Yesu Kristo na anayaeneza. Yesu aliweka viwango vya juu kwa wale wanaotaka kuwa wanafunzi *wake*. Alisema kwamba kuwa mwanafunzi wake kunamaanisha kudumu katika [kuishi katika] Neno lake, Yohana 8:31-32. Tambua kwamba alikuwa akizungumza na Waumini katika vifungu hivyo viwili. Yesu aliongeza kusema kwamba upendo wetu sisi kwa sisi unadhihirishia ulimwengu kwamba sisi ni wanafunzi wake, Yohana 13:35. Aidha, alieleza kwamba tunamtukuza Baba na *kuthibitisha kuwa*, kumaanisha *tunakuwa*, wanafunzi wake kwa kuzaa matunda mengi, Yohana 15:8. Na Yesu alieleza kwamba wanafunzi wake lazima wamthamini zaidi ya maisha yao wenyewe, mahusiano yao, na mambo yote mengine, Luka 14:26-33.

### MCHAKATO WA KUFANYA WANAFUNZI

Kufanya wanafunzi ni kazi ya Mungu pamoja na kazi yetu. Hatua ya kwanza ni kumwamini Yesu. Mtu asiyeamini anakuwa muumini kwa imani pekee katika Yesu Kristo pekee. Wokovu hupokewa kwa imani katika Yesu kwa msingi wa kazi yake na kujitoa kwake kama sadaka pekee. Hata hivyo, muumini mpya hawi mwanafunzi wa Yesu moja kwa moja. Muumini mpya, aliyebatizwa na kufundishwa kutii, hukua na kuwa mwanafunzi. Kuwa mwanafunzi kunatokana na kazi na kujitolea kwa muumini … akiwezeshwa na Mungu. Na mchakato wa kufanya wanafunzi unaendelea kadiri mwanafunzi anavyofanya wengine kuwa wanafunzi. Katika Agizo Kuu, Yesu alisema kwamba tunapaswa *“kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi”*. Mojawapo ya amri alizotoa ilikuwa Agizo Kuu. Kwa hivyo, mchakato wa kufanya wanafunzi unajumuisha kuwafundisha wanafunzi jinsi ya kuwafanya wengine kuwa wanafunzi.

## KUJITOLEA

*“Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine,”* 2 Timotheo 2:2

Paulo alimwagiza Timotheo kukabidhi yale aliyomfundisha kwa watu waaminifu wanaoweza kuwafundisha wengine. Mchakato huo ulipaswa kuzidishwa hadi kizazi cha nne ... kutoka kwa Paulo hadi Timotheo ... kutoka kwa Timotheo hadi kwa watu waaminifu ... na kutoka kwa watu hao waaminifu hadi kwa wengine. Mchakato huo kisha ulipaswa kuendelea kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Aina hiyo ya uzidishaji ndio lengo la kozi hii. Kila somo ni hatua katika mchakato wa kuwa mwanafunzi na kuwa mtu anayefanya wengine kuwa mwanafunzi. Ili mchakato huu ufaulu, unahitaji bidii kutoka kwa mwalimu na mwanafunzi.

## KUJITOLEA KUFANYA KOZI HII

**Patikana.** Tenga muda kwa ajili ya masomo haya.

**Kuwa makini.** Hiyo inahitaji juhudi … omba, soma, na ufanye marudio.

**Kuwa Mberoya.** Chunguza Maandiko kuona kama mambo haya ni kweli.

**Kuwa mtu anayeweza kufundishika.** Kuwa tayari kujifunza, kufikiria, kukua na kubadilika. Tumia kile unachojifunza katika maisha yako mwenyewe. Kisha mfundishe mtu mwingine. Tumia *na* uzidishe.

## KUJITOLEA KUFUNDISHA KOZI HII

**Jitolee kwa wanafunzi wako.** Toa muda wako kama mwalimu na kama rafiki kwa wale unaowafundisha. Jitolee kwao. Kumbuka, wanapaswa kuwa wanafunzi wa Yesu Kristo ... si kuwa wanafunzi wako.

**Kuwa mfano bora.** Maisha yako ni dhihirisho la kujitolea kwako kwa Mungu, kwa Neno lake, na kwa mchakato wa kufanya wanafunzi. Ufahamu wako wa kina wa nyenzo za kozi utaonyesha kuwa masomo haya yanaweza kueleweka.

**Kuwa mnyumbufu na imara.** Kuwa na subira. Inachukua muda kujifunza na kutumia maudhui ya masomo haya. Toa muda wa kutosha kwa wanafunzi wako kujifunza, kukua na hata kushindwa. Wahimize na uwawajibishe kujifunza ... kutumia kile wanachojifunza ... kisha kuwafundisha wengine pia.

**Kuwa tayari.** Elewa kila somo kikamilifu ... na usome kiambatisho kuhusu kuboresha ujuzi wako wa kufundisha.

Acts One Eight [Matendo Moja Nane]huchapisha tafsiri hii ya Kiswahili ya kozi ya lugha ya Kiingereza ya *Disciplemaking 1 … Abiding in His Word*. Unaweza kunakili kozi hii au sehemu yake yoyote bila malipo au kwa gharama ya usambazaji pekee, bila kubadilisha maudhui yake na ukiwa umeambatanisha kauli hii ya chanzo. Kozi hii inapatikana bila malipo katika lugha ya Kiswahili kutoka katika www.Theolojia.org au katika lugha ya Kiingereza kutoka katika www.VIrtualBibleAcademy.org. Kwenye tovuti hizi, unaweza kusoma mtandaoni, kufundishwa, kupakua, au kuchapisha nakala zako mwenyewe. Nukuu za Biblia ya Kiswahili zimetoka katika Biblia [ya Swahili Union Version (SUV) ya 1997].

*Kufanya Wanafunzi 1 - Maswali ya Marudio*

# Utangulizi … ukurasa wa 6 - 7

Sehemu ya kujifunza ni kufanya marudio … kuhifadhi maarifa mapya kwenye kumbukumbu yako ya muda mrefu. Chapisha mtihani huu wa marudio au tumia karatasi tofauti kujibu maswali yafuatayo. Kisha rudia mtihani huu, ukisoma maelezo ya kozi au bila kuyasoma, hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi.
*Mitihani hii ya marudio* pamoja na majibu sahihi yanapatikana kwenye www.Theolojia.org.

1. Baada ya Yesu kusulubiwa, aliwatokea wanafunzi wake mara kadhaa kabla ya kupaa Mbinguni. Katika mojawapo ya matukio hayo ya kujitokeza kwake kwenye mlima huko Galilaya, Yesu alitoa Agizo Kuu.
    a. Je, rejeo kuu la Agizo Kuu katika Mathayo ni lipi?
    b. Andika Agizo Kuu kwa maneno yako mwenyewe.

2. Kutii Agizo Kuu ni mchakato wa ________________________________________.
   Matokeo ni ___________________________.

3. Katika Luka 14:26-33, Yesu alieleza kwamba wanafunzi wake lazima wamthamini zaidi ya ____________________ yao wenyewe, zaidi ya _____________________ yao, na zaidi ya _______________________________________________ *la sivyo* hawawezi kuwa ____________________________ wake.

4. Katika Yohana 8:31, Yesu aliwaambia ________________________ kwamba kuwa wanafunzi wake kunamaanisha _______________________________ katika Neno lake.

5. Kulingana na Yohana 13:35, ______________ wetu sisi kwa sisi kama wanafunzi unadhihirisha kwa ______________ kwamba sisi ni ________________________ wake.

6. Tunamletea Baba utukufu na tunathibitisha kuwa sisi ni wanafunzi wake [yaani, *tunakuwa* wanafunzi wake] kwa ____________________________, Yohana 15:8.

7. Agizo Kuu ni zaidi ya uinjilisti. Hata hivyo, katika mchakato wa kufanya wanafunzi, hatua ya kwanza lazima iwe _____________________________________ Yesu.

8. Katika mchakato wa kufanya wanafunzi, kulingana na Mathayo 28:18-20, muumini mpya anahitaji ______________________na kufundishwa __________________ yote ambayo Yesu _______________________________. Lengo ni kwa muumini huyo mpya awe mwanafunzi na _______________________________________.

9. Mchakato wa kuzidisha wa kufanya wanafunzi unaonekana katika maneno ya 2 Timotheo 2:2 ukipitishwa katika vizazi vinne ... kutoka kwa Paulo hadi kwa________________________ hadi _____________________________ kwaambao wataweza kuwafundisha __________________________ pia.

10. Kwa kutafakari na kuomba, jibu *"ndiyo"* au *"hapana"* kwa maswali yafuatayo:

    a. Je, utafanya kile kinachohitajika ili kujifunza masomo haya?

    b. Je, utakuwa makini na mwenye kufundishika?

    c. Je, utatumia yale unayojifunza katika maisha yako mwenyewe?

    d. Je, uko tayari kumfundisha mtu mwingine Mungu akikupa nafasi?

*Kufanya Wanafunzi 1 - Majibu ya Maswali ya Marudio*

# Utangulizi … maswali ukurasa wa 8 - 9

Usitumie karatasi hizi za majibu kupata majibu yako. Tafadhali zitumie tu kukagua majibu yako. Rudi kwenye somo ili kupata taarifa za kurekebisha majibu yako. Rudia mtihani hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi. Masomo yote, mitihani ya marudio, na kurasa za majibu zinapatikana katika www.Theolojia.org.

1. Baada ya Yesu kusulubiwa, aliwatokea wanafunzi wake mara kadhaa kabla ya kupaa Mbinguni. Katika mojawapo ya matukio hayo ya kujitokeza kwake kwenye mlima huko Galilaya, Yesu alitoa Agizo Kuu.

    a. Je, rejeo kuu la Agizo Kuu katika Mathayo ni lipi?

    *Mathayo 28:18-20*

    b. Andika Agizo Kuu kwa maneno yako mwenyewe.

    *Haya yote yanapaswa kujumuishwa katika jibu:*
    *Yesu alipewa mamlaka yote … kwa hivyo nendeni mkafanye wanafunzi … mkiwabatiza … mkiwafundisha watu kutii yote aliyoamuru Yesu … na Yesu yuko pamoja nanyi katika mchakato huo.*

2. Kutii Agizo Kuu ni ___*kuzidisha*___ mchakato wa. Matokeo ni ___*mwanafunzi wa Yesu*___ .

3. Katika Luka 14:26-33, Yesu alieleza kwamba wanafunzi wake lazima wamthamini zaidi ya ___*maisha*___ , yao wenyewe, zaidi ya ___*mahusiano*___ , yao, na zaidi ya ___*vitu vyote vingine – vinavyoonekana na visivyoonekana*___ *la sivyo* hawawezi kuwa ___*wanafunzi*___ wake.

4. Katika Yohana 8:31, Yesu aliwaambia ___*waumini*___ kwamba kuwa wanafunzi wake kunamaanisha ___*kudumu au kuishi*___ katika Neno lake.

5. Kulingana na Yohana 13:35, ___*upendo*___ wetu sisi kwa sisi kama wanafunzi unadhihirisha kwa ___*ulimwengu*___ kwamba sisi ni ___*wanafunzi*___ wake.

6. Tunamletea Baba utukufu na tunathibitisha kuwa sisi ni wanafunzi wake [yaani, *tunakuwa* wanafunzi wake] kwa __*kuzaa matunda mengi*__ , Yohana 15:8.

7. Agizo Kuu ni zaidi ya uinjilisti. Hata hivyo, katika mchakato wa kufanya wanafunzi, hatua ya kwanza lazima iwe __*kumwamini*__ Yesu.

8. Katika mchakato wa kufanya wanafunzi, kulingana na Mathayo 28:18-20, muumini mpya anahitaji __*kubatizwa*__ na kufundishwa __*kutii*__ yote ambayo Yesu __*aliamuru*__ . Lengo ni kuwa muumini huyo mpya awe mwanafunzi na __*aweze kufanya wengine kuwa wanafunzi*__.

9. Mchakato wa kuzidisha wa kufanya wanafunzi unaonekana katika maneno ya 2 Timotheo 2:2 ukipitishwa katika vizazi vinne ... kutoka kwa Paulo hadi kwa __*Timotheo*__ hadi kwa __*watu waaminifu*__ ambao wataweza kuwafundisha __*wengine*__ pia.

10. Kwa kutafakari na kuomba, jibu *“ndiyo”* au *“hapana”* kwa maswali yafuatayo:

    a. Je, utafanya kile kinachohitajika ili kujifunza masomo haya?

    b. Je, utakuwa makini na mwenye kufundishika?

    c. Je, utatumia yale unayojifunza katika maisha yako mwenyewe?

    d. Je, uko tayari kumfundisha mtu mwingine Mungu akikupa nafasi?

## Kufanya Wanafunzi 1 - Kudumu Katika Neno Lake

# SOMO LA 1 - WOKOVU

*“Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.”* Warumi 6:23

### UAMUZI WA MILELE

Biblia inaweka wazi kwamba kila mtu ataishi milele ... swali ni maisha hayo yatakuwa wapi. Jibu la hilo linategemea uamuzi wa kila mtu kuhusu Yesu Kristo ... *kumwamini* au kumkataa. Kwa vile matokeo ni kupata au kukosa uzima wa milele, hakuna uamuzi mwingine ulio muhimu kama uamuzi wa kila mtu kuhusu Yesu.

### TATIZO

Kwa ufupi, dhambi zetu zinatutenganisha na Mungu. Tuna hatia kwa msingi wa kuwa sehemu ya jamii ya wanadamu, yaani, tumerithi dhambi. Tuna tabia ya asili ya kutenda dhambi, yaani, asili ya dhambi iliyorithiwa. Na sisi wenyewe, tunafanya mambo mabaya [dhambi za kibinafsi] ambayo yanatutenganisha na Mungu. Mungu asingeingilia kati, tungekuwa tunakabiliwa na umilele mbali naye.

### SULUHU

Sisi wenyewe, hatuna uwezo wa kutatua tatizo hilo ... lakini Mungu ana uwezo wa kulitatua. Kwa msingi wa upendo, Mungu alichukua hatua ya kwanza. Alimtuma Mwanawe kufa msalabani badala yetu. Tunapomwamini Yesu kama Mwokozi wetu binafsi, nafasi aliyochukua kuwa mbadala wetu inalipia dhambi zetu [ukombozi] ... inamridhisha Mungu [ondoleo la ghadhabu] ... inatubadilisha [upatanisho] ... na inatuondolea dhambi zetu na kutupa haki yake [uhamisho] ... Kisha Mungu anatangaza kwamba sisi ni wenye haki [kuhesabiwa haki]. Wokovu huu ni kwa njia ya imani pekee katika Kristo pekee. Wokovu haupatikani kwa tamko la hiari au lisilo la hiari la imani fulani wala haupatikani kwa kutia saini hati fulani. Ni kwa imani wala si kwa juhudi zozote za kibinafsi au kazi ya kibinafsi. *“Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; na hii haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; si matokeo ya matendo, mtu awaye yote asije akajisifu,”* Waefeso 2:8-9.

### MATOKEO

Tunazaliwa katika familia ya Mungu tunapoweka imani yetu binafsi katika Yesu. Matendo yetu mema hayatuokoi ... hayazai imani. Lakini matendo mema yanadhihirisha imani ya kweli. Matendo mema ni matokeo ya wokovu wetu wala si jambo tunalopaswa kufanya ili tustahili kupata wokovu. Kama Waumini, tuna fursa nzuri ajabu ya kujua kwamba tuna uzima wa milele. Tuko salama milele kwa sababu hakuna awezaye kutunyakua kutoka mkononi mwa Mungu.

## DHAMBI … UHALISIA WAKE, MATOKEO YAKE, NA SULUHU YAKE

Biblia inatoa kauli za wazi kuhusu dhambi. Inasema kwamba dhambi ni kitu halisi katika maisha yetu. Matokeo ya dhambi zetu ni mabaya sana ... yanatutenganisha na Mungu ... na kutuacha peke yetu kukabiliana na umilele mbali na uwepo wake. Hata hivyo, Mungu alitoa suluhu. Anatupatia suluhu hiyo kama zawadi.

**UHALISIA WA DHAMBI.** Dhambi ni kitu chochote kisichoambatana na wema wa Mungu. Inaweza kuwa wazo, Mathayo 5:27-28 ... tendo lililotendwa, Yohana 8:34 ... au tendo ambalo halikutendwa, Yakobo 4:17. Maneno yanayotumiwa kumaanisha dhambi katika Biblia yanamaanisha kukosa shabaha, kuvunja Sheria, kuasi, ukaidi, kutotii, uovu, na ukosefu wa uadilifu. Dhambi inaweza kuwa dhidi ya wengine au dhidi yetu wenyewe, 1 Wakorintho 6:18. Kwa jumla dhambi zote ni dhidi ya Mungu, Mwanzo 39:9, Zaburi 41:4 na 51:4, na Warumi 8:7. Aina tatu za dhambi zimeelezwa katika Biblia. Kundi la kwanza ni dhambi ya kurithi iliyoelezwa katika Warumi 5:12-21. Ni kuwa na hatia kwa msingi wa kuwa sehemu ya jamii ya wanadamu ... kupitia Adamu wote wametenda dhambi. Kundi la pili ni asili yetu ya dhambi ya kurithi inayorejelewa katika Waefeso 2:3 na Zaburi 51:5. Tabia yetu ya asili ya kutenda dhambi. Tabia hiyo ya asili, bila kuepuka, inatuleta kwenye kundi la tatu, dhambi za kibinafsi. Dhambi za kibinafsi ni zile tunazofanya kupitia mawazo au matendo ... kupitia mtazamo, matendo tunayotenda na tusiyotenda.

**MATOKEO YA DHAMBI.** Uhalisia wa dhambi maishani mwetu hauwezi kuepukika. *“Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu,”* Warumi 3:23. Pia ni jambo lisiloepukika kwamba ni lazima tukabiliane na matokeo ya dhambi hiyo. Moja ya matokeo ni kwamba tunatenganishwa na Mungu. Sisi ni maadui zake, Warumi 5:10. Tumetenganishwa naye. *“Lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu,”* Isaya 59:2. Tunasimama mbele za Mungu tukiwa wenye hatia na tumehukumiwa. Tukiwa peke yetu bila Mungu kuingilia kati, tumehukumiwa kupata umilele wa *“kutengwa na uso wa Bwana,”* 2 Wathesalonike 1:9 … na tumehukumiwa kupata *“aibu na kudharauliwa milele,”* Danieli 12:2.

**SULUHU YA DHAMBI.** Dhambi na matokeo yake ya kuhukumiwa na kupewa adhabu ni hali ambazo mwanadamu hana uwezo wa kuziepuka. Hata hivyo, Mungu ametoa suluhu ya dhambi katika kifo cha Yesu Kristo msalabani. *“Tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu,”* Warumi 5:6. *“Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti,”* 1 Petro 2:24. *“Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu; ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote,”* 1 Timotheo 2:5-6. *“Kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi,”* Matendo 10:43. Kila mtu atakabiliana na tatizo la dhambi kwa njia moja kati ya njia mbili: (1) kwa kutengwa na Mungu milele, au (2) kwa suluhu ya Mungu iliyopokewa kupitia imani katika Yesu Kristo.

## WOKOVU … VIPENGELE SITA

Kwa upendo wake mkuu, Mungu alitoa wokovu kupitia kifo cha Yesu kwa wale wote *watakaomwamini* Yesu. Wokovu una vipengele tofauti ... unaelekezwa kwa Mungu, unaelekezwa kwa dhambi, na unaelekezwa kwa mwanadamu. Kuelewa wokovu kunapatikana katika vipengele hivi tofauti vya zawadi hii kuu ya Mungu. Vinaelezwa hapa chini.

**MBADALA … YESU ALICHUKUA NAFASI YANGU**. Yesu alikufa msalabani kama mbadala wetu. Wokovu wote una msingi wake katika ukweli huu mmoja. Ni zaidi ya kufa kwake kwa faida yetu. Alikufa badala yetu.

> *"Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu."* Warumi 5:6
>
> *"Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu."* 1 Petro 3:18

**UKOMBOZI … DHAMBI YANGU ILILIPIWA.** Hii inaelekezwa kwenye dhambi. Ukombozi ni kununua au kuwasilisha baada ya kutoa malipo fulani. Ukombozi ni malipo kwa ajili ya dhambi. Malipo hayo yalitolewa kwa Mungu. Malipo yalikuwa damu ya Kristo. Uhai, au nafsi, ya mwili iko katika damu, Mambo ya Walawi 17:11. Malipo yalikuwa maisha ya Yesu Kristo. Yesu Kristo alitoa maisha yake kwa ajili ya dhambi zetu … alitoa malipo hayo kwa ajili yetu.

> *"Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu."* Wagalatia 3:13
>
> *"Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo."* 1 Petro 1:18-19
>
> *"Kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa."* Ufunuo 5:9-10

**ONDOLEO LA GHADHABU … MUNGU ALIRIDHIKA**. Hii inaelekezwa kwa Mungu. Ondoleo la ghadhabu inamaanisha kuridhika. Biblia inasema kwamba Kristo mwenyewe ndiye dhabihu inayomridhisha Mungu ... inayotuliza ghadhabu ya Mungu. Haki ya Mungu ilikuwa ni lazima iridhishwe.

> *"Hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote, apate kuwa kuhani mkuu mwenye rehema, mwaminifu katika mambo ya Mungu, ili afanye suluhu kwa dhambi za watu wake."* Waebrania 2:17
>
> *"Naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote."* 1 Yohana 2:2
>
> *"Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu."*
> 1 Yohana 4:10

## WOKOVU … mwendelezo

**UPATANISHO ... NILIBADILISHWA NA NINAWEZA KUBADILISHWA.** Haya ni mabadiliko yanayoelekezwa kwa mwanadamu. Yanamfanya mwanadamu akubalike na Mungu. Upatanisho unamleta Mungu na mwanadamu katika hali ya kuelewana ... unawafanya wapatane tena. Mungu hakubadilika. Mungu hahitaji kubadilika. Mwanadamu anahitaji kubadilishwa. Msalabani, mwanadamu alibadilishwa ... alifanywa aweze kuokolewa. Na tunabadilishwa kibinafsi tunapoamini. Kisha tunapewa huduma na neno la upatanisho ... kushiriki Injili na watu waliopotea wa ulimwengu wetu.

> *“Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake.”* Warumi 5:10

> *“Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho; yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao; naye ametia ndani yetu neno la upatanisho. Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu.”* 2 Wakorintho 5:18-20

**UHAMISHO … UHAMISHO WA MARA MBILI.** Baada ya kumwamini Kristo, dhambi zetu zote zinahamishiwa kwake ... na haki yake yote inahamishiwa kwetu. Kristo asiye na dhambi alifanyika dhambi kwa ajili yetu ... na sisi, tusio wenye haki, tulipewa haki yake.

> *“Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.”* 2 Wakorintho 5:21

> *“Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa.”* 1 Petro 2:24

**KUHESABIWA HAKI ... MUNGU ALITANGAZA KUWA MIMI NI MWENYE HAKI.** Kuhesabiwa haki ni tangazo la kuwa mwenye haki. Ni tamko la Mungu kwamba tuko sawa mbele zake. Msalaba unatufanya tuwe wenye haki. Kuhesabiwa haki kunatangaza kwamba sisi ni wenye haki. Kama sehemu ya wokovu wetu, tunahesabiwa haki kwa msingi wa kazi ya Kristo msalabani. Baada ya kuokolewa, matendo yetu mema yanayotokana na wokovu wetu yanatuhesabia haki ... yanatangaza wokovu wetu, Yakobo 2:24.

> *“Wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu.”* Warumi 3:24

> *“Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.”* Warumi 5:1

> *“Basi tena, kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu, kadhalika kwa tendo moja la haki watu wote walihesabiwa haki yenye uzima. Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki.”* Warumi 5:18-19

## MARUDIO KUHUSU DHAMBI NA WOKOVU

### DHAMBI

Dhambi ni jambo halisia katika maisha ya kila mtu ... na huleta matatizo makubwa kama matokeo. Asili ya dhambi iliyorithiwa ya kila mtu [tabia ya asili ya kutenda dhambi] bila kuepuka husababisha dhambi za kibinafsi. Kisha dhambi hizo za kibinafsi zinamtenganisha na Mungu. Bila Mungu kuingilia kati, tungelipa deni la dhambi zetu. Deni hilo ni kutenganishwa milele na Mungu. Hata hivyo, Yesu alilipia dhambi zetu kwa kifo chake msalabani. Tunazaliwa upya tunapompokea Yesu kama Mwokozi wetu kwa kumwamini. Malipo yake msalabani yanakuwa malipo yetu kwa ajili ya dhambi wakati tunapomwamini.

### WOKOVU

Yesu alipokufa msalabani, kule kuwa mbadala wetu kuliondoa ghadhabu ya Mungu [kulimridhisha] dhidi ya wanadamu … na kulikomboa [kulilipia] dhambi ya mwanadamu … na kulimpatanisha mwanadamu [kulimbadilisha kwa kumfanya aweze kuokolewa].

Hata hivyo, hakuna mtu aliyeokolewa au anayeokolewa moja kwa moja kutokana na mambo hayo. Yote hayo hapo juu yalitimizwa msalabani ... lakini hakuna wokovu wa jumla uliookoa wanadamu wote. Kila mtu lazima azaliwe upya kupitia imani ya kibinafsi katika Yesu.

Unapoweka imani yako binafsi katika Yesu, uhamisho mara mbili unatekelezwa kwa ajili yako kwa kuwa dhambi yako inatwaliwa na Yesu [inahamishwa] na haki yake inatwaliwa na wewe [inahamishwa]. Ni lazima uchukue hatua ya imani [Waefeso 2:8-9]. Imani yako ya kibinafsi ni muhimu ... hakuna wokovu wa jumla.

Kisha, kwa njia ya imani, Yesu kuwa mbadala wetu msalabani … kunaondoa ghadhabu ya Mungu [kunamridhisha] dhidi yako … na kunakomboa [kunalipia] dhambi yako binafsi … na kunakupatanisha [kunakubadilisha]. Na hivyo, unahesabiwa haki [unatangazwa kuwa mwenye haki] na Mungu.

**UNA UHAKIKA KABISA?** Je, una uhakika kabisa kwamba uko sawa mbele za Mungu milele? Unaweza kumpenda Mungu, unaongea naye, unaenda katika Nyumba yake, na unatoa muda wako na rasilimali zako kwake … lakini hujawahi kuweka imani yako kwake. Yesu alisema, *“Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni,”* Mathayo 7:21. Yesu aliendelea katika Mathayo 7 kusimulia kuhusu mtu aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba. Ilikuwa ni mwamba, msingi, uliomwokoa mtu huyo kutokana na dhoruba. Je, una uhakika kabisa kwamba msingi wako ni salama. Yesu ndiye mwamba pekee utakaokuokoa milele. Ikiwa unataka kusuluhisha jambo hili milele, unaweza kufanya hivyo kwa kuomba sala hii rahisi ya imani. Ikiwa … ikiwa kweli inadhihirisha tamanio la moyo wako, nakualika uiombe sasa.

> *Bwana Mungu,*
> *Nakubali hitaji langu ... mimi ni mwenye dhambi.*
> *Natubu ... nakugeukia kutoka kwa dhambi yangu.*
> *Namwamini Yesu ... kwamba akiwa Mungu, alikufa msalabani kwa ajili yangu.*
> *Namwalika kuwa Mwokozi wangu. Amina*

Ikiwa umeomba sala hiyo sasa hivi, tafadhali tuma barua pepe kwa John, mwandishi wa kozi hii, ukitumia anwani John@Theolojia.org ili aweze kufurahi na kukuombea. Ikiwa hukuwa tayari kuomba sala hiyo, tafadhali tembelea www.Mbinguni.org kwa maelezo zaidi na kupata baadhi ya majibu ya maswali kuhusu Mungu na Biblia.

## USALAMA WA MILELE

**Wingi wa Vifungu.** Kuna vifungu vingi katika Biblia vinavyotangaza usalama wa milele. Na kuna vifungu vichache ambavyo, vinapotafsiriwa kimakosa, vinaonekana kupinga usalama wa milele. Kumbuka kwamba vifungu vyote ni kweli ... na vinahitaji kueleweka ili kusiwe na vifungu vyovyote vitakavyopuuzwa. Kuamini kwamba wokovu si wa milele ni kukana maneno ya Yesu katika vifungu vilivyoorodheshwa hapa chini kutoka katika kitabu cha Yohana.

**Biblia inasema kwamba wokovu ni wa milele.** Wokovu ni zawadi ya kudumu kutoka kwa Mungu. Haiwezi kupotea au kurudishwa ... punde unapookoka, unaookoka daima. Usalama wako wa milele unategemea kazi ya Mungu, si kazi yako. Humshikili Mungu kwa nguvu zako ... Yeye ndiye anayekushikilia kwa nguvu zake. Hakuna mtu yeyote, hata wewe, aliye na nguvu kuliko Mungu. Umeshikiliwa kwa nguvu na kwa usalama mkononi mwake milele na milele.

Yesu aliahidi, *"Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea **kamwe**; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu. Baba yangu … ni mkuu kuliko wote; wala **hakuna mtu** awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu,"* Yohana 10:28-29.

Yesu aliahidi, *"Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka **yuna** uzima wa milele; wala **haingii** hukumuni, bali **amepita** kutoka mautini kuingia uzimani,"* Yohana 5:24.

Yesu aliahidi, *"Wote anipao Baba watakuja kwangu; wala ye yote ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe,"* Yohana 6:37.

**Matendo mema hayakuokoi.** Hakuna matendo mema yoyote yanayoweza kuongeza chochote katika gharama ambayo Yesu alilipa kwa ajili ya wokovu wako. *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; **wala si kwa matendo**, mtu awaye yote asije akajisifu,"* Waefeso 2:8-9. Kazi nzuri ya kushikilia wokovu wako haikuokoi. Kazi nzuri ya kutokuacha wokovu wako haikuokoi. Damu ya Yesu yenye thamani kuu ya ililipa gharama kamili. *"Mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo … bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo,"* 1 Petro 1:18-19. Uliokolewa kwa damu yake wala hakuna chochote unachoweza kuongeza kwa hilo.

**Kuhesabiwa** haki ni *tangazo* la kuwa mwenye haki. Maisha yako yaliyobadilika yanatangaza kwamba umeokolewa ... lakini hayakuokoi. *"Mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake,"* Yakobo 2:24. Ulimwengu hauwezi kuona imani yako, lakini unaweza kuona maisha yako yaliyobadilika.

**Matendo mema ni muhimu.** *"Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema,ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo,"* Waefeso 2:10. Na matendo yako yatahukumiwa kwa moto, 1 Wakorintho 3:10 -15. Kinachobaki baada ya moto, kitaamua thawabu utakayopata. Ikiwa hakuna kitu kinachobaki, *"atapata hasara; ila yeye mwenyewe ataokolewa," msitari wa 1*5. Wokovu hauwezi kupotezwa kamwe … lakini thawabu zinaweza kuptoezwa.

**Nyakati tatu za wokovu ... wakati uliopita, wakati uliopo na wakati ujao**. *Tumeokolewa* kutokana na adhabu ya dhambi, Luka 7:50, Waefeso 2:5,8. *Tunaokolewa* kutokana na nguvu ya dhambi, Wafilipi 2:12, 1 Wakorintho 1:18, na 2 Wakorintho 2:15. Na *tutaokolewa* kutokana na uwepo wa dhambi, Warumi 5:9-10, 13:11. Hakuna muumini anayepotea katika hatua hizi tatu. Kwa kweli kinyume chake kinasemwa wazi ... wote ambao wameokolewa hatimaye wataokolewa kikamilifu siku ya mwisho, Yohana 6:39 na Warumi 8:30.

**Nidhamu ya Mungu.** Waebrania 12:4-13 inaeleza nidhamu yake kwa Waumini wote. Hata hivyo, Yeye hachukui wokovu wetu kama sehemu ya nidhamu yake. Na Waebrania 5:11 - 6:8 inaeleza kwamba muumini aliyekuwa mdhaifu anahitaji kukua katika imani badala ya kuzaliwa upya tena. Waebrania 6:6 inaongeza kusema kwamba *anayejikwaa* [maana ya Kigiriki iliyotafsiriwa kama *aliyeanguka* katika mstari wa 6] hahitaji toba iokoayo [kwa vile tayari ameokolewa] kwa sababu hilo tayari limetekelezwa na itakuwa ni kama kudhihaki kazi ya Kristo kama kazi ambayo haitoshi.

**Hitimisho lenye nguvu.** Hakuna kitu chochote wala mtu yeyote atakayeweza *"Kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu,"* Warumi 8:35-39.

## MIFANO YA *"KUAMINI"*

**Ndoa.** Nilikutana na mwanamke mchanga mrembo na mzuri ... na nikampenda. Nilimpenda kweli, nilizungumza naye karibu kila siku, nilisoma barua zake, nilienda nyumbani kwake mara nyingi, nilimpa zawadi, na niliwaambia watu wengine juu yake. Lakini ... hatukuwa tumefunga ndoa. Kisha siku moja, kama tulivyopanga, tulisimama mbele ya Mchungaji Love [jina lake halisi] ili kutangaza viapo vyetu vya ndoa. Akauliza, "Je, utamchukua mwanamke huyu awe mke wako wa ndoa halali?" Wakati huo, ilinibidi nifanye uamuzi wangu wa mwisho ... je, nitamwamini *yeye* au *nitaamini kumhusu* yeye? Nilisema "ndiyo" na Mchungaji Love akatutangaza kuwa mume na mke. Vivyo hivyo watu wengi *wanaamini kuhusu* Yesu. Wanampenda, wanazungumza naye, wanasoma Biblia, wanaenda kanisani, wanampa sadaka zao za muda na pesa, na wanawaambia wengine juu yake … lakini hawajawahi kumwambia "Ndiyo." Kwa kweli *wanaamini kuhusu* Yesu … lakini pia wanahitaji *kumwamini* Yesu.

**Parachuti.** Naamini *kuhusu* parachuti. Funga parachuti mgongoni mwako na uruke nje ya ndege na itakufikisha chini salama. Hiyo ni rahisi kwangu kusema kwa sababu sijawahi kufanya hivyo. Nimeona parachuti zikifanya kazi mara nyingi ... lakini sijawahi kulazimika kuweka imani yangu katika parachuti. Hebu fikiria umesimama kwenye mlango ulio wazi wa ndege ambayo imepoteza nguvu na hakika inaelekea kuanguka mlimani. Kuruka kutoka kwenye ndege ndio wakati ambapo *kuamini kuhusu* parachuti kunabadilika na kuwa kuamini parachuti. Kukaa kwenye ndege na *kuamini kuhusu* parachuti hakutakuokoa kutokana na uangamizo. Vivyo hivyo *kuamini kuhusu* Yesu hakumwokoi mtu. Ni lazima *umwamini* ili uokolewe. Kuruka kutoka kwenye ndege na parachuti yenye hitilafu pia hakutakuokoa. Vivyo hivyo kuamini mungu wa uwongo hakutakuokoa. Kuruka kutoka kwenye ndege ni hatua ya imani ... si ile kazi nzuri unayofanya. Kazi yote ya uokoaji inafanywa na parachuti ... inakufikisha chini salama. Kumwamini Yesu ni hatua ya imani ... kisha anakubeba katika maisha hadi katika usalama wa milele.

**Tohara ya Agano la Kale.** Hii ilikuwa ni desturi ya Kiebrania iliyoanzishwa katika Sheria ya Agano la Kale. Lakini desturi hiyo haikumwokoa mtu yeyote kiroho. Kilichohitajika ni tohara ya moyo. Yeremia 9:25-26 inaeleza watu ambao watakaohukumiwa na Mungu kama wale *"waliotahiriwa katika hali yao ya kutokutahiriwa … hawakutahiriwa mioyo yao."* Na mojawapo ya kauli wazi zaidi katika Biblia kuhusu hitaji la moyo uliyotolewa kwa Mungu ni Yeremia 4:4, *"Jitahirini kwa BWANA, mkaziondoe govi za mioyo yenu."* Kumwamini Yesu hakuhusu desturi na viapo … ni kumwamini kutoka moyoni.

**Mifano mingine.** Kuna vielelezo vingine kuhusu kuamini unavyoweza kubuni kwa ajili ya kueleza Injili kama vile:

**Ndege** … kuabiri ndege kwa ajili ya safari yako ya kwanza kwa ndege.

**Upasuaji wa moyo** … kumwamini daktari wa upasuaji kupasua kifua chako na moyo wako.

**Dawa** … kumeza mchanganyiko wa kemikali ili kuokoa maisha yako.

**Mto Kongo** … kupanda boti ili kusafiri kwenye maji yanayokwenda kasi ya Livingstone Falls Rapids.

Acts One Eight [Matendo Moja Nane]huchapisha tafsiri hii ya Kiswahili ya kozi ya lugha ya Kiingereza ya *Disciplemaking 1 … Abiding in His Word*. Unaweza kunakili kozi hii au sehemu yake yoyote bila malipo au kwa gharama ya usambazaji pekee, bila kubadilisha maudhui yake na ukiwa umeambatanisha kauli hii ya chanzo. Kozi hii inapatikana bila malipo katika lugha ya Kiswahili kutoka katika www.Theolojia.org au katika lugha ya Kiingereza kutoka katika www.VIrtualBibleAcademy.org. Kwenye tovuti hizi, unaweza kusoma mtandaoni, kufundishwa, kupakua, au kuchapisha nakala zako mwenyewe. Nukuu za Biblia ya Kiswahili zimetoka katika Biblia ya Swahili Union Version (SUV) ya 1997.

*Kufanya Wanafunzi 1 - Maswali ya Marudio*

# Somo la 1 - Wokovu ... ukurasa wa 12 - 18

Sehemu ya kujifunza ni kufanya marudio … kuhifadhi maarifa mapya kwenye kumbukumbu yako ya muda mrefu. Chapisha mtihani huu wa marudio au tumia karatasi tofauti kujibu maswali yafuatayo. Kisha rudia mtihani huu, ukisoma maelezo ya kozi au bila kuyasoma, hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi. *Mitihani hii ya marudio* pamoja na majibu sahihi yanapatikana kwenye www.Theolojia.org.

1. Weka mviringo au pigia mstari mambo yafuatayo ambayo ni dhambi au yanaweza kuwa dhambi katika maisha yako.

   Wazo        Tendo lililotendwa        Tendo lisilotendwa        mtazamo

2. Jaza pengo kwa kutumia nambari kutoka machaguo yaliyowekwa nambari upande wa kulia.

| | |
|---|---|
| Dhambi ya kurithi ni ________. | 1. Tabia yangu ya asili ya kutenda dhambi. |
| Asili ya dhambi ni __________. | 2. Dhambi yangu mwenyewe. |
| Dhambi ya kibinafsi ni _______. | 3. Uhusiano wangu na Adamu. |

3. Kabla ya wokovu, kwa sababu ya dhambi, huna _________________________ na Mungu, na ________________________ na yeye, na unasimama mbele za Mungu ukiwa mwenye hatia na ______________________________________.

Kamilisha kauli hizi sita kwa kujaza nafasi iliyo wazi kwa herufi kutoka kwenye orodha iliyo upande wa kulia.

| | |
|---|---|
| 4. Kuwa mbadala kunamaanisha ___________. | a. Mungu alitangaza kuwa mimi ni mwenye haki. |
| 5. Ukombozi unamaanisha ________________. | b. Mungu aliridhika. |
| 6. Ondoleo la ghadhabu inamaanisha ________________. | c. Uhamisho mara mbili. |
| 7. Upatanisho unamaanisha_______________. | d. Yesu alichukua nafasi yangu. |
| 8. Uhamisho unamaanisha________________. | e. Nilibadilishwa. |
| 9. Kuhesabiwa haki kunamaanisha ___________________. | f. Dhambi yangu ililipiwa. |

10. Kulingana na Yohana 3:16, ni nini unachomiliki sasa punde ulipomwamini Yesu Kristo? ______________________________________________________ .

11. Kulingana na Yohana 5:24, ulipomwamini Yesu, una ahadi tatu:
    a. Una ________________________________________.
    b. Hutaingia _____________________________________________.
    c. Umepita kutoka _________________ na kuingia _____________.

12. Kulingana na Yohana 6:37, ____________% ya wale ambao Baba anampa Yesu wanakuja kwake, na _____________% wanatupwa nje.

13. Kulingana na Yohana 10:28-29, _____________________ anayeweza kukunyakua kutoka mkononi mwa Mungu kwa sababu Mungu ni mwenye ____________________________________________ kuliko wote.

14. Kwa hivyo, ikiwa unaamini kwamba unaweza kupoteza wokovu wako, unaamini kwamba una ________________________ ya kutosha kujinyakua kutoka mkononi mwa Mungu.

15. Kwa maneno machache, eleza kwa nini Yakobo 2:24 haipingi Waefeso 2:8-9 ukitumia 2 Wakorintho 13:5 katika jibu lako.

***Swali maalum na muhimu zaidi:*** *Je, una uhakika kabisa kwamba umeweka imani yako katika Yesu kama Mwokozi wako? Ikiwa huna uhakika, ikiwa una shaka yoyote, unaweza kuweka imani yako katika Yesu Kristo kama Mwokozi wako sasa na utatue suala hilo milele. Tafadhali tembelea www.Mbinguni.org ambapo unaweza kusoma maelezo ya jinsi unavyoweza kuwa na uhakika kwamba uko sawa mbele za Mungu.*

# Somo la 1 - Wokovu … maswali ukurasa wa 19 - 20

Usitumie karatasi hizi za majibu kupata majibu yako. Tafadhali zitumie tu kukagua majibu yako. Rudi kwenye somo ili kupata taarifa za kurekebisha majibu yako. Rudia mtihani hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi. Masomo yote, mitihani ya marudio, na kurasa za majibu zinapatikana katika www.Theolojia.org.

1. Weka mviringo au pigia mstari mambo yafuatayo ambayo ni dhambi au yanaweza kuwa dhambi katika maisha yako.

   _*Wazo*_ _*Tendo lililotendwa*_ _*Tendo lisilotendwa*_ _*mtazamo*_.

2. Jaza pengo kwa kutumia nambari kutoka machaguo yaliyowekwa nambari upande wa kulia.

   Dhambi ya kurithi ni __*3*__. 1. Tabia yangu ya asili ya kutenda dhambi.

   Asili ya dhambi ni __*1*__ . 2. Dhambi yangu mwenyewe.

   Dhambi ya kibinafsi ni __*2*__. 3. Uhusiano wangu na Adamu.

3. Kabla ya wokovu, kwa sababu ya dhambi, huna __*uhusiano*__ na Mungu, na __*umetenganishwa*__ na yeye, na unasimama mbele za Mungu ukiwa mwenye hatia na __*umehukumiwa*__ .

Kamilisha kauli hizi sita kwa kujaza nafasi iliyo wazi kwa herufi kutoka kwenye orodha iliyo upande wa kulia.

4. Kuwa mbadala kunamaanisha __*d*__. — a. Mungu alitangaza kuwa mimi ni mwenye haki.
5. Ukombozi unamaanisha __*f*__. — b. Mungu aliridhika.
6. Ondoleo la ghadhabu inamaanisha __*b*__. — c. Uhamisho mara mbili.
7. Upatanisho unamaanisha __*e*__. — d. Yesu alichukua nafasi yangu.
8. Uhamisho unamaanisha __*c*__. — e. Nilibadilishwa.
9. Kuhesabiwa haki kunamaanisha __*a*__. — f. Dhambi yangu ililipiwa.

10. Kulingana na Yohana 3:16, ni nini unachomiliki sasa punde ulipomwamini Yesu Kristo? __*uzima wa milele*__.

11. Kulingana na Yohana 5:24, ulipomwamini Yesu, una ahadi tatu:
    a. Una __*uzima wa milele*__ .
    b. Hutaingia __*hukumuni*__ .
    c. Umepita kutoka __*mauti*__ na kuingia __*uzimani*__ .

12. Kulingana na Yohana 6:37, __*100*__% ya wale ambao Baba anampa Yesu wanakuja kwake, na __*sufuri*__% wanatupwa nje.

13. Kulingana na Yohana 10:28-29, __*hakuna yeyote*__ anayeweza kukunyakua kutoka mkononi mwa Mungu kwa sababu Mungu ni mwenye __*nguvu*__ kuliko wote.

14. Kwa hivyo, ikiwa unaamini kwamba unaweza kupoteza wokovu wako, unaamini kwamba una __*nguvu*__ ya kutosha kujinyakua kutoka mkononi mwa Mungu.

15. Kwa maneno machache, eleza kwa nini Yakobo 2:24 haipingi Waefeso 2:8-9 ukitumia 2 Wakorintho 13:5 katika jibu lako.

    *Kuhesabiwa haki kwa matendo (Yakobo 2:24) ina maana kwamba unatangazwa kuwa mwenye haki kwa msingi wa matendo mema. Matendo mema hayaokoi mtu yeyote … imani pekee katika Kristo pekee ndio inayomwokoa mtu. Wokovu huzaa matendo mema. (agizo la kujichunguza katika 2 Wakorintho 13:5) lakini matendo mema hayazai wokovu.*

***Swali maalum na muhimu zaidi:*** *Je, una uhakika kabisa kwamba umeweka imani yako katika Yesu kama Mwokozi wako? Ikiwa huna uhakika, ikiwa una shaka yoyote, unaweza kuweka imani yako katika Yesu Kristo kama Mwokozi wako sasa na utatue suala hilo milele. Tafadhali tembelea www.Mbinguni.org ambapo unaweza kutazama video au kusoma maelezo ya jinsi unavyoweza kuwa na uhakika kwamba uko sawa mbele za Mungu.*

### Kufanya Wanafunzi 1 - Kudumu Katika Neno Lake

## SOMO LA 2 - SALA

*"Ikawa alipokuwa mahali fulani akiomba, alipokwisha, mmoja katika wanafunzi wake alimwambia, 'Bwana, tufundishe sisi kusali, kama vile Yohana alivyowafundisha wanafunzi wake.'"* Luka 11:1

Utaratibu wa sala uko wazi katika mafundisho na mifano ya Biblia. Utaratibu huo unajumuisha sifa, shukrani, ungamo, na mahitaji. Haya yote manne si lazima yawe katika kila sala ... lakini yote yanapaswa kujumuishwa katika maisha yetu ya sala.

**SIFA** … kwa sababu yeye ni Mungu. Kumsifu Mungu kunamwinua, kunamheshimu, na kunamtukuza, Zaburi 34:1-3. Sifa ni sehemu muhimu sana ya jinsi sala zetu zinavyopaswa kuwa. Tunafundishwa kwamba *"tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima,"* Waebrania 13:15. Mifano bora ya kibiblia ya kumsifu Mungu inapatikana katika Zaburi 144-150. Mifano mingi ya sifa inaweza kupatikana katika Zaburi zote na katika vitabu vingine vya Biblia.

**SHUKRANI** … kwa sababu ya yale aliyofanya. Mungu hutupatia mengi ya kushukuru katika maisha yetu ... kulingana na maombi yetu ... na mara nyingi kwa sababu anatupenda, *"Ni neno jema kumshukuru BWANA,"* Psalm 92:1. *"Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani,"* Wakolosai 4:2. *"Shukuruni kwa kila jambo,"* 1 Wathesalonike 5:18. Na kukosa shukrani ni dhambi ya siku za mwisho, 2 Timotheo 3:1-5.

**UNGAMO** … kwa sababu ya dhambi yetu. Kuungama ni kukiri dhambi zetu kwa Mungu. Tunapofanya hivyo, ameahidi kwamba *"atatuondolea dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote,"* 1 Yohana 1:9. Daudi alieleza baraka kuu za msamaha katika Zaburi 32 ... na akatupa mfano mkuu wa ungamo katika Zaburi 51:1-13. Dhambi isiyoungamwa inazuia ushirika wetu na Mungu.

**MAHITAJI** … kwa sababu anatupenda. Ni hamu ya Mungu kukidhi mahitaji yetu na kutupa matamanio ya mioyo yetu, Zaburi 37:4. Tumeagizwa *"haja zenu na zijulikane na Mungu,"* Wafilipi 4:6. Hata hivyo, wakati mwingine hatupokei kwa sababu hatuombi ... au kwa sababu tunaomba kwa nia mbaya, Yakobo 4:2,3. Mahitaji ya kiroho mara nyingi ni muhimu zaidi kuliko mahitaji ya kimwili. Mifano ya aina zote mbili inapatikana katika Sala ya Bwana katika Mathayo 6:9-13.

**MSISITIZO WA KIBIBLIA**. Biblia ni kumbukumbu ya wanaume na wanawake waliojitolea katika sala. Zaburi zina mifano mingi ya mwanadamu akimimina moyo wake kwa Mungu. Sehemu nyingine ya Biblia ina zaidi ya sala 600 na majibu 400 mahususi. Adamu na Hawa walizungumza wazi na Mungu katika bustani ya Edeni. Ni katika siku za mwana wao wa tatu, Sethi, *"ndipo watu walipoanza kuliitia Jina la BWANA,"* Mwanzo 4:26. Wanaume na wanawake wakuu wa Agano la Kale na Agano Jipya walijitolea katika sala ... Musa, Hana, Samweli, Daudi, Danieli, na Paulo. Hata maneno machache ya mwisho ya Biblia yanajumuisha sala ya, *"Na uje, Bwana Yesu,"* Ufunuo 22:20.

**MFANO WA YESU**. Yesu alionyesha na alifundisha kwamba sala inapaswa kupewa kipaumbele sana. Mwanzoni mwa huduma yake, aliomba wakati wa ubatizo wake. Pia aliwafundisha wanafunzi wake jinsi ya kuomba. Alijiombea yeye mwenyewe ... wanafunzi wake ... na ulimwengu. Alienda mahali peke yake asubuhi na mapema ili kuzungumza na Baba yake. Wakati mwingine aliomba usiku kucha. Yesu aliombea chakula alichokula na kile alichowaandalia wengine. Usiku kabla ya kufa kwake, aliomba kwa bidii sana katika bustani ya Gethsemane kiasi kwamba jasho lake likawa kama matone ya damu. Kisha alipokuwa akining'inia msalabani, aliomba, *"Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo."* Luka 23:34. Kama mwombezi mkuu, Yesu anatuombea sasa, Waebrania 7:25, Warumi 8:34. Roho Mtakatifu pia hutuombea wakati hatujui jinsi ya kuomba, Warumi 8:26.

**CHANGAMOTO KWETU**. Kwa msingi wa msisitizo huo wa sala katika Biblia nzima, tunapaswa kujitolea sisi kwa sala na kujifunza jinsi ya kuomba kwa ufanisi zaidi. Ni fursa yetu maalum kuzungumza na Mungu aliye hai. *"Macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, na masikio yake hukielekea kilio chao,"* Zaburi 34:15. *"Kwa hiyo, kila mtu mtauwa akuombe,"* Zaburi 32:6. *"Mtu wa kwenu amepatikana na mabaya? Na aombe. Ana moyo wa kuchangamka? Na aimbe zaburi,"* Yakobo 5:13. Majibu ya maswali matano yafuatayo yanasaidia kuelewa sala.

**1. JE, NINAPASWA KUSALI WAPI?** Ni jambo la kawaida kufikiria kusali katika jengo la kidini. Yesu alitaja hekalu kama *"nyumba ya sala,"* Mathayo 21:13. Hata hivyo, maombi hayahusu tu majengo ya kidini na mikutano ya hadhara. Alipokuwa akizungumza na mwanamke kwenye kisima katika Yohana 4, Yesu alionyesha wazi kabisa kwamba ibada ya kweli ilitolewa *"katika roho na kweli"* na haikutegemea mahali ambapo ibada hiyo inafanywa. Aliwashutumu wanafiki kwa maombi yao ya hadhara katika masinagogi na barabarani ili waonekane na watu ... na akapendekeza kwamba sala ifaayo ni bora itolewe faraghani katika chumba cha ndani mbali na wengine, Mathayo 6:5-6. Ni wazi kwamba sala ifaayo haitegemei mahali inaposaliwa. Inategemeana hali ya moyo ya yule anayesali.

**2. JE, NINAPASWA KUPIGA MAGOTI NINAPOSALI?** Yesu alipiga magoti na kusali, Luka 22:41. Danieli alipiga magoti na kusali mara tatu kwa siku, Danieli 6:10. Kabla ya kuondoka Efeso, Paulo alipiga magoti na kusali, Matendo 20:36. Yehoshafati aliinamisha kichwa na kusali, 2 Mambo ya Nyakati 20:18. Kwa sababu ya dhambi za watu, Ezra alirarua nguo zake na akapiga magoti na kunyoosha mikono yake ... lakini hakuinua uso wake kwa Mungu, Ezra 9:5-6. Alipokuwa akiuawa kwa ajili ya imani yake, Stefano aliinua uso wake na kutazama Mbinguni huku akisali, Matendo 7:55-60. Kusujudu mbele za Mungu katika sala na ibada, hata kufikia hatua ya kuinamisha nyuso zao hadi ziguse chini, kulikuwa jambo la kawaida katika maisha ya watu wa Biblia. Kusimama wakati wa kusali kunapatikana katika Marko 11:25. Hezekia aligeuza uso wake ukutani na kusali, 2 Wafalme 20:2. Jinsi mwili unavyowekwa haina manufaa yoyote katika ufanisi wa sala. Ni muhimu tu kadiri inavyodhihirisha hali ya moyo.

**3. JE, NINAPASWA KUMWOMBA NANI?** Katika vipengele vyote vya sala, tunapaswa kujitahidi kufuata mafundisho na mifano ya Maandiko. Biblia haitaji kamwe sala iliyoelekezwa kwa mtu yeyote isipokuwa kwa Mungu mwenyewe. Hakuna mifano au mafundisho yanayotuongoza kusali kwa malaika, watu watakatifu, au Wakristo wowote waliokufa. *Mahitaji* ya sala yanapaswa kuelekezwa kwa Baba, Yohana 15:16, 16:23. Tunapaswa kuomba katika Roho, Waefeso 6:18, Yuda 20 ... chini ya uongozi wa Mungu. Tumeagizwa kuomba *"kwa jina la Yesu,"* Yohana 14:3, 15:16 … yaani, kulingana na mapenzi yake na kwa nguvu yake. Utaratibu huu wa Kibiblia unatuhakikishia kwamba rasilimali zote za Mungu mwenye nafsi tatu ziko pamoja nasi tunaposali.

**4. JE, NI JINSI GANI NINAPASWA KUSALI?** *Jinsi* ya kusali ni muhimu kama, au muhimu zaidi kuliko, *kile* unachoombea. Yesu aliwafundisha wanafunzi wake Sala ya Bwana, Mathayo 6 na Luka 11, kama kielelezo cha kufuata. Mifano ya kibiblia ni pamoja na Danieli aliwaombea watu, Danieli 9 ... Daudi aliomba msamaha, Zaburi 51 ... Yesu aliomba, Yohana 17 ... na Mfarisayo na Mtoza Ushuru waliomba, Luka 18. Sala ya Kibiblia ni kumimina moyo kwa Mungu kwa njia wazi nay a kweli. Miongozo ya Maandiko ni pamoja na kusali ...

Kwa unyenyekevu, 2 Mambo ya Nyakati 7:14, 34:27.
Kwa moyo wa shukrani, 1 Wathesalonike 5:18, Wafilipi 4:6.
Kutoka moyoni, si kwa kukariri, Isaya 29:13.
Kwa uwazi na moja kwa moja, Isaya 37:14.
Kwa kujitolea sana, Wakolosai 4:2.
Bila kukoma, 1 Wathesalonike 5:17.
Bila kukata tamaa, Luka 11:5-10, 18:1-8.
Kwa kujitahidi sana, Warumi 15:30.
Kwa njia rahisi, Mathayo 6:7.
Bila ghadhabu wala mafarakano, 1 Timotheo 2:8.
Kwa umoja na Waumini wengine, Mathayo 18:19-20.
Kwa imani kuu, Yakobo 1:6-7, Waebrania 11:6.
Kulingana na mapenzi yake, Yohana 15:7, 1 Yohana 5:14-15.

**5. JE, NINAPASWA KUOMBEA NINI?** Ni baraka kumwomba Mungu ahusike katika maisha yetu. Ni baraka inayopaswa kuchukuliwa kwa uzito. Katika Sala ya Bwana, Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuombea mahitaji yao ya kila siku ya kimwili na kiroho. Katika sala yake ya Yohana 17, alijiombea yeye mwenyewe, wanafunzi wake, na ulimwengu akitaja mahitaji mahususi sana. Yesu aliahidi kwamba sala ya imani, inayolingana na mapenzi ya Mungu, inayotolewa kwa Baba, katika jina lake, itajibiwa, Yohana 15:7,16, 16:23, 1 Yohana 5:14-15.

Mapendekezo mengine ya Kibiblia ni pamoja na kuombea ...
Hekima, Yakobo 1:5, 2 Mambo ya Nyakati 1:7-12.
Mafanikio ya kiroho, Wakolosai 1:9-12.
Wale wanaowaonea, Luka 6:28.
Uponyaji, Yakobo 5:14-15, 2 Wakorintho 12:7-9.
Wenzetu, Waefeso 6:18, Yakobo 5:16.
Serikali, 1 Timotheo 2:1-2.
Chakula chetu, Marko 6:41, 8:6 .
Wale wanaomhitaji Kristo, Warumi 10:1.
Watenda kazi ili watangaze Injili, Mathayo 9:37-38.
Milango ifunguke kwa ajili ya injili, Wakolosai 4:3-4.

## KUNYIMWA NA KUCHELEWESHWA

Mungu husikia sala zetu zote na hujibu sala zetu zote. Jibu lake linaweza kuwa *ndiyo*, *hapana*, au *subiri* [jibu la endelea kuomba lakini hakuna jibu bado]. Wakat mwingine Mungu hufanya zaidi ya kusema ndiyo na anatupatia zaidi ya yote tunayoomba au kufikiria, Waefeso 3:20. Wakati mwingine jibu lake ni *hapana* au *subiri*. Baadhi ya sababu za jibu la *hapana* au *subiri* ziko hapa chini.

**Kutoomba.** Kanuni ya Yakobo 4:2 inatumika kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwenye suala hili … *"Hamna kitu kwa kuwa hamwombi."* Usitarajie Mungu ajibu maombi yasiyoombwa.

**Nia mbaya.** *"Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu,"* Yakobo 4:3.

**Jinsi mume anavyomtendea mke wake.** Biblia inafundisha kwamba mume anapaswa kumpenda mke wake kama Kristo anavyolipenda kanisa, kumthamini, kuwa na subira naye, na kumheshimu kama mrithi sawa wa neema ya uzima ... kama 1 Petro 3:7 inavyosema, *"kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe."*

**Roho ya kutosamehe.** Kutosamehe huzuia sala zetu na msamaha wetu kwa wengine unaonyesha msamaha tunaopaswa kutarajia kutoka kwa Mungu, Marko 11:25, Mathayo 5:23-24, 6:12-15. Katika sala ya Bwana, kimsingi tunamwomba Mungu atusamehe kwa njia ile ile tunayowasamehe wengine.

**Ukosefu wa uadilifu.** Tunapaswa kuwa safi mbele za Mungu, kisha sala zetu zitatimiza mengi. *"Maombi ya mtu mnyofu ni furaha yake,"* Mithali 15:8. Mtu akiasi sheria ya Mungu, *"hata sala yake ni chukizo,"* Mithali 28:9.

**Ulinzi, maandalizi, au ukamilifu**. Kunyimwa na kucheleweshwa kwa jibu kunaweza kuwa kwa faida yetu. Wakati mwingine Mungu hutulinda kwa sababu hatujui kwamba tunachoomba kitatuumiza. Mungu anatujua vizuri zaidi kuliko jinsi tunavyojijua wenyewe ... na wakati mwingine, anasema *hapana* kwa sababu anajua ni nini kilicho bora kwetu. Wakati mwingine kucheleweshwa kunakuwepo ili kutupa muda wa kujiandaa, au kuandaliwa, kwa ajili ya jibu lake. Na wakati mwingine kunyimwa na kucheleweshwa hutumika kukamilisha imani yetu.

**Kunyimwa kikamilifu.** Baadhi ya majibu ya kunyimwa ni ya mwisho. Kwa Musa, *"BWANA alikuwa amenikasirikia kwa ajili yenu, asinisikize; BWANA akaniambia, 'Na ikutoshe, usinene nami zaidi jambo hili. Kwea katika kilele cha Pisga ukainue macho yako upande wa magharibi, na kaskazini, na kusini, na mashariki, ukatazame kwa macho yako, kwa maana huuvuki mto huu wa Yordani,'"* Kumbukumbu la Torati 3:26-27. Naye Paulo aliomba kwamba mwiba uliokuwa mwilini mwake uondolewe. Lakini kama alivyoandika, *"Na makusudi nisipate kujivuna kupita kiasi, kwa wingi wa mafunuo hayo nalipewa mwiba katika mwili, mjumbe wa Shetani ili anipige, nisije nikajivuna kupita kiasi. Kwa ajili ya kitu hicho nalimsihi Bwana mara tatu kwamba kinitoke. Naye akaniambia, 'Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu.' Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu,"* 2 Wathesalonike 12:7-10. Kubali jibu la Mungu la hapana kwa moyo wa shukrani … Mungu anajua kile anachofanya.

Acts One Eight [Matendo Moja Nane]huchapisha tafsiri hii ya Kiswahili ya kozi ya lugha ya Kiingereza ya *Disciplemaking 1 … Abiding in His Word*. Unaweza kunakili kozi hii au sehemu yake yoyote bila malipo au kwa gharama ya usambazaji pekee, bila kubadilisha maudhui yake na ukiwa umeambatanisha kauli hii ya chanzo. Kozi hii inapatikana bila malipo katika lugha ya Kiswahili kutoka katika www.Theolojia.org au katika lugha ya Kiingereza kutoka katika www.VIrtualBibleAcademy.org. Kwenye tovuti hizi, unaweza kusoma mtandaoni, kufundishwa, kupakua, au kuchapisha nakala zako mwenyewe. Nukuu za Biblia ya Kiswahili zimetoka katika Biblia [ya Swahili Union Version (SUV) ya 1997].

## Somo la 2 - Maombi ... ukurasa wa 23 - 26

Sehemu ya kujifunza ni kufanya marudio … kuhifadhi maarifa mapya kwenye kumbukumbu yako ya muda mrefu. Chapisha mtihani huu wa marudio au tumia karatasi tofauti kujibu maswali yafuatayo. Kisha rudia mtihani huu, ukisoma maelezo ya kozi au bila kuyasoma, hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi.
*Mitihani hii ya marudio* pamoja na majibu sahihi yanapatikana kwenye www.Theolojia.org.

1. Vipengele vinne vya msingi vya sala ni vipi?
   a.
   b.
   c.
   d.

2. Kuna tofauti gani kati ya sifa na shukrani? Toa mfano wa kila moja.

3. Fafanua ungamo.

4. Kwa nini unapaswa kumwambia Mungu mahitaji yako?
   a.
   b.
   c.
   d.

5. Katika siku sita zijazo, tumia angalau dakika mbili na nusu ya sala kila siku katika kila moja ya mambo haya: sifa, shukrani, ungamo, na mahitaji. Weka mviringo katika kila siku ambayo umekamilisha zoezi hilo kwa ufanisi.

   Siku ya 1 ... Siku ya 2 ... Siku ya 3 ... Siku ya 4 ... Siku ya 5 ... Siku ya 6

6. Tuna mifano gani ya kibiblia ya watu waliosali [ukurasa wa 24]?

7. Unapaswa kusali wapi? Je, ni maeneo gani mapya utaongeza katika maisha yako ya sala?

8. Ni majibu gani ya *Je, ni jinsi gani ninapaswa kusali?* katika ukurasa wa 25 yalikuwa ya maana zaidi kwako?

9. Je, unapaswa kumwomba nani … na hupaswi kumwomba nani?

10. Ni njia gani za mkao wa mwili wakati wa sala ni mpya kwako?

11. Ukizingatia "Napaswa kuombea nini?" [ukurasa wa 25] utaongeza nini kwenye sala zako?

12. Kwa nini baadhi ya sala huzuiwa au hazijibiwi?

13. Sala za waadilifu ni ________________________________________ na sala za wasiotii ni ________________________________________________________.

14. Kwa nini *kunyimwa* mahitaji ya sala kunaweza kuwa jambo jema?

15. Kwa nini *kucheleweshwa* kupata majibu ya mahitaji ya sala kunaweza kuwa jambo jema?

16. Umefanya mabadiliko gani katika maisha yako ya sala kwa sababu ya somo hili?

*Kufanya Wanafunzi 1 - Maswali ya Marudio*

# Somo la 2 - Sala … maswali ukurasa wa 27 - 28

Usitumie karatasi hizi za majibu kupata majibu yako. Tafadhali zitumie tu kukagua majibu yako. Rudi kwenye somo ili kupata taarifa za kurekebisha majibu yako. Rudia mtihani hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi. Masomo yote, mitihani ya marudio, na kurasa za majibu zinapatikana katika www.Theolojia.org.

1. Vipengele vinne vya msingi vya sala ni vipi?
   a. *Sifa*
   b. *Shukrani*
   c. *Ungamo*
   d. *Mahitaji*

2. Kuna tofauti gani kati ya sifa na shukrani? Toa mfano wa kila moja.

   *Sifa ni kuhusu Mungu ni nani.*

   *Shukrani ni kuhusu kile Mungu amefanya au anachofanya.*

   *Mfano wangu wa sifa:*

   *Mfano wangu wa shukrani:*

3. Fafanua ungamo.

   *Ungamo ni kukubaliana na Mungu kwamba dhambi zangu mahususi ni dhambi.*

4. Kwa nini unapaswa kumwambia Mungu mahitaji yako? Baadhi ya sababu zimeorodheshwa hapa.
   a. *Kwa sababu ananipenda.*
   b. *Kwa sababu mara nyingi hatuna kwa sababu hatuombi.*
   c. *Kwa sabau tuna mahitaji ya kiroho na ya kimwili.*
   d. *Kwa sababu Mungu anataka kutupatia matamanio ya miyo yetu.*

5. Katika siku sita zijazo, tumia angalau dakika mbili na nusu ya sala kila siku katika kila moja ya mambo haya: sifa, shukrani, ungamo, na mahitaji. Weka mviringo katika kila siku ambayo umekamilisha zoezi hilo kwa ufanisi.

   Siku ya 1 ... Siku ya 2 ... Siku ya 3 ... Siku ya 4 ... Siku ya 5 ... Siku ya 6

6. Tuna mifano gani ya kibiblia ya watu waliosali [ukurasa wa 24]?

    *Adamu na Hawa, watu wa siku za Sethi, Musa, Hana, Samweli, Daudi, Danieli, Paulo, na Yesu*

7. Unapaswa kusali wapi? Je, ni maeneo gani mapya utaongeza katika maisha yako ya sala?

    *Kila mahali … na maeneo mapya kama vile:*

8. Ni majibu gani ya Je, ni jinsi gani ninapaswa kusali? katika ukurasa wa 25 yalikuwa ya maana zaidi kwako?

9. Je, unapaswa kuwmomba nani … na hupaswi kumwomba nani nani?

    *Kimsingi kwa Mungu Baba ... lakini pia kwa Yesu na Roho Mtakatifu. Hatupaswi kamwe kuelekeza sala zetu kwa sanamu yoyote au kwa mtu mwingine yeyote (aliye hai au aliyekufa).*

10. Ni njia gani za mkao wa mwili wakati wa sala ni mpya kwako? *Tazama ukurasa wa 24.*

11. Ukizingatia "Napaswa kuombea nini?" [ukurasa wa 25] utaongeza nini kwenye sala zako?

12. Kwa nini baadhi ya sala huzuiwa au hazijibiwi?

    *Nia mbaya, roho ya kutosamehe, dhambi, mume kumtesa mke wake.*

13. Sala za waadilifu ni __*furaha ya Mungu*__ na sala za wasiotii ni __*chukizo kwa Mungu*__.

14. Kwa nini kunyimwa mahitaji ya sala kunaweza kuwa jambo jema?

    *Kutunyima mahitaji yetu kunaweza kuwa ni njia ya Mungu ya kutulinda.*

15. Kwa nini kucheleweshwa kupata majibu ya mahitaji ya sala kunaweza kuwa jambo jema?

    *Kucheleweshwa kunaweza kutuandaa ... na/au … kututayarisha kwa jibu la Mungu.*

16. Umefanya mabadiliko gani katika maisha yako ya sala kwa sababu ya somo hili?

## Kufanya Wanafunzi 1 - Kudumu Katika Neno Lake

# Somo la 3 - Kujifunza Biblia

*"Imeandikwa, 'Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.'"* Mathayo 4:4 [rejeo: Kumbukumbu la Torati 8:3]

**UKUU WA MAANDIKO**. Hakuna kitabu kingine kinachofanana na Biblia. Hakuna kitabu kingine ambacho kimechapishwa zaidi ya Biblia. Hakuna kitabu kingine ambacho kimetafsiriwa katika lugha nyingi zaidi ya Biblia. Hakuna kitabu kingine ambacho kimesambazwa zaidi ya Biblia. Hakuna kitabu ambacho kimebadilisha maisha ya watu wengi kwa njia bora zaidi ya Biblia. Biblia ndicho kitabu muhimu zaidi kuwahi kuandikwa kwa sababu ni ujumbe wa Mungu kwetu. Ni zaidi ya kitabu cha kutia moyo. Ni kitabu kilichoandikwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Ni pumzi ya Mungu. Waandishi wa Biblia waliongozwa na Roho Mtakatifu walipokuwa wakiandika. Kwa hivyo Biblia ni kweli ... ni sahihi ... ni safi ... ni ya milele ... na ina nguvu. Biblia ni zaidi ya ujumbe wa mwanadamu kuhusu Mungu ... ni ujumbe wa Mungu kwa mwanadamu. Ni kitabu kutoka kwa Mungu ... si tu kitabu kuhusu Mungu. Ni Kitabu kikuu zaidi. Ni kitabu kilicho na mamlaka kuu na ya mwisho katika kile tunachopaswa kuamini na jinsi tunapaswa kuishi. Biblia si kitabu tu. Ni *Kitabu muhimu* zaidi. Ni *Kitabu* tunachopaswa kusoma.

**UMUHIMU WA KUJIFUNZA BIBLIA**. Kifungu kilichonukuliwa juu ya ukurasa huu kinaonyesha jinsi Yesu alivyojitolea kwa dhati kwa Neno la Mungu. Hayo yalikuwa maneno yake wakati wa majaribu yake nyikani. Neno la Mungu lilikuwa muhimu zaidi kwa Yesu kuliko chakula cha kimwili ... hata baada ya siku 40 bila kula. Biblia imetolewa ili iwe lishe yetu ya kiroho. Upatikanaji wa Neno lake unatupatia fursa kubwa na changamoto nzito ya maisha yetu yote katika kusoma Biblia. Ikiwa kweli tunataka kujifunza na kukua ... basi lazima tuwekeze muda na nguvu zote katika mchakato wa kujifunza Biblia. Hakuna njia za mkato. Ni lazima tutenge muda wa kutosha mara kwa mara katika kujifunza Neno la Mungu.

**HATUA ZA KUJIFUNZA BIBLIA**. Petro alitumia mfano wa jinsi mtoto mchanga alivyo na hamu kubwa ya maziwa kuonyesha jinsi hamu yetu ya Neno la Mungu inavyopaswa kuwa, *"Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu,"* 1 Petro 2:2. Kisha, kadiri tunavyokua, tunahitaji kuanza kula chakula kigumu kutokana na kujifunza Maandiko kwa kina zaidi, Waebrania 5:11-14. Ni muhimu kuweka malengo yanayoweza kufikiwa kwa ajili ya kujifunza Biblia mara kwa mara ... tukianza na sehemu rahisi na vitabu rahisi vya Biblia ... tukiongeza wingi na ugumu wa yale tunayojifunza kadiri tunavyozidi kukua. Katika mchakato huu wa kujifunza wa maisha yote, sala yetu wakati wote inapaswa kuwa kama ile ya mwandishi wa Zaburi, *"Unifumbue macho yangu niyatazame Maajabu yatokayo katika sheria yako."* Zaburi 119:18

**KITABU CHA KUJIFUNZA**. Biblia ndicho kitabu muhimu zaidi. Ni ujumbe wa Mungu kwetu, na hiyo inakifanya kiwe tofauti na vitabu vingine vyote. Ni kitabu muhimu sana kujifunza kwa sababu ...

### Biblia imeandikwa kwa mwongozo wa Roho Mtakatifu … ni pumzi ya Mungu.

> *"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu."* 2 Timotheo 3:16

### Biblia ni kweli.

> *"Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli."* Yohana 17:17

### Biblia ni sahihi.

> *"Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie."* Mathayo 5:18

### Biblia ni safi.

> *"Maneno ya BWANA ni maneno safi, Ni fedha iliyojaribiwa kalibuni juu ya nchi; Iliyosafishwa mara saba."* Zaburi 12:6

> *"Sheria ya BWANA ni kamilifu, Huiburudisha nafsi. Ushuhuda wa BWANA ni amini, Humtia mjinga hekima.Maagizo ya BWANA ni ya adili, Huufurahisha moyo. Amri ya BWANA ni safi, Huyatia macho nuru."* Zaburi 19:7-8

### Biblia ni ya milele.

> *"Majani yakauka, ua lanyauka; Bali neno la Mungu wetu litasimama milele."* Isaya 40:8

> *"Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe."* Mathayo 24:35

### Biblia ina nguvu.

> *"Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo."* Waebrania 4:12

## AMRI YA KUJIFUNZA BIBLIA.

Biblia iko wazi kabisa kwamba mwanamume au mwanamke wa Mungu amejitolea kwa Neno lake ... amejitolea kujifunza na kulitumia Neno lake. Hilo si jambo la hiari kwetu ... ni amri.

### Ili kuwa mwanafunzi ... dumu, yaani ishi katika Neno ... si kulitembelea Neno tu.

> *"Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, 'Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli.'"* Yohana 8:31

### Ili ukubaliwe … jifunze Neno.

> *"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli."* 2 Timoheo 2:15

### Ili uwe mzazi mzuri … wafunze watoto wako Neno.

> *"Kwa hiyo yawekeni maneno yangu mioyoni mwenu na rohoni mwenu; yafungeni yawe dalili juu ya mikono yenu, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yenu. Nayo wafunzeni vijana vyenu kwa kuyazungumza uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo."*
> Kumbukumbu la Torati 11:18-19

## MANUFAA YA KUJIFUNZA NENO.

Neno lina nguvu na ni la milele. Mungu hutubariki kadiri tunavyojifunza Neno lake. Faida za kufanya hivyo ni nyingi sana.

### Biblia hutuandaa.

> *"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."*
> 2 Timotheo 3:16-17

### Biblia hutusaidia tusitende dhambi.

> *"Jinsi gani kijana aisafishe njia yake? Kwa kutii, akilifuata neno lako … Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, Nisije nikakutenda dhambi."* Zaburi 119:9-11

### Biblia inatupatia mwongozo kwa ajili ya leo na kwa ajili ya siku zetu za usoni.

> *"Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu."* Zaburi 119:105

## MANUFAA YA KUJIFUNZA NENO … mwendelezo

### Biblia inatupatia hekima.

*"Maagizo yako hunitia hekima kuliko adui zangu, Kwa maana ninayo sikuzote. Ninazo akili kuliko wakufunzi wangu wote, Maana shuhuda zako ndizo nizifikirizo. Ninao ufahamu kuliko wazee, Kwa kuwa nimeyashika mausia yako … Kufafanusha maneno yako kwatia nuru, Na kumfahamisha mjinga."* Zaburu 119:98-100, 130

### Biblia hutusaidia tunapopitia hali ngumu.

*"Hii ndiyo faraja yangu katika taabu yangu, Ya kwamba ahadi yako imenihuisha … Ilikuwa vema kwangu kuwa naliteswa, Nipate kujifunza amri zako."* Zaburi 119:50, 71

### Biblia inaleta tumaini.

*"Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini."* Warumi 15:4

### Biblia inatupatia amani.

*"Wana amani nyingi waipendao sheria yako, Wala hawana la kuwakwaza."* Zaburi 119:165

### Biblia inatupatia furaha.

*"Maneno yako yalionekana, nami nikayala; na maneno yako yalikuwa ni furaha kwangu, na shangwe ya moyo wangu; maana nimeitwa kwa jina lako."* Yeremia 15:16

### Biblia inaleta baraka zenye masharti.

*"Haleluya. Heri mtu yule amchaye BWANA, Apendezwaye sana na maagizo yake."* Zaburi 112:1

*"Kila alidharauye neno hujiletea uharibifu; Bali yeye aiogopaye amri atapewa thawabu."* Mithali 13:13

*"Lakini yeye alisema, Afadhali, heri walisikiao neno la Mungu na kulishika."* Luka 11:28

## MCHAKATO WA KUJIFUNZA NENO

**Chagua wakati na mahali pamoja pa kujifunza kusoma.** Kuza tabia ya kujifunza Neno. Chagua wakati wa msingi wa kujifunza Biblia kila siku ili kuwe na uwezekano zaidi kwamba utajifunza kila siku.

**Weka kile ulichosoma katika muktadha wake.** Kirai cha maneno au mstari mmoja wa Maandiko mara nyingi hauna taarifa za kutosha za kukuwezesha kufikia hitimisho mwafaka. Ni muhimu kuelewa kile kilicho katika mistari iliyo karibu ... na jinsi kinavyojumuishwa katika picha kubwa ya kile Mungu anachosema. Majibu ya maswali yafuatayo yatatoa ufahamu zaidi kwa mstari wowote.

Je, sentensi yote inasema nini?

Aya au sehemu husika inafundisha nini?

Sura husika inafundisha nini?

Jambo hilo linalofundishwa linajumuishwaje katika Biblia nzima?

Marejeo mengine ya Maandiko, Biblia zenye maelezo, na vitabu vinavyofasiri Biblia vinaweza kusaidia katika kuelewa muktadha wa jumla.

**Omba hekima ya kuelewa na kutumia kile unachojifunza.** Tafuta majibu ya maswali yafuatayo.

Inasema nini?

Inamaanisha nini?

Nawezaje kufanya hii iwe sehemu ya maisha yangu?

### Chambua sehemu unayosoma ukitafuta …

Mawazo makuu.

Sarufi.

Sababu na athari.

Ulinganisho na tofauti.

Viunganishi.

Mambo yanayorudiwarudiwa.

Ahadi na masharti.

Amri – kauli za fanya na usifanye.

Vielelezo na mifano.

Watu, maeneo, na wakati.

**Weka kile unachofunza katika hali inayoweza kutumika**. Andika kumbukumbu na mawazo katika Biblia yako na/au katika daftari lako. Kariri vifungu hasa vyenye maana ... ukiviandika andika katika akili na katika moyo wako.

**Tumia kile unachojifunza.** Lengo la kujifunza Biblia ni ili uweze kuishi maisha kamili ... si kuwa na daftari iliyojaa kumbukumbu. Siku zote jifunze Neno la Mungu kwa moyo ulio wazi kwa kazi yake ndani na katika maisha yako.

## JE, NAHITAJI VIFAA GANI VYA KUJIFUNZA?

**Kitabu muhimu zaidi cha kujifunza Biblia ni Biblia nzuri**. Anza na tafsiri bora zaidi ya neno kwa neno inayopatikana katika lugha yako. Panga kuandika ndani ya Biblia hiyo. Lakini tafakari kabla hujaandika au kupigia mstari kitu chochote kwenye kurasa za Biblia yako. Hakikisha kwamba kumbukumbu zako zitakuwa na maana na ni rahisi kusoma. Kumbuka kwamba vitabu vinavyofasiri Biblia, tafsiri za kisasa zilizo rahisi kusoma, vidokezo vya maelezo katika Biblia, vitabu, jumbe, na mafundisho ya mtandaoni yanaweza kukusaidia kuelewa Neno la Mungu ... lakini Biblia pekee ndilo Neno la Mungu lisilokuwa na makosa. Wekeza muda wako mwingi zaidi au wote wa kujifunza moja kwa moja katika Biblia yako.

**Unapaswa kutumia Biblia gani?** Tumia tafsiri bora zaidi ya neno kwa neno inayopatikana katika lugha yako. Biblia ya Swahili Union Version [si Biblia ya Swahili Union Iliyorekebishwa] imetumiwa katika kozi hii kwa sababu ni tafsiri nzuri inayopatikana kwa urahisi. Kuna tafsiri nyingine za Biblia ya Kiswahili ambazo ni rahisi kusoma kuliko Biblia ya Swahili Union Version. Hata hivyo, nyingi kati yao hazifuati kwa ukaribu lugha za asili za Biblia kama vile Biblia ya Swahili Union. Mara nyingi zinakuambia zaidi kile ambacho Biblia inamaanisha badala ya kile ambacho Biblia inasema. Hata hivyo, Biblia yoyote ni bora kuliko kutokuwa na Biblia kabisa. Lakini … usitumie Biblia au vitabu kutoka kwa mashirika ambayo yanaongeza, yanaondoa, au yanabadilisha mafundisho ya Biblia kama yalivyoandikwa katika lugha za asili. Mashirika hayo ni pamoja na Wamormoni na Mashahidi wa Yehova. Kaa mbali nao.

**Vitabu gani vinaweza kusaidia?** Ikiwezekana, kusanya vitabu vya marejeo vya kibinafsi, vya kikanisa au vya kichungaji kutokana na aina za vitabu vifuatavyo. Baadhi ya vitabu hivi vinapatikana bila malipo mtandaoni. Na vinapatikana zaidi katika lugha ya Kiingereza kuliko katika lugha nyingine.

> *Biblia yenye maelezo* iliyo na vidokezo, mihtasari, marejeo ya vifungu vya Biblia, ramani, na konkodansi fupi.
>
> *Konkodansi* ya kutumika kama kifaa cha kupata neno na Kifungu cha Biblia ... inapatikana kama toleo fupi au kamili. Ikiwezekana, konkodansi inayolingana na toleo lako la Biblia ndio rahisi zaidi kutumia.
>
> *Kamusi ya Biblia* kwa ajili ya taarifa za kweli na za kina kuhusu watu, maeneo, vitu, na nyakati zinazorejewa katika Biblia.
>
> *Kitabu kinachofasiri Biblia* kinachotoa maelezo ya Biblia mstari kwa mstari, sehemu kwa sehemu, na kitabu baada ya kitabu.

**Ni vifaa gani vinavyopatikana vya kujifunza Biblia kwenye mtandao?** Biblia na Programu nyingi za mtandaoni [katika tafsiri na lugha mbalimbali] na vitabu vya marejeo ya Biblia vinapatikana bila malipo au kwa gharama inayokubalika. Njia rahisi ya kupata baadhi ya rasilimali hizi ni kwa utafutaji rahisi mtandaoni. Kwa mfano, unaweza kutafuta *Yohana 3:16* au *Zaburi 119:133* ili kupata tovuti ambayo ina kile unachohitaji.

**Je, utafanyaje ikiwa huwezi kumudu au kufikia rasilimali unazohitaji?** Biblia nzuri ndio kitabu bora zaidi unachoweza kumiliki. Yesu aliahidi kwamba Roho Mtakatifu atakuongoza katika ukweli, Yohana 16:13. Na atafanya hivyo kwa kutumia au bila kutumia rasilimali hizi nyingine ikiwa una bidii katika kujifunza Biblia.

Acts One Eight [Matendo Moja Nane]huchapisha tafsiri hii ya Kiswahili ya kozi ya lugha ya Kiingereza ya *Disciplemaking 1 … Abiding in His Word*. Unaweza kunakili kozi hii au sehemu yake yoyote bila malipo au kwa gharama ya usambazaji pekee, bila kubadilisha maudhui yake na ukiwa umeambatanisha kauli hii ya chanzo. Kozi hii inapatikana bila malipo katika lugha ya Kiswahili kutoka katika www.Theolojia.org au katika lugha ya Kiingereza kutoka katika www.VIrtualBibleAcademy.org. Kwenye tovuti hizi, unaweza kusoma mtandaoni, kufundishwa, kupakua, au kuchapisha nakala zako mwenyewe. Nukuu za Biblia ya Kiswahili zimetoka katika Biblia ya Swahili Union Version (SUV) ya 1997.

*“Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.”* 2 Timotheo 2:15

**KARATASI YA KUJIFUNZA BIBLIA KILA SIKU** … kutoka katika www.Theolojia.org.

*“Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.”* 2 Timotheo 3:16-17

Jina: Tarehe:

Somo la leo la _______________________________ limekuwa lenye manufaa ...

Katika *kunifundisha* kweli na ahadi hizi ili niziamini:

Katika *kunionya* ili kunionyesha nina hatia katika dhambi za mtazamo, kutenda na kutotenda:

Katika *kuniongoza* ili kunisaidia kurudi katika njia sahihi kwa:

Katika *kuniadibisha* ili niti amri hizi, nitumie kanuni hizi, na nifuate mifano hii:

Katika kunipa kifungu au wazo hili la msingi la leo:

Nakili au chapisha karatasi hii kwa ajili ya masomo yako ya kila siku ... moja kwa kila siku. Jifunze kila siku. Omba na utafakari unapojifunza. Pitia kumbukumbu za jana unapoanza somo la leo. Soma sura ya leo au sehemu ya Biblia mara moja, kisha uisome tena, ukijaza majibu yanayofaa hapo juu. Tafuta mshirika atakayehakikisha unajifunza na unawajibika ili mtiane moyo. Anza kujifunza ukitumia vitabu vifupi kama vile Wakolosai, 1 Yohana, na 2 Timotheo. Kisha endelea na vitabu kama vile Marko, Yohana, Waefeso, na Wafilipi. Endelea na vitabu virefu zaidi kama vile Warumi na Waebrania. Jifunze Agano la Kale na Agano Jipya, ukitafuta ushauri kamili wa Neno la Mungu.

*Kufanya Wanafunzi - Maswali ya Marudio*

# Somo la 3 - Kujifunza Biblia ... Ukurasa wa 31 - 37

Sehemu ya kujifunza ni kufanya marudio … kuhifadhi maarifa mapya kwenye kumbukumbu yako ya muda mrefu. Chapisha mtihani huu wa marudio au tumia karatasi tofauti kujibu maswali yafuatayo. Kisha rudia mtihani huu, ukisoma maelezo ya kozi au bila kuyasoma, hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi.
*Mitihani hii ya marudio* pamoja na majibu sahihi yanapatikana kwenye www.Theolojia.org.

1. Ni sifa gani zinazoweza kuonekana za Biblia zinaifanya iwe kuu?

2. Ni sifa gani za kiroho zinafanya Biblia iwe kuu?

3. Kama ilivyo katika ukuaji wa mwanadamu, maendeleo mazuri katika kujifunza Biblia yana lishe inayoendelea kutoka _____________ hadi _______________.

4. Ukirejelea Biblia, eleza tofauti kati ya *inayotia moyo* na *iliyoongozwa na Roho Mtakatifu.*

5. Eleza maana ya kwamba Biblia ni ya kweli, sahihi, na safi.

6. Je, Biblia kuwa ya milele ina maana gani kwako?

7. Biblia kuwa na nguvu ina maana gani kwako?

8. Weka Yohana 8:31 kwa maneno yako mwenyewe.

9. Weka 2 Timotheo 2:15 kwa maneno yako mwenyewe.

10. Mzazi anapaswa kuzungumza na watoto wake kuhusu Biblia wakati gani na mara ngapi?

11. Baadhi ya manufaa ya kujifunza Biblia ni yapi?

    a. e.

    b. f.

    c. g.

    d. h.

12. Muktadha ni muhimu kwa kiasi gani katika kujifunza Biblia?

13. Unapojifunza Biblia, unapaswa kusali na kujibu maswali gani 3?

    a.

    b.

    c.

14. Weka 2 Timotheo 3:16-17 kwa maneno yako mwenyewe.

15. Kwa siku sita zinazofuata, tumia nakala ya ukurasa wa 37 katika somo lako la sehemu yoyote ya Biblia ... ukijifunza angalau dakika 15 kwa siku. Fanya hivi katika masomo yako ya kawaida au anza somo jipya. Weka mviringo katika kila siku baada ya kukamilisha zoezi hilo vizuri.

    Siku ya 1 ... Siku ya 2 ... Siku ya 3 ... Siku ya 4 ... Siku ya 5 ... Siku ya 6.

16. Ni jambo gani muhimu zaidi ambalo umejifunza katika somo hili la kujifunza Biblia?

17. Umefanya au utafanya mabadiliko gani katika kujifunza Biblia kila siku?

## Somo la 3 - Kujifunza Biblia … maswali ukurasa wa 38 - 39

Usitumie karatasi hizi za majibu kupata majibu yako. Tafadhali zitumie tu kukagua majibu yako. Rudi kwenye somo ili kupata taarifa za kurekebisha majibu yako. Rudia mtihani hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi. Masomo yote, mitihani ya marudio, na kurasa za majibu zinapatikana katika www.Theolojia.org.

1. Ni sifa gani zinazoweza kuonekana za Biblia zinaifanya iwe kuu?
   *Nakala nyingi zaidi zimechapishwa … imetafsiriwa katika lugha nyingi zaidi … na imesambazwa zaidi kuliko kitabu chochote kingine katika historia yote.*

2. Ni sifa gani za kiroho zinafanya Biblia iwe kuu? *Imebadilisha maisha ya watu wengi zaidi kuliko kitabu chochote kingine … ni ujumbe wa Mungu kwetu … ni pumzi ya Mungu (imeandikwa kwa mwongozo wa Mungu na si tu kitabu cha kutia moyo) … ina mamlaka makuu zaidi katika kile tunachopaswa kuamini na jinsi tunavyopaswa kuishi.*

3. Kama ilivyo katika ukuaji wa mwanadamu, maendeleo mazuri katika kujifunza Biblia yana lishe inayoendelea kutoka __*maziwa*__ hadi __*nyama (chakula kigumu)*__.

4. Ukirejelea Biblia, eleza tofauti kati ya inayotia moyo na iliyoongozwa na Roho Mtakatifu.
   *Iliyoongozwa na Roho Mtakatifu inazungumzia chanzo … ni pumzi ya Mungu. Inayotia moyo ni kile inachotufanyia … inatutia moyo na kutupa uzima.*

5. Eleza maana ya kwamba Biblia ni ya kweli, sahihi, na safi.
   *Kweli inamaanisha taarifa zake ni za kweli. Sahihi inamaanisha haina makosa. Safi inamaanisha haina doa ... haihitaji kuchujwa.*

6. Je, Biblia kuwa ya milele ina maana gani kwako?
   *Haijawekewa mipaka au haiathiriwi na wakati. Ina maana kwangu leo kama ilivyokuwa kwa wasomaji wa asili.*

7. Biblia kuwa na nguvu ina maana gani kwako?
   *Inaleta mabadiliko yenye nguvu ndani yangu.*

8. Weka Yohana 8:31 kwa maneno yako mwenyewe.
   *Waumini wanahitaji kudumu, kuishi ndani ya Neno ili wawe wanafunzi wa Yesu.*

9. Weka 2 Timotheo 2:15 kwa maneno yako mwenyewe.
   *Jifunze kwa bidii ili upate kukubaliwa na Mungu na uwe mtu asiye na haya, ukitumia Neno kwa usahihi.*

10. Mzazi anapaswa kuzungumza na watoto wake kuhusu Biblia wakati gani na mara ngapi?
    *Asubuhi, mchana, na usiku … akiwa na mazungumzo yanayoendelea kuhusu Neno.*

11. Baadhi ya manufaa ya kujifunza Biblia ni yapi?
    a. *Kunaniandaa.*
    b. *Kunanizuia kutenda dhambi.*
    c. *Kunanipa mwongozo.*
    d. *Kunanipa hekima.*
    e. *Kunanisaidia katika hali ngumu.*
    f. *Kunanipa tumaini.*
    g. *Kunanipa amani.*
    h. *Kunanipa furaha.*

12. Muktadha ni muhimu kwa kiasi gani katika kujifunza Biblia?
    *Muktadha ni muhimu sana katika kuelewa sehemu yoyote ya Biblia.*

13. Unapojifunza Biblia, unapaswa kusali na kujibu maswali gani 3?
    a. *Inasema nini?*
    b. *Inamaanisha nini?*
    c. *Nawezaje kufanya hii iwe sehemu ya maisha yangu?*

14. Weka 2 Timotheo 3:16-17 kwa maneno yako mwenyewe.
    *Jibu lako linapaswa kujumuisha: kufundisha, kuonya, kurekebisha na kufunza katika haki ... ili uwe kamili na umeandaliwa kwa ajili ya matendo mema.*

15. Kwa siku sita zinazofuata, tumia nakala ya ukurasa wa 37 katika somo lako la sehemu yoyote ya Biblia ... ukijifunza angalau dakika 15 kwa siku. Fanya hivi katika masomo yako ya kawaida au anza somo jipya. Weka mviringo katika kila siku baada ya kukamilisha zoezi hilo vizuri.
    Siku ya 1 ... Siku ya 2 ... Siku ya 3 ... Siku ya 4 ... Siku ya 5 ... Siku ya 6.

16. Ni jambo gani muhimu zaidi ambalo umejifunza katika somo hili la kujifunza Biblia?

17. Umefanya au utafanya mabadiliko gani katika kujifunza Biblia kila siku?

### Kufanya Wanafunzi 1 - Kudumu Katika Neno Lake

## SOMO LA 4 - AGANO LA KALE

*“Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini.”*

Warumi 15:4

Historia ya Agano la Kale inaanza katika kitabu cha Mwanzo na mwanzo wa mwanadamu na mwanzo wa Israeli. Mwanzo wa mwanadamu umeelezewa katika matukio manne ya kihistoria ... uumbaji, anguko, gharika, na mkanganyo wa lugha kwenye Mnara wa Babeli. Mwanzo wa Israeli unaonekana katika watu wanne mashujaa ... Abrahamu, Isaka, Yakobo [aliyepewa jina jipya Israeli], na Yusufu. Kaka wakubwa wa Yusufu walimuuza utumwani Misri ambako aliinuliwa hadi kuwa wa pili katika uongozi. Yusufu aliungana tena na familia yake njaa ilipowasukuma kuhamia Misri. Makabila 12 ya Israeli [wazao wa wana 12 wa Yakobo] yalistawi sana huko Misri ... lakini yalifanywa watumwa kwa miaka 430 baada ya kifo cha Yusufu. Mungu alimwita Musa kuwakomboa Waisraeli kutoka utumwani. Aliwaongoza kuvuka Bahari ya Shamu ... kisha mpaka Mlima Sinai ambapo Mungu alitoa Sheria.

Waisraeli walihesabiwa. Walisafiri kaskazini kutoka Mlima Sinai hadi Kadesh-Barnea na wapelelezi 12 wakatumwa katika nchi ya Kanaani. Watu waliwaamini wale wapelelezi kumi wasio na imani na hivyo hawakuingia katika nchi ya Kanaani. Mungu aliwahukumu wote waliokuwa na umri wa miaka 20 na zaidi kutangatanga na kufa nyikani isipokuwa wale wapelelezi wawili wazuri, Yoshua na Kalebu. Miaka 40 baadaye, upande wa mashariki wa Yordani kwenye nchi tambarare ya Moabu, Waisraeli walihesabiwa tena. Musa alitoa jumbe zake za mwisho [kueleza tena Sheria] ... akatazama nchi kutoka Mlima Nebo ... kisha akafa. Yoshua aliwaongoza Waisraeli kuingia Kanaani ili kuiteka, kuigawanya, na kukaa katika nchi hiyo. Katika enzi ya Waamuzi, Waisraeli walipitia mizunguko 17 ya kushindwa. Walitenda dhambi ... Mungu aliwahukumu kupitia watesi wa nje ... wakatubu ... Mungu alimtuma mwamuzi ili awakomboe kutokana na watesi wao ... amani na hali ya kusahau ikafuata ... kisha wakarudia mzunguko huo wa dhambi.

Kisha Waisraeli walitaka mfalme kwa sababu mataifa yote mengine yalikuwa na mfalme. Walikataa utawala wa Mungu [theokrasi] na wakachagua utawala wa mwanadamu [ufalme]. Ufalme mmoja ulitawaliwa na wafalme watatu ... Sauli, kisha Daudi, kisha Sulemani. Kwa sababu ya dhambi za Sulemani, Ufalme uligawanywa katika Ufalme wa Kaskazini na Kusini. Ufalme wa Kaskazini wa Israeli [makabila kumi] uliongozwa na wafalme wabaya 19 kabla ya kupelekwa utumwani Ashuru na kutawanywa. Ufalme wa Kusini wa Yuda [makabila ya Yuda, Benyamini, na Lawi], uliongozwa na malkia mmoja na wafalme 19 [wengine wazuri na wengine wabaya]. Walipelekwa utumwani kwa miaka 70 huko Babeli kupitia uhamisho mara tatu. Waisraeli walirudi Yerusalemu baada ya Babeli kutekwa na Uajemi. Zerubabeli aliongoza wimbi la kwanza la Waisraeli kurudi na akajenga upya hekalu. Ezra aliongoza wimbi la pili kurudi na akaleta uamsho wa kiroho. Nehemia aliongoza wimbi la tatu na akajenga upya kuta za Yerusalemu. Miaka mia nne ya ukimya wa Bibila unatenganisha historia ya Agano la Kale na kuzaliwa kwa Yesu.

## 1. MWANZO WA MWANADAMU – MATUKIO MANNE YA KIHISTORIA [Mwanzo 1-11]


**UUMBAJI … MWANZO 1 - 2**. Sura ya 1 inatoa muhtasari wa uumbaji wa mbingu, dunia, na mwanadamu. Mungu alisema, *“, natumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu,”* 1:26. Sura ya 2 inaeleza kuhusu uumbaji wa mwanadamu katika siku ya sita. Mungu alimuumba mwanaume kutokana na mavumbi ya ardhi na kumweka katika bustani ya Edeni. Kisha Mungu akaumba mwanamke kutokana na ubavu wa mwanamume ... alimuumba kuwa msaidizi wa mwanaume, *“Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana,”* Mwanzo 1:31.

**ANGUKO ... MWANZO 3 - 5**. Sura ya 3 inaanza na nyoka akimjaribu Hawa kutilia shaka ukweli wa Neno la Mungu na kuasi amri yake. Alikula tunda lililokatazwa kisha akampa mume wake, ambaye naye alikula. Hiyo ilivunja ushirika wao mzuri na Mungu. Matokeo yalikuwa ni kwamba Mungu alilaani nyoka, mwanamke, mwanamume, na ardhi, Mwanzo 3:14-19. Kisha Mungu akawafukuza kutoka katika bustani ya Edeni. Sura ya 4 inaeleza kuhusu kuzaliwa kwa Kaini na Habili, Kaini alivyomuua Habili, na kuzaliwa kwa Sethi ili kuendeleza ukoo unaomcha Mungu. Sura ya 5 inaonyesha ukoo kuanzia Adamu hadi Nuhu na kuzaliwa kwa wanawe watatu Shemu, Hamu, na Yafethi.

**GHARIKA … MWANZO 6 - 9**. Katika enzi ya Nuhu, wanadamu walikuwa waovu sana, na Mungu alihukumu ulimwengu kupitia gharika. Kwa maagizo ya Mungu, Nuhu alikuwa amejenga safina ili kujiokoa yeye mwenyewe, mke wake, wana wao watatu na wake zao watatu, na sampuli ya wanyama. Mwanzo sura ya 7 na 8 inaeleza kuhusu gharika lililodumu kwa mwaka mzima. Mungu aliahidi kwamba hatamwangamiza tena mwanadamu kwa gharika na akaweka upinde wa mvua angani kama ishara ya agano lake na Nuhu. Dhambi ya Hamu na laana ya Nuhu dhidi ya Kanaani mwana wa Hamu inakamilisha Sura ya 9.

**MKANGANYO WA LUGHA ... MWANZO 10 - 11**. Vizazi vilivyomfuata Nuhu vyote vilizungumza lugha moja. Lakini huko Babeli wanadamu waliamua kujijengea jiji, mnara, na jina ... ili kuzuia wasitawanyike duniani kote. Hiyo ilikuwa ni kutotii moja kwa moja amri ya Mungu aliposema, *“zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi,”* Mwanzo 9:1. Kwa uasi walisema, *“Haya, na tujijengee mji, na mnara, na kilele chake kifike mbinguni, tujifanyie jina; ili tusipate kutawanyika usoni pa nchi yote,”* Mwanzo 11:4. Mungu aliwahukumu kwa kukanganya lugha yao ... akawatawanya juu ya uso wa dunia yote. Ukoo wa familia ya Shemu unaweza kufuatiliwa kutoka kwa wana wa Nuhu hadi kwa Abramu [Abrahamu] ... na zaidi ya hapo.

# UKOO WA AGANO LA KALE



## 2. MWANZO WA ISRAELI - WATU WANNE MASHUJAA [Mwanzo 12 - 50]


**ABRAHAMU … MWANZO 11:27 - 25:11**. Mungu alimwita Abrahamu akiwa na umri wa miaka 75 ili awe baba wa mataifa mengi. Abrahamu alisafiri kutoka Uru ya Wakaldayo, pamoja na mkewe Sara na mpwa wake Lutu, hadi Harani ambako baba yake Tera alikufa [tazama A kwenye ramani, ukurasa wa 46]. Waliendelea kusafiri hadi Kanaani [tazama B kwenye ramani, ukurasa wa 46]. Mungu aliahidi kubariki dunia yote kupitia Abrahamu, Mwanzo 12:1-3 ... kumpa nchi ya Kanaani, Mwanzo 12:7, 13:14-15, 15:18 ... kumpa wazao wengi, Mwanzo 13:16, 15:5 ... na kumpa mrithi pamoja na Sara, 15:4. Akiwa anazeeka na kukosa kumwamini Mungu, Sara alimpa Abrahamu mwenye umri wa miaka 86, mjakazi wake Hajiri. Akazaa mwana, Ishmaeli, ambaye ni Baba wa mataifa ya Kiarabu. Hata hivyo, kama Mungu alivyoahidi, Sara alimzaa mrithi wao Isaka mnamo 2065 KK Abrahamu alipokuwa na umri wa miaka 100. Mungu alimjaribu Abrahamu kwa kumwagiza amtoe Isaka kama dhabihu, Mwanzo 22:1-19 ... na Mungu alitoa kondoo kama dhabihu mbadala [taswira ya Yesu kama mbadala wetu].

**ISAKA ... MWANZO 21 - 27**. Isaka alimuoa Rebeka na akapata mapacha mnamo mwaka 2005 KK ... Yakobo [ambaye ni baba wa Wayahudi] na Esau [ambaye ni baba wa Waedomu]. Esau alimpa Yakobo haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa kuibadilisha kwa chakula cha mchuzi wa dengu. Baadaye Rebeka alimsaidia Yakobo [aliyempenda zaidi] kumdanganya Isaka ili ampe Yakobo baraka ya mzaliwa wa kwanza ambayo Esau ndiye aliyestahili kupewa. Mungu alitimiza ahadi yake licha ya dhambi yao.

**YAKOBO … MWANZO 25 - 36**. Yakobo aliwaoa Raheli na Lea ... binti za Labani, kaka ya Rebeka. Yakobo alizaa wana 12 na wake zake wawili pamoja na vijakazi wao wawili Bilha na Zilpa. Mungu akampa Yakobo jina jipya. Jina lake jipya lilikuwa Israeli, Mwanzo 35:10. Mungu alimwahidi Israeli kwamba agano lake na Abrahami na Isaka litatimizwa kupitia Yakobo, 35:11-12. Wana 12 wa Yakobo wanaitwa makabila 12 ya Israeli.

**YUSUFU … MWANZO 37 - 50**. Yusufu aliota ndoto kwamba familia yake itamsujudia. Kwa sababu hiyo na kwa sababu alikuwa kipenzi cha Yakobo, kaka zake kumi wakubwa walimuuza kwa msafara uliokuwa ukipita. Walimpeleka Misri na kumuuza kama mtumwa kwa Potifa [tazama C kwenye ramani, ukurasa wa 46]. Yusufu akawa mkuu wa pili katika nyumba ya Potifa lakini akashtakiwa kwa kusingiziwa uwongo na mke wa Potifa na akawekwa gerezani ... ambapo aliinuliwa na kuwa wa pili katika uongozi. Baada ya kufasiri kwa usahihi ndoto za mnyweshaji na mwokaji, alifasiri ndoto za Farao, akitabiri miaka saba ya shibe itakayofuatiwa na miaka saba ya njaa. Kisha Yusufu akainuliwa hadi kuwa wa pili katika uongozi katika Misri yote mnamo mwaka 1884 KK. Njaa ilipoenea hadi nchi ya Kanaani, familia yake ilikuja Misri kwa ajili ya chakula, na wakaungana naye tena. Yakobo [Israeli] na Yusufu wote walikufa Misri.

## MWANZO WA ISRAELI



## 3. UTUMWANI MISRI HADI MPAKA WA KANAANI

[Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu, na Kumbukumbu la Torati]


**UTUMWANI NCHINI MISRI**. Makabila 12 ya Israeli yalisitawi na kuongezeka nchini Misri. Walifanywa watumwa kwa miaka 430 baada ya kifo cha Yusufu.

**MUSA NA KUTOKA**. Musa alizaliwa na mwanamke Mlawi ... lakini alilelewa kama mwana wa binti ya Farao. *"Kwa imani Musa alipokuwa mtu mzima, akakataa kuitwa mwana wa binti Farao; akaona ni afadhali kupata mateso pamoja na watu wa Mungu kuliko kujifurahisha katika dhambi kwa kitambo; akihesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri,"* Waebrania 11:24-26. Akiwa na umri wa miaka 40 Musa alimuua Mmisri kwa sababu alikuwa akimpiga Mwebrania kisha akatorokea Midiani ambako aliishi kwa miaka 40 iliyofuata akichunga kondoo. Mungu alimwita Musa kupitia kichaka kilichokuwa kikiwaka moto, Kutoka 3, kuwaongoza watu wake kutoka utumwani. Mungu alifanya kazi kupitia Musa na kaka yake Haruni kwa njia ya mapigo kumi ili kuwaweka uhuru Waisraeli mnamo mwaka 1445 KK. Pasaka ilianzishwa, Kutoka 12, ili kuwalinda Waebrania kutokana na pigo la mwisho. Musa aliwaongoza watu [watu zaidi ya 600000, Kutoka 12:37] kuvuka Bahari ya Shamu hadi kufika Mlima Sinai [tazama **D** kwenye ramani, ukurasa wa 48].

**MLIMA SINAI**. Mungu alianzisha Agano la Kale alipotoa sheria kupitia Musa kwenye Mlima Sinai, Kutoka 19 na Mambo ya Walawi. Sheria, iliyotolewa kwenye Mlima Sinai, ilijumuisha Amri Kumi, Kutoka 20.

**KUHESABIWA, KUTANGATANGA, NA KIFO.** Katika nyika ya Sinai watu walihesabiwa [sensa #1]. Kisha wakasafiri kuelekea kaskazini hadi Kadesh-Barnea. Walituma wapelelezi 12 kwenda Kanaani kutoka Kadesh-Barnea [tazama **E** kwenye ramani, ukurasa wa 48]. Watu waliwaamini wale wapelelezi kumi wasio na imani, wakanung'unika, wakalalamika, na wakatamani sana kurudi Misri. Walikataa kuingia katika nchi ya Kaanani. Kwa hivyo Mungu aliwahukumu watu wote waliokuwa na umri wa miaka 20 na zaidi [isipokuwa wale wapelelezi wawili wazuri, Yoshua na Kalebu] kutangatanga na kufa nyikani, Hesabu 14:28-30. Baada ya miaka 40 ya kutangatanga [tazama **F** kwenye ramani, ukurasa wa 48], wanung'unikaji wasio na imani walikuwa wamekufa. Kisha kizazi kipya kililetwa kwenye nchi tambarare ya Moabu upande wa mashariki wa Mto Yordani. Walihesabiwa tena [sensa #2]. Musa alitoa jumbe zake za mwisho, Kumbukumbu la Torati. Alimteua Yoshua kuwa mrithi wake. Kisha Musa akakwea Mlima Nebo kutazama Nchi ya Ahadi. Musa alikufa na Mungu akamzika katika bonde katika nchi ya Moabu. Mungu hakumruhusu Musa kuingia katika nchi ya Ahadi kwa sababu hakumtii, Hesabu 20:8-12, Kumbukumbu la Torati 3:27.

## UTUMWANI MISRI HADI MPAKA WA KANAANI




## 4. MAFANIKIO NA KUSHINDWA KANAANI [Yoshua, Waamuzi, na 1 Samweli 1-8]

**YOSHUA NA MAFANIKIO KANAANI**. Yoshua aliwaongoza Waisraeli kuingia Kanaani mnamo mwaka 1405 KK ili kuiteka, kuigawanya, na kukaa katika nchi hiyo. Yakobo [Israeli] alikuwa amewabariki wana wa Yusufu, Efraimu na Manase, kwa baraka iliyokuwa imetengewa wanawe mwenyewe, Mwanzo 48:8-22. Kwa hivyo makabila yao yote mawili yalipewa mgao wa nchi ... kama yale makabila mengine ya Israeli. Dani na Manase walipokea nchi yao katika vipande viwili. Walawi hawakupokea ardhi yoyote. Mungu ndiye aliyekuwa urithi wao, Yoshua 13:33. Hata hivyo, Walawi walipewa miji 48, Yoshua 21:41. Mungu alikuwa amewaagiza Waisraeli wasifanye maagano na watu wa nchi ya Kaanani ... wasiitumikie miungu yao bali wabomoe madhabahu yao ... na waangamize kabisa wenyeji wa nchi hiyo, Kutoka 23:32, 34:12 -16, na Kumbukumbu la Torati 7:1-5,16. Sababu za hukumu kali ya Mungu dhidi ya watu waovu wa Kanaani ziko katika Mambo ya Walawi 18. Yoshua na Waisraeli hawakutii amri hizi ... na wao na wazao wao walipata matokeo ya kuishi katika nchi hiyo pamoja na maadui wao na miungu yao ya uongo. Licha ya mapungufu yao, *“Israeli wakamtumikia BWANA siku zote za Yoshua,”* Yoshua 24:31.

**WAAMUZI NA KUSHINDWA KATIKA NCHI YA KAANANI**. Mizunguko kumi na saba ya kushindwa kwa Waisraeli kwa zaidi ya miaka 330 imeandikwa katika Waamuzi [mizunguko 13] na 1 Samweli [mizunguko 4]. Mzunguko wa matukio hayo yote ya kushindwa uko katika Waamuzi 2:11-19. Watu walifanya maovu na kumkasirisha Mungu. Akawatia mikononi mwa watesi ... kwa sababu ya kilio chao aliwatumia mwokozi [Mwamuzi] ili awakomboe ... kisha katika kipindi cha amani kilichofuata, walisahau na wakarudi kwenye njia zao ovu ... na mzunguko huo ulianza tena. Mizunguko saba ya kushindwa imeelezewa kwa kina ikiwa ni pamoja na ile ya waamuzi Gideoni na Samsoni. Waamuzi kumi na watatu wanapatikana katika kitabu cha Waamuzi na wanne wanapatikana katika 1 Samweli. Ruthu, nyanya mkuu wa Daudi, alikuwa kielelezo cha mwanamke mcha Mungu katika enzi ya Waamuzi.

**BAADA YA WAAMUZI**. Baada ya mizunguko 17 ya kushindwa katika enzi ya Waamuzi, Waisraeli walitaka mfalme [ufalme] kama mataifa yote mengine, 1 Samweli 8:5-20 ... na walikataa utawala wa Mungu [theokrasi]. Kwa sababu ya ombi lao, Samweli, mmoja wa waamuzi wa mwisho, alimteua mfalme wa kwanza ... Sauli, 1 Samweli 8-10.

## NCHI ZA MAKABILA 12 NA MZUNGUKO WA KUSHINDWA KWA WAAMUZI




## 5. UFALME MMOJA NA WAFALME 3 [1 Samweli 9-31, 2 Samweli, na 1 Wafalme 1-11]

**SAULI.** Waisraeli walitaka mfalme, 1 Samweli 8. Walimkataa Mungu kwa kusisitiza kuwa walitaka mfalme, 1 Samweli 8:7. Sauli, wa kabila la Benyamini, alichaguliwa kuwa mfalme, 1 Samweli 9 - 12. Sauli, mfalme wa kwanza wa Israeli, alianza kutawala akiwa na umri wa miaka 40. Alitawala miaka 32. Mfalme Sauli alikuwa mtu asiye thabiti, mwenye pupa, mtenda dhambi, na hakumtii Mungu kikamilifu. Kwa hivyo, Mungu alimkataa kama mfalme, 1 Samweli 13:8-14 na 15:9-11, 26. Sauli alijaribu kuwasiliana na roho ya marehemu Samweli, 1 Samweli 28:7 ... akafa kwa sababu alifanya hivyo; 1 Mambo ya Nyakati 10:13-14.

**DAUDI**. Samweli alimchagua Daudi kumrithi Sauli, akimpita Yonathani mwana wa Sauli. Daudi alikuwa mwanamuziki stadi, shujaa hodari, mpiganaji, mwenye busara katika usemi, na mwenye sura nzuri, 1 Samweli 16:18. Baada ya miaka mingi ya vita dhidi ya Sauli, akawa mfalme mnamo mwaka 1011 KK na akafanikiwa ... akapanua sana ufalme katika kipindi chake cha utawala cha miaka 40. Daudi alifanya uzinzi na Bathsheba ... na, alipogundua kwamba alikuwa na mimba, alipanga kumuua mumewe Uria katika vita. Walifunga ndoa ... lakini mtoto wao wa kwanza alikufa. Sulemani, mwana wao wa pili, alikuwa mrithi wa kiti cha enzi. Ushuhuda wa Biblia kwamba Daudi alikuwa mtu anayeupendeza moyo wa Mungu, 1 Samweli 13:14 na Matendo 13:22, unaeleza tabia yake kabla ya kuwa mfalme. Ushuhuda huo haukutolewa kuelezea tabia ya Daudi baada ya dhambi yake na Bathsheba. Kwa kweli, Mfalme Daudi aliteseka sana baada ya uzinzi huo, 2 Samweli 12:10-14.

**SULEMANI**. Alikuwa mfalme wa tatu wa Israeli mnamo mwaka 971 KK na alikuwa na hekima aliyopewa na Mungu, 1 Wafalme 3:7-12. Sulemani alinena mithali 3000 na alikuwa na nyimbo 1005, 1 Wafalme 4:32. Alikuwa mkuu kuliko wafalme wote wa dunia kwa utajiri na hekima. Kwa kujibu ombi la Daudi, na kwa maagizo ya Daudi, Sulemani alijenga Hekalu. Hata hivyo, Mungu alikuwa amewaagiza wafalme wasijizidishie farasi, wake, fedha na dhahabu, Kumbukumbu la Torati 17:16-17 ... lakini Sulemani alifanya mambo hayo yote. Mungu aliwaagiza Waisraeli wasifunge ndoa na wageni wala wasiabudu miungu yao. Sulemani alifanya mambo hayo, 1 Wafalme 11:1-11. Mungu alimkasirikia Sulemani kwa sababu ya dhambi zake. Mungu alihukumu ufalme mmoja wa Israeli ugawanyike baada ya kifo cha Sulemani ... baada ya kifo cha Sulemani sababu ya ahadi ya Mungu kwa Daudi, 1 Wafalme 11:9-13. Sulemani alitawala Israeli kwa miaka 40.

## UFALME MMOJA WA ISRAELI



## 6. UFALME ULIOGAWANYIKA, WALIOHAMISHWA, NA MATUKIO MATATU YA KURUDI

[1 Wafalme 12 - 22, 2 Wafalme, Ezra, na Nehemia]

### FALME MBILI, UTAWANYIKO, NA UHAMISHO WA MIAKA 70

Utawala wa Sulemani uliisha na Ufalme mmoja wa Israeli ukagawanyika katika Falme mbili mnamo mwaka 931 KK ... Ufalme wa kaskazini na Ufalme wa kusini. Falme hizo mbili ziliongozwa na watawala tofauti.

**Ufalme wa Kaskazini wa Israeli** ulikuwa na makabila kumi yakiwemo makabila ya wana wa Yusufu Manase na Efraimu yaliyohesabiwa kama makabila mawili tofauti. Israeli ilitawaliwa na wafalme 19 wabaya. Hatimaye Wayahudi wa Israeli walihamishwa hadi Ashuru mnamo 722 KK na kutawanywa. Manabii **Eliya** na **Elisha** walihudumu wakati huo.

Ufalme wa Kusini wa Yuda ulijumuisha makabila ya Yuda, Benyamini, na Lawi. Yuda iliongozwa na watawala wazuri na wabaya. Kulikuwa na wafalme 19 na malkia mmoja [Athalia]. Yuda ilitekwa … na Wayahudi wa Yuda walipelekwa uhamishoni Babeli kupitia matukio matatu ya uhamisho. Danieli alikuwa miongoni mwa wale waliohamishwa katika uhamisho wa kwanza mnamo mwaka 606 KK. Ezekieli alikuwa miongoni mwa wale waliohamishwa katika uhamisho wa pili mnamo mwaka 597 KK, na Wayahudi wengine walihamishwa mnamo mwaka 586 KK wakati Yerusalemu na hekalu vilipoharibiwa. Babeli ilitekwa na Uajemi mnamo mwaka 539 KK. Baada ya Yuda kuwa uhamishoni kwa miaka 70 kutoka mwaka 606 KK hadi mwaka 536 KK, waliweza kuanza kurudi Yerusalemu. Muda kutoka uhamisho wao wa kwanza hadi kurudi kwao kwa mara ya kwanza unaitwa ***Uhamisho wa Miaka 70***. Kitabu cha Esta kina kumbukumbu ya kisa cha mwanamke mcha Mungu miongoni mwa wale waliohamishwa katika nchi ya Uajemi. Wazao wa makabila ya Yuda [Mariamu, Yosefu, na Yesu], Benyamini [Mtume Paulo], na Lawi [Barnaba] wanatambulishwa hivyo katika Agano Jipya.

**MATUKIO MATATU YA KURUDI KWA UFALME WA KUSINI**. Wayahudi wa Ufalme wa Yuda walipelekwa uhamishoni kupitia matukio matatu ya uhamisho. Baada ya kuishi uhamishoni kwa miaka 70, walirudi katika mawimbi matatu.

**Z**erubabeli aliongoza wimbi la kwanza, zaidi ya watu 40,000, kurudi Yerusalemu mnamo mwaka 536 KK ili kujenga upya hekalu ambalo lilikamilika mnamo 516 KK.

**E**zra aliongoza wimbi la pili kurudi mnamo mwaka 458 KK. Aliwaletea watu uamsho wa kiroho.

**N**ehemia aliongoza wimbi la tatu kurudi mnamo 445 KK. Alijenga upya kuta za Yerusalemu.

**MIAKA MIA NNE YA UKIMYA**. Miaka mia nne ya ukimya wa Biblia unatenganisha tamatisho la historia ya Agano la Kale na kuzaliwa kwa Kristo. Hakuna vitabu katika mkusanyiko rasmi wa Maandiko viliandikwa katika miaka hiyo 400. Wakati huo, Aleksanda Mkuu na Wagiriki walitawala sehemu hiyo ya ulimwengu. Kisha Ufalme wa Kirumi ukawa na mamlaka kabla na wakati wa kuzaliwa kwa Kristo na maisha yake.

## Vitabu 39 vya Agano la Kale Vilipangwa hivi 5 - 9 - 3 5 5 - 9 - 3

**5 - Vitabu Vitano vya Historia ... vilivyoandikwa na Musa**
Mwanzo ... mwanzo wa mwanadamu na mwanzo wa Israeli.
Kutoka ... kutoka utumwani Misri ... na Sheria katika Mlima Sinai.
Mambo ya Walawi ... Walawi na Sheria.
Hesabu ... sensa, kutangatanga, kifo, na sensa nyingine.
Kumbukumbu la Torati ... jumbe za mwisho za Musa ... na kifo cha Musa.

**9 - Vitabu Tisa vya Historia ... katika nchi ya Kanaani kabla ya uhamisho**
Yoshua ... mafanikio katika kuteka, kugawanya, na kukaa Kanaani.
Waamuzi ... mizunguko 17 ya kushindwa.
Ruthu ... mwanamke mcha Mungu katika enzi ya Waamuzi.
1 Samweli ... Waamuzi wa mwisho na Mfalme Sauli wa kwanza.
2 Samweli ... Mafanikio na kushindwa kwa Mfalme Daudi.
1 Wafalme ... Mfalme Sulemani na mgawanyiko wa Ufalme.
2 Wafalme ... Falme za Israeli na Yuda.
1 Mambo ya Nyakati ... inafanana na 2 Samweli.
2 Mambo ya Nyakati ... inafanana na 1 na 2 Wafalme.

**3 - Vitabu Vitatu vya Historia ... wakati na baada ya Uhamisho wa Miaka 70**
Ezra … Zerubabeli alijenga upya hekalu ... Ezra aliwajenga upya watu.
Nehemia ... Nehemia alijenga upya kuta za Yerusalemu.
Esta ... Mwanamke Myahudi mcha Mungu miongoni mwa waliohamishwa nchini Uajemi.

**5 - Vitabu Vitano vya Ushairi**
Ayubu ... Simulizi la awali la ukuu wa Mungu katika mateso ya mwanadamu.
Zaburi ... kitabu cha nyimbo cha Israeli.
Mithali ... hekima ya Mungu.
Mhubiri ... ubatili wa maisha ya mwanadamu bila Mungu.
Wimbo Ulio Bora ... uzuri wa ndoa.

**5 - Manabii Wakuu Watano ... kabla na wakati wa Uhamisho wa Miaka 70**
Isaya ... alitabiri hukumu na faraja ... Kitabu cha kimasihi.
Yeremia ... Nabii anayelia anawaonya Yuda na mataifa.
Maombolezo ... Yeremia anaomboleza kwa sababu ya kuharibiwa kwa Yerusalemu.
Ezekieli ... anawakumbusha Wayahudi dhambi zilizowafanya wapelekwe uhamishoni.
Danieli ... unabii wa mtu mcha Mungu aliyehamishwa mahali paovu.

**9 - Manabii Tisa Wadogo ... kabla ya Uhamisho wa Miaka 70**
Hosea ... upendo wa Mungu kwa Israeli.
Yoeli ... hukumu ya Mungu katika Siku ya Bwana.
Amosi ... hukumu dhidi ya Israeli.
Obadia ... hukumu ya Mungu dhidi ya taifa la Edomu.
Yona ... Mji wa Mataifa wa Ninawi unapewa nafasi ya pili.
Mika ... utabiri wa hukumu na Ufalme unaokuja.
Nahumu ... kuharibiwa kwa Ninawi miaka 150 baada ya Yona.
Habakuki ... Subira ya Mungu na adhabu dhidi ya Yuda.
Sefania ... hukumu na baraka.

**3 - Manabii Watatu Wadogo ... baada ya Uhamisho wa Miaka 70**
Hagai ... Wayahudi wanahimizwa kujenga upya Hekalu.
Zekaria ... wito wa kutubu ... utabiri kuhusu Masihi anayekuja.
Malaki ... mtazamo wa kutojali unakosolewa ... utabiri kuhusu Yohana Mbatizaji na Yesu.

## UPANGAJI WA VITABU 39 VYA AGANO LA KALE

### 17 VITABU VYA HISTORIA

**5** Uumbaji hadi Kanaani

Mwanzo
Kutoka
Mambo ya Walawi
Hesabu
Kumbukumbu la Torati

**9** Nchini Kanaani…
kabla ya Uhamisho
wa Miaka 70

Yoshua
Waamuzi
Ruthu
1 Samweli
2 Samweli
1 Wafalme
2 Wafalme
1 Mambo ya Nyakati
2 Mambo ya Nyakati

**3** Nchini Kanaani…
baada ya Uhamisho
wa Miaka 70

Ezra
Nehemia
Esta … akiwa Uajemi

### 5 VITABU VYA MAISHAIRI

**5** Vitabu 5 vya Ushairi

Ayubu
Zaburi
Methali
Mhubiri
Wimbo Ulio Bora

### 17 VITABU VYA UNABII

**5** Manabii Wakuu…
kabla na wakati wa Uhamisho
wa Miaka 70

Isaya
Yeremia
Maombolezo
Ezekieli
Danieli


**9** Manabii Wadogo...
kabla ya Uhamisho
wa Miaka 70

Hosea
Yoeli
Amosi
Obadia
Yona
Mika
Nahumu
Habakuki
Sefania


**3** Manabii Wadogo...
baada ya Uhamisho
wa Miaka 70

Hagai
Zekaria
Malaki

# AGANO LA KALE



## CHATI YA MTIRIRIKO WA AGANO LA KALE




Acts One Eight [Matendo Moja Nane] huchapisha tafsiri hii ya Kiswahili ya kozi ya lugha ya Kiingereza ya *Disciplemaking 1 … Abiding in His Word*. Unaweza kunakili kozi hii au sehemu yake yoyote bila malipo au kwa gharama ya usambazaji pekee, bila kubadilisha maudhui yake na ukiwa umeambatanisha taarifa hii ya chanzo. Kozi hii inapatikana bila malipo katika lugha ya Kiswahili kutoka katika www.Theolojia. org au katika lugha ya Kiingereza kutoka katika www.VIrtualBibleAcademy.org. Kwenye tovuti hizi, unaweza kusoma mtandaoni, kufundishwa, kupakua, au kuchapisha nakala zako mwenyewe. Nukuu za Biblia ya Kiswahili zimetoka katika Biblia ya Swahili Union Version (SUV) ya 1997.

# Somo la 4 - Agano la Kale ... kurasa 42 - 57

Sehemu ya kujifunza ni kufanya marudio … kuhifadhi maarifa mapya kwenye kumbukumbu yako ya muda mrefu. Chapisha mtihani huu wa marudio au tumia karatasi tofauti kujibu maswali yafuatayo. Kisha rudia mtihani huu, ukisoma maelezo ya kozi au bila kuyasoma, hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi.
*Mitihani hii ya marudio* pamoja na majibu sahihi yanapatikana kwenye www.Theolojia.org.

*KWELI* AU *UWONGO* ... weka alama kwa kila moja ya kauli hizi [1 - 14] ukitumia "K" (Kweli) au "U" (Uwongo)

1. Tukio la Mnara wa Babeli lilitokea kabla ya gharika lakini baada ya Anguko.
2. Yakobo alipewa jina jipya la Israeli.
3. Babu yake Yusufu alikuwa Isaka.
4. Yusufu alikuwa mtawala Edomu.
5. Mungu alitoa Sheria kupitia Musa kwenye Mlima Sinai.
6. Mambo ya Walawi inanakili tukio la kutoka katika nchi ya Misri.
7. Yoshua inanakili mizunguko ya kushindwa katika enzi ya Waamuzi.
8. Sensa moja tu ndio iliyochukuliwa kama inavyonakiliwa katika Hesabu.
9. Samweli, Daudi, na Sulemani walikuwa wafalme wa Ufalme mmoja wa Israeli.
10. Mungu aligawanya Ufalme kwa sababu ya dhambi za Sulemani.
11. Ufalme wa Kaskazini wa Israeli ulikuwa na wafalme 19 na malkia mmoja.
12. Ufalme wa Kusini ulitawanywa katika nchi ya Uajemi.
13. Ufalme wa Kusini ulijumuisha makabila ya Yuda, Benyamini, na Lawi.
14. Zerubabeli, Ezra, na Yeremia waliwaongoza watu kurudi Yerusalemu baada ya uhamisho wa miaka 70.

MAJIBU YA KUCHAGUA ... kwa swali la 15 hadi 24 ... jibu kila swali kwa herufi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| A. Isaka | D. Daudi | G. Nehemia | J. Yusufu | M. Musa |
| B. Ezra | E. Esta | H. Sulemani | K. Ruthu | N. Nuhu |
| C. Yoshua | F. Abrahamu | I. Sethi | L. Samsoni | O. Samweli |

15. Ni mwanamke yupi aliyeishi katika enzi ya Waamuzi? _________

16. Ni nani aliyewaongoza Waisraeli kutoka Misri? _________

17. Ni nani aliyeteka, akagawanya, na akawawezesha Waisraeli kukaa Kanaani? _________

18. Ni nani aliyekuwa Mfalme wa pili wa Ufalme mmoja? _________

19. Ni nani aliyekuwa mwana wa Daudi? _________

20. Mbali na Adamu, babu ya Nuhu alikuwa nani? _________

21. Ni nani aliyejenga upya kuta za Yerusalemu? ________

22. Ni nani aliyekuwa nyanya mkuu wa Daudi? ________

23. Ni nani aliyekuwa mwana wa Abrahamu? ________

24. Ni nani aliyekuwa mwana wa kumi na moja wa Israeli? ________

MPANGILIO WA MATUKIO...WEKA MVIRINGO AU PIGIA MSTARI KWENYE JINA LA MTU ALIYETANGULIA

| | | |
|---|---|---|
| 25. Musa | Nuhu | Yakobo |
| 26. Lawi | Sethi | Hamu |
| 27. Sauli | Sulemani | Samsoni |
| 28. Raheli | Sara | Dina |
| 29. Isaka | Manase | Ishmaeli |
| 30. Ezra | Ezekieli | Zerubabeli |
| 31. Ruthu | Esta | Sefania |
| 32. Israeli | Baba yake Yusufu | Yakobo |

33. Eleza jibu lako la swali tatanishi #32.

# Somo la 4 - Agano la Kale … maswali ukurasa wa 58 - 59

Usitumie karatasi hizi za majibu kupata majibu yako. Tafadhali zitumie tu kukagua majibu yako. Rudi kwenye somo ili kupata taarifa za kurekebisha majibu yako. Rudia mtihani hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi. Masomo yote, mitihani ya marudio, na kurasa za majibu zinapatikana kwenye www.Theolojia.org.

KWELI AU UWONGO ... weka alama kwenye kila moja ya kauli hizi [1 - 14] ukitumia “K” (Kweli) au “U” (Uwongo)

1. Tukio la Mnara wa Babeli lilitokea kabla ya gharika lakini baada ya Anguko. ***U***
2. Yakobo alipewa jina jipya la Israeli. ***K***
3. Babu ya Yusufu alikuwa Isaka. ***K***
4. Yusufu alikuwa mtawala Edomu. ***U***
5. Mungu alitoa Sheria kupitia Musa kwenye Mlima Sinai. ***K***
6. Mambo ya Walawi inanakili tukio la kutoka katika nchi ya Misri. ***U***
7. Yoshua inanakili mizunguko ya kushindwa katika enzi ya Waamuzi. ***U***
8. Sensa moja tu ndio iliyochukuliwa kama inavyonakiliwa katika Hesabu. ***U***
9. Samweli, Daudi, na Sulemani walikuwa wafalme wa Ufalme mmoja wa Israeli. ***U***
10. Mungu aligawanya Ufalme kwa sababu ya dhambi za Sulemani. ***K***
11. Ufalme wa Kaskazini wa Israeli ulikuwa na wafalme 19 na malkia mmoja. ***U***
12. Ufalme wa Kusini ulitawanywa katika nchi ya Uajemi. ***U***
13. Ufalme wa Kusini ulijumuisha makabila ya Yuda, Benyamini, na Lawi. ***K***
14. Zerubabeli, Ezra, na Yeremia waliwaongoza watu kurudi Yerusalemu baada ya uhamisho wa miaka 70. ***U***

MAJIBU YA KUCHAGUA ... kwa maswali 15 hadi 24 ... jibu kila swali kwa herufi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| A. Isaka | I. Sethi | B. Ezra | J. Yusufu | C. Yoshua |
| K. Ruthu | D. Daudi | L. Samsoni | E. Esta | M. Musa |
| F. Abrahamu | N. Nuhu | G. Nehemia | O. Samweli | H. Sulemani |

15. Ni mwanamke yupi aliishi katika enzi ya Waamuzi? ___*K*___

16. Ni nani aliyewaongoza Waisraeli kutoka Misri? ___*M*___

17. Ni nani aliyeteka, akagawanya, na akawawezesha Waisraeli kukaa Kanaani? ___*C*___

18. Ni nani aliyekuwa Mfalme wa pili wa Ufalme mmoja? ___*D*___

19. Ni nani aliyekuwa mwana wa Daudi? ___*H*___

20. Mbali na Adamu, babu ya Nuhu alikuwa nani? ___*I*___

21. Ni nani aliyejenga upya kuta za Yerusalemu? ___*G*___

22. Ni nani aliyekuwa nyanya mkuu wa Daudi? ___*K*___

23. Ni nani aliyekuwa mwana wa Abrahamu? ___*A*___

24. Ni nani aliyekuwa mwana wa kumi na moja wa Israeli? ___*J*___

MPANGILIO WA MATUKIO...WEKA MVIRINGO AU PIGIA MSTARI KWENYE JINA LA MTU ALIYETANGULIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 25. | Musa | *Nuhu* | Yakobo |
| 26. | Lawi | *Sethi* | Hamu |
| 27. | Sauli | Sulemani | *Samsoni* |
| 28. | Raheli | *Sara* | Dina |
| 29. | Isaka | Manase | *Ishmaeli* |
| 30. | Ezra | *Ezekieli* | Zerubabeli |
| 31. | *Ruthu* | Esta | Sefania |
| 32. | *Israeli* | *Baba yake Yusufu* | *Yakobo* |

33. Eleza jibu lako la swali tatanishi #32.

*Hawa watatu wote ni mtu mmoja. Yakobo alikuwa baba ya Yusufu. Na Yakobo aliitwa Israeli.*

## Kufanya Wanafunzi 1 - Kudumu Katika Neno Lake

# SOMO LA 5 - MAISHA YA KRISTO

*"Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena … alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba. Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa yesu kristo ni bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba."* Wafilipi 2:5-11

Maisha ya Yesu hayakuanza wakati alipozaliwa kama binadamu huko Bethlehemu. Yesu alikuwepo kabla ya uumbaji na atakuwepo milele. Hana mwanzo. Mungu Baba hakumzaa Yesu. Kuwa kwake Mwana wa Mungu si kwa msingi wa kuzaliwa … bali kwa msingi wa nafasi aliyopewa. Hakuna wakati ambapo Yesu hakuwepo. Alikuwa Muumba katika Mwanzo 1 na 2. Katika historia ya Agano la Kale, alijitokeza kama Malaika wa Bwana. Aliiokoa na kuilinda Israeli. Alizaliwa kama binadamu huko Bethlehemu ... aliishi Misri kwa muda mfupi kama mtoto mdogo ... kisha akahamia Nazareti katika Galilaya. Aliishi huko na familia yake, akisafiri nao kila mwaka kwenda Yerusalemu kwa Pasaka.

Akiwa na takriban miaka 30 Yesu alianza huduma yake ... katika maeneo manne ya kijografia. Yohana Mbatizaji alimbatiza katika mto Yordani. Kisha Roho akamwongoza kwenda jangwani ili akajaribiwe na Shetani kwa muda wa siku 40. Katika miezi ya kwanza, Yesu alihudumu katika eneo la ***Uyahudi na Galilaya***. Huko alikutana na wanafunzi wake wa kwanza … alifanya muujiza wake wa kwanza . . . na akatakasa hekalu kwa mara ya kwanza. Umaarufu wa Yesu uliongezeka wakati wa huduma yake ***Galilaya***. . . lakini upinzani na uhasama pia uliongezeka. Alifundisha, alifanya miujiza, na kuponya. Alichagua na akaanza kuhudumu pamoja na wanafunzi wake. Huduma yake ilipanuka hadi katika maeneo ya ***kaskazini na mashariki mwa Galilaya*** ambako sura yake iligeuzwa kwenye Mlima Hermoni. Katika miezi ya mwisho, kitovu cha huduma ya Yesu kilikuwa katika eneo la ***Uyahudi na Perea.***

Kuingia kwa Ushindi Yerusalemu kuliashiria mwanzo wa wiki ya msalaba na kulitangaza kwamba Yesu ni Mfalme wa Wayahudi. Jumatatu na Jumanne zilikuwa sikukuu za umma. Alitakasa hekalu, akaulaani mtini usiozaa, akawashutumu Waandishi na Mafarisayo, na kutabiri kuhusu kurudi kwake. Baadaye wiki hiyo alishinda siku moja peke yake na wanafunzi wake. Aliosha miguu yao kabla ya Mlo wa Mwisho, akawafundisha, na kuwaombea. Yesu alikwenda kusali katika bustani ya Gethsemane. Alikamatwa huko. Baada ya kesi tatu mbele ya Wayahudi na tatu mbeye ya Warumi, alihukumiwa kusulubishwa. Alisulubishwa msalabani. Alikufa na akazikwa katika kaburi la kuazima. Alifufuka kutoka kwa wafu siku ya tatu. Kwa siku arobaini baada ya kufufuka kwake, Yesu alijitokeza mara kumi au zaidi. . . kwa wanawake, kwa wanafunzi wake, na kwa wafuasi wake. Alipaa Mbinguni ambako anatuhudumia sasa tunaposubiri kurudi kwake.

## UNABII ULIOTIMIA

Yesu alisema, *"Lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi,"* Luka 24:44. Linganisha tabiri na timizo zifuatazo. Ni jambo la kushangaza kulinganisha usulubisho kama ulivyotabiriwa katika Zaburi 22 na kutimizwa katika Mathayo 27. *Sheria* inarejelea vitabu vitano vya kwanza vya Biblia … pia huitwa Torati au Pentateuki.

| **22 kati ya Zaidi ya Unabii 300** | **Agano la Kale** | **Agano Jipya** |
|---|---|---|
| 1. Kuzaliwa na bikira | Isaya 7:14 | Mathayo 1:18-25 |
| 2. Uzao wa Abrahamu | Mwanzo 22:18 | Mathayo 1:1 |
| 3. Mwana wa Isaka | Mwanzo 21:12 | Luka 3:34 |
| 4. Kabila la Yuda | Mwanzo 49:10 | Luka 3:33 |
| 5. Ukoo wa Yese | Isaya 11:1 | Luka 3:32 |
| 6. Nyumba ya Daudi | Yeremia 23:5 | Luka 3:31 |
| 7. Atazaliwa Bethlehemu | Mika 5:2 | Mathayo 2:1 |
| 8. Ataitwa Imanueli | Isaya 7:14 | Mathayo 1:23 |
| 9. Atatanguliwa na mjumbe | Isaya 40:3 | Mathayo 3:1-2 |
| 10. Atafanya miujiza | Isaya 35:5-6 | Mathayo 9:35 |
| 11. Atafundisha akitumia mifano | Zaburi 78:2 | Mathayo 13:34 |
| 12. Kuingia kwa Ushindi | Zekaria 9:9 | Luka 19:35-37 |
| 13. Atasalitiwa na rafiki | Zaburi 41:9 | Mathayo 10:4 |
| 14. Vipande 30 vya fedha | Zekaria 11:12 | Mathayo 26:15 |
| 15. Ataachwa na Wanafunzi wake | Zekaria 13:7 | Marko 14:40 |
| 16. Atanyamaza mbele ya washtaki wake | Isaya 53:7 | Mathayo 27:12 |
| 17. Atasulubiwa | Zaburi 22:16 | Luka 23:33 |
| 18. Atahesabiwa pamoja wakosaji | Isaya 53:12 | Mathayo 27:38 |
| 19. Mavazi | Zaburi 22:18 | Yohana 19:23-24 |
| 20. Hakuna mifupa iliyovunjika | Zaburi 34:20 | Yohana 19:33 |
| 21. Katika Kaburi la Tajiri | Isaya 53:9 | Mathayo 27:57-60 |

## INJILI NNE . . . KUMBUKUMBU NNE ZA KIHISTORIA

Injili nne zinatupa masimulizi manne ya maisha ya Yesu Kristo. Kila mwandishi, akiongozwa na Roho wa Mungu, alitoa rekodi na taswira ya maisha ya Yesu . . . zikitupatia ufahamu tofauti kulingana na asili tofauti za waandishi, haiba, wasikilizaji wa asili na msisitizo.

Injili *sinoptiki* [masimulizi yanayofanana ya Mathayo, Marko, na Luka] zinazungumzia matukio mengi yanayofanana. Yohana aliandika habari zaidi ambazo ziko kwenye simulizi lake pekee ... ni simulizi lenye upekee wa 90%. Yohana alisisitiza uungu wa Kristo zaidi ya walivyofanya wengine ... na katika Injili yake alitaja *kumwamini* Yesu jumla ya mara 98. *Luka* ndio Injili pekee inayosema kwamba inasimulia matukio kama yalivyofuatana katika wakati, Luka 1:3.

Injili nne zinaeleza karibu nusu ya Agano Jipya. Ndani ya Injili zenyewe, theluthi moja ya Maandiko yanazungumzia wiki saba kutoka Kuingia kwa Ushindi hadi Kupaa kwa Yesu.

Watu wanne . . . aliyekuwa mtoza kodi Mathayo, kijana Marko, tabibu wa Mataifa Luka, na mvuvi Yohana . . . walitupa kumbukumbu ya Mungu ya maisha ya Yesu duniani na kifo chake.

| | **Mathayo** | **Marko** | **Luka** | **Yohana** |
|---|---|---|---|---|
| Mwandishi | Mtoza kodi na Mwanafunzi | Kijana | Tabibu wa Mataifa | Mvuvi na Mwanafunzi |
| Tarehe | Miaka ya 60 BK | Miaka ya 50 BK | 60 BK | 85-90 BK |
| Wasomaji | Wayahudi | Warumi | Wagiriki | Watu wote |
| Msisitizo | Masihi Aliyetabiriwa | Vitendo na Miujiza | Rekodi ya kihistoria | Amini [mara 98] |
| Yesu kama | Mfalme wa Wayahudi | Mtumishi wa wa Mungu | Mwana wa Adamu | Mwana wa Adamu |
| Miujiza | 20 | 17 | 20 | 8 |
| Mifano | 19 | 6 | 24 | 0 |
| Sura ya | 28 | 16 | 24 | 21 |
| Upekee* | 40% | 60% | 5% | 90% |

* Upekee unamaanisha ni asilimia ngapi ya maudhui hayajaandikwa katika Injili nyingine.

## YESU TANGU KABLA YA UUMBAJI HADI BETHLEHEMU

**Yesu amekuwepo daima. Amekuwepo tangu kabla ya uumbaji.**

Mika 5:2
Isaya 9:6

**Alikuwepo kabla ya vitu vyote vilivyouumbwa.**

Yohana 1:1,2
Wakolosai 1:17
Yohana 8:56-58
Yohana 17:5

**Alikuwa Muumba katika Mwanzo 1 na 2.**

Yohana 1:3
Wakolosai 1:16

**Kabla ya kuvaa mwili wa kibinadamu, Yesu alijitokeza kama Malaika wa Bwana.**

Kwa Hajiri - Mwanzo 16:7-13, 21:17-20
Kwa Musa - Kutoka 3
Kwa Gideoni - Waamuzi 6:11-14
Kwa Wazazi wa Samsoni - Waamuzi 13:1-22

**Anaonekana kujitokeza katika sehemu zingine za Agano la Kale.**

Kwa Abrahamu - Mwanzo 18:1, 22:11-18
Kwa Yakobo - Mwanzo 31:11-13, 32:24-32
Hakuna Aliyemwona Baba - Yohana 1:18, 6:46, 14:9

**Yesu alikuwa mpiganaji, mtetezi, na mkombozi wa Israeli.**

Yoshua 5:13 - 6:3
2 Wafalme 19:35
1 Mambo ya Nyakati 21:14-27
Zaburi 34:7

**Utatu wa Mungu umeonyeshwa wazi katika Agano la Kale.**

Isaya 48:12-17 [iliyoandikwa takriban mwaka 700KK]

**Yesu alishuka kutoka Mbinguni kuja duniani.**

Yohana 3:13,31
Yohana 6:33, 38, 41, 50, 51, 58, na 62

**Alifanyika mfano unaoonekana wa Mungu asiyeonekana.**

Wakolosai 1:15
Yohana 14:9

**Alifanyika mwili Bethlehemu na akaishi kati yetu.**

Mika 5:2
Yohana 1:14

## KUZALIWA NA UTOTO WA YESU

### Kuzaliwa Kwake

Yesu alizaliwa katika mji mdogo wa Bethlehemu takriban [kilomita 8] kusini mwa Yerusalemu kati ya mwaka 6 KK na mwaka 4 KK. Kumbuka: kalenda ya Gregori yenye BC inayomaanisha *kabla ya Kristo*, yaani, kabla ya kuzaliwa kwa Kristo, na AD inayomaanisha *Anno Domini*, yaani, katika *mwaka wa Bwana wetu*, inaonekana ilianza na tarehe isiyo sahihi ya kuzaliwa kwa Kristo.

### Wazazi Wake

Ukoo wa Mariamu unafuatiliwa katika Luka 3:23-38 hadi kwa Nathani na baba yake Mfalme Daudi ... kisha hadi kwa Yuda, Shemu, Nuhu, Sethi, Adamu, na Mungu. Mariamu alichukua mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu [si kupitia Yusufu] na akabaki bikira hadi baada ya kuzaliwa kwa Yesu. Yusufu, seremala, ingawa hakuwa baba wa kimwili wa Yesu, kisheria alikuwa baba yake wa kambo wa kidunia. Ukoo wa Yusufu unafuatiliwa katika Mathayo 1:1-17 hadi kwa Sulemani na Mfalme Daudi baba yake Sulemani, kwa Yuda, kisha kwa Abrahamu.

### Alizaliwa Bathlehemu

Yusufu na Mariamu walisafiri kusini takriban [kilomita 110] hadi Bethlehemu kutoka Nazareti katika Galilaya ... ili kuhesabiwa katika sensa. Wakiwa huko, Yesu alizaliwa. Kitanda chake cha kwanza kilikuwa ni chombo cha kulisha mifugo [hori]. Kuzaliwa kwake kulitangazwa na malaika kwa wachungaji. Alipowekwa wakfu katika hekalu la Yerusalemu, angalau siku 40 baada ya kuzaliwa kwake, Simeoni na Ana walimtambua Yesu mchanga kama Masihi wa Mungu.

### Mamajusi na Herode

Baada ya Yesu kuzaliwa, idadi isiyojulikana ya mamajusi kutoka Mashariki walifuata nyota hadi Yerusalemu ili kumtafuta Mfalme wa Wayahudi aliyezaliwa. Walimpata yeye na Mariamu katika *nyumba* Bethlehemu na wakamwabudu. Herode alijaribu kumwangamiza Yesu kwa kuwaua watoto wote wa kiume wenye umri wa hadi miaka miwili ndani ya Bethlehemu na viunga vyake.

### Kwenda Misri

Malaika alimuonya Yusufu achukue familia yake na atorokee Misri, na walikaa huko mpaka malaika alipowaambia kwamba ni salama kurudi.

### Galilaya

Familia ya Yusufu ilirudi kuishi Nazareti. Yesu alikulia huko … akifanya safari za kila mwaka kwenda Yerusalemu kwa Pasaka [takriban maili 65 au kilomita 100 kusini]. Na akiwa na umri wa miaka 12, Yesu aliwashangaza walimu wa hekalu kwa maarifa yake na majibu yake. Wakati huo Yesu aliliita hekalu *“nyumba ya Baba yangu.”* Yesu aliishi na kaka zake Yakobo, Yusufu, Simoni, na Yuda na dada zake [zaidi ya mmoja] huko Nazareti, Mathayo 13:55-56.

### Huduma ya Hadharani

Akiwa na umri wa takriban miaka 30, Yesu alianza huduma yake ya hadharani . . . iliyotangazwa na jamaa yake, Yohana Mbatizaji.

## HUDUMA YA HADHARANI YA YESU


**Katika Galilaya na Uyahudi - mwanzo**. Yohana Mbatizaji alimbatiza Yesu katika Mto Yordani karibu na Bethania. Kisha Roho wa Mungu akamwongoza Yesu hadi katika jangwa la Uyahudi ili ajaribiwe na Shetani kwa siku 40. Baadaye, Yesu alikutana na wanafunzi wake wa kwanza ... Andrea, Simoni, Filipo na Nathanaeli. Alifanya muujiza wake wa kwanza kwenye harusi huko Kana ... kwa kugeuza maji kuwa divai. Yesu alitakasa Hekalu kwa mara ya kwanza ... akiwafukuza wafanyabiashara nje ya nyumba ya Baba yake. Alitangaza, *"Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha."* Yohana 2:19. Kiongozi wa Wayahudi, Mfarisayo Nikodemo, alimwendea Yesu usiku huko Yerusalemu. Yesu akamwambia, *"Hamna budi kuzaliwa mara ya pili,"* Yohana 3:7. Akiwa njiani kurudi Galilaya, Yesu alipitia Samaria ambako alikutana na mwanamke kwenye kisima cha Yakobo karibu na Sikari. Mwanamke huyo alimwamini Yesu na akawaleta wengi kwake.

**Katika Galilaya - umaarufu na uhasama unaongezeka**. Yesu alisafiri hadi Galilaya ambako alikataliwa katika mji wake wa nyumbani wa Nazareti. Aliendelea hadi Kapernaumu. Baada ya kuwawezesha wavuvi kuvua samaki wengi sana kimuujiza kwenye Bahari ya Galilaya, aliwaita wavuvi Andrea, Simoni, Yakobo, na Yohana kuwa wavuvi wa watu. Pia alimwita Lawi, mtoza ushuru, amfuate. Yesu alirudi Yerusalemu ambako aliponya siku ya Sabato ... hilo lilikuwa kosa kwa viongozi wa Wayahudi. Baada ya usiku wa kusali, Yesu aliwachagua wanafunzi 12. Alishangaza umati kwa mafundisho yake yenye mamlaka katika Mahubiri ya Mlimani. Alifundisha kwa mifano na akaponya. Aliwatuma wale wanafunzi 12 wawili wawili kuwahudumia kondoo waliopotea wa Israeli . . . kuhubiri na kuponya. Yesu aliwalisha kimuujiza watu 5,000. Kisha akafundisha kwamba yeye ni mkate wa uzima ... jambo lililowafanya wafuasi wengi wamuache.

**Kaskazini na mashariki mwa Galilaya**. Yesu alisafiri kaskazini kuelekea Tiro na Sidoni katika eneo la Foinike ambako aliendelea kufundisha na kuponya. Alisafiri mashariki kupitia Dekapoli na Bashani. Yesu aliwachukua Petro, Yakobo, na Yohana juu ya Mlima Hermoni [yamkini hapo ndipo walienda] ambapo aling'aa kama nuru katika tukio la Kugeuzwa Sura. Musa na Eliya wakatokea na wakazungumza naye. Pia, Mungu alisema, *"Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye!"* Mathayo 17:5. Yaonekana hii ilikuwa mara ya kwanza Musa kuingia katika Nchi ya Ahadi.

**Katika Uyahudi na Perea - miezi ya mwisho**. Mafundisho, uponyaji, na miujiza yake iliendelea. Alidai kuwa yeye ni Nuru ya ulimwengu na yuko sawa na Mungu ... kwa hivyo Wayahudi walijaribu kumpiga mawe. Baada ya kueleza gharama ya kuwa mwanafunzi, Yesu aliwatuma wafuasi 70 wakiwa wawili wawili kuhudumu. Yesu alichelewesha ziara yake ya Bethania ambako siku 4 baadaye alimfufua rafiki yake Lazaro kutoka kwa wafu. Makuhani wakuu na Mafarisayo waliamua kumuua. Yesu alisafiri kwenda Yerusalemu akipitia Samaria na Galilaya. Aliendelea kufundisha na kuponya. Aliwaambia wanafunzi wake juu ya kifo na ufufuo wake. Hatimaye, alienda nyumbani kwa Lazaro huko Bethania ili kuanza wiki yake ya mwisho kabla ya kusulubishwa na kufufuka kwake.

## NCHI WAKATI WA YESU



## WIKI YA MSALABA

### Jumapili – Kuingia kwa Ushindi

Yesu alisafiri kutoka nyumbani kwa Lazaro huko Bethania hadi Yerusalemu. Njiani, Yesu alisimama kwenye Mlima wa Mizeituni upande wa mashariki wa Yerusalemu. Aliwatuma wanafunzi wake wamletee punda na mwana punda. Yesu aliingia Yerusalemu akiwa amempanda mwana punda, na hivyo akajitangaza kuwa Mfalme wa Israeli, Mathayo 21, Marko 11, Luka 19, Yohana 12 ... akitimiza unabii wa Zekaria 9:9. Watu wakatandaza mavazi na matawi yao barabarani mbele zake na kumwabudu Mungu. Katika Yerusalemu, Yesu aliona hali ya hekalu ... likiwa limejaa wafanyabiashara tena. Alirudi Bethania.

### Jumatatu - utakaso mwingine wa Hekalu

Akiwa njiani kurudi Yerusalemu Yesu aliulaani mtini usiozaa matunda, ambao ulinyauka siku iliyofuata, Mathayo 21, Marko 11. Alitakasa hekalu mara ya pili kwa kuwafukuza wanunuzi, wauzaji na wabadilishaji fedha, Mathayo 21, Marko. 11, Luka 19. Utakaso huu wa Hekalu ulifanyika karibu na mwisho wa huduma yake ya hadharani. Utakaso wake wa kwanza wa Hekalu ulifanyika karibu na mwanzo wa huduma yake ya hadhara, Yohana 2:13-22.

### Jumanne – sikukuu ya umma

Viongozi wa Kiyahudi walimhoji Yesu kuhusu mamlaka yake na wakajaribu kumtilia shaka kwa kumuuliza maswali ya hila kuhusu kodi, ndoa na amri. Yesu alifundisha mfano wa wakulima waovu waliomuua mwana wa mmiliki wa shamba la mizabibu. Yesu aliwashutumu vikali Waandishi na Mafarisayo. Na alitabiri juu ya kuharibiwa kwa Yerusalemu na juu ya kurudi kwake, Mathayo 24-25, Marko 13, Luka 21. Pia ilikuwa ni siku hii ndipo Yuda alifanya mpango wake wa kumsaliti Yesu.

### Siku moja kabla ya msalaba - siku ya kibinafsi

Yesu alishinda na wanafunzi wake siku hii ... mbali na umati. Kuna utata ikiwa siku hii ilikuwa Jumatano au Alhamisi. Walikusanyika katika chumba cha juu kwa ajili ya mlo wa Pasaka. Aliosha miguu ya wanafunzi. Wakati wa mlo, Yuda aliondoka kwenda kumsaliti Yesu. Katika Hotuba ya Chumba cha Juu, Yohana 13-16, Aliwafundisha wanafunzi kuhusu kuondoka kwake na ujio wa Roho Mtakatifu. Yesu na Wanafunzi wake walitembea hadi kwenye bustani ya Gethsemane. Yesu aliomba mpaka jasho lake likawa kama damu. Wanafunzi wake, wakielewa kwamba atakufa karibuni, walilala kwa sababu ya huzuni, Luka 22:45.

## WIKI YA MSALABA ... mwendelezo

**Usiku wa kuamkia msalaba – Kesi zake sita**. Baada ya usiku wa manane, Yuda aliwaleta viongozi wa Kiyahudi na askari kumkamata Yesu katika bustani ya Gethsemane. Walikuja na mapanga na marungu ili kumkamata Mfalme wa Amani. Walimfunga Yesu na kumpeleka kwa viongozi wa Kiyahudi ili kesi yake isikizwe.

1. Kesi yake mbele ya Anasi [Kesi ya 1] haikuwa halali ... haikuwa na mashahidi. Afisa mmoja alimpiga.

2. Alipelekwa kwa kuhani mkuu Kayafa kwa kesi nyingine [Kesi ya 2] ... kesi hii ilijumuisha mashahidi wa uwongo. Viongozi wa Kiyahudi waliuliza, *"Wewe ndiwe Kristo, Mwana wake Mtukufu?"* … "Mimi ndiye," Marko 14:61-62. Kuhani Mkuu akararua vazi lake kama ishara ya kulaani kufuru. Makuhani walimhukumu kuwa anastahili kifo. Walinzi walimtemea mate usoni, wakampiga ngumi na makofi. Wakati wa kesi hii, Petro alimkana Yesu mara tatu ... kisha Petro akatoka nje na akalia kwa uchungu.

3. Walimleta Yesu mbele ya Baraza Kuu la Wayahudi kwa ajili ya kesi nyingine walipokutana asubuhi [Kesi ya 3]. Waliuliza, *"Wewe ndiwe Mwana wa Mungu?"* … Na Yesu akajibu, *"Ninyi mwasema kwamba mimi ndiye,"* Luka 22:70.

4. Kesi yake ilisikizwa mbele ya Pilato [Kesi ya 4].

5. Alipelekwa kwa Herode ili kesi yake isikizwe [Kesi ya 5].

6. Kisha alirudishwa kwa Pilato [Kesi 6]. Umati ulikataa aachiliwe. Pilato alimhukumu adhabu ya kifo. Yesu alipigwa, alidhihakiwa, alitemewa mate, akachapwa viboko vibaya sana, na akavishwa taji la miiba kichwani. Yesu alikuwa dhaifu sana kubeba msalaba wake hadi Golgotha ili asulubiwe. Simoni Mkirene alimsaidia kuubeba. Golgotha, mahali pa fuvu la kichwa, hapakuwa mahali pakupendeza mlimani ... palikuwa ni sehemu ya kuua watu kando ya barabara ya kwenda mahali pakutupa taka.

**Siku ya msalaba – kujitoa kwake kama dhabihu kuu.** Karibu saa tatu asubuhi, Yesu alisulubishwa msalabani katikati ya wezi wawili. Juu ya kichwa chake kulikuwa na ishara iliyosema, *"Mfalme wa Wayahudi."* Yesu aliomba, *"Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo."* Wengi walimdhihaki ... wakiwemo viongozi wa Kiyahudi, wapita njia, askari, na hata mmoja wa wale wezi wawili. Yule mwizi mwingine aliamini. Yesu akamwambia, *"Leo hivi utakuwa pamoja nami peponi."* Walinzi wakagawana mavazi yake na wakalipigia kura kanzu yake. Saa sita mchana, giza likatanda angani. Takriban saa tisa mchana Yesu alisema, *"Mungu wangu, Mungu wangu mbona umeniacha?"* ... *"Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu ... Imekwisha."* Yesu aliinamisha kichwa chake na akafa. Tetemeko la ardhi lilitokea Yerusalemu. Pazia la Hekalu likapasuka vipande viwili. Akida mlinzi aliyekuwa chini ya msalaba alianza kumsifu Mungu ... na akatangaza, *"Mtu huyu hakuwa na hatia ... mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu."* Baada ya Yesu kufa, mlinzi mmoja alimdunga mkuki ubavuni ili kuhakikisha kwamba alikuwa amekufa. Kwa kweli alikuwa amekufa. Hivyo hapakuwa na sababu ya kuvunja miguu yake. Mungu-mwanadamu mkamilifu, asiye na dhambi alikuwa amelipia dhambi za ulimwengu. Yesu alishushwa kutoka msalabani ili akazikwe katika kaburi la kuazima. Kaburi lilifungwa na likalindwa na askari wa Kirumi kwa sababu Yesu alikuwa ametabiri kwamba atafufuka kutoka kwa wafu baada ya siku tatu. Simulizi la kusulubishwa na nukuu zilizo katika aya hii zinatoka katika Mathayo 27, Marko 15, Luka 23, na Yohana 19.

## KUTOKA KUFUFUKA KWAKE HADI KURUDI KWAKE

### Ufufuo

Tetemeko la ardhi lilitokea Yerusalemu na malaika akaliviringisha jiwe kutoka kwenye kaburi la Yesu, Mathayo 28:2. Yesu alikuwa ameshinda kifo. Alikuwa amefufuka ... akawa hai tena kiroho na kimwili, Mathayo 28:9, Luka 24:39, na Luka 24:41-43.

### Kaburi Tupu

Wanawake [Mariamu Magdalene, Mariamu mama ya Yakobo, Salome, Yoana, na wengine] walikuja kaburini wakiwa na manukato ili wayapake kwenye mwili wa Yesu. Walikuta kaburi likiwa wazi na tupu. Malaika wawili waliwatokea na kuwaambia, *“Kwa nini mnamtafuta aliye hai katika wafu?”* Luka 24:5. Maria Magdalene na wale wanawake wengine walirudi kuwaambia Petro na Yohana yaliyojiri nao pia wakaenda kaburini.

### Yesu Anajitokeza - Siku Arobaini za Uthibitisho

[Mathayo 28, Marko 16, Luka 24, Yohana 20-21, Matendo 1, 1 Wakorintho 15]

Kwa Mariamu Magdalene ... kaburini.

Kwa Mariamu [mama ya Yakobo], Salome, na Yoana ... kaburini.

Kwa Petro … kaburini.

Kwa watu 2 katika njia ya kuelekea Emau ... nje ya Yerusalemu.

Kwa Mitume 10 katika Chumba cha Juu jioni ya Ufufuo.

Kwa Mitume 11 siku 8 baadaye ... yamkini huko Galilaya.

Kwa Mitume 7 ... kando ya Bahari ya Galilaya.

Kwa watu 500 ili kutoa Agizo Kuu ... kwenye mlima huko Galilaya.

Kwa kaka yake wa kambo Yakobo ... katika eneo lisilojulikana.

Kwa Mitume 11 ... huko Yerusalemu.

Wakati wa Kupaa kutoka kwenye Mlima wa Mizeituni ... mashariki mwa Yerusalemu.

## Maagizo Yake Mawili ya Mwisho:

**1. Nendeni mkafanye wanafunzi.** Akiwa juu ya mlima huko Galilaya, siku kadhaa kabla ya Kupaa, Yesu alitoa Agizo Kuu, *"Enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi,"* Mathayo 28:18-20. Hao na sisi tuliamriwa kuwafundisha wengine kuwa wafuasi wa Yesu ... kufanya wanafunzi. Wasioamini wanahitaji kuwa Waumini. Waumini wapya wanapaswa kubatizwa. Tunapaswa kuwafundisha kutii yote ambayo Yesu ameamuru ... ikijumuisha kutii Agizo Kuu.

**2. Muwe mashahidi Wangu.** Siku kadhaa baadaye, Yesu alijitokeza kwenye Mlima wa Mizeituni ambapo aliwaambia wanafunzi wake, *"Mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi,"* Matendo 1:8. Baada ya maneno hayo, Yesu aliinuliwa na akapaa mbinguni. Wingu likampokea na akapotea machoni pao. Yesu alipaa na akaketi kwenye mkono wa kuume wa Baba.

## Huduma yake ya sasa inajumuisha:

Yesu ndiye kichwa cha Mwili, Waefeso 1:22-23, 4:14-16.

Yeye ni Kuhani wetu Mkuu, Waebrania 8:1-2.

Yeye ni mtetezi wetu anayetuombea, Waebrania 7:25, 9:24-25.

Anatuandalia mahali, Yohana 14:1-3.

Yuko pamoja nasi, Mathayo 18:20.

**Kurudi kwake kulikoahidiwa:** Agano Jipya linataja kurudi kwa Kristo zaidi ya mara 300 katika sura zake 260. . . hiyo ni wastani ya mara moja kila baada ya vifungu 25.

> *"Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo."* Yohana 14:3
>
> *"Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni."* Matendo 1:11

Marejeleo mengine ni pamoja na:

- Mathayo 24
- 1 Wathesalonike 4:13-18
- 1 Wakorintho 15:51-58
- Ufunuo

## MIFANO YA YESU … yamkini jinsi yanavyofuatana

| | Mathayo | Marko | Luka | Yohana* |
|---|---|---|---|---|
| 1. Nyumba juu ya mwamba | 7:24-27 | | 6:47-49 | |
| 2. Bwana harusi, vazi, divai | 9:14-17 | 2:18-22 | 5:33-39 | |
| 3. Watoto wa sokoni | 11:16-19 | | 7:31-35 | |
| 4. Mbegu na aina nne za udongo | 13:3-9 | 4:3-9 | 8:5-8 | |
| 5. Mbegu na mavuno | | 4:26-29 | | |
| 6. Ngano na magugu | 13:24-30 | | | |
| 7. Punje ya haradali | 13:31-32 | 4:30-32 | 13:18-19 | |
| 8. Chachu | 13:33 | | 13:20-21 | |
| 9. Hazina iliyofichwa | 13:44 | | | |
| 10. Lulu ya thamani kuu | 13:45-46 | | | |
| 11. Wavu wa kuvua samaki | 13:47-50 | | | |
| 12. Wadeni wawili | | | 7:41-43 | |
| 13. Mtumwa asiye na huruma 1 | 8:23-35 | | | |
| 14. Msamaria mwema | | | 10:30-37 | |
| 15. Rafiki asiyekata tamaa | | | 11:5-8 | |
| 16. Tajiri mjinga | | | 12:16-21 | |
| 17. Mtini usiozaa matunda | | | 13:6-9 | |
| 18. Kiti cha chini kabisa | | | 14:7-11 | |
| 19. Mialiko iliyokataliwa | | | 14:16-24 | |
| 20. Mnara na vita | | | 14:25-35 | |
| 21. Kondoo aliyeopotea | 18:12-14 | | 15:3-7 | |
| 22. Sarafu iliyopotea | | | 15:8-10 | |
| 23. Mwana mpotevu | | | 15:11-32 | |
| 24. Wakili mwerevu | | | 16:1-9 | |
| 25. Watumwa wasiostahili | | | 17:7-10 | |
| 26. Mjane asiyekata tamaa | | | 18:1-8 | |
| 27. Maombi ya watu wawili | | | 18:9-14 | |
| 28. Thawabu za shamba la mzabibu | 20:1-20 | | | |
| 29. Watumwa kumi | | | 19:11-27 | |
| 30. Wana wawili katika shamba la mizabibu | 21:28-32 | | | |
| 31. Wakulima waovu | 21:33-44 | 12:1-12 | 20:9-18 | |
| 32. Karamu ya harusi | 22:1-14 | | | |
| 33. Watumishi wawili | 24:45-51 | | 12:42-48 | |
| 34. Mlinda mlango mwangalifu | | 13:34-37 | | |
| 35. Wanawali kumi wenye taa | 25:3-13 | | | |
| 36. Watumwa watatu | 25:14-30 | | | |

Mifano ni tamathali za usemi katika muundo wa hadithi zinazoonyesha ukweli wa kiroho kupitia vielelezo vya kawaida. Agano la Kale lilitabiri kwamba Yesu atafundisha kwa mifano, Zaburi 78:2. Yesu alifundisha kwa mifano ili kuwapa Waumini ufahamu ... na kuwazuia wasioamini wasipate ufahamu, Mathayo 13:10-17, Marko 4:10-12. Mifano inaonyesha ukweli lakini haizalishi ukweli. Kwa kawaida inaonyesha ukweli mmoja tu ... si ukweli mwingi. Fasiri kwa njia rahisi na uzingatie lengo la msingi na muktadha wa mfano husika. **Kumbuka* kwamba Injili ya Yohana haina mifano ingawa Yohana 10:6 katika tafsiri fulani za Biblia inatafsiri neno fulani la Kigiriki kama “mfano.” Hata hivyo, ni bora zaidi kutafsiri neno hilo la Kigiriki katika kifungu hicho kama “tamathali ya usemi.” Na ni aina ya kielelezo ambacho ni tofauti na mfano ulio katika muundo wa hadithi.

## MIUJIZA YA YESU … yamkini jinsi ilivyofuatana

| | Mathayo | Marko | Luka | Yohana |
|---|---|---|---|---|
| 1. Maji kuwa divai | | | | 2:1-11 |
| 2. Mwana wa diwani | | | | 4:46-54 |
| 3. Pepo katika sinagogi | | 1:21-28 | 4:33-37 | |
| 4. Mama mkwe wa Petro | 8:14-15 | 1:29-31 | 4:38-39 | |
| 5. Uvuaji wa kwanza wa samaki | | | 5:1-11 | |
| 6. Mgonjwa wa ukoma Genesareti | 8:1-4 | 1:40-45 | 5:12-15 | |
| 7. Kilema wa Kapernaumu | 9:1-8 | 2:1-12 | 5:17-26 | |
| 8. Uponyaji katika bwawa | | | | 5:1-16 |
| 9. Mkono uliopooza | 12:9-13 | 3:1-5 | 6:6-11 | |
| 10. Mtumishi wa akida | 8:5-13 | | 7:1-10 | |
| 11. Mwana wa mjane | | | 7:11-17 | |
| 12. Kipofu mwenye pepo | 12:22 | | | |
| 13. Alituliza bahari | 8:23-27 | 4:35-41 | 8:22-25 | |
| 14. Pepo katika nguruwe | 8:28-34 | 5:1-20 | 8:26-39 | |
| 15. Binti ya Yairo | 9:18-26 | 5:22-43 | 8:41-56 | |
| 16. Mwanamke aliyetokwa na damu | 9:20-22 | 5:25-34 | 8:43-48 | |
| 17. Vipofu wawili | 9:27-31 | | | |
| 18. Bubu mwenye pepo | 9:32-33 | | | |
| 19. Aliwalisha watu 5000 | 14:15-21 | 6:32-44 | 9:10-17 | 6:5-14 |
| 20. Alitembea juu ya maji | 14:22-33 | 6:45-52 | | 6:15-21 |
| 21. Msichana Mkanaani | 15:21-28 | 7:24-30 | | |
| 22. Kiziwi bubu aponywa | | 7:31-37 | | |
| 23. Aliwalisha watu 4000 | 15:32-38 | 8:1-9 | | |
| 24. Kipofu wa Bethsaida | | 8:22-26 | | |
| 25. Mtoto mwenye pepo | 17:14-21 | 9:14-29 | 9:37-42 | |
| 26. Samaki, mdomo, na sarafu | 17:24-27 | | | |
| 27. Mtu aliyezaliwa kipofu | | | | 9:1-8 |
| 28. Bubu mwenye pepo | | | 11:14 | |
| 29. Mwanamke ameinama | | | 13:10-17 | |
| 30. Mtu mwenye ugonjwa wa safura | | | 14:1-6 | |
| 31. Lazaro afufuliwa | | | | 11:1-45 |
| 32. Watu kumi wenye ukoma | | | 17:11-19 | |
| 33. Bartimayo kipofu | 20:29-34 | 10:46-52 | 18:35-43 | |
| 34. Mtini uliolaaniwa | 21:17-22 | 11:12-24 | | |
| 35. Sikio la Malko | | | 22:49-51 | |
| 36.Uvuaji wa pili wa samaki | | | | 21:1-14 |

Miujiza ni matendo yasiyo ya kawaida ambayo kiasili hayaelezeki. Yanaonyesha uungu, nguvu, na kusudi la Mungu. Miujiza ya Yesu ilitoa ushuhuda wa yeye ni nani, Yohana 10:25. Miujiza yake iliwafanya watu wamwamini, Yohana 14:11, 20:30-31. Ili kuelewa miujiza, ni muhimu kuzingatia masuala kadhaa . . . nani alikuwa hapo, nini kilitendeka, kwa nini kilitendeka, ni vitu gani vilivyohitajika vilikuwa hapo, ni athari gani zilitokea, na nini cha Mungu kilidhihirishwa.

## WANAFUNZI KUMI NA WAWILI WA YESU

**Miito Miwili ya Wanafunzi.** Wanafunzi wa Yesu walichaguliwa na yeye, *"Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda,"* Yohana 15:16. Waliitwa kwa miito miwili tofauti, Yohana 1:37-51 kisha Mathayo 4:18-22 na Marko 1:16-20.

**Orodha nne.** Wanafunzi wameorodheshwa katika sehemu nne kwenye Biblia … Mathayo 10:2-4, Marko 3:16-19, Luka 6:14-16, na Matendo 1:13. Katika orodha hizo inaonekana kuna vikundi vitatu vya Wanafunzi 4 huku Petro, Filipo, na Yakobo Mdogo wakichukua nafasi ya kwanza katika kila kundi katika kila orodha … katika nafasi ya 1, 5, na 9 kama ilivyoorodheshwa hapa chini.

1. **Petro** … aliandika *1 na 2 Petro* … mvuvi … pia anaitwa Simoni Petro … na alikuwa ameoa, Marko 1:30, Luka 4:38.
2. **Yohana** …. kaka ya Petro ... mwandishi wa *Injili ya Yohana, 1, 2 na 3 Yohana*, na *Ufunuo*.
3. **Yakobo**… ambaye si yule mwandishi wa *Yakobo* … kaka ya Yohana … pamoja na Yohana, walikuwa wana wa Zebedayo, Wana wa Ngurumo.
4. **Andrea** … Kaka ya Petro.
5. **Filipo** ... yamkini si yule Filipo wa Matendo 6, 8, na 21.
6. **Tomaso** … alikuwa na shaka mpaka alipomwona Yesu aliyefufuka.
7. **Nathanieli / Bartholomayo** ... Yohana 1:45-49 na 21:2, labda jina alilopewa mwana [Bar] wa Tholomais [yaani, Bar Tholomayo].
8. **Mathayo** ... mwandishi wa *Injili ya Mathayo* ... Lawi mtoza ushuru, Lk 5:27-29.
9. **Yakobo Mdogo** … si yule mwandishi wa *Yakobo* … mwana wa Alfayo.
10. **Simoni Mkananayo** … awali alikuwa mpigania uhuru.
11. **Yuda / Thadayo** ... labda ni mwandishi wa kitabu cha *Yuda* ... mwana wa Yakobo.

12a. **Yuda Iskariote** … msaliti … daima aliorodheshwa wa mwisho katika wale 12 wa asili … hakuwa ameokoka, Yohana 6:70 na 17:12.

12b. Na baadaye, **Mathiya** … aliyechukua nafasi ya Yuda Iskariote, Matendo 1:15-26.

**Vifo vya Wanafunzi.** Yohana ndiye Mwanafunzi pekee aliyeishi hadi uzeeni. Inaaminika kuwa Yohana alikufa huko Efeso baada ya uhamisho wake huko Patmo. Inaaminika kwamba Wanafunzi wengine wote waliuawa kwa sababu ya imani yao kabla ya kifo cha Yohana.

**Mtume Paulo.** *Sauli* [jina lake la Kiebrania] pia aliitwa kwa jina lake la Kigiriki *Paulo*. Sauli hakubadilishwa jina na Yesu au na mtu mwingine yeyote. Katika Agano Jipya, aliitwa kwa majina yote mawili. Paulo alichaguliwa na Yesu kuwa Mtume … lakini hakuitwa kamwe kama mmoja wa Wanafunzi.

# CHATI YA MTIRIRIKO WA MAISHA YA KRISTO




Acts One Eight [Matendo Moja Nane] huchapisha tafsiri hii ya Kiswahili ya kozi ya lugha ya Kiingereza ya *Disciplemaking 1 … Abiding in His Word*. Unaweza kunakili kozi hii au sehemu yake yoyote bila malipo au kwa gharama ya usambazaji pekee, bila kubadilisha maudhui yake na ukiwa umeambatanisha taarifa hii ya chanzo. Kozi hii inapatikana bila malipo katika lugha ya Kiswahili kutoka katika www.Theolojia. org au katika lugha ya Kiingereza kutoka katika www.VIrtualBibleAcademy.org. Kwenye tovuti hizi, unaweza kusoma mtandaoni, kufundishwa, kupakua, au kuchapisha nakala zako mwenyewe. Nukuu za Biblia ya Kiswahili zimetoka katika Biblia ya Swahili Union Version (SUV) ya 1997.

# Somo la 5 - Maisha ya Kristo ... ukurasa wa 62 - 76

Sehemu ya kujifunza ni kufanya marudio … kuhifadhi maarifa mapya kwenye kumbukumbu yako ya muda mrefu. Chapisha mtihani huu wa marudio au tumia karatasi tofauti kujibu maswali yafuatayo. Kisha rudia mtihani huu, ukisoma maelezo ya kozi au bila kuyasoma, hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi.
*Mitihani hii ya marudio* pamoja na majibu sahihi yanapatikana kwenye www.Theolojia.org.

MAJIBU YA KUCHAGUA KWA SWALI LA 1-10

| | | |
|---|---|---|
| A. Galilaya | F. Perea | K. Malaika wa Bwana |
| B. Bethlehemu | G. Uru | L. Jangwa la Uyahudi |
| C. Nabii | H. Misri | M. Uumbaji |
| D. Juu ya Mlima Kalvari | I. Golgotha | N. Mfalme wa Wayahudi |
| E. Kabla ya uumbaji | J. Samaria | O. Kutembea juu ya maji |

1. Maisha ya Yesu Kristo yanaweza kufuatiliwa hadi ________.

2. Kitendo cha kwanza cha Yesu kilichonakiliwa kilikuwa ________.

3. Yesu alijitokeza mara kadhaa katika Agano la Kale kama ________.

4. Baada ya kuzaliwa Bethlehemu, Yesu aliishi kwa muda mfupi katika nchi ya ________.

5. Mara tu baada ya kubatizwa na Yohana, Yesu alikwenda katika ________.

6. Miezi ya mwanzo ya huduma yake ilifanyika katika Uyahudi na ________.

7. Vipindi vya katikati vya huduma yake vilifanyika kaskazini na mashariki mwa ________.

8. Huduma yake ya baadaye ya hadharani ilifanyika katika Uyahudi na ________.

9. Kuingia kwake kwa ushindi Yerusalemu kulimtangaza kuwa ________.

10. Yesu alisulubishwa ________.

JAZA MAPENGO KWA SWALI LA 11 - 20 UKITUMIA NAMBARI ZILIZO KATIKA ORODHA HII

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | 3 | 4 | 6 |
| 7 | 10 | 25 | 30 |
| 40 | 50 | 70 | 100 |
| 200 | 250 | 300 | 500 |

11. Kuna zaidi ya unabii ____________ katika Agano la Kale kuhusu Yesu.

12. Yesu alianza huduma yake ya hadharani akiwa na umri wa takriban miaka ____________.

13. Alijaribiwa na Shetani kwa siku ____________.

14. Yesu alipitia angalau kesi ____________ kabla ya kusulubishwa.

15. Mwili wa Yesu ulikuwa kaburini kwa siku ___________.

16. Baada ya kifo na ufufuo wake, alijitokeza angalau mara ___________.

17. Alijitokeza kwa umati mkubwa wa zaidi ya watu ___________.

18. Alijitokeza kwa muda wa siku ___________.

19. Agano Jipya linataja kurudi kwa Kristo zaidi ya mara __________.

20. Kurudi kwa Kristo kunatajwa katika Agano Jipya takriban mara moja kila baada ya mistari ___________.

21. Taja angalau Wanafunzi 6 kati ya wale 12 isipokuwa Petro na Yohana.

    1.

    2.

    3.

    4.

    5.

    6.

# Somo la 5 - Maisha ya Kristo … maswali ukurasa wa 77 - 78

Usitumie karatasi hizi za majibu kupata majibu yako. Tafadhali zitumie tu kukagua majibu yako. Rudi kwenye somo ili kupata taarifa za kurekebisha majibu yako. Rudia mtihani hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi. Masomo yote, mitihani ya marudio, na kurasa za majibu zinapatikana katika www.Theolojia.org.

MAJIBU YA KUCHAGUA KWA SWALI LA 1 - 10

| | | |
|---|---|---|
| A. Galilaya | F. Perea | K. Malaika wa Bwana |
| B. Bethlehemu | G. Uru | L. Jangwa la Uyahudi |
| C. Nabii | H. Misri | M. Uumbaji |
| D. Juu ya Mlima Kalvari | I. Golgotha | N. Mfalme wa Wayahudi |
| E. Kabla ya uumbaji | J. Samaria | O. Kutembea juu ya maji |

1. Maisha ya Yesu Kristo yanaweza kufuatiliwa hadi *E. Kabla ya uumbaji*.

2. Kitendo cha kwanza cha Yesu kilichonakiliwa *M. Uumbaji*.

3. Yesu alijitokeza mara kadhaa katika Agano la Kale kama *K. Malaika wa Bwana*.

4. Baada ya kuzaliwa Bethlehemu, Yesu aliishi kwa muda mfupi katika nchi ya *H. Misri*.

5. Mara tu baada ya kubatizwa na Yohana, Yesu alikwenda katika *L. Jangwa la Uyahudi*.

6. Miezi ya mwanzo ya huduma yake ilifanyika katika Uyahudi na *A. Galilaya*.

7. Vipindi vya katikati vya huduma yake vilifanyika kaskazini na mashariki mwa *A. Galilaya*.

8. Huduma yake ya baadaye ya hadharani ilifanyika katika Uyahudi na *F. Perea*.

9. Kuingia kwake kwa ushindi Yerusalemu kulimtangaza kuwa *N. Mfalme wa Wayahudi*.

10. Yesu alisulubishwa *I. Golgotha* .

JAZA MAPENGO KWA SWALI LA 11 - 20 UKITUMIA NAMBARI ZILIZO KATIKA ORODHA HII

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | 3 | 4 | 6 |
| 7 | 10 | 25 | 30 |
| 40 | 50 | 70 | 100 |
| 200 | 250 | 300 | 500 |

11. Kuna zaidi ya unabii __*300*__ katika Agano la Kale kuhusu Yesu.

12. Yesu alianza huduma yake ya hadharani akiwa na umri wa takriban miaka __*30*__.

13. Alijaribiwa na Shetani kwa siku __*40*__ .

14. Yesu alipitia angalau kesi __*6*__ kabla ya kusulubishwa.

15. Mwili wa Yesu ulikuwa kaburini kwa siku __*3*__.

16. Baada ya kifo na ufufuo wake, alijitokeza angalau mara __*10*__.

17. Alijitokeza kwa umati mkubwa wa zaidi ya watu __*500*__.

18. Alijitokeza kwa muda wa siku __*40*__.

19. Agano Jipya linataja kurudi kwa Kristo zaidi ya mara __*300*__.

20. Kurudi kwa Kristo kunatajwa katika Agano Jipya takriban mara moja kila baada ya vifungu __*25*__.

21. Taja angalau Wanafunzi 6 kati ya wale 12 isipokuwa Petro na Yohana.

| | | |
|---|---|---|
| *~~Petro~~* | *Filipo* | *Yakobo Mdogo* |
| *~~Yohana~~* | *Tomaso* | *Simoni Mkananayo* |
| *Yakobo* | *Nathanieli (Bartholomayo)* | *Yuda (Thadayo) mwana wa Yakobo* |
| *Andrea* | *Mathayo (Lawi)* | *Yuda Iskariote Mathiya* |

## Kufanya Wanafunzi 1 - Kudumu Katika Neno Lake

# SOMO LA 6 - AGANO JIPYA ... zaidi ya Vitabu vya Injili

*"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi."* Matendo 1:8

Wakati wa tukio la Kupaa katika Matendo 1, Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba watapokea nguvu Roho Mtakatifu atakapowashukia na kwamba watakuwa mashahidi, wakianzia pale walipokuwa Yerusalemu ... kisha wataenda katika maeneo jirani ya Uyahudi na Samaria ... kisha mpaka sehemu ya mbali zaidi za dunia. Walipokea nguvu siku ya Pentekoste katika Matendo 2 na wakawa mashahidi. Sehemu iliyosalia ya kitabu cha Matendo ya Mitume ilinakili kuenea kwa huduma yao hadi Yerusalemu, Uyahudi na Samaria, na katika ulimwengu wa Mataifa na hatimaye Rumi.

Petro na Mitume wengine walianzia Yerusalemu. Kanisa liliongezeka kwa kiasi kikubwa. Mateso makali, yaliyoanza na Stefano kupigwa mawe, yalisukuma kanisa la awali hadi Uyahudi, Samaria, na Galilaya. Kuongoka kwa Paulo katika barabara ya kwenda Dameski na maono ya Petro kulifungua mlango wa kupanuka ili kuwafikia watu wa Mataifa ... na hatimaye katika sehemu za mbali zaidi za dunia. Mtume Yakobo aliuawa.

*Safari ya kwanza ya umisionari* iliwasafirisha Paulo na Barnaba kutoka Antiokia hadi kusini mashariki mwa Asia Ndogo. Baada ya safari hii, wawili hao pamoja na Petro walihudhuria Baraza la Yerusalemu ambalo lilitambua kwamba Waumini wapya wa Mataifa hawakuhitaji kutahiriwa ili kuokolewa.

*Safari ya pili ya umisionari* iliwasafirisha Paulo na Sila kutoka Antiokia hadi Makedonia na Ugiriki wakiambatana na Luka na Timotheo. Kwa sababu ya kutoelewana na Paulo, Barnaba alimchukua Yohana Marko katika safari yao wenyewe ya umisionari hadi katika kisiwa cha Kipro.

*Safari ya tatu ya umisionari* iliwasafirisha Paulo na wenzake kutoka Antiokia wakipitia Asia Ndogo ya magharibi. Mwishoni mwa safari hiyo, walirudi Yerusalemu. Paulo alikamatwa huko na akafungwa katika mji wa Kaisaria. Hiyo ilimpa Paulo nafasi ya kuwatangazia Injili Magavana Feliki na Festo ... na Mfalme Agripa.

Akikata rufaa ili kesi yake isikizwe mbele ya Kaisari, Paulo alisafiri kwa meli akiwa mfungwa hadi Rumi katika *safari yake ya nne ya umisionari*. Meli hiyo ilivunjika baharini ... na hiyo ikampa fursa ya kuhudumu katika Kisiwa cha Malta.

Wakati wa kifungo chake cha kwanza huko Rumi, Paulo alihudumia watu wengi akiwa chini ya kifungo cha nyumbani kwa miaka miwili. Aliachiliwa na akatembelea tena makanisa. Paulo alikamatwa mara ya pili na kufungwa katika gereza la Kirumi. Kisha akauawa.

Baada ya Yerusalemu kuharibiwa mwaka wa 70 BK, mtume Yohana alihamia Efeso kisha akapelekwa uhamishoni katika kisiwa cha Patmo ambako aliandika kitabu cha Ufunuo.

## VITABU 27 VYA AGANO JIPYA ... 5 - 9 - 4 - 9

Vitabu vya Agano Jipya vimepangwa katika mpangilio unaoeleweka kwa urahisi. Kuna vitabu vitano vya historia, Injili na Matendo ... nyaraka tisa ambazo Paulo aliandikia makundi ya watu ... nyaraka nne ambazo Paulo aliwaandikia watu binafsi ... na hatimaye vitabu tisa vilivyoandikiwa na waandishi wengine. [ 5 - 9 - 4 - 9 ]

### Vitabu 5 vya historia

Vitabu vinne vya kwanza vya Agano Jipya vinazungumzia maisha ya Yesu Kristo. Kisha masimulizi ya Luka yaendelezwa katika kitabu cha Matendo. Kitabu hiki cha tano cha historia kinanakili kile Yesu aliendelea kufanya kupitia wafuasi wake baada ya Kupaa.

### 9 Nyaraka za Paulo kwa makundi ya watu

Paulo aliandikia makanisa mapya nyaraka tisa ili kuwatia moyo, kuwafundisha na kuwarekebisha. Wakati wa safari zake za umisionari, aliandika Wagalatia, 1 na 2 Wathesalonike, Warumi, na 1 na 2 Wakorintho. Baada ya safari hizo, wakati wa kifungo chake cha kwanza huko Rumi, aliandika Waefeso, Wakolosai, na Wafilipi. Vitabu hivi tisa vimepewa majina kulingana na wapokeaji wa nyaraka husika.

### 4 Nyaraka za Paulo kwa watu binafsi

Paulo pia aliandika nyaraka nne kwa watu binafsi. Wakati wa kifungo chake cha kwanza huko Rumi, alimwandikia Filemoni, ndugu katika kanisa la Kolosai. Baada ya kuachiliwa kwake aliwaandikia viongozi wawili wa kanisa . . . Timotheo huko Efeso kisha Tito huko Krete. Kisha wakati wa kifungo chake cha mwisho huko Rumi, kabla tu ya kifo chake, Paulo aliandika waraka wake wa mwisho . . . kwa Timotheo. Vitabu hivi vinne vimepewa majina kulingana na wapokeaji wa nyaraka husika.

### 9 Vitabu vilivyoandikwa na waandishi wengine

Yakobo [kaka wa kambo wa Yesu] na mwandishi asiyejulikana wa Waebrania kila mmoja aliandika waraka kwa Waumini wa Kiyahudi. Vitabu saba vilivyobaki vinajumuisha viwili vya mtume Petro, vitatu vya mtume Yohana, kimoja cha Yuda [kaka wa kambo wa Yesu], na Ufunuo wa kinabii wa mtume Yohana juu ya Yesu Kristo.

## MPANGILIO WA AGANO JIPYA … 5 - 9 4 - 9

**5** Vitabu vya Historia

Mathayo
Marko
Luka
Yohana
Matendo

**9** Nyaraka za Paulo kwa makundi ya watu

Warumi
1 Wakorintho
2 Wakorintho
Wagalatia
Waefeso
Wafilipi
Wakolosai
1 Wathesalonike
2 Wathesalonike

**4** Nyaraka za Paulo kwa watu binafsi

1 Timotheo
2 Timotheo
Tito
Filemoni

**9** Vitabu vilivyoandikwa na wengine

Waebrania
Yakobo
1 Petro
2 Petro
1 Yohana
2 Yohana
3 Yohana
Yuda
Ufunuo

**27** Vitabu Vyote

## KITABU CHA MATENDO - MUHTASARI WA HISTORIA YA AGANO JIPYA

**Mwandishi.** Luka alikuwa mtu wa Mataifa, Mgiriki, tabibu, mwanahistoria wa kanisa la awali, na mmisionari. Alikuwa mwenza wa Paulo awali tangu katika safari ya pili ya umisionari ... na baadaye wakati wa kifungo cha pili cha Paulo huko Rumi. Luka aliandika sehemu kubwa zaidi ya Agano Jipya kuliko mtu mwingine yeyote tukichukulia kwamba Paulo hakuandika Waebrania.

**Kitabu cha Matendo** ni mwendelezo wa Injili ya Luka ... na ni kumbukumbu ya utiifu wa Mitume kwa Agizo Kuu. Baada ya Kupaa kwa Kristo katika Matendo 1 na ujio wa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste katika Matendo 2, Mitume walianza kazi. Matendo 2-7 inarekodi huduma yao huko Yerusalemu ambako maelfu ya watu walimwamini Yesu.

Mateso, yaliyoanza na Stefano kupigwa mawe, yaliwalazimisha Wakristo wa awali waondoke Yerusalemu na waende Uyahudi, Samaria, na Galilaya. Linganisha Matendo 1:8 na Matendo 8:1. Mtesi Sauli aliongoka kwenye barabara ya kwenda Dameski ... na mlango wa kuipeleka Injili hadi sehemu za mbali zaidi za dunia ukaanza kufunguka. Maono ya Petro yalifungua mioyo ya Mitume kupeleka Injili kwa Mataifa. Sauli akawa Mtume mkuu Paulo, Mtume kwa Mataifa. Aidha, Mtume Yakobo aliuawa.

*Safari ya kwanza ya umisionari* ya Paulo ilimpeleka yeye na Barnaba katika eneo la Kusini mashariki mwa Asia Ndogo. Mzozo kuhusu waongofu wa Mataifa ukazuka. Paulo na Barnaba walihudhuria baraza pamoja na Petro huko Yerusalemu ili kutatua tatizo hilo. Ukweli ulitambuliwa kwamba Waumini wapya wa Mataifa hawakupaswa kutahiriwa ili kuokolewa ... na kanuni hiyo potovu ikaepukwa. Paulo na Sila waliondoka Antiokia kwenda katika *safari ya pili ya umisionari* ... hadi Makedonia na Ugiriki. Luka na Timotheo walikuwa pamoja nao. Barnaba na Yohana Marko walitengana nao mwanzoni mwa safari hiyo ili kupeleka Injili kwenye kisiwa cha Kipro. *Safari ya tatu ya umisionari* ya Paulo ilimpeleka yeye na wenzake kwenye eneo la magharibi mwa Asia Ndogo. Kisha wakarudi Yerusalemu.

Paulo alikamatwa Yerusalemu ... kisha akazuiliwa mjini Kaisaria. Akiwa amezuiliwa huko, aliwatangazia Habari Njema magavana Feliki na Festo na Mfalme Agripa. Paulo alitumia haki yake kama raia wa Rumi kukata rufaa ili kesi yake isikizwe mbele ya Kaisari. Hiyo ilimfanya asafiri kwenda Rumi ... ambayo ilikuwa *safari yake ya nne ya umisionari*. Akiwa njiani kuelekea Rumi meli ilivunjika baharini karibu na Kisiwa cha Malta, na hiyo ikampa fursa ya kuhudumu huko. Hatimaye huko Rumi, aliwekwa katika kifungo cha nyumbani kwa miaka miwili katika nyumba ya kupangisha. Umati mkubwa wa watu ulienda kwake, na akawaeleza juu ya Ufalme wa Mungu na habari za Yesu. Na baadhi ya watu waliamini.

**Zaidi ya kitabu cha Matendo**. Paulo aliachiliwa kutoka gerezani na akahudumu kwa miaka michache kabla ya kutiwa gerezani huko Rumi. Inaonekana aliuawa katikati hadi mwishoni mwa miaka ya 60 BK. Huduma ya Mtume Yohana iliendelea hata baada ya Mitume wengine kufa. Yerusalemu ilipoharibiwa mwaka wa 70 BK, Yohana alihamia Efeso ambako aliandika Yohana wa 1, wa 2, na wa 3. Alipokuwa uhamishoni kwenye Kisiwa cha Patmo, aliandika Ufunuo.


## MATENDO ... KUPANUKA KWA KANISA LA AWALI


*“Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.”* Matendo 1:8

| | |
|---|---|
| **Matendo 1** | Kupaa ... Yesu alikwenda Mbinguni. |
| **Matendo 2** | Pentekoste ... Roho Mtakatifu alishuka.<br>*“Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu...”* |
| **Matendo 3-6** | Kanisa lilienda Yerusalemu.<br>*“nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu…”* |
| **Matendo 7** | Stefano alitoa ujumbe wake na akauawa. |
| **Matendo 8** | Kanisa lilienda Uyahudi na Samaria.<br>*“katika Uyahudi wote, na Samaria…”* |
| **Matendo 9-12** | Paulo aliongoka, Petro alipata maono, Yakobo aliuawa. |
| **Matendo 13-14** | Safari ya kwanza ya umisionari ya Paulo ... kwenda eneo la kusini mashariki mwa Asia Ndogo. |
| **Matendo 15** | Baraza la Yerusalemu kuhusu tohara ilidumisha usafi wa Injili. |
| **Matendo 15:36** | Safari ya pili ya umisionari ya Paulo ... kwenda Makedonia na Ugiriki. |
| **Matendo 18:23** | Safari ya tatu ya umisionari ya Paulo ... kwenda Asia Ndogo magharibi. |
| **Matendo 21:17** | Paulo alikamatwa Yerusalemu na kufungwa Kaisaria. |
| **Matendo 27-28** | Safari ya nne ya umisionari ya Paulo ... kwenda Malta na Rumi |


*“…na hata mwisho wa nchi.”* Matendo 1:8.


## SAFARI YA PAULO YA KWANZA NA YA PILI YA UMISIONARI



## SAFARI YA PAULO YA TATU NA YA NNE YA UMISIONARI



## NYARAKA ZA PAULO KWA MAKUNDI YA WATU

**Mwandishi.** Sauli wa Tarso alikuwa Myahudi aliyesoma sana, Mfarisayo wa kabila la Benyamini. Alikuwa raia wa Rumi kwa kuzaliwa. Mtesi huyu wa kanisa la awali aliongoka baada ya tukio alilopitia katika barabara ya kwenda Dameski. Pia anajulikana kama Paulo [jina lake la Kigiriki] kuanzia Matendo 13:9 na kuendelea, akawa mmisionari kwa Mataifa na mwandishi wa vitabu 13 vya Agano Jipya.

**Warumi -** Paulo aliandika waraka huu kwa *wote walioko Rumi, wapendwao na Mungu.* Aliwaandikia kabla ya kutembelea jiji lao kuu. Waraka huu uliandikwa kutoka Korintho, karibu na mwisho wa safari ya tatu ya umisionari katikati ya miaka ya 50 BK. Kitabu cha Warumi ndio waraka wa kikanuni na wa kirasmi zaidi kati ya nyaraka za Paulo. Aliandika ukweli wa kina wa msingi unaoshughulikia mada za dhambi [sura 1-3] ... wokovu [sura 3-5] ... utakaso [sura ya 6-8] ... mamlaka ya Mungu [sura 9-11] ... na huduma [sura 12-16].

**1 Wakorintho -** Waraka huu uliandikiwa *kanisa la Mungu lililoko Korintho*. Ni kanisa lililoanzishwa katika safari ya pili ya umisionari ya Paulo. Kanisa hilo lilikuwa linakumbwa na matatizo likiwa katika jiji hilo la bandari lililokuwa na uovu mwingi. Paulo aliwaandikia kutoka Efeso wakati wa safari yake ya tatu ya umisionari katikati ya miaka ya 50 BK. Uovu wa Korintho ulikuwa umeingia ndani ya kanisa lao. Paulo aliandika kuhusu migawanyiko, uasherati, kushtakiana kotini, ndoa, chakula, Meza ya Bwana, na matumizi ya karama za kiroho. Sura ya 15 inatoa mafundisho ya kina kuhusu umuhimu wa Ufufuo wa Yesu.

**2 Wakorintho -** Inaonekana Waumini wa Korintho hawakuitikia vyema waraka wa kwanza wa Paulo. Akafunga safari kwenda kuwaona. Na akawaandikia waraka mwingine mkali wa kuwarekebisha. Waraka huo haujajumuishwa katika Biblia. Kufuatia toba ya watu wengi, Paulo aliandika waraka mwingine, 2 Wakorintho, wakati wa safari yake ya tatu ya umisionari katikati ya miaka ya 50 BK. Aliuandika akiwa mahali fulani huko Makedonia. Paulo aliandika kuhusu furaha yake kwamba walikuwa wametubu ... alitetea tabia yake na huduma yake ... alifundisha kuhusu kutoa ... na alitetea mamlaka yake kama Mtume.

**Wagalatia -** Paulo aliandika waraka huu kwa makanisa ya *Galatia* [yaani jimbo si mji mmoja tu]. Alikuwa amewatembelea katika safari yake ya kwanza au ya pili ya umisionari. Hata hivyo, tarehe na mahali ambapo waraka huu uliandikwa havijulikani. Waumini wa Galatia walikuwa wamepotoshwa katika kujumuisha sheria [matendo mema] katika wokovu. Paulo aliwasilisha kwa nguvu kanuni ya wokovu kwa imani pekee. Alionya dhidi ya hatari ya kutii sheria ili kupata wokovu. Pia alionya dhidi ya utumizi mbaya wa uhuru ... alipokuwa akieleza kuhusu uhuru wa Kikristo.

**Waefeso -** Waraka huu ulitumwa kwa *watakatifu walioko Efeso*. Paulo alikuwa huko katika safari yake ya kwanza na ya tatu ya umisionari. Aliwaandikia waraka huu wakati wa kifungo chake cha kwanza mjini Rumi mwanzoni mwa miaka ya 60 BK. Paulo alieleza utajiri wa kiroho wa Waumini ... wamechaguliwa, wametiwa muhuri, wameokolewa kwa neema, na wameunganishwa katika Mwili mmoja wa Waumini. Kisha akawahimiza waenende kama inavyoustahili wito wao uliotoka mbinguni na nafasi waliyopewa katika Mwili. Alieleza jinsi ya kumfuata Mungu katika maisha, katika kukataa dhambi, katika Roho, nyumbani, kazini, na katika vita.

**Wafilipi -** Paulo aliwaandikia watakatifu wote katika Kristo Yesu walioko Filipi. Alikuwa ameenda Filipi wakati wa safari yake ya pili ya umisionari. Aliwaandikia akiwa katika kifungo chake cha pili mjini Rumi katikati ya miaka ya 60 BK. Paulo alieleza shukrani zake kwa ajili ya ushuhuda wao thabiti ... na kwa ajili ya msaada wao kwa huduma yake. Aliwahimiza wawe na amani ... wawe wanyenyekevu kama Kristo ... wawe macho ... na wawe na furaha.

**Wakolosai -** Paulo aliwaandikia *watakatifu na ndugu waaminifu katika Kristo walioko Kolosai*. Epafra, mwongofu wakati wa huduma ya Paulo huko Efeso, alileta Ukristo Kolosai. Filemoni alikuwa sehemu ya kanisa lao. Waraka huu uliandikwa wakati wa kifungo cha kwanza cha Paulo mjini Rumi mwanzoni mwa miaka ya 60 BK. Alisisitiza uungu na ukuu wa Kristo ili kurekebisha athari ya mafundisho ya uwongo yaliyojumuishwa katika Ukristo ... ambayo yalikuwa yameleta ndani ya kanisa shawishi mbaya za kutii sheria ili kupata wokovu, falsafa, na mafundisho ya kimafumbo. Paulo aliandika kwamba Kristo ndiye mkuu zaidi [sura 1-2] na hivyo, Waumini wanapaswa kutafuta yaliyo juu na kuishi ipasavyo [sura 3-4].

**1 Wathesalonike -** Paulo aliandikia *kanisa la Wathesalonike* ambalo lilianzishwa wakati wa safari yake ya pili ya umisionari. Mateso yalikuwa yamemlazimisha Paulo kuwaacha, Matendo 17:1–10. Aliandika akiwa Korintho mwanzoni mwa miaka ya 50 BK. Maelezo ya kibinafsi ya Paulo kuhusu huduma yao na kuhusu huduma yake mwenyewe yalitoa mifano ya mwenendo unaomstahili Mungu anayemwita kila muumini. Aliwasihi kustahimili majaribu ya ngono ... kuishi maisha ya utulivu ... kufanya kazi ... kuwa na amani kuhusu kurudi kwa Kristo ... na kutimiza wajibu wao kwa viongozi wa kiroho, katika tabia, na katika ibada.

**2 Wathesalonike -** Paulo aliandika waraka huu wa pili kwa *kanisa la Wathesalonike* muda mfupi baada ya waraka wake wa kwanza ... akiwa Korintho mwanzoni mwa miaka ya 50 BK. Aliwatia moyo katika kukua na katika kuvumilia chini ya mateso. Baadhi yao walikuwa wameelewa vibaya mafundisho yake kuhusu kurudi kwa Kristo na walikuwa wameacha kazi zao, wakifikiri Siku ya Bwana ilikuwa imewadia. Paulo aliandika kuhusu matukio yatakayotokea ya siku za mwisho. Aliwaamuru wafanye kazi ikiwa wanatarajia kula ... wakifanya kazi na kungoja huku wakiishi maisha matakatifu.

## NYARAKA ZA PAULO KWA WATU BINAFSI

**Paulo na watu.** Nyaraka za Paulo zilifuata muundo wa msingi. Kwanza, aliwasilisha wasiwasi na salamu zake binafsi. Kisha alifundisha ukweli wa kiroho. Kisha alifundisha matumizi ya ukweli huo. Alihitimisha kwa maoni ya kibinafsi. Kujitolea kwa Paulo kwa ukweli wa Mungu kulienda sambamba na jinsi alivyowajali watu. Aliwasilisha ukweli ... kisha akawafundisha kuishi kulingana na ukweli huo. Hata katika Warumi, waraka wake wa kirasmi na wa mafundisho zaidi, alitumia sura nzima [16] kuwasilisha salamu na wasiwasi wake wa kibinafsi. Paulo alijitolea kwa mambo matatu maishani ambayo yanadumu milele . . . Mungu, Neno la Mungu, na watu. Nyaraka nne zinazoelezwa katika sehemu hii zinazingatia kimahususi wasiwasi wake juu ya Timotheo, Tito, Filemoni, na Onesimo, mtumwa wa Filemoni aliyetoroka.

**1 Timotheo -** Paulo alimwandikia Timotheo kama *mwanangu hasa katika imani*. Timotheo alikuwa mwana wa baba Mgiriki na mama Myahudi ... na alihusishwa na Paulo kuanzia safari ya pili ya umisionari. Paulo alimwacha Timotheo katika mji wa Efeso ili asimamie huduma huko. Waraka huu uliandikwa mwanzoni mwa miaka ya 60 BK baada ya kifungo cha kwanza cha Paulo mjini Rumi. Paulo alimwagiza na kumhimiza Timotheo awe kiongozi bora. Mada nyingi zinashughulikiwa . . . sala, wanawake katika kanisa, viongozi, hatari na kujilinda, wanaume na wanawake wazee, wajane, wazee wa kanisa, mabwana na watumwa, walimu wa uwongo na pesa. Paulo alimhimiza Timotheo *kupiga vile vita vizuri vya imani.*

**2 Timotheo -** Paulo aliandika waraka huu wa mwisho katikati hadi mwishoni mwa miaka ya 60 BK akiwa katika kifungo chake cha pili mjini Rumi. Aliuandika muda mfupi kabla ya kifo chake. Huu ni waraka wa kibinafsi sana kutoka kwa Paulo kwa *mwanawe mpendwa* Timotheo. Paulo alimhimiza Timotheo awe hodari . . . asione haya . . . ahudumu kwa uaminifu . . . asimame imara dhidi ya kuasi imani kunakokuja … afanye kazi ya mwinjilisti . . . na atimize huduma yake.

**TITO -** Paulo alimwandikia Tito, *mwanangu hasa katika imani tuishirikiyo*, katikati ya miaka ya 60 BK baada ya kifungo chake cha kwanza mjini Rumi. Alimwacha Tito huko Krete *ayatengeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji*. Paulo alimhimiza Tito atekeleze kazi hiyo. Paulo alimfundisha Tito kuhusu wazee wa kanisa ... kuhusu watu waasi, wadanganyifu, wenye mazungumzo yasiyo na maana ... na kuhusu wanaume wazee, wanawake wazee, wanaume vijana, wanawake vijana, na watumwa. Aliandika kuhusu kutii serikali, kujali watu wote, walimu wa uwongo, na wokovu unaotoa watu wenye bidii kwa ajili ya matendo mema.

**FILEMONI -** Paulo aliandika waraka huu mwanzoni mwa miaka ya 60 BK wakati wa kifungo chake cha kwanza mjini Rumi. Ni ombi la kibinafsi la Paulo kwa rafiki yake Filemoni aliyeishi Kolosai. Mtumwa Onesimo alikuwa amemtoroka bwana wake Filemoni. Onesimo alimwamini Kristo kupitia huduma ya Paulo wakati Paulo alikuwa gerezani huko Rumi. Paulo alimrudisha muumini huyo mpya kwa bwana wake na ombi hili la kibinafsi la msamaha wa mtumwa ambaye amekuwa ndugu mpendwa. Paulo alijitolea kulipa chochote ambacho Onesimo alidaiwa.

## MATUKIO MUHIMU KATIKA MAISHA YA PAULO

| | Umri wa Paulo | Rejeleo |
|---|---|---|
| Stefano akipigwa mawe | miaka ya katikati ya 30 | Matendo 7-8 |
| Akilitesa Kanisa la Awali | | Matendo 8 |
| Kupofushwa njiani akielekea Dameski | | Matendo 9 |
| Kuongoka na kuponywa | | Matendo 9 |
| Pamoja na Mitume Yerusalemu | | Matendo 9 |
| Kutishiwa maisha – kutoroshwa hadi Tarso | | Matendo 9 |
| … *p e n g o* … | | Wagalatia 1:17 - 2:1 |
| Kuchukuliwa na Barnaba | mwanzoni mwa miaka ya 40s | Matendo 11 |
| Kubeba pesa hadi Yerusalemu | miaka ya katikati ya 40s | Matendo 11 |
| Kuteuliwa huko Antiokia | | Matendo 12-13 |
| Safari ya 1 ya umisionari | mwishoni mwa miaka ya 40s | Matendo 13-14 |
| Safari ya 2 ya umisionari | mwanzoni mwa miaka ya 50s | Matendo 15-18 |
| Safari ya 3 ya umisionari | miaka ya katikati ya 50s | Matendo 18-21 |
| Kukamatwa Yerusalemu | mwishoni mwa miaka ya 50s | Matendo 21-23 |
| Kuzuiliwa huko Kaisaria | takriban miaka 60 | Matendo 23-26 |
| Kusafiri kwa meli hadi Rumi na meli kuvunjika Malta | takriban miaka 60 | Matendo 27-28 |
| Kifungo vha nyumbani huko Rumi | mwanzoni mwa miaka ya 60s | Matendo 28 |
| Kuachiliwa kuhudumu | katikati ya miaka ya 60s | baada ya Matendo |
| Gerezani huko Rumi | mwishoni mwa miaka ya 60s | baada ya Matendo |
| Kuuawa na Nero | takriban miaka 70? | baada ya Matendo |

## VITABU 9 VILIVYOANDIKWA NA WAANDISHI WENGINE 5

**Waandishi.** Wanaume watano waliandika vitabu tisa vya mwisho vya Agano Jipya. Utambulisho wa mwandishi wa Waebrania haujulikani kwetu. Yamkini haikuwa Paulo kwa sababu maudhui ya Waebrania ni ya Kiyahudi zaidi tofauti na nyaraka za Paulo ... na kwa sababu inatumia msamiati tofauti na ni tofauti na maandishi ya Paulo kimuundo. Yamkini Waebrania iliandikwa na Luka, Barnaba, au Sila. Yakobo [si yule mtume] na Yuda walikuwa kaka wa kambo wa Yesu ... kila mmoja aliandika waraka mmoja. Petro, mvuvi aliyegeuka kuwa mfuasi, aliandika nyaraka mbili. Yohana, mvuvi na *mwanafunzi ambaye Yesu alimpenda*, aliandika nyaraka zake tatu na Ufunuo [kitabu cha mwisho cha kinabii cha Biblia].

**Waebrania -** Waraka huu uliandikiwa Waumini wa Kiyahudi yamkini katikati hadi mwishoni mwa miaka ya 60 BK. Mwandishi, mahali ulipoandikiwa, na wasomaji wa asili hawajulikani leo. Mada yake ni kwamba Kristo aliye mkuu zaidi anatupa maisha bora zaidi katika Kristo. Yesu anaonyeshwa kuwa bora kuliko manabii ... bora kuliko malaika ... bora kuliko Musa ... bora kuliko Yoshua ... na bora kuliko makuhani Walawi. Kuhani huyu mkuu zaidi wa milele alitoa dhabihu ya kiwango cha juu zaidi. Zaidi ya hayo, alitupatia uzima wa milele ulio bora zaidi pamoja naye.

**Yakobo -** Kitabu hiki kiliandikiwa *yale makabila kumi na mawili* [Makabila ya Wayahudi] *waliotawanyika.* Ni kitabu cha kwanza cha Agano Jipya, kilichoandikwa mwishoni mwa miaka ya 40 BK. Yakobo aliandika maagizo ya kiutendaji ya maisha ya kila siku ya Kikristo. Alizungumzia majaribu ... kuwa mtendaji wa Neno ... kutoonyesha upendeleo wa kibinafsi ... na kugeuza imani kuwa matendo. Pia alitoa maagizo kuhusu matumizi ya ulimi ... kutumia hekima kutoka juu ... na kutopenda mambo ya kidunia. Yakobo alitamatisha waraka wake, akionyesha nguvu ya sala.

**1 Petro na 2 Petro -** Nyaraka hizi mbili, zilizoandikwa katikati ya miaka ya 60 BK, zinashughulikia matatizo na hatari zinazowakabili Wakristo. Upinzani wa nje dhidi ya Mwili unaelezwa katika 1 Petro na 2 Petro inazungumzia upinzani kutoka ndani ya Mwili.

> Katika 1 Petro, Petro alionyesha kwamba wokovu hutoa tumaini jipya tunapokabiliwa na mateso kutoka nje. Aliwahimiza wasomaji wake, *"Vifungeni viuno vya nia zenu, na kuwa na kiasi; mkiitumainia kwa utimilifu ile neema mtakayoletewa katika ufunuo wake Yesu Kristo."* Aliendelea na mafundisho katika utakatifu, kumcha Mungu, kupendana, kukua, kunyenyekea, kuteseka, na utumishi.
>
> Katika 2 Petro, alishughulikia tatizo la upinzani kutoka *ndani*. Alitilia mkazo hitaji la ukuaji unaoendelea uliokita mizizi katika Yesu Kristo na Neno la Mungu. Aliandika dhidi ya walimu wa uwongo ... akiwakumbusha wasomaji kuwatarajia walimu wa uwongo katika siku za mwisho kabla ya kurudi kwa Yesu Kristo. Petro aliwahimiza kutazamia kurudi kwa Yesu kulikoahidiwa na kuwa na bidii ya kupatikana watakatifu wakati atakaporudi.

**VITABU 9 VILIVYOANDIKWA NA WAANDISHI WENGINE 5 … mwendelezo**

**1 Yohana -** Kitabu hiki kinaeleza kwamba Waumini wanaweza kujua kwamba wana uzima wa milele. Yohana aliandika kwamba Waumini wanapaswa kuishi katika nuru badala ya giza ... katika msamaha na utiifu badala ya dhambi ... katika upendo badala ya chuki ... na katika uhakikisho badala ya hofu. Nyaraka za Yohana ziliandikwa takriban mwaka 90 BK ... yamkini akiwa Efeso.

**2 Yohana -** Ujumbe huu mfupi kwa *mwanamke mteule na watoto wake,* uliwahimiza kupendana ... kutii amri za Mungu ... na kuwa macho dhidi ya walimu wa uwongo, na kutowaonyesha ukarimu.

**3 Yohana -** Huu ni ujumbe kwa Gayo rafiki ya Yohana. Yohana alizungumza kuhusu ripoti nzuri ambayo alikuwa amepokea juu ya Gayo. Yohana pia aliandika shutuma kali dhidi ya Diotrefe.

**Yuda -** Waraka huu uliandikwa kati ya miaka ya 60 na 70 BK. Waraka huu mfupi ulikuwa wito wenye nguvu wa *kuishindania imani* kwa sababu ya hatari kutoka kwa walimu wa uwongo. Yuda aliandika kwamba kuna *watu waliojiingiza kwa siri* … na ni *miamba yenye hatari* ... wanung'unikaji, wenye tamaa, wenye kiburi, na wenye kusifu ili wajifaidi wenyewe. Walimu wa uwongo kama hao wanapaswa kutarajiwa katika siku za mwisho. Yuda aliwahimiza Waumini waenende kwa utiifu.

**Ufunuo -** Kitabu cha mwisho cha Yohana ndicho kitabu cha mwisho cha Agano Jipya. Alikiandika wakati wa uhamisho wake kwenye Kisiwa cha Patmo katika miaka ya 90 BK. Muhtasari wa kitabu ni, *“Mambo hayo uliyoyaona, nayo yaliyopo, na yale yatakayokuwa baada ya hayo,”* Ufunuo 1:19. Sura ya kwanza inazungumzia, *“Mambo hayo uliyoyaona.”* Kisha, *“nayo yaliyopo”* yanazungumziwa katika nyaraka kwa makanisa saba katika sura ya 2 na ya 3. Kisha sura ya 4-22 zinazungumzia *“yale yatakayokuwa baada ya hayo.”* Katika sura hizi za baadaye, Yohana aliandika kuhusu Kiti cha Enzi na Kitabu kilicho Mbinguni, mihuri saba, baragumu saba, na vitasa saba vya hukumu. Sura hizi zinaeleza kurudi kwa Kristo, Milenia, Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi, na Mbingu Mpya na Dunia Mpya. Katika mistari ya mwisho ya Ufunuo maneno ya Yesu yanatuambia, *“Tazama, naja upesi.”* Naye Yohana akaongeza “Amina” yake na sala, *“Na uje, Bwana Yesu.”*

**VITABU VINGINE …** Hakuna vitabu vingine vya kidini vilivyoandikwa leo au nyakati za awali vina pumzi ya Mungu kama vitabu 66 vya Agano la Kale na Agano Jipya. Hakuna maandishi mengine ya kidini, ya Kikristo au mengine, yanalingana na Biblia au ni bora kuliko Biblia. Na kanisa lolote au kiongozi yeyote wa kanisa anayetangaza jambo lolote kinyume na Biblia haneni kwa niaba ya Mungu. Watu kama hao wanapaswa kuzingatia onyo hili kutoka kwa Yesu, *“Isaya alitabiri vema juu yenu ninyi wanafiki, kama ilivyoandikwa, ‘Watu hawa huniheshimu kwa midomo ila mioyo yao iko mbali nami; nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu, ninyi mwaiacha amri ya Mungu, na kuyashika mapokeo ya wanadamu. Akawaambia, Vema! Mwaikataa amri ya Mungu mpate kuyashika mapokeo yenu,”* Marko 7:6-8.

# CHATI YA MTIRIRIKO WA AGANO JIPYA




Acts One Eight [Matendo Moja Nane] huchapisha tafsiri hii ya Kiswahili ya kozi ya lugha ya Kiingereza ya *Disciplemaking 1 … Abiding in His Word*. Unaweza kunakili kozi hii au sehemu yake yoyote bila malipo au kwa gharama ya usambazaji pekee, bila kubadilisha maudhui yake na ukiwa umeambatanisha taarifa hii ya chanzo. Kozi hii inapatikana bila malipo katika lugha ya Kiswahili kutoka katika www.Theolojia. org au katika lugha ya Kiingereza kutoka katika www.VIrtualBibleAcademy.org. Kwenye tovuti hizi, unaweza kusoma mtandaoni, kufundishwa, kupakua, au kuchapisha nakala zako mwenyewe. Nukuu za Biblia ya Kiswahili zimetoka katika Biblia ya Swahili Union Version (SUV) ya 1997.

# Somo la 6 - Agano Jipya ... ukurasa wa 81 - 93

Sehemu ya kujifunza ni kufanya marudio … kuhifadhi maarifa mapya kwenye kumbukumbu yako ya muda mrefu. Chapisha mtihani huu wa marudio au tumia karatasi tofauti kujibu maswali yafuatayo. Kisha rudia mtihani huu, ukisoma maelezo ya kozi au bila kuyasoma, hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi.
*Mitihani hii* ya marudio pamoja na majibu sahihi yanapatikana kwenye www.Theolojia.org.

MAJIBU YA KUCHAGUA ILI KUKAMILISHA KAULI ZOTE 1-19 HAPA CHINI

| | | |
|---|---|---|
| Antiokia | Krete | Patmo |
| Kupaa | Kanisa la Awali | Kuteswa |
| Ubatizo | Misri | Nguvu |
| Walibatizwa | Galilaya | Mwisho wa nchi |
| Biblia | Maagizo | Ufufuo |
| Kaisaria | Yerusalemu | Rumi |
| Tohara | Uyahudi na Samaria | Kusini mashariki mwa Asia Ndogo |
| Uwanja wa michezo | Makedonia na Ugiriki | Asia Ndogo ya Magharibi |
| Korintho | Malta | Mashahidi |

1. Kitabu cha Matendo kinaanza na ______________________________.

2. Wakati huo, Yesu aliwaambia wanafunzi kwamba watapokea _________________.

3. Wakati huo, Yesu aliwaambia wanafunzi kwamba watakuwa _________________.

4. Yesu alisema kwamba watafanya hivyo kuanzia ________________________.

5. … *na* kisha katika _________________________________________.

6. … *na* hatimaye katika _________________________________________.

7. Matendo inanakili kuenea kwa Injili kuanzia _______________________________.

8. … na kisha katika ___________________________________________.

9. … na hatimaye katika ______________________________________________.

10. Matendo inafikia tamati Paulo akiwa katika nyumba ya kukodisha huko ______________________.

11. Safari ya Kwanza ya Umisionari ya Paulo ilipitia ___________________________.

12. Petro na Paulo walisuluhisha mzozo wa mapema kwenye Baraza huko ____________________________.

13. … ambapo walijadili wokovu na _____________________________.

14. Safari ya Pili ya Umishonari ya Paulo iliingia ___________________________.

15. Meli ambayo Paulo alikuwa akisafiria ilivunjika katika Kisiwa cha __________________________.

16. Safari ya Tatu ya Umisionari ya Paulo iliingia ______________________________.

17. Paulo aliwahubiria Feliki na Festo alipokuwa kifungoni huko _________________.

18. Paulo alitiwa gerezani mara mbili huko ____________________.

19. Mtume Yohana alihamishwa kwenye Kisiwa cha ___________________.

20. Jibu la swali hili ni nambari.

    Je, ni jibu gani kati ya 11-19 halifuati jinsi matukio yalivyofuatana katika wakati? _____________________________________.

# Somo la 6 - Agano Jipya … maswali ukurasa wa 94 - 95

Usitumie karatasi hizi za majibu kupata majibu yako. Tafadhali zitumie tu kukagua majibu yako. Rudi kwenye somo ili kupata taarifa za kurekebisha majibu yako. Rudia mtihani hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi. Masomo yote, mitihani ya marudio, na kurasa za majibu zinapatikana katika www.Theolojia.org.

MAJIBU YA KUCHAGUA ILI KUKAMILISHA KAULI ZOTE 1-19 HAPA CHINI

| | | |
|---|---|---|
| Antiokia | Krete | Patmo |
| Kupaa | Kanisa la Awali | Kuteswa |
| Ubatizo | Misri | Nguvu |
| Walibatizwa | Galilaya | Mwisho wa nchi |
| Biblia | Maagizo | Ufufuo |
| Kaisaria | Yerusalemu | Rumi |
| Tohara | Uyahudi na Samaria | Kusini mashariki mwa Asia Ndogo |
| Uwanja wa michezo | Makedonia na Ugiriki | Asia Ndogo ya Magharibi |
| Korintho | Malta | Mashahidi |

1. Kitabu cha Matendo kinaanza na ___*Kupaa*___.

2. Wakati huo, Yesu aliwaambia wanafunzi kwamba watapokea ___*nguvu*___ .

3. Wakati huo, Yesu aliwaambia wanafunzi kwamba watakuwa ___*mashahidi*___.

4. Yesu alisema kwamba watafanya hivyo wakianzia: ___*Yerusalemu*___.

5. … *na* kisha katika ___*Uyahudi na Samaria*___ .

6. … *na* hatimaye katika ___*mwisho wa nchi*___ .

7. Matendo inarekodi kuenea kwa Injili kuanzia ___*Yerusalemu*___.

8. … na kisha katika ___*Uyahudi na Samaria*___ .

9. … na hatimaye katika ___*mwisho wa nchi*___ .

10. Matendo inafikia tamati Paulo akiwa katika nyumba ya kukodisha huko ___*Rumi*___ .

11. Safari ya Kwanza ya Umisionari ya Paulo ilipitia ___*Kusini mashariki mwa Asia Ndogo*___ .

12. Petro na Paulo walisuluhisha mzozo wa mapema kwenye Baraza huko ___*Yerusalemu*___ .

13. … ambapo walijadili wokovu na ___*Tohara*___ .

14. Safari ya Pili ya Umishonari ya Paulo iliingia ___*Makedonia na Ugiriki*___ .

15. Meli ambayo Paulo alikuwa akisafiria ilivunjika katika Kisiwa cha ___*Malta*___ .

16. Safari ya Tatu ya Umisionari ya Paulo iliingia ___*Asia Ndogo ya Magharibi*___ .

17. Paulo aliwahubiria Feliki na Festo alipokuwa kifungoni huko ___*Kaisaria*___ .

18. Paulo alitiwa gerezani mara mbili huko ___*Rumi*___ .

19. Mtume Yohana alihamishwa kwenye Kisiwa cha ___*Patmo*___ .

20. Jibu la swali hili ni nambari.

    Je, ni jibu gani kati ya 11-19 halifuati jinsi matukio yalivyofuatana katika wakati? ___*15*___ .

**Kufanya Wanafunzi 1 - Kudumu Katika Neno Lake**

## SOMO LA 7 - KUMJUA MUNGU

*"Mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake; bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifahamu mimi, na kunijua, ya kuwa mimi ni BWANA, nitendaye wema, na hukumu, na haki, katika nchi; maana mimi napendezwa na mambo hayo, asema BWANA."* Yeremia 9:23-24

Kumjua Mungu ni jambo muhimu na la thamani zaidi kuliko hekima, uwezo, na utajiri wa wanadamu. Hata hivyo, ni lazima tuzingatie maswali ya kutatanisha katika Ayubu 11:7, *"Je! Wewe waweza kuuvumbua ukuu wa Mungu? Waweza kuufikilia upeo wa huyo Mwenyezi?"* Majibu ya maswali hayo ni dhahiri. Hatuwezi kumwelewa Mungu asiye na kikomo bila yeye kutuwezesha kufanya hivyo. Kuwa na kikomo kama wanadamu kunaweka kizuizi katika ufahamu wetu wa kile kisichokuwa na kikomo.

Mungu amechukua hatua ya kujidhihirisha kwetu. Hivyo, tunaweza kumwelewa na kumjua. Mungu ametupa Roho Mtakatifu ili atuongoze katika ukweli, Yohana 16:13. Amejidhihirisha katika uumbaji, Warumi 1:20, kwa kuwa tunaona sifa zake zisizoonekana, nguvu zake za milele, na asili yake ya kiungu. Tunamwona Mungu ndani ya mwanadamu. Alimuumba mwanadamu kwa mfano wake na kwa sura yake, Mwanzo 1:26-27. Biblia ni Neno la Mungu kwetu na kwa ajili yetu, Mathayo 4:4, 2 Timotheo 3:16-17, Waebrania 4:12. Zaidi ya hayo, Mungu amejidhihirisha kwetu kupitia Yesu Kristo, Waebrania 1:1-12, 1 Yohana 5:20. Yesu alisema, *"Aliyeniona mimi amemwona Baba,"* Yohana 14:9. Tunaweza kumjua Mungu wa kweli asiye na kikomo. Yesu alisema, *"Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma,"* Yohana 17:3. Mungu ametupa njia hizi tano za kumjua ... Roho, uumbaji, mwanadamu, Biblia, na Yesu.


Kuna mengi sana kuhusu Mungu ambayo tunaweza kujua hata katika mapungufu ya maneno yetu yenye kikomo. Tunaweza kujua kwamba Mungu ni mmoja. Tunaweza kujua kwamba ana nafsi tatu. Pia, tunaweza kujua kwamba yeye ni watatu katika mmoja. Hata hivyo, hatuwezi kujua jinsi hilo linawezekana. Sifa za jumla za Mungu zinatupatia ufahamu kuhusu jinsi alivyo mkuu, jinsi alivyo mkubwa, jinsi asivyopimika ... lakini ufahamu wenye kikomo hauwezi kuelewa kile kisichokuwa na kikomo.

Nafsi zote za Utatu ziko sawa. Kila moja ni Mungu kikamilifu. Wakati huo huo, nafsi zote zinatofautiana kwa njia za kipekee. Baba alimtuma Yesu kwetu. Yesu alirudi kwa Baba. Kisha Yesu akamtuma Roho Mtakatifu kutoka kwa Baba ili atusaidie ... akae ndani yetu ... atutie nguvu. Maisha yetu pamoja na Roho Mtakatifu ni muhimu sana katika kutuwezesha kuwa kama vile Mungu mwenye nafsi tatu anataka tuwe.

## ASILI YA MUNGU

**Mungu ni mmoja.** Biblia inasema kwamba Mungu ni mmoja. Hawezi kugawanywa. Kuna Mungu mmoja tu, *"Sikiza, Ee Israeli; BWANA, Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja."* Kumbukumbu la Torati 6:4. Hakuna Mungu mwingine, *"Wewe umeonyeshwa haya, ili upate kujua ya kuwa BWANA ndiye Mungu, hapana mwingine ila yeye."* Kumbukumbu la Torati 4:35

**Mungu ana nafsi tatu.** Mungu ni mmoja. Mungu pia ana nafsi tatu. Alijirejelea katika hali ya wingi katika Mwanzo 1:26, 3:22, 11:7, na Isaya 6:8. Baba ni Mungu, Yohana 6:27. Yesu ni Mungu, Tito 2:13. Na Roho Mtakatifu ni Mungu, Matendo 5:3-4. Kila nafsi ni tofauti na nafsi zingine, Yohana 14:24-26, 15:26-27, na Isaya 48:16. Baba si Mwana ... na Baba si Roho Mtakatifu. Mwana si Roho Mtakatifu ... na Mwana si Baba. Roho Mtakatifu si Baba ... na Roho Mtakatifu si Mwana. Hata hivyo, kila mmoja ni Mungu kikamilifu. Kila nafsi katika Utatu inadhihirisha kikamilifu sifa zote za Mungu.




**Mungu ana nafsi tatu katika moja … umoja wa watatu … utatu**. Mchanganyiko wa *Mungu ni mmoja* na *Mungu ana nafsi* tatu unapelekea kumweleza Mungu kama watatu katika mmoja ambayo inajulikana kama Utatu … ingawa neno Utatu halipatikani katika Biblia. Utatu unarejelewa katika Mathayo 28:18-20 ambayo inajumuisha kubatiza kwa jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, *"Enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu."* Nafsi zote tatu zinaonekana katika ubatizo wa Yesu ... Yesu alibatizwa ... Roho Mtakatifu alishuka … na Baba alizungumza. *"Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, 'Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye,'"* Mathayo 3:16-17. Nafsi tatu za Utatu zimetajwa katika Isaya ambayo iliandikwa takriban mwaka 700 KK. *"Nisikilize mimi, Ee Yakobo; na Israeli, niliyekuita; mimi ndiye. Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho pia. Naam, mkono wangu umeuweka msingi wa dunia, na mkono wangu wa kuume umezitanda mbingu; niziitapo husimama pamoja. ... Nikaribieni, sikieni haya; tokea mwanzo sikunena kwa siri; tangu yalipokuwapo, mimi nipo; na sasa Bwana MUNGU amenituma, na roho yake,"* Isaya 48:12-13,16.

## SIFA ZA MUNGU

Sifa hizi zinatoa taswira ya Mungu isiyo kamili. Sifa hizi zinamweleza Mungu kama mmoja na watatu… zikielezea kwa usawa kila nafsi ya Utatu. "*Basi, mtamlinganisha Mungu na nani? Au mtamfananisha na mfano wa namna gani?", I*saya 40:18.

**1. Mungu hana kikomo.** Mungu hana mipaka. Hawezi kuzuiliwa kwa njia yoyote. Hajazuiwa na nafasi na wakati. Uwepo wake ni mkubwa sana ... haupimiki kwa njia zozote.

*"BWANA ndiye mkuu mwenye kusifiwa sana, Wala ukuu wake hautambulikani."* Zaburi 145:3

*"Walakini uyaelekee maombi ya mtumwa wako, na dua yake, Ee BWANA, Mungu wangu, uisikilize sauti na maombi ya mtumwa wako, aombayo mbele zako leo."* 1 Wafalme 8:27

**2. Mungu ni wa milele**. Mungu hana kikomo katika wakati. Amekuwepo daima. Yuko. Atakuwepo daima. Mungu amekuwepo bila kikomo kabla ya uumbaji na atakuwepo milele.

*"Kabla haijazaliwa milima, wala hujaiumba dunia, Na tangu milele hata milele ndiwe Mungu."* Zaburi 90:2

*"Lakini Wewe U Yeye yule; Na miaka yako haitakoma."* Zaburi 102:27

**3. Mungu ni mweza yote.** Uwezo wa Mungu hauna kikomo. Yeye ni mwenye uwezo wote. Nguvu zake hazina kikomo. Anaweza kufanya chochote anachotaka kufanya. Hakuna mtu wala hakuna kitu kimewahi kuwa na nguvu, kina nguvu, au kitakuwa na nguvu kuliko Mungu.

*"Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote, Na ya kuwa makusudi yako hayawezi kuzuilika."* Ayu 42:2

*"Aa! Bwana MUNGU, tazama, wewe umeziumba mbingu na nchi, kwa uweza wako mkuu na kwa mkono wako ulionyoshwa; hapana neno lililo gumu usiloliweza."* Yeremia 32:17

**4. Mungu ni mwenye mamlaka makuu.** Mungu hana kikomo katika mamlaka, uwezo, udhibiti, na uhuru. Yeye ndiye mwenye mamlaka ya juu zaidi. Yeye ndiye mtawala mkuu zaidi. Ana udhibiti wa mwisho na ulio huru wa vitu vyote.

*"BWANA amefanya kila lililompendeza, Katika mbingu na katika nchi, Katika bahari na katika vilindi vyote."* Zaburi 135:6

*"Ee BWANA, ukuu ni wako, na uweza, na utukufu, na kushinda, na enzi; maana vitu vyote vilivyo mbinguni na duniani ni vyako; ufalme ni wako, Ee BWANA, nawe umetukuzwa, u mkuu juu ya vitu vyote."* 1 Mambo ya Nyakati 29:11

**5. Mungu habadiliki.** Mungu hana kikomo katika kubakia jinsi alivyo. Hajawahi kubadilika ... habadiliki ... hatabadilika kamwe. Uwepo wake haubadiliki, haukui wala hauendelei. Hii haimaanishi kwamba kile anachofanya [tabia yake] hakibadiliki.

*"Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga; kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka."* Yakobo 1:17

*"Kwa kuwa mimi, BWANA, sina kigeugeu; ndio maana ninyi hamkuangamizwa, enyi wana wa Yakobo." Malaki 3:6*

**6. Mungu ni mjua yote.** Mungu hana kikomo katika maarifa. Maarifa yake hayana mipaka. Mungu anajua mambo yote yaliyotokea ... ambayo yangeweza kutokea ...

yanayotokea ... yanayoweza kutokea ... na yatakayotokea. Maarifa yake hayana kikomo, yakienea bila kikomo zaidi ya mipaka ya ulimwengu ulioumbwa ... zaidi ya nafasi ... na zaidi ya wakati.

*“Kwa maana Mungu ni mkuu kuliko mioyo yetu naye anajua yote.”* 1 Yohana 3:20

*“Wala hakuna kiumbe kisichokuwa wazi mbele zake, lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pake yeye aliye na mambo yetu.”* Waebrania 4:13

**7. Mungu yuko kila mahali.** Mungu hana kikomo katika uwepo na mahali. Yuko kila mahali. Mungu yuko kila mahali akiwa na nafsi yake yote. Hiyo haimaanishi kwamba Mungu ameumbwa kwa sehemu au kikamilifu na vitu alivyoumba [hiyo ni imani ya kwamba vitu vilivyoumbwa ndio Mungu]. Mungu ni tofauti na ulimwengu ... lakini yuko kila mahali ndani na nje ya ulimwengu.

*“Mimi ni Mungu aliye karibu, asema BWANA, mimi si Mungu aliye mbali. Je, mtu ye yote aweza kujificha mahali pa siri, nisimwone? Asema BWANA. Je! Mbingu na nchi hazikujawa nami? Asema BWANA.”* Yeremia 23:23-24

*“Niende wapi nijiepushe na roho yako? Niende wapi niukimbie uso wako? Kama ningepanda mbinguni, Wewe uko; Ningefanya kuzimu kitanda changu, Wewe uko. Ningezitwaa mbawa za asubuhi, Na kukaa pande za mwisho za bahari; Huko nako mkono wako utaniongoza, Na mkono wako wa kuume utanishika.”* Zab 139:7-10

**8. Mungu ni mtakatifu.** Mungu hana kikomo katika usafi. Ametenganishwa na kila kitu kilicho kiovu. Yeye ni mwema, safi, na mwadilifu. Haathiriwi na kile ambacho ni kiovu, najisi, na cha kawaida. Utakatifu ni zaidi ya kutokuwepo kwa uovu. Utakatifu ni uwepo chanya wa usafi.

*“Kwa kuwa mimi ni BWANA, Mungu wenu; takaseni nafsi zenu basi; iweni watakatifu, kwa kuwa mimi ni Mtakatifu.”* Mambo ya Walawi 11:44

*“Maana BWANA, Mungu wetu, ndiye mtakatifu.”* Zaburi 99:9

**9. Mungu ni mkweli.** Mungu anajiwakilisha bila kikomo kwa njia inayolingana na nafsi yake. Yeye ni mwaminifu na anategemeka kikamilifu kwa njia yoyote anayojidhihirisha. Maneno yake yanalingana na asili yake.

*“Katika tumaini la uzima wa milele, ambao Mungu asiyeweza kusema uongo aliuahidi tangu milele.”* Tito 1:2

*“Mungu si mtu, aseme uongo; Wala si mwanadamu, ajute; Iwapo amesema, hatalitenda? Iwapo amenena, hatalifikiliza?”* Hesabu 23:19

**10. Mungu ni mwenye haki.** Mungu ni mwenye haki isiyo na kikomo ndani yake na katika jinsi anavyoshughulikia mema na mabaya. Yeye ni mwenye haki [anazingatia haki] katika jinsi anavyotendea vitu vyote alivyoumba.

*“Yeye Mwamba, kazi yake ni kamilifu; Maana, njia zake zote ni haki. Mungu wa uaminifu, asiye na uovu, Yeye ndiye mwenye haki na adili.”* Kumbukumbu la Torati 32:4

*“Kicho cha BWANA ni kitakatifu, Kinadumu milele. Hukumu za BWANA ni kweli, Zina haki kabisa.”* Zaburi 19:9

**11. Mungu ni upendo**. Mungu hana kikomo katika kudhihirisha utakatifu. Anatimiza yaliyo bora kwake na kwa wanadamu. Mungu ni upendo. Kinyume cha hayo, *kwamba upendo ni Mungu*, si kweli.

*“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.”* Yohana 3:16

*“Yeye asiyependa, hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni upendo.”* 1 Yohana 4:8

## UPEKEE WA KILA NAFSI KATIKA UTATU

Kila nafsi katika Utatu ni dhihirisho kamili la Mungu. Hata hivyo, kila nafsi ni tofauti na zingine. Kila nafsi ni sawa na zingine. Hakuna yoyote iliyo chini au juu ya zingine. Hata hivyo, kila moja imefanya, inafanya, au itafanya mambo yatakayoitofautisha na nafsi zingine. Nafsi mbili au tatu katika Utatu zinashiriki vitendo na shughuli nyingi. Mpangilio ulio katika kila moja ya orodha zifuatazo haujapewa kipaumbele ... na nafasi na vitendo vyote vinavyotofautisha nafsi hizo havijatajwa. Kuna mambo mengine mengi ambayo Mungu amefanya, anafanya, na atafanya.

**UPEKEE WA BABA.** Baba amekuwepo daima, yuko, na daima atakuwa Mungu kikamilifu. Hata hivyo, tunamwona akifanya mambo mahususi yanayomtofautisha na Mwana na Roho.

**Yeye ndiye baba wa wanadamu wote kwa mtazamo wa muumba/kiumbe.** Hii inarejelea ubaba wa kimwili badala ya ubaba wa kiroho wa Mungu. Ubaba wa *kiroho* wa Mungu ni tofauti ... na unategemea imani, Malaki 2:10, Matendo 17:29.

**Yeye ndiye Baba wa Israeli.** Yeye ndiye baba wa Israeli. Hiyo haimaanishi kwamba yeye ndiye baba wa kiroho wa kila Mwisraeli ... hiyo inatokana na imani ya mtu binafsi. Yeye kuwa baba wa Israeli si sawa na yeye kuwa baba wa Kanisa. Kanisa ni bibi arusi wa Kristo ... Yesu ndiye bwana arusi ... na Mungu Baba ndiye baba wa bwana arusi, Kutoka 4:22, Isaya 63:16.

**Yeye ni Baba wa Bwana Yesu Kristo.** Nafsi zote za Utatu ziko sawa ... lakini Mungu Baba katika nafasi yake ni Baba wa Yesu Kristo. Hiyo haimaanishi kwamba Baba ni mkuu kuliko Mwana, Waefeso 1:3, Yohana 3:16, Yohana 5:37. Baba hakumzaa Yesu. Yesu kuwa Mwana wa Mungu ni kwa msingi wa nafasi. Yesu amekuwepo daima. Yesu hakuwa na mwanzo. Yesu ni wa milele.

**Yeye ni Baba, Baba wa kiroho, wa wote wanaomwamini Kristo.** Sisi ni watoto wake, Zaburi 103:13, Yohana 1:12, Wagalatia 3:26.

**Huwapa mamlaka watawala wa dunia na huwekea mataifa mipaka na nyakati**, Matendo 17:26, Warumi 13:1-7, 1 Petro 2:13-14.

**Yeye ndiye chanzo cha wokovu.** Yeye ndiye anayechagua ... anayeteua ... anayewaita watu kuamini, Waefeso 1:3-12, Warumi 8:28 - 9:24.

**Anatupa mwelekeo.** Baba anatupa mapenzi yake kwa ajili ya siku zetu na maisha yetu, Mithali 3:5-6, Zaburi 32:8, Yeremia 29:11.

**Yeye ndiye mlinzi wetu.** Anatulinda katika vita vyetu dhidi ya ulimwengu, mwili, na ibilisi, Zaburi 23, Zaburi 37, Zaburi 56:3-4.

**Yeye ndiye anayekidhi mahitaji yetu.** Anakidhi mahitaji yetu ya kimwili na ya kiroho. Yeye ndiye chanzo cha zawadi zote nzuri, Mathayo 6:25-34, Yakobo 1:17.

**Anatupa usalama wa milele.** Tuko salama mikononi mwa Mungu milele ... salama kwa sababu hakuna aliye na nguvu za kutosha kutunyakua kutoka mikononi mwake, Yohana 10:27-29.

**Anasikia maombi yetu.** Wakristo mara nyingi humwomba Yesu. Hata hivyo, Yesu alifundisha kwamba tunapaswa kumwomba Baba, Mathayo 6:8-9, Yohana 16:23.

**Huwaadhibu watoto wake.** Kama Baba mwenye upendo, yeye hutuadhibu ili tuwe kila tunachoweza kuwa. Yeye ndiye mkulima anayetupogoa ili tuzae matunda zaidi, Waebrania 12:4-13, Yohana 15:1-2.

**UPEKEE WA MWANA.** Bwana Yesu Kristo amekuwepo daima, yuko, na daima atakuwa Mungu kikamilifu. Hata hivyo, tunamwona akifanya mambo mahususi yanayomtofautisha na Baba na Roho.

**Yeye ndiye Muumba.** Yesu ndiye Muumba na mhimili wa vitu vyote vilivyoumbwa, Yohana 1:3, Wakolosai 1:16-17.

**Yeye ndiye mlinzi na mkombozi wa Israeli**, Yoshua 5:13 - 6:2, Zaburi 34:7.

**Alifanyika Mungu-Mwanadamu.** Yesu alifanyika mwanadamu ... akiongeza ubinadamu katika uungu wake ambao haukudidimia. Akawa *logos*, mfano wa kimwili wa Mungu duniani, Wafilipi 2:5-8, Yohana 1:1-2, 14.

**Yeye ni Mtume wa imani yetu.** Yeye ndiye mwanzilishi na mtangulizi wa imani yetu, Waebrania 3:1.

**Yeye ndiye Kuhani Mkuu wa imani yetu.** Yeye ndiye kuhani mkuu na wa kudumu, Waebrania 3:1, 4:14-15, 7:23-24, 9:11-12.

**Alikuwa nabii.** Musa alitabiri kuwa Yesu atakuwa nabii, Kumbukumbu la Torati 18:15. Yesu alitangaza Neno la Mungu kwa mamlaka katika Mahubiri ya Mlimani, Mathayo 5-7 ... kwenye Mlima wa Mizeituni, Mathayo 24-25 ... na katika chumba cha juu, Yohana 13-16. Alitabiri usaliti wa Yuda, Mathayo 26:21. Alitabiri kifo na ufufuo wake, Mathayo 16:21, 20:17-19.

**Yeye ndiye Kichwa cha Mwili wake, ambao ni kusanyiko la Waumini wote.** Anajenga Mwili wake, kanisa la ulimwengu wote, Waefeso 1:20-23, 4:15, Mathayo 16:18.

**Anaupatia mwili wake karama za kuwaandaa Waumini.** Karama hizi nne ni watu maalum. Ni mitume, manabii, wainjilisti, na wachungaji-walimu. Wanatolewa ili kuwaandaa Waumini kwa ajili ya kazi ya huduma. Vipawa hivi ni tofauti na karama za uwezeshaji [uwezo maalum] zinazotolewa na Roho Mtakatifu kwa Waumini binafsi, Waefeso 4:11-13.

**Anatuombea.** Yesu anatuombea, Warumi 8:34, Waebrania 7:25.

**Anatutayarishia mahali katika uwepo wa Mungu,** Yohana 14:1-3.

**Yeye ni Mfalme ... na atatawala kama Mfalme,** Yohana 12:14-15, 1 Timotheo 6:13-16, na Ufunuo 19:15-16.

**Atarudi kutuchukua**, Yohana 14:3, 1 Wathesalonike 4:15-18.

**Atawahukumu watu wote.** Atawahukumu Waumini na wasioamini, Yohana 5:22, 27, 1 Wakorintho 3:11-15, 2 Wakorintho 5:10, Ufunuo 20:11-15.

**UPEKEE WA ROHO MTAKATIFU.** Mungu Roho daima amekuwepo, yuko, na daima atakuwa Mungu kikamilifu. Hata hivyo, tunamwona akifanya mambo mahususi yanayomtofautisha na Mwana na Baba.

**Aliwaongoza watu walioandika Biblia.** Aliwawezesha kuandika Neno. Neno liliandikwa kwa njia ya pumzi ya Mungu kupitia Roho aliyefanya kazi kupitia watu walioandika Neno. Neno la Mungu ni upanga wa Roho, 2 Petro 1:21, Mathayo 22:43, Matendo 28:25, Waefeso 6:17.

**Roho alikuwa ndani na juu ya watu fulani katika nyakati za Agano la Kale.** Watu hawa ni pamoja na Yusufu, Mwanzo 41:38 ... Yoshua, Hesabu 27:18 ... Danieli, Danieli 4:8 ... Gideoni, Waamuzi 6:34 ... Samsoni, Waamuzi 13:25 ... na Sauli, 1 Samweli 10:10.

**Husadikisha ulimwengu juu ya dhambi, haki, na hukumu.** Roho Mtakatifu huwashawishi na kuwasadikisha watu juu dhambi ya kutoamini kwao. Anawasadikisha na kuwahukumu watu juu ya haki ya Kristo. Anawasadikisha na kuwahukumu watu juu ya uhakika wa hukumu, Yohana 16:8-12.

**Humtukuza Kristo.** Anawaelekeza watu kimahususi kwa Bwana Yesu Kristo. Roho Mtakatifu humtukuza Yesu badala ya kujitukuza yeye mwenyewe, Yohana 16:14.

**Yeye ndiye wakala wa kuzaliwa kwetu kiroho.** Roho Mtakatifu hutufanya upya. Anatuzaa upya. Kuzaliwa huko katika Mwili kunaelezwa katika Biblia kama ubatizo katika Roho, Tito 3:3-5, Yohana 3:5-6, 1 Wakorintho 12:13.

**Hukaa ndani ya Waumini wote.** Roho Mtakatifu hukaa ndani ya kila muumini tangu wakati wa wokovu kwa njia ya kudumu, bila ubatilisho na bila mabadiliko. Kukaa huko kwa Roho kwa njia ya kudumu na bila masharti ni tofauti na kujazwa na Roho kunakoweza kubadilika, Yohana 14:16-17, 1 Wakorintho 6:19.

**Huwajaza Waumini.** Hii ni hali ya sisi kuwa chini ya ushawishi na udhibiti wa Roho kwa hiari. Ni kumruhusu Roho Mtakatifu kufanya kazi ndani yetu na kupitia kwetu. Anatujaza kwa masharti ... hali hiyo ya kujazwa inaweza kubadilika kulingana na itikio letu na upatikanaji wetu. Kujazwa huko kwa Roho ni tofauti na kukaa kwa Roho ndani yetu, Waefeso 5:18.

**Hutuhakikishia kwamba sisi ni watoto wa Mungu.** Roho Mtakatifu ndiye ahadi na muhuri wetu tuliopewa na Mungu kwamba tuko salama milele. Roho Mtakatifu anatuhakikishia wokovu wetu, Warumi 8:16, Waefeso 1:13-14, 4:30, 2 Wakorintho 5:5.

**Huupatia Mwili karama za uwezeshaji.** Roho Mtakatifu humpa kila muumini angalau uwezo mmoja maalum wa kumwezesha. Karama hizi huwezesha kila sehemu ya Mwili wa Kristo kufanya sehemu yake ili kuujenga Mwili katika upendo. Hizi ni tofauti na wale waandaaji wa Waefeso 4 wanaotolewa na Yesu. Vipawa vinavyotolewa na Yesu ni watu maalum. Karama zinazotolewa na Roho ni *uwezo* maalum, Luka 24:49, Matendo 1:8, 1 Wakorintho 12:11.

**Huwaongoza Waumini.** Roho Mtakatifu hutoa mwongozo kwa Waumini ... kama alivyofanya na Yesu wakati wa maisha yake hapa duniani, Luka 4:1, Warumi 8:14, Matendo 8:29.

**Huwafundisha Waumini.** Roho Mtakatifu huwafundisha Waumini katika masomo yao ya kibinafsi ... na huwafundisha kupitia walimu wao. Huwaongoza Waumini katika ukweli ... akiwapa ufahamu wa Neno la Mungu, Yohana 14:26, 16:13.

**Hutufariji.** Roho Mtakatifu ameitwa kutusaidia, Yohana 14:16-17.

**Hutuombea wakati hatujui kuomba katika udhaifu wetu.** Roho Mtakatifu hutuombea ... hutuombea wakati hatujui jinsi ya kuomba. Hiyo haimaanishi kwamba yeye huomba *kupitia* kwetu, Warumi 8:26.

**Huzaa matunda katika maisha yetu.** Utu na sifa za Roho Mtakatifu za upendo, furaha, amani, subira, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, na kiasi huonekana tunapoishi chini ya ushawishi wake, Wagalatia 5:22-23.

## MUUMINI NA ROHO MTAKATIFU

Yesu alisema, *“Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu,”* Yohana 14:16-17. Roho Mtakatifu, msaidizi wetu, yuko pamoja nasi na yuko ndani yetu. Roho huwapa Waumini uwezo maalum ili kutumika kwa manufaa ya wote. Hata hivyo, kuna mengi zaidi katika maisha yetu katika Roho kuliko karama za kiroho. Ni lazima tumuitikie ipasavyo ili tupate manufaa ya huduma yake kwetu na kupitia kwetu.

**Jazwa na Roho.** Kuwa chini ya ushawishi wa Roho Mtakatifu. Mpe uhuru katika maisha yako. Kuwa tayari kwa ujazo wake kwa kujitenga na vishawishi vya dunia, vya mwili, na vya ibilisi. Waefeso 5:18

**Fuata Roho.** Omba kwa ajili ya mwongozo wa Roho Mtakatifu. Kuwa makini na mwongozo wa Roho Mtakatifu. Mwache akuongoze, Zaburi 143:10, Warumi 8:14, Wagalatia 5:18. Roho anapokuongoza ... mfuate. Mruhusu aongoze hatua zako. Enenda kwa Roho, Warumi 8:4, Wagalatia 5:16,25.

**Omba katika Roho.** Hii ni kuomba chini ya ushawishi na mwongozo wa Roho Mtakatifu. Unapaswa kuomba chini ya ushawishi wake ... kama vile unavyopaswa kufanya mambo yote chini ya ushawishi wake, Waefeso 6:18, Yuda 1:20.

**Weka akili yako katika Roho.** Elekeza akili yako kwa Roho Mtakatifu badala ya mwili. Maisha yako yatafuata mwelekeo wa akili yako, Warumi 8:6-8.

**Panda katika Roho.** Utavuna kile unachopanda. Wekeza maisha yako katika mambo ya Roho. Panda katika shamba la Roho badala ya shamba la mwili, Wagalatia 6:7-8.

**Usimzimishe na usimhuzunishe Roho.** *Msimzimishe* Roho, 1 Wathesalonike 5:19. Usizime, usididimishe, au usiponde ushawishi wake katika maisha yako. Kutopatikana kwako kwa Roho humzima Roho. *Msimhuzunishe* Roho, Waefeso 4:30. Usimtie Roho Mtakatifu huzuni na dhiki. Dhambi humhuzunisha Roho Mtakatifu. Usimhuzunishe ... mfurahishe.

**Hifadhi umoja unaoletwa na Roho.** Umoja katika Mwili wa Kristo *unaletwa* na Roho Mtakatifu. Hatujiletei umoja sisi wenyewe. Tumeitwa kuhifadhi umoja unaoletwa na Roho Mtakatifu. Tunapaswa kuwa kitu kimoja na Waumini wengine ... wamoja katika moyo, katika nafsi na katika akili. Waefeso 4:3-4

Acts One Eight [Matendo Moja Nane] huchapisha tafsiri hii ya Kiswahili ya kozi ya lugha ya Kiingereza ya *Disciplemaking 1 … Abiding in His Word*. Unaweza kunakili kozi hii au sehemu yake yoyote bila malipo au kwa gharama ya usambazaji pekee, bila kubadilisha maudhui yake na ukiwa umeambatanisha kauli hii ya chanzo. Kozi hii inapatikana bila malipo katika lugha ya Kiswahili kutoka katika www.Theolojia.org au katika lugha ya Kiingereza kutoka katika www.VIrtualBibleAcademy.org. Kwenye tovuti hizi, unaweza kusoma mtandaoni, kufundishwa, kupakua, au kuchapisha nakala zako mwenyewe. Nukuu za Biblia ya Kiswahili zimetoka katika Biblia ya Swahili Union Version (SUV) ya 1997.

*Kufanya Wanafunzi 1 - Maswali ya Marudio*

# Somo la 7 - Kumjua Mungu ... ukurasa wa 98 - 105


Sehemu ya kujifunza ni kufanya marudio … kuhifadhi maarifa mapya kwenye kumbukumbu yako ya muda mrefu. Chapisha mtihani huu wa marudio au tumia karatasi tofauti kujibu maswali yafuatayo. Kisha rudia mtihani huu, ukisoma maelezo ya kozi au bila kuyasoma, hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi.
*Mitihani hii ya marudio* pamoja na majibu sahihi yanapatikana kwenye www.Theolojia.org.

1. Weka mviringo au piga mstari kwenye kile kilicho muhimu zaidi kati ya haya manne.

   Utajiri ... Hekima ... Kumjua Mungu ... Nguvu

Weka mviringo au pigia mstari kwenye *"Kweli"* au *"Uwongo"* katika taarifa ya 2 - 7.

2. Mungu hawezi kugawanywa. *Kweli* ... au ... *Uwongo*
3. Kuna "Miungu" mingine isiyo na umuhimu. *Kweli* ... au ... *Uwongo*
4. Hakuna marejeo kuhusu Utatu katika Agano la Kale. *Kweli* ... au ... *Uwongo*
5. Mungu ni Mmoja na ana nafsi Tatu kwa wakati mmoja. *Kweli* ... au ... *Uwongo*
6. Umoja wa Mungu ni muhimu zaidi kuliko utatu wake. *Kweli* ... au ... *Uwongo*
7. Nafsi zote katika Utatu hufanya mambo yale yale. *Kweli* ... au ... *Uwongo*
8. Kamilisha ifuatayo kwa mistari, na kwa maneno *"NI"* na *"SI"* inapohitajika.



KAMILISHA KAULI YA 9 - 19 UKITUMIA MAJIBU HAYA YA KUCHAGUA

| | | |
|---|---|---|
| mwenye uwezo wote | yuko vile vile milele | anadhihirisha utakatifu |
| hana kikomo katika wakati | mwadilifu | uwepo wake uko kila mahali |
| hana mipaka yoyote | anaaminika kikamilifu | mtawala mkuu |
| anajua mambo yote | ana kikomo kiasi | safi |

9. Mungu hana kikomo inamaanisha ________________________________.
10. Mungu ni wa milele inamaanisha _________________________.
11. Mungu ni mweza yote inamaanisha kwamba yeye ni ________________________.
12. Mungu ni mwenye mamlaka makuu inamaanisha kwamba yeye ni _____________ ______________________.
13. Mungu habadiliki inamaanisha kwamba __________________________________.
14. Mungu yuko kila mahali inamaanisha kwamba ____________________________.
15. Mungu ni mjua yote inamaanisha kwamba _______________________________.
16. Mungu ni mtakatifu inamaanisha kwamba yeye ni __________________________.
17. Mungu ni mwenye haki inamaanisha kuwa yeye ni _________________________.
18. Mungu ni ukweli inamaanisha _________________________.
19. Mungu ni upendo inamaanisha kwamba _________________________.

ANDIKA *BABA, MWANA,* AU *ROHO MTAKATIFU* ILI KUJIBU SWALI LA 20 - 26.

20. Ni nani anaupatia Mwili karama za kuwaandaa Waumini? ____________________.
21. Ni nani anayezaa matunda maishani mwetu? _________________________.
22. Ni nani hasa husikia sala zetu? _________________________.
23. Ni nani chanzo cha zawadi zote nzuri? _________________________.
24. Ni nani anayetuandalia mahali? _________________________.
25. Nani huwapa Waumini karama za kuwawezesha? _________________________.
26. Ni nani Mwanzilishi wa wokovu? _________________________.

27. Eleza maana ya kupanda katika shamba la Roho.

# Somo la 7 - Kumjua Mungu ... maswali ukurasa wa 106 - 107


Usitumie karatasi hizi za majibu kupata majibu yako. Tafadhali zitumie tu kukagua majibu yako. Rudi kwenye somo ili kupata taarifa za kurekebisha majibu yako. Rudia mtihani hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi. Masomo yote, mitihani ya marudio, na kurasa za majibu zinapatikana katika www.Theolojia.org.

1. Weka mviringo au piga mstari kwenye kile kilicho muhimu zaidi kati ya haya manne.

   Utajiri ... Hekima ... *Kumjua Mungu* ... Nguvu

Weka mviringo au pigia mstari kwenye *"Kweli"* au *"Uwongo"* katika taarifa ya 2 - 7.

2. Mungu hawezi kugawanywa. *Kweli* ... au ... *Uwongo*
3. Kuna "Miungu" mingine isiyo na umuhimu . *Kweli* ... au ... *Uwongo*
4. Hakuna marejeo kuhusu Utatu katika Agano la Kale. *Kweli* ... au ... *Uwongo*
5. Mungu ni Mmoja na ana nafsi Tatu kwa wakati mmoja. *Kweli* ... au ... *Uwongo*
6. Umoja wa Mungu ni muhimu zaidi kuliko utatu wake. *Kweli* ... au ... *Uwongo*
7. Nafsi zote katika Utatu hufanya mambo yale yale. *Kweli* ... au ... *Uwongo*
8. Kamilisha ifuatayo kwa mistari, na kwa maneno *"NI"* na *"SI"* inapohitajika.



KAMILISHA KAULI YA 9 - 19 UKITUMIA MAJIBU HAYA YA KUCHAGUA

| | | |
|---|---|---|
| mwenye uwezo wote | yuko vile vile milele | anadhihirisha utakatifu |
| hana kikomo katika wakati | mwadilifu | uwepo wake uko kila mahali |
| hana mipaka yoyote | anaaminika kikamilifu | mtawala mkuu |
| anajua mambo yote | ana kikomo kiasi kidogo | safi |

9. Mungu hana kikomo inamaanisha __*hana mipaka yoyote*__ .
10. Mungu ni wa milele inamaanisha __*hana kikomo katika wakati*__ .
11. Mungu ni mweza yote inamaanisha kwamba yeye ni __*mwenye uwezo wote*__ .
12. Mungu ni mwenye mamlaka makuu inamaanisha kwamba yeye ni __*mtawala mkuu*__ .
13. Mungu habadiliki inamaanisha kwamba __*yuko vile vile milele*__ .
14. Mungu yuko kila mahali inamaanisha kwamba __*uwepo wake uko kila mahali*__ .
15. Mungu ni mjua yote inamaanisha kwamba __*anajua mambo yote*__ .
16. Mungu ni mtakatifu inamaanisha kwamba yeye ni __*safi*__ .
17. Mungu ni mwenye haki inamaanisha kuwa yeye ni __*mwadilifu*__ .
18. Mungu ni ukweli inamaanisha __*anaaminika kikamilifu*__ .
19. Mungu ni upendo inamaanisha kwamba __*anadhihirisha utakatifu*__ .

ANDIKA BABA, MWANA, AU ROHO MTAKATIFU ILI KUJIBU SWALI LA 20 - 26.

20. Ni nani anaupatia Mwili vipawa vya kuwaandaa Waumini? __*Mwana*__ .
21. Ni nani anayezaa matunda maishani mwetu? __*Roho Mtakatifu*__ .
22. Ni nani hasa husikia sala zetu? __*Baba*__ .
23. Ni nani chanzo cha zawadi zote nzuri? __*Baba*__ .
24. Ni nani anayetuandalia mahali? __*Mwana*__ .
25. Nani huwapa Waumini karama za kuwawezesha? __*Roho Mtakatifu*__ .
26. Ni nani Chanzo cha wokovu? __*Baba*__ .

27. Eleza maana ya kupanda katika shamba la Roho.

    *Tunavuna kile tunachopanda. Kupanda katika Roho ni kuwekeza maisha yetu katika mambo ya Roho.*

## Kufanya wafuasi 1 - Kudumu katika Neno Lake

# SOMO LA 8 - MAPENZI YA MUNGU

*"Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu."* Warumi 12:1-2

Kuyajua mapenzi ya Mungu ni muhimu sana kwa kila muumini. Hata hivyo, lengo letu lisiwe tu kuyajua mapenzi ya Mungu. Lengo letu pia lastahili kuwa kutenda mapenzi ya Mungu. Sehemu kubwa ya mwongozo wake katika maisha yetu ni wa kijumla kwa Waumini wote. Pia ana mapenzi mahususi kwa kila muumini. Hakuna njia ya mkato, sarakasi wala mazingaombwe kupambanua mapenzi ya Mungu. Mara nyingi Mungu hatimaye hufunua mapenzi yake kwetu tunapoendelea kukua na kutembea naye. Ni matokeo ya utaratibu wa kutembea naye katika uaminifu.

Umuhimu wa kuyafuata mapenzi ya Mungu unajidhihirisha katika maisha ya Yesu. Alisema bayana, *"Yesu akawaambia, Chakula changu ndicho hiki, niyatende mapenzi yake aliyenipeleka, nikaimalize kazi yake,"* Yohana 4:34. Yesu pia alisema, *"Kwa kuwa mimi sikushuka kutoka mbinguni ili niyafanye mapenzi yangu, bali mapenzi yake aliyenipeleka,"* Yohana 6:38. Ni dhahiri kwamba kabla ya kutenda mapenzi ya Mungu lazima tuelewe mapenzi yake ni nini, *"Kwa sababu hiyo msiwe wajinga, bali mfahamu ni nini mapenzi ya Bwana,"* Waefeso 5:17.

Tunaweza kuyajua mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yetu. *"Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea; Nitakushauri, jicho langu likikutazama,"* Zaburi 32:8. *"Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atayanyosha mapito yako,"* Mithali 3:5-6. Biblia inatuhakikishia kuwa mapenzi yake kwetu ni mema. *"Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake,"* Warumi 8:28. *"Hatua za mtu zaimarishwa na BWANA, Naye aipenda njia yake. Ajapojikwaa hataanguka chini, BWANA humshika mkono na kumtegemeza,"* Zaburi 37:23-24. Kanunni hiyo inajitokeza kwa uwazi katika, *"Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema BWANA, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho,"* Yeremia 29:11.

Tunajua mapenzi ya jumla ya Mungu au kwa waumini wote moja kwa moja kutoka katika Bibilia. Mapenzi yake ya jumla ni sawa kwa kila muumini. Tunajua mapenzi binafsi ya Mungu kwa kila muumini yanatokana na maisha ya uaminifu kwa jumla katika Mungu. Kutoka kwa msingi huo wa utii, tunafuata hatua tatu za kubainisha na kuchukua hatua kwa mapenzi ya Mungu kwa mtu binafsi … Tunamuuliza Baba … tunapata mwongozo kutoka katika Neno Lake. Hekima Yake, watu wake na amani yake … na tunatenda tunapojua mapenzi yake.

**MAPENZI YAKE YA JUMLA.** Sehemu kubwa ya mapenzi ya Mungu katika maisha yetu ni sawa kwa waumini wote bila ubaguzi. Tunaelewa mapenzi ya jumla ya Mungu moja kwa moja kutoka kwenye Bibilia. Tunajifunza kuhusu mapenzi yake ya jumla kwetu sisi kupitia amri zake Mungu, kanuni na mifano ipatikanayo katika neno lake.

**Amri.** Kuna amri za jumla na zisizojadilika katika Bibilia ambazo zimetolewa kwa kila muumini. *"Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu ... mwepukane na uasherati,"* 1 Wathesalonike 4:3. *"Furahini siku zote; ombeni bila kukoma; shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu. Msimzimishe Roho,"* 1 Wathesalonike 5:16-18. *"Tiini kila kiamriwacho na watu, kwa ajili ya Bwana … Kwa sababu ndiyo mapenzi ya Mungu,"* 1 Petro 2:13-15. Yesu anatarajia tutii amri hizi na nyinginezo, *"Mkinipenda, mtazishika amri zangu,"* Yohana 14:15. Utiifu unastahili kuwa zaidi ya uamuzi wa saa baada ya saa. Utiifu unastahili kuwa mtindo wa maisha.

**Kanuni.** Kuna kanuni katika Bibilia zinazoshughulikia hali tofauti. Kuna kanuni ya usimamizi mwema mwanzoni mwa sura ya 16 ya kitabu cha Luka. Gharama ya uanafunzi ipo mwishoni mwa sura ya 14 ya kitabu cha Luka. Kanuni ya kutenga muda wa kuwa na watu waliopotea imewakilishwa kwenye hadithi tatu zenye mafumbo katika sura ya 15 ya Luka. Tunahitaji kuzielewa na kuzitumia kanuni hizi nyingi zilizo kwenye agano la kale na agano jipya la Bibilia. Kanuni hizo na amri zinatupa taswira ya mapenzi ya jumla ya Mungu kwa maisha yetu.

**Mifano.** Bibilia ina mifano mizuri ya kufuatwa … na mibaya ya kuepuka. Mfano mzuri ni maisha ya Kristo. Akiosha miguu ya wafuasi wake, Yesu alisema, *"Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo,"* Yohana 13:15. Tunapaswa kufuata mfano wake wa unyenyekevu, Wafilipi 2:5. Tunapaswa kutembea kwenye nyayo zake, 1 Petro 2:21, 1 Yohana 2:6. Na kuna aina nyingi zaidi ya mifano tunayostahili kuifuata kama vile hadithi nzuri ya Danieli ya kumheshimu na kumhudumia Bwana mahala ambapo hakuna Mungu. Mtume Paulo alitoa mfano mzuri kwenye kitabu cha Matendo ya Mitume sura ya 17. Paulo aliandika hivi, *"Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo,"* 1 Wakorintho 11:1. Aidha, kuna mifano mibaya ya kuepukwa kama ule wa Mfalme Sauli ambaye hakumheshimu Mungu kikamilifu … Uzinzi wa Daudi na Bathsheba … na kushindwa mara 17 katika nyakati za Waamuzi.

**MAPENZI YAKE MAHUSUSI.** Mungu ana mapenzi mahususi kwa kila muumini kama tunavyoona katika Zaburi 32:8, Mithali 3:5-6, Warumi 8:28, Zaburi 37:23-24, na Yeremiah 29:11. Kuna mifano mingi katika Bibilia. Daudi aliandika, *"Maana Wewe ndiwe uliyeniumba mtima wangu, Uliniunga tumboni mwa mama yangu … Macho yako yaliniona kabla sijakamilika; Chuoni mwako ziliandikwa zote pia, Siku zilizoamriwa kabla hazijawa bado,"* Zaburi 139:13, 16. Mungu alikuwa na mapenzi maalumu kwa nabii Yeremia, *"Kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua, na kabla hujatoka tumboni, nalikutakasa; nimekuweka kuwa nabii wa mataifa, … maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema kila neno nitakalokuamuru,"* Yeremia 1:5, 7. Mapenzi mahususi ya Mungu kwa Ayubu yalitokana na mazungumzo mara mbili huko mbinguni, Ayubu 1 na 2. Nuhu aliitwa ili kujenga Safina, Mwanzo 6. Ibrahimu aliamriwa na familia kwenda katika nchi ya kigeni, Mwanzo 12, na akaambiwa amtoe mwanawe Isaka kama dhabihu, Mwanzo 22. Rebeka aliteuliwa kuwa mke wa Isaka, Mwanzo 24:14, 44. Yona aliagizwa kwenda Ninawi, Yona 1. Yesu aliwachagua wafuasi wake, wao hawakumchagua, Yohana 15:16. Paulo aliitwa ili kuwa Mtume, 1 Wakorintho 1:1. Na Roho Mtakatifu huwapa waumini karama mbalimbali jinsi kama anavyoongozwa na Yesu [Angalia sura ya 9 ya somo hili].

**KUTAMBUA MAPENZI YAKE MAHUSUSI**

**Hatua Tatu.** Fuata hatua hizi tatu ili kujifunza na kufanya mapenzi yake mahususi. Kwanza **muulize** Mungu akuambie. Pili, **pata ushauri** kutoka kwa Neno Lake, Hekima Yake, Watu Wake na Amani yake. Na tatu, chukua **hatua** … tenda lile Mungu anakwambia utende.

**Uliza.** Mahala pa kuanzia kujua Mapenzi Yake mahususi kwako ni maombi. Ombi la mwandishi wa Zaburi linapaswa kuwa letu, *"Unifundishe kuyatenda mapenzi yako,"* Zaburi 143:10. Katika sala ya Bwana, Yesu aliwafundisha wafuasi wake kuomba, *"Mapenzi yako yatimizwe,"* Mathayo 6:10. Mtume Paulo aliomba kuwa waumini wa Kolosai, *"mjazwe maarifa ya mapenzi yake,"* Wakolosai 1:9. Epafras alifanya bidii siku zote kwa ajili yenu katika maombi yake, *"ili kwamba msimame wakamilifu na kuthibitika sana katika mapenzi yote ya Mungu,"* Wakolosai 4:12. Maombi ya dhati kwa ajili yetu, na wengine, yanapaswa kuwa kujua na kuyatenda mapenzi ya Mungu.

**Pata mwongozo.** Mungu hutupatia mapenzi yake mahususi kupitia kwa Neno Lake, hekima yake, watu wake, na amani yake. Tunamwomba Bwana aweze kutufunulia mapenzi yake kwetu … na anayajibu maombi hayo kupitia kwa njia nne nilizoelezea hapa chini.

> **Neno Lake.** Kuyajua mapenzi mahususi ya Mungu kwako mara nyingi ni matokeo ya utaratibu wa usomaji wa Biblia. Au kunaweza kutokana na usomaji wa neno kuambatana na hali fulani. Mapenzi mahususi ya Mungu kwetu yanabainika tunapoendelea kupata hekima na uelewa wa neno la Mungu. Kamwe hatatuongoza kutenda jambo kinyume cha Neno Lake.
>
> **Hekima Yake.** Hekima ya Mungu hutokana na maisha ya utiifu kwa roho mtakatifu, 1 Wakorintho 2:14-3:3. Tunapotembea na Mungu kwa utiifu, ndipo tunapolielewa Neno Lake na mapenzi yake. Paulo aliandika, *"Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu,"* Warumi 12:2. Hekima ni tofauti na maarifa. Muombe Mungu kwa ajili ya Hekima Yake, *"Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu ... naye atapewa,"* Yakobo 1:5.
>
> **Watu Wake.** Watu wa Mungu ni nyenzo kwa ajili ya kuelewa mapenzi ya Mungu. Wale wafundishao Neno Lake kupitia unenaji au maandishi wanaweza kusaidia, Wakolosai 1:28. Ni vyema kupata ushauri nasaha kutoka kwa waumini waliopevuka. Ni bora zaidi kuwa na zaidi ya mshauri mmoja, *"Pasipo mashauri makusudi hubatilika; Bali kwa wingi wa washauri huthibithika,"* Mithali 15:22. Lakini kumbuka ushauri ni ushauri tu. Wingi wa kura kwa washauri wengi huenda ukawa sawa … au waweza kuwa usio sawa. Kumi kati ya wapelelezi waliotumwa Kanani katika kitabu cha Hesabu sura za 13 na 14 hawakuwa sawa. Waumini waliopevuka wanaweza kutupatia ushauri wa kutuwezesha kuelewa mapenzi ya Mungu.
>
> **Amani Yake.** Amani ya Mungu, ikiwa inatoka kwake, yaweza kuwa uthibitisho kamili wa mapenzi mahususi ya Mungu, "Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu," Wakolosai 3:15. *"Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu,"* Wafilipi 4:7. Amani hii inatokana na Mungu na kuna usahihi kuhusu uamuzi huo. Hautokani na mihemko au hamu ya binadamu. Amani yake ni uthibitisho unaotokana na maombi, usomaji wa Bibilia, hekima ya kiroho na inaakisi busara kutoka kwa washauri kadhaa waliopevuka katika mambo ya kiroho.Tafuta na uitumainie Amani Yake.

**Tenda.** Tunapojua mapenzi ya Mungu kwetu, ndio wakati wa kutenda. Huenda jibu likawa *hapana* kama ilivyokuwa kwa Paulo kwenye 2 Wakorintho 12:7-10. Inaweza kuwa, *subiri* … ikimaanisha tuendelee kutafuta mapenzi yake. Jibu la *subiri* laweza kuwa baraka kubwa, Isaya 40:31. Ikiwa jibu leke ni *ndiyo* inatupasa kutenda mapenzi yake hata kama ni kuhusu jambo gumu, lisilo la raha, lisilopendeza au la gharama kubwa. Inatubidi tufurahie kutenda mapenzi yake … na tufanye kutoka mioyoni mwetu, Zaburi 40:8 na Waefeso 6:5-6.

**MAONYO**

**Neno Lake.** Mungu *hatatupatia* ushauri wake mahususi unaokwenda kinyume cha Neno lake. *Hataongoza* kinyume cha Neno lake … haijalishi kiwango cha ushauri tunadhani tunacho … haijalishi ushauri tutakaopata … au aina gani ya mazingira tulimo, wala amani tunayoihisi. Liamini neno la Mungu katika hali hizi zote.

**Miadi.** Gideoni alifanya miadi na Mungu ili apate kujua mapenzi yake kuhusu hali ya vita iliyomkabili. Hiki chaweza kuwa kitendo hatari kufanya. Gedioni alihofia hasira ya Mungu ingewaka juu yake kwa kutomwamini kikamilifu. Hali ya kumtaka Mungu kuthibitisha ikiwa yuko upande wako si jambo rahisi kudiriki kufanya siku hizi, jinsi ilivyokuwa zamani. Siku hizi tunaweza kuweka miadi kama hiyo na Mungu, lakini baada ya maombi na kujihoji kwingi.

**Mateso.** Mateso si lazima yatokane na mapenzi ya Mungu. Mara nyingi ni mapenzi ya Mungu kuwa muumini apitie mateso. 1 Petro 3:17, 1 Petro 4:19, 2 Wakorintho 4:7-18. Mateso huenda yakakusaidia kutenda mapenzi ya Mungu. Mateso yanaweza kukusaidia kutenda mapenzi ya Mungu, 1 Petro 4:1-2. Mfano mzuri ni mateso wakati wa kanisa la awali, Matendo ya Mitume 8:1-4, ambayo yaliwalazimu waumini kupeleka injili nje ya Yerusalemu kama sehemu ya kuafiki taarifa ya Yesu kwenye kitabu cha Matendo ya Mitume 1:8. Dhahabu hupitishwa kwenye tanuri ili kuifua, Isaya 48:10. Maisha rahisi na yenye ufanisi yanayoahidiwa na wale wanaohubiri injili ya afya nzuri na utajiri, hayamo kwenye ushauri wa bibilia.

**Uwakili Endelevu.** Mapenzi ya Mungu kwetu yanajumuisha ukuaji imara, jinsi tunavyojifunza kutembea naye. Musa alichukua muda wa maka 40 akitayarishwa kwa ajili ya majukumu yaliyokuwa mbele yake, akianza na kuchunga kondoo wasumbufu, kabla ya kipindi cha miaka 40 na wana wa Israeli jangwani. Baada ya kukutana na Mungu, ilimchukua mtume Paulo miaka 14 kujiandaa kwa ajili ya safari yake ya kwanza ya kimishenari. Yesu alifundisha kanuni hii katika Luka 16:10-13.

**Mikingamo.** Kutambua mapenzi ya Mungu kunahitaji uwiano. Ni hatari kuangazia tu upande mmoja wa kujua mapenzi ya Mungu [bila kuweka uwiano] huku tukipuuza sehemu nyingine za kujua mapenzi ya Mungu. Kuelekeza fikra zetu zote kwa kutumia hekima, bila kuzingatia amani ya Mungu ni jambo hatari … Huenda tukajaribiwa hata kutoshirikisha mwongozo wa Roho Mtakatifu kwenye lolote tufanyalo.

**Majibu ghushi.** Jihadhari na majibu ghushi yanayofundishwa katika jina la Ukristo. Hakuna njia za mkato, vimbwanga wala majibu ya kimiujiza kuhusu kumjua Mungu. Hakuna ujuzi wa mara moja unaotupatia majibu ya kujua mapenzi ya Mungu. Hakuna ujuzi mmoja tu unaotosha kutupatia hekima.

Acts One Eight [Matendo Moja Nane] huchapisha tafsiri hii ya Kiswahili ya kozi ya lugha ya Kiingereza ya *Disciplemaking 1 … Abiding in His Word*. Unaweza kunakili kozi hii au sehemu yake yoyote bila malipo au kwa gharama ya usambazaji pekee, bila kubadilisha maudhui yake na ukiwa umeambatanisha kauli hii ya chanzo. Kozi hii inapatikana bila malipo katika lugha ya Kiswahili kutoka katika www.Theolojia.org au katika lugha ya Kiingereza kutoka katika www.VIrtualBibleAcademy.org. Kwenye tovuti hizi, unaweza kusoma mtandaoni, kufundishwa, kupakua, au kuchapisha nakala zako mwenyewe. Nukuu za Biblia ya Kiswahili zimetoka katika Biblia ya Swahili Union Version (SUV) ya 1997.

*Kufanya wafuasi 1 - Maswali ya Marudio*

# Somo la 8 - Mapenzi ya Mungu … ukurasa wa 110 - 113

Sehemu ya kujifunza ni kupitia kwa njia ya kutathmini … kuhifadhi maarifa mapya kwenye hifadhi ya muda mrefu. Chapisha nakala hii ya uchunguzi au utumie karatasi ya ziada kujibu maswali yafuatayo. Kisha rudia jaribio hili kwa kurejelea kitabu au bila kurejelea kitabu, fungua hadi utakapofanikiwa kujibu maswali yote. *Mitihani hii ya kujitathmini* inapatikana ikiwa na majibu sahihi kwenye VirtualBibleAcademy.org.

ANDIKA *"KWELI"* AU *"SI KWELI"* KANDO YA KAULI YA 1 - 9

1. *Mapenzi ya jumla* ya Mungu yanawahusu waumini wengi.

2. *Mapenzi mahususi* ya Mungu yanaweza kuwa tofauti kwa waumini tofauti.

3. Si mara moja Mungu hudhihirisha mapenzi yake kwetu kama matokeo ya utiifu wetu.

4. Waumini wanaweza kujua *mapenzi ya jumla* na *mapenzi mahususi* ya Mungu kwa ajili yao.

5. Mara nyingi mapenzi ya Mungu kwa Waumini ni mazuri.

6. Kanuni kutoka kwenye Bibilia zinahusu hali nyingi tofauti.

7. Mifano yote ya Kibiblia sharti ifuatwe.

8. Mungu hatatuongoza kutotii Neno Lake.

9. Hatua ya kwanza ya kupata *mapenzi mahususi* ya Mungu ni kutafuta amani yake.

10. Orodhesha amri tatu zilizo na maneno *"mapenzi ya Mungu."*

   a.

   b.

   c.

11. Hatua tatu za kujifunza *mapenzi mahususi* ya Mungu kwetu ni:

   a.

   b.

   c.

12. Katika kutafuta *mapenzi mahususi* ya Mungu, Waumini hupata mwongozo kutoka katika ______________________, ya Mungu, kutoka kati ka ______________________, yake, kutoka kwa ______________________, kutoka katika ___________________ yake.

13. *Kweli* au *Si Kweli*: Kwa kutafuta mapenzi ya Mungu kuhusu mtu binafsi, wengi watakaopiga kura ya kutafuta mapenzi yake, wingi wa kura miongoni mwa waumini ni kweli. ______________________

14. *Kweli* au *Si Kweli*: Amani ya Mungu ni uthibitisho wa mwisho kwa Muumini anayetafuta mapenzi mahususi ya Mungu. ______________________

15. *Kweli* au *Si Kweli*: Amani ya Mungu ni uthibitisho wa mwisho kwa muumini anayetafuta *mapenzi mahususi* ya Mungu kwake. ______________________

16. Kwa kutafuta *mapenzi mahususi* ya Mungu, majibu haya matatu yanawezekana:

    a.

    b.

    c.

17. Tunapojua *mapenzi yake mahususi*, sharti tuchukue ______________________.

18. Andika Isaya 40:31 hapa chini … kama ilivyoandikwa kwenye Bibilia yako.

# Somo la 8 - Mapenzi ya Mungu … maswali ukurasa wa 114 -115

Usitumie karatasi hizi za majibu kutafuta majibu yako. Tafadhali zitumie tu kuangalia ikiwa umepata majibu sahihi. Rejelea somo lako hadi utakapopata habari za kukusaidia kusahihisha majibu kwa maswali yako. Masomo yote, majaribio ya kutathmini na karatasi za majibu zinapatikana kwenye VirtualBibleAcademy.org.

ANDIKA *"KWELI"* AU *"SI KWELI"* KATIKA KAULI ZA 1 - 9

1. *Mapenzi ya jumla* ya Mungu yanawahusu waumini wengi. *SI KWELI*
2. *Mapenzi mahususi* ya Mungu yanaweza kuwa tofauti kwa waumini tofauti. *KWELI*
3. Si mara moja Mungu hudhihirisha mapenzi yake kwetu kama matokeo ya utiifu wetu. *KWELI*
4. Waumini wanaweza kujua *mapenzi ya jumla* na *mapenzi mahususi* ya Mungu kwa ajili yao. *KWELI*
5. Mara nyingi mapenzi ya Mungu kwa Waumini ni mazuri. *SI KWELI*
6. Kanuni kutoka kwenye Bibilia zinahusu hali nyingi tofauti. *KWELI*
7. Mifano yote ya Kibiblia sharti ifuatwe. *SI KWELI*
8. Mungu hatatuongoza kutotii Neno Lake. *KWELI*
9. Hatua ya kwanza ya kupata *mapenzi mahususi* ya Mungu ni kutafuta amani yake. *SI KWELI*
10. Orodhesha amri tatu zilizo na maneno *"mapenzi ya Mungu."*

    a. *Jiepushe na mtego wa uzinzi.*

    b. *Furahini kila wakati, ombeni bila kukoma, katika kila jambo mshukuruni Mungu.*

    c. *Tii kila mamlaka ya binadamu.*

11. Hatua tatu za kujifunza kujua *mapenzi mahususi* ya Mungu kwetu ni:

    a. *Uliza (omba).*

    b. *Pata mwongozo.*

    c. *Tenda.*

12. Katika kutafuta *mapenzi mahususi* ya Mungu, Waumini hupata mwongozo kutoka katika ______*Neno*______, ya Mungu, kutoka katika ______*Hekima*______, yake, kutoka kwa ______*Watu*______, kutoka katika ______*Amani*______ yake.

13. *Kweli* au *Si Kweli*: Kwa kutafuta mapenzi ya Mungu kuhusu mtu binafsi, wengi watakaopiga kura ya kutafuta mapenzi yake, wingi wa kura miongoni mwa waumini ni kweli. ______*Si Kweli*______

14. *Kweli* au *Si Kweli*: Amani ya Mungu ni uthibitisho wa mwisho kwa Muumini anayetafuta mapenzi mahususi ya Mungu. ______*Si Kweli*______

15. *Kweli* au *Si Kweli*: Amani ya Mungu ni uthibitisho wa mwisho kwa muumini anayetafuta *mapenzi mahususi* ya Mungu kwake. ______*Kweli*______

16. Kwa kutafuta *mapenzi mahususi* ya Mungu, majibu haya matatu yanawezekana:

a. *Ndiyo*

b. *Hapana*

c. *Subiri*

17. Tukijua *mapenzi yake mahususi*, sharti tuchukue ___*hatua (ikiwa na maana kutii)*___

18. Andika Isaya 40:31 hapo chini … kama ilivyoandikwa katika Bibilia.

*(Inapaswa kunakiliwa neno kwa neno kama ilivyoandikwa katika Biblia yako)*

## Kufanya Wanafunzi 1 - Kudumu Katika Neno Lake

# SOMO LA 9 - KATIKA MWILI

*“Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo.”* Waefeso 4:15-16

Kuzaliwa kwetu kiroho kulituweka katika familia ya Mungu ... katika Mwili wa Kristo. Mambo ya ajabu yalitokea *tulipomwamini* Yesu Kristo. Kabla ya hapo tulikuwa wafu ... kisha tukawa hai. Tulikuwa maadui wa Mungu ... na baadaye tukawa marafiki zake. Tulikuwa gizani ... kisha tukaingia kwenye nuru. Hata hivyo, maisha yetu mapya yana umuhimu zaidi kuliko mabadiliko ya kibinafsi yaliyotokea maishani mwetu. Pia tuliweza kuwa sehemu ya Mwili wake. Tukawa viungo sawa na muhimu katika Mwili pamoja na Waumini wengine.

Maisha yetu katika Mwili pamoja na Waumini wengine yana baraka na majukumu maalum. Biblia inatupa vielelezo kadhaa ili kutusaidia kuelewa maana ya kuwa katika Mwili. Sisi ni sehemu ya Mwili wa Kristo ... familia ya Mungu ... bibi arusi wa Kristo ... nyumba ya Mungu ... hekalu ... nuru ... taifa ... mzabibu ... na kundi la kondoo. Kuelewa maana ya vielezo hivi kunatusaidia kufanya kazi ipasavyo kama sehemu ya Mwili.

Biblia inatupa maagizo ya wazi juu ya jinsi ya kufanya kazi katika Mwili. Kwa kutii Neno la Mungu, tunapaswa kufuatilia kuzaliwa kwetu kiroho kwa ubatizo wa maji kama ishara ya nje ya utambulisho wetu na kifo chake, kuzikwa kwake, na ufufuo wake. Zaidi ya hayo, tunahitaji kuwa pamoja ... kushiriki rasilimali zetu ... kufundishwa ... kuabudu ... kuomba ... na kukumbuka kifo chake kwa njia ya Meza ya Bwana. Pia tumeagizwa kupendana, kuhifadhi umoja, kuwa safi, na kuonyesha upendo kwa matendo.

Mungu ametupa rasilimali tunazohitaji ili tufanye kazi ipasavyo katika Mwili. Yesu ametoa aina nne za *watu maalum* ili kutuandaa. Zaidi ya hayo, Roho Mtakatifu huwapa Waumini *uwezo maalum*, karama za kiroho ... akituwezesha kufanya sehemu yetu katika Mwili wa Kristo. Matumizi yetu ya rasilimali hizi kwa njia inayofaa, kadiri tunavyochukua nafasi zetu zinazotufaa katika Mwili wake, husababisha Mwili mzima kukua katika nyanja zote ili kumletea Kristo utukufu.

## VIELELEZO TISA VYA MAISHA PAMOJA NA WAUMINI WENGINE

Vielezo hivi vinatoa ufahamu kuhusu nafasi, baraka, na wajibu wetu katika Mwili wa Kristo. Kuna athari za kila moja ya vielelezo hivi vinavyohusu uhusiano wetu na Mungu ... na Waumini wengine ... na watu waliopotea.

**1. Mwili wa Kristo.** Yesu Kristo ndiye Kichwa cha Mwili, Waefeso 1:22-23 na Wakolosai 1:18. Hakuna mshirika mwingine ambaye ni Kichwa ... Yesu pekee ndiye kichwa. Kila muumini ni sehemu muhimu ya Mwili, Warumi 12:4-5, Waefeso 5:30, 1 Wakorintho 12:12-27. Kuna sehemu nyingi tofauti za Mwili. Sehemu zote hazifanani. Kila sehemu lazima ifanye kazi yake binafsi. Hakuna nafasi kwa ubinafsi au upendeleo. Lengo letu ni kukua katika upendo hadi Mwili ufikie kimo kamili kinacholingana na Kichwa, Waefeso 4:11-16.

**2. Familia ya Mungu.** Mungu ni baba yetu, Mathayo 6:9, 23:9, 2 Wakorintho 6:18. Sisi ni watoto wake, Wagalatia 3:26, 1 Yohana 3:1-2. Yesu ni ndugu yetu mzaliwa wa kwanza, Waebrania 1:6, 2:17. Mzaliwa wa kwanza ni nafasi ya mamlaka katika familia ... hiyo haimaanishi kwamba Yesu hakuwepo kabla ya Bethlehemu. Alizaliwa huko kama Mungu-mwanadamu. Alizaliwa kama ndugu yetu mzaliwa wa kwanza. Hata hivyo, amekuwepo daima. Pia, sisi ni warithi pamoja naye, Warumi 8:14-17, Wagalatia 4:7. Tuna ushirika na Baba, Yesu, na kila mmoja wetu, 1 Yohana 1:3, 1 Wakorintho 1:9, Mathayo 23:8. Sisi ni sehemu ya familia ya ajabu ya Mungu. Na katika muktadha huo, Yesu alisema, “Msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni mmoja, aliye wa mbinguni,” Mathayo 23:9.

**3. Bibi Harusi wa Kristo.** Yesu ndiye bwana arusi, Yohana 3:29, Mathayo 25:1-13, Luka 5:34. Sisi ni bibi harusi, tulioposwa na Kristo, tukijiandaa kwa ajili ya arusi, 2 Wakorintho 11:2, Waefeso 5:25-33. Kielelezo hiki ni cha kutarajia. Tunasubiri kurudi kwa Bwana arusi wetu na karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo, Ufunuo 19:7-9.

**4. Nyumba ya Mungu.** Tunajengwa kuwa makao yake. Mungu ndiye mjenzi wa nyumba yake, Waebrania 3:2-6. Kristo ndiye jiwe la pembeni ... na mitume na manabii ndio msingi, Waefeso 2:19-22. Sisi ni mawe yaliyo hai yaliyotumiwa kujenga nyumba yake, 1 Petro 2:4-5. Nyumba ya Mungu haikujengwa kwa matofali na vijiti. Nyumba ya Mungu inajengwa kwa damu na nyama. *“Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho,”* Waefeso 2:22. *“Bali Kristo, kama mwana, juu ya nyumba ya Mungu; ambaye nyumba yake ni sisi,”* Waebrania 3:6.

**5. Hekalu la Mungu.** Israeli ilikuwa na hekalu. Hata hivyo, sisi ni hekalu. Yesu ndiye Kuhani wetu Mkuu, Waebrania 3:1, 4:14-15, 5:5-6, 9:11-12. Na sisi ni makuhani binafsi wanaojiwakilisha wenyewe moja kwa moja kwa Mungu. Kama makuhani katika Hekalu lake, tunapaswa kutoa *dhabihu sita.*

| | |
|---|---|
| Dhabihu 1 | ni miili yetu kama dhabihu iliyo hai ... takatifu na ya kumpendeza Mungu, Warumi 12:1. |
| Dhabihu ya 2 | ni sifa zetu ... kumtambua Mungu kwa shukrani kwa ajili ya jinsi alivyo, Waebrania 13:15. |
| Dhabihu ya 3 | ni *matendo yetu mema* ... kama mwitikio wetu kwa wokovu, Waebrania 13:16. |
| Dhabihu ya 4 | ni *koinonia* yetu ... neno la Kigiriki linalomaanisha ushiriki wa muumini katika rasilimali za pamoja na ushirika, Waebrania 13:16. |
| Dhabihu ya 5 | ni *mioyo yetu iliyovunjika na kupondeka* ... iliyonyenyekea, iliyojeruhiwa, na kupondwa, Zaburi 51:17. |
| Dhabihu ya 6 | ni tunda letu la Waumini wapya ... wale tunaowasaidia kumwamini Kristo, Warumi 15:16. |

**VILELEZO TISA … mwendelezo**

**6. Nuru.** Mungu ni nuru na ndani yake hamna giza, 1 Yohana 1:5, Ufunuo 21:23. Sisi ni wana wa nuru, 1 Wathesalonike 5:5. Yohana alisema kwamba Yesu alikuwa nuru ya kweli, Yohana 1:4-5, 9.

Yesu alisema kuwa yeye ni nuru ya ulimwengu, Yohana 8:12, 12:46. Alisema, *"Muda nilipo ulimwenguni, mimi ni nuru ya ulimwengu,"* Yohana 9:5.

Baada ya kupaa kwake, tulifanyika nuru ya ulimwengu. Yesu alisema, *"Ninyi ni nuru ya ulimwengu,"* Mathayo 5:14. Ni lazima tuenende katika nuru, Waefeso 5:8, 1 Yohana 1:7. Sisi ni nuru inayoangaza katika ulimwengu unaoishi gizani, Mathayo 5:14-16, Wafilipi 2:15.

**7. Taifa.** Israeli ni taifa maalum kwa Mungu ... mboni ya jicho lake, Zekaria 2:8. Kanisa pia linatajwa kuwa taifa takatifu, 1 Petro 2:9. Hiyo haimaanishi kwamba Israeli na Kanisa viko sawa ... haviko sawa.

Kama Waumini, uraia wetu uko Mbinguni, Wafilipi 3:20. Sisi, kama Wakristo, ni raia wenza pamoja na watakatifu, Waefeso 2:19.

Zaidi ya hayo, sisi ni wageni katika ulimwengu huu. Tuko ulimwenguni ... lakini si wa ulimwengu, Yohana 17:14-16. Tuna jukumu katika nchi hii ya kigeni kama mabalozi wa Mfalme, 2 Wakorintho 5:20. Kama mabalozi, tuna huduma na ujumbe wa upatanisho, 2 Wakorintho 5:18-19.

**8. Mzabibu.** Yesu ni mzabibu na sisi ni matawi Yohana 15:1, 5. Hii inaonyesha jinsi tunavyomtegemea Yesu. Pia inatuonyesha wajibu wetu wa kuzaa matunda, Yohana 15:1-16. Tunamletea Baba utukufu kwa kuzaa matunda, Yohana 15:2 ... matunda mengi, Yohana 15:8 ... na matunda yanayodumu, Yohana 15:16.

Baba yetu ndiye mkulima, Yohana 15:1. Anatupogoa, wakati mwingine kwa uchungu, ili tuzae matunda zaidi, Yohana 15:1-2. Na kuzaa matunda huyatia maombi yetu nguvu, Yohana 15:16.

**9. Kundi la Kondoo.** Yesu ndiye Mchungaji Mkuu, 1 Petro 5:4, Waebrania 13:20. Yeye ndiye Mchungaji Mwema, Yohana 10:14-16. Yeye ndiye mlango wa kondoo, Yohana 10:7. Sisi ni kondoo wake ... tukifuata sauti yake, Yohana 10:3-4, 27-28.

Mchungaji huwaongoza na kuwalinda kondoo wake. Alitoa maisha yake ili kutulinda kutokana na hatari ya milele ya dhambi, Yohana 10:11. Jinsi Mungu anavyowatunza kondoo wake kwa njia ya ajabu imeelezwa katika Zaburi 23, Ezekieli 34:1-31, na Yohana 10:1-30.

Mungu alisema, *"Na ninyi, kondoo zangu, kondoo za malisho yangu, ni wanadamu, na mimi ni Mungu wenu, asema Bwana MUNGU,"* Ezekieli 34:31. Mungu ndiye mchungaji wetu ... hiyo ni faraja kuu. Siku moja tutakuwa kundi moja la kondoo pamoja na Israeli, Yohana 10:6.

## MAISHA KATIKA MWILI WA KRISTO

**Kuzaliwa.** Hatua yetu ya kwanza ni kuzaliwa kiroho. Yesu alimwambia Nikodemo, *"Hamna budi kuzaliwa mara ya pili,"* Yohana 3:7. Hakuna mtu ambaye ni sehemu ya Mwili hadi yeye binafsi azaliwe mara ya pili. Tumezaliwa katika Mwili wa Kristo. Paulo alieleza hiyo kama ubatizo wa kiroho katika 1 Wakorintho 12:13, *"Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja."* Kuanzia hatua hiyo ya kwanza, kila muumini anahitaji kukua ili awe sehemu ya Mwili inayofanya kazi ipasavyo ... achukue nafasi yake inayomfaa ... akitumika na akitumikiwa.

**Ubatizo.** Ubatizo wa maji ni dhihirisho la nje la ubatizo wa ndani wa kiroho wa wokovu wetu. Yesu alibatizwa, Mathayo 3:13-17. Kila muumini anapaswa kubatizwa. Agizo Kuu linajumuisha amri ya *"mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu,"* Mathayo 28:19. Ubatizo wa maji ni tangazo la kujitambulisha kwetu na Kristo katika kifo chake, kuzikwa kwake na kufufuka kwake, Warumi 6:1-7. Utekelezaji rahisi wa amri hii ya Biblia ni ubatizo wa kuzamishwa majini baada ya kuzaliwa upya kiroho.

**Mifano Kutoka Katika Kanisa la Awali.** Kanisa la awali lilitutolea mifano mizuri ... mifano ya kile ambacho maisha yetu ya pamoja yanapaswa kujumuisha.

Kukusanyika pamoja, Matendo 2:1.

Kufundishwa, Matendo 2:42.

Ushirika, Matendo 2:42.

Kumega mkate [Meza ya Bwana], Matendo ya 2:42 na 46.

Kuomba pamoja, Matendo 2:42.

Kushiriki mali zao, Matendo 2:44-45.

Kula pamoja mara kwa mara, Matendo 2:46.

Kumsifu Mungu, Matendo 2:47.

Kuongezeka katika idadi … tunda la Waumini wapya, Matendo 2:47.

**Ibada.** Ibada ni sehemu muhimu ya maisha yetu kama Waumini ... tukiwa peke yetu au pamoja na wengine. Wanaume na wanawake wa Agano la Kale na Jipya walimwabudu Mungu katika maeneo na hali nyingi tofauti. Ibada inaweza kuwa kwa maneno au nyimbo. Yesu alisema, *"Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli,"* Yohana 4:24.

**Meza ya Bwana.** Mfano na mafundisho ya Kristo katika Mlo wa Mwisho, na maelezo ya Paulo, yalianzisha Meza ya Bwana kama wakati maalum wa ukumbusho kwa Wakristo tunapokusanyika pamoja. Tunapokula mkate na kunywa divai katika Meza ya Bwana, tunakumbuka dhabihu ya Kristo ya mwili wake na umwagaji wa damu yake kwa ajili yetu. Tunakumbuka gharama kubwa aliyolipa kwa ajili yetu. Katika Meza ya Bwana, pia tunapaswa kuangalia ndani yetu katika kujichunguza ... na tunapaswa kutazamia siku ambayo tutashiriki mlo wa Meza ya Bwana pamoja na Yesu katika ufalme wake, Mathayo 26:26-30, Marko 14:22-26; Luka 22:14-20, na 1 Wakorintho 11:23-24.

**Amri Nne.** Yesu alitangaza kwamba, *"Mkinipenda, mtazishika amri zangu,"* Yohana 14:15. Amri hizi nne ni muhimu sana kwa Mwili ili ufanye kazi ipasavyo. Amri hizi ni za kibinafsi na za pamoja. Mwili hufanya kazi ipasavyo ikiwa kila kiungo kinafanya kazi ipasavyo kwa kushirikiana na viungo vingine, Waefeso 4:16. Tumeamrishwa kupendana sisi kwa sisi ... kuhifadhi umoja ... kuwa safi ... na kuonyesha upendo kwa matendo.

**Amri ya 1 … Pendaneni.** Yesu alisema, *"Amri yangu ndiyo hii, Mpendane, kama nilivyowapenda ninyi,"* Yohana 15:12. Amri hii ndiyo msingi wa amri tatu zinazofuata. Upendo unapaswa kuwa mtazamo wetu wa kibinafsi na wa pamoja. Upendo unapaswa kuwa motisha ya matendo yetu yote kwa Waumini wenzetu. Mungu alitupenda ... kwa hivyo, tunapaswa kupendana sisi kwa sisi, 1 Yohana 4:11. Tunapaswa kupendana kwa dhati kutoka moyoni, 1 Petro 1:22. Kama vile Kristo alivyoyatoa maisha yake kwa ajili yetu, tunapaswa kuyatoa maisha yetu kwa ajili ya wenzetu, 1 Yohana 3:16. Ulimwengu utajua kwamba sisi ni wanafunzi wake kwa sababu ya upendo wetu sisi kwa sisi, Yohana 13:34-35. Kupendana huanza na mabadiliko katika mtazamo. *"Kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake,"* Wafilipi 2:3. Tumeamriwa kuonyesha upendo kwa matendo. *"Tumikianeni kwa upendo,"* Wagalatia 5:13.

**Amri ya 2 … Hifadhi umoja.** Hatujaamrishwa kuleta umoja. Umoja unatoka kwa Roho ... si kwetu. Kibinafsi na kwa pamoja, lazima *"tujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani,"* Waefeso 4:3. Yesu aliomba kwamba tuwe wamoja, Yohana 17:11, 21-23. Sala yake katika mstari wa 23 kimsingi ni kwamba tuwe kamili katika umoja ili ulimwengu uamini kwamba alitoka kwa Baba. Tunapaswa kuwa na moyo mmoja na roho moja, Matendo 4:32, Warumi 15:5. Tunapaswa kuwa na nia moja, 1 Wakorintho 1:10. Kuhifadhi umoja si rahisi. Kuhifadhi umoja kunahitaji kuchukua hatua bila kukoma.

*"Mfuate mambo ya amani,"* Warumi 14:19.

Onyesheni *"uvumilivu, mkichukuliana katika upendo,"* Waefeso 4:2.

Mkubaliane ninyi kwa ninyi, Warumi 15:7.

*"Basi tusizidi kuhukumiana,"* Warumi 14:13.

*"Mtu asitie kitu cha kumkwaza ndugu au cha kumwangusha,"* Warumi 14:13.

*"Lakini angalieni huu uwezo wenu usije ukawakwaza wale walio dhaifu,"* 1 Wakorintho 8:9.

*"Basi, mtu asiwahukumu ninyi,"* Wakolosai 2:16-17.

*"Msiwe nayo kwa kupendelea watu,"* Yakobo 2:1-9.

*"Ndugu, msisingiziane,"* Yakobo 4:11.

*"Ndugu, msinung'unikiane,"* Yakobo 5:9.

*"Lakini mkiumana na kulana, angalieni msije mkaangamizana,"* Wagalatia 5:15.

*"Hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo,"* Waefeso 5:21.

**Amri ya 3 … Kuwa safi.** *"Hamjui kwamba chachu kidogo hulichachusha donge zima?"* 1 Wakorintho 5:6. Swali hili la balagha (lisilohitaji jibu) linasisitiza athari ya dhambi ya mtu binafsi kwenye kikundi. Upendo haimaanishi kupuuza dhambi na madhara inayosababisha. Umoja si umoja ikiwa unapuuza usafi. Lazima tupendane sisi kwa sisi na tuhifadhi umoja ... kwa kukabiliana kwa ufanisi na dhambi iliyo katikati yetu. Aina tatu za dhambi lazima ziondolewe kutoka katika Mwili ... dhambi zetu za kibinafsi ... dhambi za wenzetu ... na dhambi ya mtu anayesababisha mgawanyiko au asiyetubu.

*Kwanza ...* lazima tukabiliane na <u>*dhambi zetu za kibinafsi*</u>. Dhambi ya mtu mmoja inaweza kuangamiza kundi kama ilivyofanya katika Yoshua 7 ... ambapo tamaa ya mtu mmoja ilipelekea kushindwa kwa jeshi lote la Israeli. Mwili unaweza kupata madhara kwa sababu ya kudanganyana ... na uasherati, uchafu wa kutamani, tamaa, maneno ya kipuuzi na mizaha michafu, Wakolosai 3:9, Waefeso 5:3-4. Zaidi ya hayo, muumini anayefanya uasherati humkosea na kumlaghai ndugu yake, 1 Wathesalonike 4:3-6. Kuna dawa ya dhambi zetu za kibinafsi ... Mungu atatusamehe na kututakasa tukiziungama dhambi zetu, 1 Yohana 1:9.

*Pili …* Lazima tukabiliane na <u>*dhambi za wenzetu*</u>. Katika kufanya hivyo tunaagizwa, *"jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, mkichukuliana, na kusameheana,"* Wakolosai 3:12-13. Wakati mwingine mtu lazima akaripiwe. *"Kama ndugu yako akikosa, mwonye; akitubu msamehe,"* Luka 17:3. Kuna mchakato wa Kibiblia wa hatua tatu wa kumkaripia ndugu, Mathayo 18:15-17. Kwanza, mkabili yeye binafsi. Akitubu, msamehe ... na mambo yaishie hapo. Hii ni hatua ya faragha. Haipaswi kufanywa hadharani kwa namna yoyote ile. Ikiwa hatua hiyo haitafua dafu, nenda kwa hatua ya pili. Mkabili ndugu huyo tena ... lakini wakati huu kuwa na shahidi mmoja au mashahidi wawili. Hawa ni zaidi ya mashahidi wa mkutano wako na ndugu huyo. Ni lazima wawe walishuhudia dhambi ya ndugu huyo. Ndugu huyo akitubu, msamehe ... na mambo yaishie hapo. Hii pia ni hatua ya faraghani. Hatimaye, ikiwa tatizo litakuwa bado halijatatuliwa, *"liambie kanisa; na asipolisikiliza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru" …* yaani kama mtu ambaye si Muumini, Mathayo 18:17. Lengo la kila moja ya hatua hizi, ikiwa ni pamoja na hatua ya 3, ni *"kumrejeza upya mtu kama huyo,"* Wagalatia 6:1. Katika kila hatua ya mchakato huu weka vifungu kama Waefeso 4:26, 32 na 1 Petro 4:8 katika akili na moyo wako.

*Tatu ...* lazima tukabiliane na <u>*dhambi ya mtu anayesababisha mgawanyiko au asiyetubu*</u>. Mtu asiyetubu, muovu, au anayesababisha mgawanyiko hapaswi kuvumiliwa. Tumeagizwa kwamba *"mtu aliye mzushi, baada ya kumwonya mara ya kwanza na mara ya pili, mkatae,"* Tito 3:9-11. Tunaagizwa *"mkajiepushe nao,"* Warumi 16:17. Hata hivyo, mtu anayesababisha mgawanyiko si lazima awe tu mtu ambaye hakubaliani na mchungaji. Tumeagizwa *"jitengeni nafsi zenu na kila ndugu aendaye bila utaratibu,"* 1 Wathesalonike 3:6. Tumeagizwa *"mwondoeni yule mbaya miongoni mwenu,"* 1 Wakorintho 5:11-13.

**Amri ya 4 … Onyesha upendo kwa matendo.** *“Watoto wadogo, tusipende kwa neno, wala kwa ulimi, bali kwa tendo na kweli,”* 1 Yohana 3:18. Upendo bila matendo si upendo hata kidogo. Upendo wa kweli ni zaidi ya maneno. Upendo wa kweli husababisha matendo ya kweli. Yesu alikuwa dhihirisho kuu na kielelezo kikuu cha upendo. Aliutoa uhai wake kwa ajili yetu, 1 Yohana 3:16. Ili tuwe kama Yesu, tunapaswa kutoa maisha yetu katika kutumikiana. Ili tutumikiane kwa upendo tunahitaji kuwa pamoja. Tunapaswa kukusanyika pamoja na Waumini wengine. Usijaribu kuishi maisha ya Kikristo peke yako. Tunaagizwa kwamba *“tusiache kukusanyika pamoja,”* Waebrania 10:25. Hii inamaanisha zaidi ya kuhudhuria mikutano ya kidini. Muumini anaweza kuwa na kumbukumbu kamili ya kuhudhuria mikutano ya Kanisa lakini hajawahi kamwe kukusanyika pamoja na Waumini wengine katika Mwili kwa njia ya kweli. Tunapaswa *“kutafuta haki, na imani, na upendo, na amani, pamoja na wale wamwitao Bwana kwa moyo safi,”* 2 Timotheo 2:22. Yesu alisema, *“Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao,”* Mathayo 18:20. Yuko pamoja nasi tunapokusanyika pamoja mahali popote ... si tu tunapokutana katika jengo la kidini. Kusanyika pamoja na Waumini wengine ... na uonyeshe upendo kwa matendo. Zifuatazo ni baadhi ya njia za kuonyesha upendo kwa matendo:

Kuonyana, Warumi 15:14.

Kukaribisha wageni, Warumi 12:13.

Kujengana, Warumi 14:19.

Kufarijiana kwa maneno ya kurudi kwake, 1 Wathesalonike 4:18.

Kutendeana wema, Wagalatia 6:10.

Kutiana moyo, 1 Wathesalonike 5:11.

Kukidhi mahitaji ya kimwili ya kila mmoja, Warumi 12:13.

Kufurahi na kulia pamoja, Warumi 12:15.

Kuimba pamoja, Wakolosai 3:16.

Kuhimizana katika upendo na matendo mema, Wabrania 10:24.

Kuteseka pamoja, 1 Wakorintho 12:26.

Kuwasaidia walimu na wafanyakazi, Wagalatia 6:6, 1 Wakorintho 9:11,14.

Kuwasaidia wajane, 1 Timotheo 5:8-12.

## KARAMA ZA KIROHO

Mungu hutoa karama za aina mbili kwa Mwili wake. Yesu hutoa <u>watu maalum</u> *"kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke,"* Waefeso 4:12. Pia, Roho Mtakatifu hutoa <u>uwezo maalum</u> kwa ajili ya utumishi … uwezo mbalimbali kwa kila muumini. Kile tunachojua kuhusu vipawa vyote viwili tunajua kutoka katika Biblia. Hatuwezi kuruhusu yale tunayofanya au yale ambayo watu wengine wanafanya yaamue kile tunachoamini kuhusu karama.

**Watu maalum ... waliotolewa na Yesu ... ili kuandaa mwili.** Hawa ni watu maalum ... waandaaji walioelezwa katika Waefeso 4:11-16. Si kila muumini ni mmoja wa hawa wanne. Hizi si nyadhifa au ofisi ambazo watu wanateuliwa kwazo. Ni baadhi tu ya Waumini ndio watu hawa maalum. Wametolewa na Yesu ili kuwaandaa Waumini. Hawa si wafanyakazi wenye weledi walioajiriwa kufanya huduma kwa niaba yetu. Wametolewa ili kutuandaa kwa ajili ya kazi ya utumishi. Aina nne za viongozi ni mitume, manabii, wainjilisti, na wachungaji-walimu. <u>*Mitume*</u> ni wale waliotumwa kuweka msingi wa huduma zinazoanzishwa. <u>*Manabii*</u> hutangazia Mwili Neno la Mungu. <u>*Wainjilisti*</u> hutangazia waliopotea Neno la Mungu. <u>*Wachungaji-walimu*</u> huwalinda na kuwalisha watu wa Mungu. Ili kuelewa jukumu la kiongozi katika Mwili, mfikirie mwinjilisti. Mwinjilisti anapaswa kufanya kazi ya uinjilisti ... na anapaswa kuwaandaa Waumini kufanya uinjilisti.

**Uwezo maalum ... unaotolewa na Roho Mtakatifu ... kuuwezesha mwili.** Uwezo huu maalum, unaotolewa na Roho Mtakatifu, huwawezesha waumini ... kufanya kazi ya utumishi. Karama hizi hazipaswi kuchukuliwa kuwa ni uwezo wa asili, wa kujifunza au vipaji. Kwa mfano ... baadhi ya Waumini wanaweza kuwa na kipaji walichopewa na Mungu cha kuimba. Huenda wamejifunza mengi kuhusu muziki. Huenda wamefanya mazoezi ya sauti. Hata hivyo, Waumini hao hawana karama ya kiroho ya uimbaji ... hakuna karama kama hiyo. Mambo fulani ya Kibiblia ni ya kweli kuhusu karama za kiroho zinazotolewa na Roho. Biblia inafafanua karama hizi za kiroho. Kile tunachoamini, yale tunayofanya, na viongozi wa kanisa hawafafanui upya karama za kiroho kwa njia yoyote inayopinga au kuongeza kitu katika ufafanuzi wa Biblia.

> Kila muumini hupewa angalau karama moja ya kiroho na Roho Mtakatifu, 1 Wakorintho 12:7, na 1 Petro 4:10.
>
> Karama zinatolewa kwa msingi wa mapenzi ya Roho badala ya matakwa yetu wenyewe, 1 Wakorintho 12:11.
>
> Karama hizi ni kwa manufaa ya wote badala ya manufaa ya mtu binafsi, Warumi 12:4-5, 1 Wakorintho 12:7 na 1 Wakorintho 12:12-27.
>
> Kuna uwezekano kwamba zinaweza kupotezwa, Mathayo 25:14-29.
>
> Kumbuka: Warumi 11:29 inahusika na Israeli, si Mwili
>
> Karama ya/za kiroho ambayo/ambazo umepewa (imeamuliwa/zimeamuliwa) na Roho, 1 Wakorintho 12:4.
>
> Huduma ambapo unazitumia zimeamuliwa na Kristo, 1 Wakorintho 12:5.
>
> Ufanisi wa karama yako ni kazi ya Baba, 1 Wakorintho 12:6.
>
> Jukumu lako ni utiifu.

**Kugundua karama yako/zako ya/za kiroho.** Kuamua una karama gani kunachukua muda na uzoefu. Unaweza kugundua karama yako/zako kwa kujifunza kwanza kile Biblia inasema juu ya karama hizo ... kwa kuhusika katika huduma ... kisha kwa kutathmini kile ambacho Mungu anafanya kupitia kwako. Fanya ubashiri wa kiroho wenye busara kuhusu karama ambayo huenda unayo ... jihusishe na huduma inayolingana na karama hiyo ... ipe muda ... kisha tathmini kile ambacho Mungu amefanya. Karama yako/zako itadhihirika/zitadhihirika unapohudumu.

**Ufafanuzi wa Biblia.** Karama za kiroho zimeelezwa katika Biblia katika marejeo mawili makuu, Warumi 12 na 1 Wakorintho 12-14. Huku akijua mwelekeo wetu wa asili wa kugawanyika, Roho Mtakatifu aliweka sura kuu juu ya upendo, 1 Wakorintho 13, katikati ya mafundisho yake juu ya karama. Acha Biblia ifafanue karama za kiroho. Omba na ujifunze Biblia ili kuunda imani yako kuhusu karama za kiroho. Usiaamue kwa msingi wa osmosisi ... ukifyonza yale unayoamini kutoka kwenye mazingira yako ya kiroho. Acha Biblia iingie katika yale unayofanya. Usiruhusu yale unayofanya yaingie katika Biblia. Kila muumini amepewa karama moja au zaidi za kiroho. Aina za uwezo huo maalum zimeorodheshwa hapa chini kwa mpangilio wa kialfabeti ... si kwa mpangilio wa umuhimu. Kila muumini hana karama zote. Hata hivyo, Waumini wote wana wajibu katika kila moja ya nyanja hizi.

**1. Kupambanua Roho.** Baadhi ya Waumini wana uwezo maalum wa kupambanua mema na mabaya ... kati ya kile ambacho ni cha Mungu au cha ulimwengu, mwili na ibilisi. Waumini wote wanapaswa kuwa na uwezo wa kupambanua mema na mabaya, Waebrania 5:14, 1 Yohana 4:1.

**2. Uhimizaji.** Huu ni uwezo maalum wa kuwachochea, kuwahamasisha, au kuwatia moyo wengine. Inaweza kuitwa karama ya kutia watu moyo. Baadhi ya Waumini wana karama hii ... lakini Waumini wote wanapaswa kutiana moyo, Waebrania 3:13, 10:25.

**3. Imani.** Huu ni uwezo wa ziada wa kumwamini Mungu kwa uthabiti kwa ajili ya mambo yasiyowezekana kwa wanadamu. Inaweza kuonekana wakati mtu anaendelea kushikilia jambo wakati wengine wanaliachilia ... au anaachilia jambo wakati wengine wanaendelea kulishikilia. Imani hii si kubuni taswira ya kitu fulani akilini mwako na kumlazimu Mungu akupe kitu hicho. Imani hii si *kutaja* kitu na kinamlazimu Mungu akupe kitu hicho kwa sababu umenena. Imani hii ni kumtumainia Mungu kwa moyo wote kufanya kile atakachoamua. Baadhi ya Waumini wana karama hii ... lakini Waumini wote wanapaswa kuwa na imani, 2 Wakorintho 5:7.

**4. Kutoa.** Huu ni uwezo maalum wa kumpa Mungu, kupitia wengine, kile alichotupa. Huu ni uwezo maalum wa kujua kile unachopaswa kutoa ... yule unayepaswa kumpa ... na wakati wa kutoa. Inahusiana zaidi na ubora wa utoaji kuliko ukubwa wa kile kinachotolewa. Wakati mwingine Mungu huchanganya karama ya kutoa na rasilimali za ziada ... hiyo ni fursa na wajibu wa ajabu kwa mtu aliye na karama hii ya kiroho. Baadhi ya Waumini wana karama hii ... lakini Waumini wote wanapaswa kutoa, 2 Wakorintho 9:7.

**5. Uponyaji**. Huu ni uwezo maalum wa kutumiwa na Mungu katika uponyaji wa kimwili, kihisia, au kiroho. Usitarajie Waumini wote waponywe kimwili. Paulo hakuponywa, 2 Wakorintho 12:7-10. Trofimo hakuponywa, 2 Timotheo 4:20. Pia, hatujawahi kuona wanaume na wanawake wakuu wa imani wakiponywa kutokana na magonjwa ya uzeeni ... watu wote hatimaye hufa. Wakati mwingine Mungu huponya baadhi ya watu kupitia wale walio na karama ya uponyaji. Si Waumini wote wana karama hii ... lakini Waumimi wote wanaweza kutafuta uponyaji, Yakobo 5:14-16.

**6. Maarifa.** Huu ni uwezo maalum wa kuelewa Neno la Mungu. Ikiwa ni maarifa yanayotolewa moja kwa moja na Mungu, yatalingana kikamilifu na Maandiko. Ikiwa si sahihi, au ikiwa yanapinga Biblia kwa njia yoyote ile, basi maarifa hayo hayajatoka kwa Mungu. Paulo aliandika kwamba kuna wakati karama hii itaondolewa, 1 Wakorintho 13:8-10. Baadhi ya Waumini wanaweza kuwa na karama hii ... lakini Waumini wote wanapaswa kutafuta zaidi maarifa ya Neno la Mungu, 2 Timotheo 2:15, Wakolosai 1:9-10.

**7. Uongozi.** Huu ni uwezo maalum wa kuwaongoza wengine katika kukamilisha kazi ya Mungu. Angalia nyuma yako. Je, kuna yeyote anayekufuata? Je, unawaongoza wengine kwa ufanisi ili watimize mapenzi ya Mungu? Uwezo wa uongozi duniani si sawa na karama ya uongozi. Kuwa kiongozi aliyechaguliwa au aliyeteuliwa katika kanisa haimaanishi kwamba mtu huyo ana karama ya uongozi. Karama hii hutolewa kwa baadhi ya Waumini ... lakini Waumini wote wana ushawishi wa uongozi juu ya watu wanaowazunguka, Mithali 12:26.

**8. Rehema.** Huu ni uwezo maalum wa kutenda matendo ya upendo. Rehema ni huruma ya kiutendaji inayoelekezwa kwa wasiostahili ... iwe ni watu wasiopendeza, maskini hohehahe, au walio katika dhiki au la. Ni baadhi tu ya Waumini walio na karama hii ... lakini Waumini wote wanapaswa kuwa wenye rehema, Yuda 1:2-23.

**9. Miujiza.** Huu ni uwezo maalum, unaotolewa na Roho Mtakatifu, wa kufanya matendo yenye nguvu yasiyoweza kufanywa na wanadamu. Hata hivyo, uwezo wa kufanya miujiza unaweza kutoka katika vyanzo vingine, Kutoka 7:10-13, Mathayo 7:21-23. Si Waumini wote wana karama hii ... lakini sote tuna nguvu, Yohana 14:12, Matendo 1:8.

**10. Unabii.** Huu ni uwezo maalum uliotolewa kwa baadhi ya Waumini kutangaza Neno la Mungu. Unabii unaweza kuwa tangazo lenye mamlaka lililo na nguvu ya *Bwana asema hivi* ... kama walivyofanya waandishi wa Agano Jipya. Pia, unabii unaweza kuwa utabiri wa kiungu wa matukio ya siku zijazo. Kutabiri matukio ya siku zijazo *kwa jina la Mungu* ni hatari, Kumbukumbu la Torati 18:22. Karama hii inaonekana ina mipaka, Ufunuo 22:18-19. Na Paulo aliandika katika 1 Wakorintho 13:8-10 kwamba kuna wakati karama hii itaondolewa. Unabii unaweza tu kuwa kutangaza, au tangazo la Neno la Mungu ... sawa na kuhubiri au tangazo la hadharani. Waumini wote wanapaswa kutangaza Neno la Mungu kwa kiasi fulani, Zaburi 145:4-12.

**11. Kuwatumikia Wengine.** Huu ni uwezo maalum wa kuwasaidia wengine. Si tu kuwasaidia wale walio katika huduma ... ingawa msaada hakika unahitajika katika muktadha huo. Aina hii ya huduma inaweza kuwa njia ya kujihusisha... na kutoka kwayo kuingia katika nyanja zingine kadiri karama nyingine zinavyodhihirika. Filipo alifanya huduma hii aliposaidia kuwagawia wajane chakula ... na kwa kufanya hivyo akawaondolea viongozi mzigo na hivyo wakapata muda wa maombi na wa Neno, Matendo 6:1-6. Muda mfupi baada ya hapo Filipo akawa mwinjilisti akimtangazia Injili towashi Mhabeshi ... kisha akawatangazia Injilia watu wa pwani ya Bahari ya Mediterania kutoka Azoto hadi Kaisaria. Wengine wana karama maalum ya kutumikia ... lakini sote tunapaswa kutumikiana, Wagalatia 5:13.

**12. Kufundisha.** Karama hii ni uwezo wa kuwasaidia wengine kujifunza na kutumia Neno la Mungu. Kufundisha watu Biblia ni zaidi ya kutangaza ukweli hadharani ... ni kufanya wanafunzi. Kushauri, kufunza mtu binafsi ana kwa ana na kufunza wanagenzi kunaweza kuwa sehemu ya mchakato huo. Kufundisha kunaweza kutekelezwa katika vikundi vikubwa, vikundi vidogo, au kwa kufundisha mtu mmoja kwa wakati mmoja. Idadi ya wanafunzi na umaarufu si kipimo cha ubora katika kufundisha, 2 Timotheo 4:3. Kipimo cha kweli cha ubora katika kufundisha ni maisha yaliyobadilika. Baadhi ya Waumini wana karama ya kufundisha ... lakini kila muumini anapaswa kumfundisha mtu, Mathayo 28:18-20.

**13. Lugha.** Karama ya kiroho ya lugha ni uwezo wa kunena katika lugha halisi, ambayo anayeizungumza haijui. Lugha si jumbe kutoka kwa Mungu kwenda kwa mwanadamu ... bali ni maombi yanayoelekezwa kwa Mungu, 1 Wakorintho 14:2,14. Karama ya kunena kwa lugha ni ishara kwa wasioamini, 1 Wakorintho 14:22. Haijengi Mwili ... bali inamnufaisha yule anayezungumza, 1 Wakorintho 14:4. Lugha hunenwa na watu wawili au wasiopungua watatu katika mkutano mmoja ... wakinena mmoja baada ya mwingine ... na siku zote hunenwa pale tu palipo na ufasiri, 1 Wakorintho 14:27-28. Matumizi ya karama ya kiroho ya lugha hayapaswi kuwa na mhemko au machafuko ... bali yanapaswa kutumika ipasavyo na kwa utaratibu, 1 Wakorintho 14:40. Paulo aliandika kwamba kuna wakati karama ya kunena kwa lugha itakoma, 1 Wakorintho 13:8-10. Si Waumini wote wana karama ya kiroho ya kunena kwa lugha, 1 Wakorintho 12:30 ... lakini Waumini wote wanapaswa kudhibiti ndimi zao wenyewe, Yakobo 1:26, 3:5-6.

**14. Ufasiri.** Huu ni uwezo unaotolewa na Roho wa kufasiri karama ya mtu mwingine ya lugha katika lugha ya wasikilizaji. Biblia haisemi ikiwa mfasiri anajua lugha moja au zote mbili. Lugha haipaswi kutumiwa kamwe bila ufasiri, 1 Wakorintho 14:27-28. Wakati ambapo lugha itakoma, ufasiri bila shaka pia utakoma.

**15. Hekima.** Huu ni uwezo maalum wa kutumia maarifa ya Neno la Mungu katika mambo magumu ya maisha. Baadhi ya Waumini wana karama hii ... lakini sote tunapaswa kujiendesha kwa hekima, Wakolosai 4:5. Tukikosa hekima tunapaswa kuomba ili tupewe, Yakobo 1:5.

## KARAMA ZA KIROHO ... Maswali na Majibu

**Majibu ya maswali kuhusu karama na ishara.** Kuna kutoelewa na kutofautiana kati ya Wakristo kuhusu ishara, maajabu, na karama za Roho. Mungu alitumia karama na ishara katika kanisa la awali ili kuthibitisha ujumbe wake, Waebrania 2:2-4. Tangu wakati huo, kanisa limeyapa mambo hayo msisitizo tofauti ... kuanzia kuyapuuza hadi kuyatumia vibaya. Tumia Biblia kama msingi wa yale unayoamini kuhusu mambo haya. Maswali kadhaa yanayojitokeza sana yamejibiwa hapa chini. Usiamini majibu haya kwa sababu tu yameandikwa hapa. Pia, usikatae mojawapo ya majibu haya kwa sababu tu yanakinzana na yale wewe au marafiki zako mnafanya. Kuza imani yako mwenyewe kuhusu mambo haya kupitia maombi na kujifunza Biblia. Kuwa Mberoya. Na usijihusishe na mambo yoyote yanayoenda kinyume cha ukweli wa Biblia. Kuwa mwangalifu sana kuhusu mambo yoyote yasiyokuwa katika Biblia ... hakika usiyatilie mkazo.

**1. *Je, ikiwa sina karama ya uinjilisti nishuhudie hata hivyo?*** Unapaswa kushuhudia. Umeamrishwa kushuhudia. Pia, *huna* karama ya uinjilisti. Hakuna aliye na karama hiyo kwa sababu hakuna karama ya uinjilisti. Kuna wainjilisti, waliotolewa na Yesu kuwaandaa Waumini, Waefeso 4:11-13. Lakini Biblia haitaji kamwe karama ya uinjilisti inayotolewa na Roho. Uinjilisti ni wajibu ... si karama.

**2. *Je, karama za Roho zinapatikana leo?*** Baadhi ya watu wanaamini kwamba karama zilitolewa kwa kanisa la karne ya kwanza tu. Wanatumia Waebrania 2:2-4 kujumuisha ishara, maajabu, miujiza na karama katika kuanzishwa kwa kanisa. Kisha wanapanua ufasiri wao wa kifungu hicho kuyatenga mambo hayo na vizazi vinavyofuata. Wanaonyesha mtindo ambapo matukio ya kimuujiza yanatokea sana wakati wa mabadiliko ... Kutoka, manabii, maisha ya Yesu, na kuundwa kwa kanisa. Hata hivyo, hakuna ushahidi wa kushawishi wa Kibiblia kwamba ishara, maajabu, miujiza na karama zilikuwa kwa ajili ya kizazi cha kwanza tu cha kanisa. Pia, ikiwa tuko katika *nyakati za mwisho*, basi hiki nacho ni kipindi cha mabadiliko.

**3. *Je, karama zote zinapatikana leo?*** Wakristo hawakubaliani kuhusu upatikanaji wa unabii, maarifa, lugha, na ufasiri ... kutokana na fasiri zinazokinzana za 1 Wakorintho 13:8-13. Kifungu hicho kinasema kwamba karama hizo zitakoma *"ile iliyo kamili"* itakapokuja. Mtazamo mmoja ni kwamba *ile iliyo kamili* ilikuwa ni kukamilika kwa Agano Jipya, ikizingatiwa kuwa Ufunuo 22:18-19 ndio mwisho wa unabii, na hivyo karama hizo nne hazipatikani tena. Mtazamo mwingine ni kwamba *ile iliyo kamili* ni kurudi kwa Kristo, na hivyo karama hizo zitapatikana kwa Waumini hadi Yesu atakaporudi. Biblia haisemi wazi *"ile iliyo kamili*" ni nini ... au itakuja lini. Kwa hivyo, kuna shaka juu ya upatikanaji wa karama hizo nne. Suala hili halijaelezwa wazi. Hivyo, ni bora zaidi utiifu wetu na yale tunayofanya yaongozwe na matumizi makamilifu ya sheria na mipaka ya Biblia. Ikiwa karama fulani inapatikana leo, na inatoka kwa Mungu, basi maagizo yake yote kuhusiana na karama hiyo yatatimizwa. Ikiwa hayatatimizwa, karama hiyo haijatoka kwa Mungu.

**4. Je, ishara, maajabu na miujiza yote ni ya Mungu?** Hapana! Mawakala wa Shetani wanaweza kufanya miujiza. Wachawi wa Farao waliiga muujiza wa Musa, Kutoka 7:10-12. Simoni, mtu ambaye hakuwa ameokoka, aliwashangaza watu kwa uchawi wake, Matendo 8:9-13. Na Shetani hujigeuza kuwa malaika wa nuru na watumishi wake hujigeuza kuwa watumishi wa haki 1 Wakorintho 11:13-15. Hao pamoja na mitume wa uwongo na wafanyakazi wadanganyifu wanaweza kufanya ishara na maajabu, Mathayo 7:22-23. Dini na madhehebu mengi ya uwongo hudhihirisha ishara, maajabu, na hata kunena kwa lugha kama vishawishi vya kuwavuta watu mbali na Mungu wa kweli.

**5. *Watu humaanisha nini wanapohalalisha yale wanayofanya kwa kusema … Mungu si Mungu wa machafuko?*** Kile wanchofanya kinaweza kuwa ni cha Mungu au la. Hata hivyo, matumizi yao ya maneno hayo kutetea kitendo fulani si jambo la

busara. Ni kweli kwamba Mungu kamwe si Mungu wa machafuko, 1 Wakorintho 14:33. Hata hivyo, kuna vyanzo vingine vya machafuko. Kuna roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani, 1 Timotheo 4:1-3. Kuna walimu wa uwongo, 2 Petro 2:1. Biblia inapaswa kuwa msingi wa yale tunayofanya. Yale tunayofanya, hata kwa msingi wa Ukristo, hayawezi kujithibitisha kuwa ni ya kweli.

**6. *Je, kuanguka chini ya nguvu ya Roho kunatoka kwa Mungu?*** *Kuanguka chini ya nguvu ya Roho* kunamaanisha mtu kuanguka chini baada ya kuguswa na kiongozi. *Kuanguka katika Roho* ni tukio hilo hilo lakini bila kuguswa na kiongozi. Wasioamini wakianguka chini, Yohana 18:6, na Roho kumnyakua Filipo kutoka kwa towashi Mhabeshi, Matendo 8:39, si mifano ya *kuanguka chini ya nguvu ya Roho.* Hakuna mifano wala mafundisho ya Kibiblia kuhusu tukio hili. Tukio la kile kinachoitwa *kuanguka chini ya nguvu ya Roho* ni tukio lisilokuwa katika Biblia ... kitu kinachoonekana kikitokea lakini hakipatikani katika Biblia.

**7. *Je, si lugha zinapaswa kuwa maarufu leo kama ilivyokuwa katika kitabu cha Matendo?*** Takriban miaka 30 ya historia ya kanisa la awali imeandikwa katika kitabu cha Matendo. Zaidi ya maeneo 50 ya kijografia yametajwa katika Matendo. Na safari za umisionari za Paulo zilikwenda zaidi ya maili 7500 [kilomita 12000]. Katika hayo yote, lugha za kimuujiza zimetajwa mara tatu tu ... katika siku ya Pentekoste huko Yerusalemu, Matendo 2 ... na Injili ilipowafikia Mataifa, Matendo 10:43-48 ... na huko Efeso wakati baadhi ya wanafunzi wa Yohana Mbatizaji walimwamini Yesu, Matendo 19:1-7. Lugha *si* jambo la kawaida katika kitabu cha Matendo.

**9. *Je, lugha ni lugha halisi au inaweza kuwa aina yoyote ya matamko?*** Hakuna chochote katika Biblia kinachoonyesha kwamba lugha si lugha halisi. Neno *isiyojulikana* limetumiwa pamoja na neno lugha mara kadhaa katika tafsiri ya King James ya 1 Wakorintho 14. Hata hivyo, hakuna neno la Kigiriki la *isiyojulikana* katika mistari hiyo kama ilivyoandikwa kiasili [2,4,13,14,19, na 27]. Lugha haikujulikana na yule anayeizungumza ... lakini yamkini ilijulikana katika historia ya wanadamu. Wengine husema inaweza kuwa ni lugha ya malaika, 1 Wakorintho 13:1 ... lakini hakuna chochote kinachoonyesha kwamba malaika huzungumza kwa kupayuka maneno yasiyo na mpangilio. Malaika katika Biblia walizungumza kwa maneno yenye mpangilio, Luka 2:8-14, Ufunuo 5:11-12. Neno la Kigiriki katika Biblia linalotumiwa kumaanisha ulimi/ndimi linamaanisha kiungo cha mwili ndani ya kinywa cha mtu ... au lugha kama inavyotumiwa katika Ufunuo 5:9, 13:7 na 17:15.

***10. Je, nitajuaje kama udhihirisho wa karama ya lugha ni ya kweli?*** Chanzo cha lugha ni muhimu. Lugha halisi inaweza kutoka kwa Roho Mtakatifu au kutoka kwa Shetani. Aina ya lugha yenye machafuko, mhemko na kupayuka inaweza kutoka kwenye upande wa kihisia wa mwili au kutoka kwa Shetani. Kuwa Mberoya, Matendo 17:11, chunguza Biblia. Lugha kutoka kwa Roho Mtakatifu italingana na kanuni *zote* za Biblia kuhusu lugha.

> Lugha ni maombi yanayoelekezwa kwa Mungu, 1 Wakorintho 14:2,14.
>
> Lugha ni ishara kwa wasioamini, 1 Wakorintho 14:22.
>
> Lugha inapaswa kunenwa na watu wasiozidi watatu katika kila mkutano, 1 Wakorintho 14:27.
>
> Lugha inenwe na mtu moja baada ya mwingine, 1 Wakorintho 14:27.
>
> Lugha inenwe tu pale palipo na ufasiri, 1 Wakorintho 14:27-28.
>
> Lugha itumike ipasavyo na kwa utaratibu, 1 Wakorintho 14:40.
>
> Na lugha kutoka kwa Roho itakuwa dhihirisho thabiti la tunda la Roho, *“Upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi,”* Wagalatia 5:22-23.

**11.** ***Je, napaswa kutafuta karama ya kunena kwa lugha?*** Si Waumini wote wamepewa karama ya kunena kwa lugha, 1 Wakorintho 12:30. Na karama zote za kiroho hutolewa kwa msingi wa mapenzi ya Roho Mtakatifu badala ya matakwa yetu, 1 Wakorintho 12:11. Paulo aliorodhesha karama kadhaa ... akiweka karama ya lugha mwishoni mwa orodha hiyo. Paulo aliandika *"Takeni sana karama zilizo kuu,"* 1 Wakorintho 12:28:31. Paulo alithamini upendo zaidi ya lugha, 1 Wakorintho 13:1. Paulo aliandika kwamba alipendelea zaidi unabii kuliko lugha, 1 Wakorintho 14:5. Pia aliandika kwamba angependelea kuzungumza maneno matano akitumia akili yake kuliko maneno 10,000 kwa lugha. Paulo alitambua karama ya lugha katika maisha ya wengine na katika maisha yake mwenyewe. Hata hivyo, mara nyingi alionya juu ya matumizi mabaya ya karama hii. Paulo aliandika, *"Msizuie kunena kwa lugha,"* 1 Wakorintho 14:39. Mtazamo mzuri kuhusiana na karama ya lugha ni hii ... *kuwa mwangalifu sana, usiitafute, na usiikataze.*

**12.** ***Na Je kuhusu lugha wakati wa maombi ya faragha?*** Wakristo wengine hupata lugha ya ajabu wanapoomba peke yao. Warumi 8:26 inafundisha kwamba Roho Mtakatifu hutuombea ... haombi kupitia kwetu. Yuda 1:20 inafundisha kwamba tunapaswa kuomba katika Roho ... lakini tunapaswa kufanya mambo yote katika Roho. Kuhalalisha lugha za faragha kutokana na vifungu hivi ni ufasiri unaovuka mipaka. Paulo alitamani kwamba wote wanene kwa lugha, 1 Wakorintho 14:5. Hata hivyo, si wote wanaweza kunena kwa lugha. Lugha inapaswa kunenwa na watu wawili au wasiozidi watatu katika mkutano ... wakinena kwa zamu ... na wanene tu ikiwa kuna mtu anafasiri, 1 Wakorintho 14:27-28. Kuanzia msitari wa 28, *"Lakini asipokuwapo mwenye kufasiri na anyamaze katika kanisa; aseme na nafsi yake tena na Mungu."* Hiyo inamaanisha watu wawili au watatu wenye karama ya kunena kwa lugha hadharani ambao wananyamazishwa kwa sababu hakuna mfasiri. Katika hali hiyo, watu hao wanaambiwa wasali faraghani badala ya hadharani. Hii inafundisha wazi kwamba lugha wakati wa maombi ya faragha si shughuli ya kawaida kwa Waumini wote. Wengine husema kwamba lugha wakati wa maombi ya faragha lilikuwa jambo maarufu sana katika kanisa la awali kiasi kwamba hapakuwa na haja ya kurekodi matukio hayo katika Biblia ... hata hivyo, mantiki ya aina hiyo ni upumbavu.

**13.** ***Kwa nini kuna mgawanyiko mwingi kuhusu ishara, maajabu, na karama za Roho?*** Paulo aliweka mistari mikuu juu ya upendo, 1 Wakorintho 13:1-8, katikati ya mafundisho yake kuhusu karama. Ukosefu wa upendo *na* ukosefu wa maarifa husababisha mgawanyiko mwingi katika Mwili. Wengine wamepata maoni yao juu ya mambo haya kutoka kwa Wakristo wengine badala ya kutoka kwa kusoma Neno kama inavyostahili ... wakichochea mgawanyiko kutokana na ukosefu wa maarifa ya Kibiblia. Pia, baadhi ya Wakristo wamekubali maoni ya viongozi wao au waandishi wanaowapenda ... badala ya kuunda maoni yao wenyewe kwa njia ya maombi na kujifunza Neno. Wachungaji wenye kushawishi wanaweza kugawanya kondoo ... wakikuza mgawanyiko kwa sababu ya maoni yao ya kibinafsi.

**14.** ***Karama ziko kwa sababu gani?*** Roho Mtakatifu ametupa *uwezo maalum* ili kutuwezesha. Na Yesu ametupa *watu maalumu* ili kutuandaa. Karama za Roho Mtakatifu na waandaaji wanaotolewa na Yesu wanatuwezesha kuishi kwa mafanikio katika Mwili wa Kristo ili tuweze *"kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo,"* Waefeso 4:15-16.

Acts One Eight [Matendo Moja Nane] huchapisha tafsiri hii ya Kiswahili ya kozi ya lugha ya Kiingereza ya *Disciplemaking 1 … Abiding in His Word*. Unaweza kunakili kozi hii au sehemu yake yoyote bila malipo au kwa gharama ya usambazaji pekee, bila kubadilisha maudhui yake na ukiwa umeambatanisha kauli hii ya chanzo. Kozi hii inapatikana bila malipo katika lugha ya Kiswahili kutoka katika www.Theolojia.org au katika lugha ya Kiingereza kutoka katika www.VIrtualBibleAcademy.org. Kwenye tovuti hizi, unaweza kusoma mtandaoni, kufundishwa, kupakua, au kuchapisha nakala zako mwenyewe. Nukuu za Biblia ya Kiswahili zimetoka katika Biblia ya Swahili Union Version (SUV) ya 1997.

# Somo la 9 - Katika Mwili ... ukurasa wa 118 - 131

Sehemu ya kujifunza ni kufanya marudio … kuhifadhi maarifa mapya kwenye kumbukumbu yako ya muda mrefu. Chapisha mtihani huu wa marudio au tumia karatasi tofauti kujibu maswali yafuatayo. Kisha rudia mtihani huu, ukisoma maelezo ya kozi au bila kuyasoma, hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi.
*Mitihani hii ya marudio* pamoja na majibu sahihi yanapatikana kwenye www.Theolojia.org.

ORODHESHA VIELELEZO 9 VYA MAISHA YETU KATIKA MWILI NA MSISITIZO WA KILA KIMOJA.

1. Kielelezo: ______________________ Msisitizo: ______________________
2. Kielelezo: ______________________ Msisitizo: ______________________
3. Kielelezo: ______________________ Msisitizo: ______________________
4. Kielelezo: ______________________ Msisitizo: ______________________
5. Kielelezo: ______________________ Msisitizo: ______________________
6. Kielelezo: ______________________ Msisitizo: ______________________
7. Kielelezo: ______________________ Msisitizo: ______________________
8. Kielelezo: ______________________ Msisitizo: ______________________
9. Kielelezo: ______________________ Msisitizo: ______________________

10. Orodhesha dhabihu sita ambazo sisi kama makuhani binafsi tunapaswa kumtolea Mungu.

    a. ____________________________________________________
    b. ____________________________________________________
    c. ____________________________________________________
    d. ____________________________________________________
    e. ____________________________________________________
    f. ____________________________________________________

11. *Nuru* ya ulimwengu ni nani? _________________________

12. *Nuru* ya ulimwengu alikuwa nani na ni nani? _________________________

13. Ni amri gani nne za jumla zinatuambia jinsi ya kufanya kazi pamoja kama waumini?

a. ______________________________

b. ______________________________

c. ______________________________

d. ______________________________

14. Hatua 3 za kukabiliana na dhambi za wenzetu zilizoelezwa katika Mathayo 18:15-17 ni:

a. Nenda____________________________________kwa mtu huyo.

b. Ikiwa tatizo bado halijatatuliwa, nenda na____ au ________________.

c. Ikiwa bado tatizo halijatatuliwa, ____________________________.

15. Tunajifunza kuhusu *"karama"* ambazo Mungu anatoa kwa Mwili moja kwa moja kutoka kwa_________________________.

16. Yesu ametoa __________________ ili __________________ Waumini.

17. Roho Mtakatifu ametoa _______________ ili _______________ Waumini.

18. Waandaaji wa aina nne katika Waefeso 4:11-16 ni:

a. ____________________ b. ____________________

c. ____________________ d. ____________________

19. *Kweli* au *Uwongo*: Waandaaji hawa hufanya huduma kwa niaba yetu. ________

20. *Kweli* au *Uwongo*: Waandaaji hawa wametolewa ili kutufundisha kufanya huduma. ________

21. Kuamua muumini ana karama gani kunahitaji ______________________ na __________________________________.

22. Marejeo makuu ya Biblia juu ya karama za kiroho ni ____________________, _________________________, na ______________________.

23. *Kweli au Uwongo:* 1 Wakorintho 13:4-8 ni muhimu katika suala la Karama za Kiroho. ____________________

24. *Kweli au Uwongo:* Uinjilisti ni Karama ya Kiroho inayotolewa na Roho Mtakatifu. __________________

# Somo la 9 - Katika Mwili … maswali ukurasa wa 132 - 133

Usitumie karatasi hizi za majibu kupata majibu yako. Tafadhali zitumie tu kukagua majibu yako. Rudi kwenye somo ili kupata taarifa za kurekebisha majibu yako. Rudia mtihani hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi. Masomo yote, mitihani ya marudio, na kurasa za majibu zinapatikana katika www.Theolojia.org.

ORODHESHA VIELELEZO 9 VYA MAISHA YETU KATIKA MWILI NA MSISITIZO WA KILA KIMOJA.

1. Kielelezo: *Mwili wa Krsito* Msisitizo: *Umoja na ukuaji*
2. Kielelezo: *Familia ya Mungu* Msisitizo: *Ushirika na uhusiano karib*u
3. Kielelezo: *Bibi harusi wa Kristo* Msisitizo: *Matarajio*
4. Kielelezo: *Nyumba ya Mungu* Msisitizo: *Makao ya Mungu*
5. Kielelezo: *Hekalu la Mungu* Msisitizo: *Dhabihu na ibada*
6. Kielelezo: *Nuru* Msisitizo: *Uinjilisti*
7. Kielelezo: *Taifa* Msisitizo: *Uraia Mbinguni*
8. Kielelezo: *Mzabibu* Msisitizo: *Matunda*
9. Kielelezo: *Kundi la kondoo* Msisitizo: *Mchungaji*

10. Orodhesha dhabihu sita ambazo sisi kama makuhani binafsi tunapaswa kumtolea Mungu.
    a. *Miili yetu*
    b. *Sifa zetu*
    c. *Matendo mema*
    d. *Koinonia (ushirika wa kweli)*
    e. *Mioyo iliyovunjika*
    f. *Waumini wapya*

11. Nuru ya ulimwengu ni nani? *Sisi kama waumini*

12. Nuru ya ulimwengu alikuwa nani na ni nani? *Yesu*

13. Ni amri gani nne za jumla zinatuambia jinsi ya kufanya kazi pamoja kama waumini?

   a. ________*Kupendane sisi kwa sisi*

   b. ________*Kuhifadhi umoja*

   c. ________*Kuwa safi*

   d. ________*Kuonyesha upendo kwa matendo*

14. Hatua 3 za kukabiliana na dhambi za wenzetu zilizoelezwa katika Mathayo 18:15-17 ni:

   a. Nenda __*peke yako*__ kwa mtu huyo.

   b. Ikiwa tatizo bado halijatatuliwa, nenda na __*shahidi mmoja*__ au __*wawili wa dhambi ya mtu huyo*__ .

   c. Ikiwa bado tatizo halijatatuliwa, __*lipeleke kwa kanisa ili litatuliwe*__ .

15. Tunajifunza kuhusu "karama" ambazo Mungu anatoa kwa Mwili moja kwa moja kutoka kwa ____*Biblia*____ .

16. Yesu ametoa __*watu maalum (viongozi)*__ ili __*kuwaandaa*__ Waumini.

17. Roho Mtakatifu ametoa __*uwezo maalum*__ ili __*kuwawezesha*__ Waumini.

18. Waandaaji wa aina nne katika Waefeso 4:11-16 ni:

   a. _____*Mitume*_____ b. _____*Manabii*

   c. _____*Wainjilisti*_____ d. _____*Wachungaji-walimu*

19. *Kweli au Uwongo:* Waandaaji hawa hufanya huduma kwa niaba yetu. __*Uwongo*

20. *Kweli au Uwongo:* Waandaaji hawa wametolewa ili kutufundisha kufanya huduma. __*Ukweli*__

21. Kuamua muumini ana karama gani kunahitaji __*muda*__ na __*uzoefu*__ .

22. Marejeo makuu ya Biblia juu ya karama za kiroho ni __*Waefeso 4:11-16*__ , __*Warumi 12*__ , na __*1 Wakorintho 12 - 14*__ .

23. *Kweli* au *Uwongo:* 1 Wakorintho 13:4-8 ni muhimu katika suala la Karama za Kiroho. __*Ukweli*__ .

24. *Kweli* au *Uwongo:* Uinjilisti ni Karama ya Kiroho inayotolewa na Roho Mtakatifu. __*Uwongo*__ .

## SOMO LA 10 - KATIKA VITA

*"Kesheni, simameni imara katika Imani, fanyeni kiume, mkawe hodari. Mambo yenu yote na yatendeke katika upendo."* 1 Wakorintho 16:13-14

**Tuko katika vita dhidi ya maadui watatu.** Maisha ya Kikristo yanaweza kuelezwa kwa usahihi kwa maneno mazuri kama vile ... faraja, kutosheka, msamaha, wema, fadhili, tumaini, furaha, fadhili, upendo, rehema, amani na kuridhika. Hata hivyo, maneno haya hayatoi taswira kamili ya uhalisia wa kuishi maisha ya Kikristo. Usipoteze mtazamo wa taswira kamili ... uko katika vita. Biblia inasema kwamba uko katika vita dhidi ya maadui watatu walioanguka ... dunia iliyoanguka, asili yako iliyoanguka, na malaika aliyeanguka. Umezaliwa katikati ya maadui ... umezaliwa katika dunia iliyoanguka. Asili yako iliyoanguka ni msaliti ... mwili wako unapigana dhidi yako kwa ndani. Isitoshe, unapigana na adui asiyeonekana ... Ibilisi. Maadui hawa watatu wanaleta vikwazo katika kuishi kwako kwa utukufu wa Mungu. Lazima uelewe maadui wako. Lazima uelewe mbinu za maadui wako. Unaweza kushinda vita vyako ikiwa utafuata maagizo ya Mungu ya vita.

**Vita dhidi ya dhambi na majaribu.** Vita dhidi ya maadui wako watatu mara nyingi hupiganwa dhidi ya dhambi na majaribu. Unahitaji kupambana na dhambi. Unahitaji kujua jinsi ya kupinga majaribu. Dhambi nyingi ni rahisi kutambua. Hata hivyo, baadhi ya mambo yanaweza kuwa sahihi katika hali moja na yasiwe sahihi katika hali nyingine ... au sahihi kwa mtu mmoja, na mabaya kwa mwingine. Unahitaji kuelewa jinsi ya kutambua dhambi. Kama Wakristo, tutajaribiwa. Tutapitia majaribu. Vita tunavyopigana ni hatari. Dhambi zetu ni kama majeraha tunayopata katika vita. Tutajeruhiwa. Ni lazima tushughulikie majeraha yetu ... tukiungama dhambi zetu kwa Mungu. Kuungama ni sharti la kusamehewa. Msamaha ni baraka kubwa kutoka kwa Mungu. Dhambi ambazo hazijaungamwa zina madhara makubwa. Waumini huumizwa katika vita. Tunahitaji kushughulikia majeraha yetu wenyewe ... na yale ya Waumini wengine.

**Tutapata ushindi wa mwisho.** Tunapigana katika vita ambavyo tayari tumeshindiwa. Yesu aliwashinda maadui wetu pale msalabani. Hata hivyo, lazima tupigane vita vyetu kila siku. Mungu ndiye kimbilio na nguvu yetu katika uwanja wa vita, *"Kwa maana ulikuwa kimbilio langu, Ngome yenye nguvu adui asinipate,"* Zaburi 61:3. Tunaweza kushinda vita vyetu ikiwa tutavipiga kulingana na maagizo ya Mungu ya vita. Kisha wakati wetu hapa duniani utakapokwisha, tutaweza kusema kile ambacho Mtume Paulo alisema karibu na mwisho wa maisha yake, *"Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda,"* 2 Timotheo 4:7.

## VITA VYETU DHIDI YA DUNIA

*“Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake.”* 1 Yohana 2:15-17

**Kumwelewa Adui.** Ulimwengu ni adui yetu. Tumezaliwa katika ulimwengu ulioanguka. Ulimwengu si rahisi wala si mkamilifu ... umelaaniwa na Mungu. *“Kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu. Kwa maana viumbe vyote pia vilitiishwa chini ya ubatili; si kwa hiari yake, ila kwa sababu yake yeye aliyevitiisha katika tumaini; kwa kuwa viumbe vyenyewe navyo vitawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu, hata viingie katika uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu,”* Warumi 8:19-21. Tumezaliwa katikati ya maadui katika ulimwengu ulioanguka unaotawalwa na Shetani, 1 Yohana 5:19. Ulimwengu wetu unatawalwa na Shetani, Yohana 12:31. Shetani ndiye mfalme wa uwezo wa anga, Waefeso 2:1-3. Sisi ni askari katika nchi ya kigeni yenye uhasama.

**Kuelewa mbinu za adui.** Maisha ya hapa duniani ni magumu. Hata hivyo, ni ya muda tu. Dunia inaweza kutukengeusha ili tusizingatie mambo yenye umuhimu wa milele ... Mungu, Neno Lake, na watu. Tunaweza kushawishiwa kujihusisha sana na mambo yasiyodumu ya dunia hii kiasi kwamba hatumtii Mungu. Kwa Waumini wengi, vikengeushi vya dunia vinaweza kupimwa kwa saa. Maisha yanaweza kuwa na shughuli nyingi sana kiasi kwamba tunaweza kushawishiwa kutotenga muda kwa ajili ya mambo ya Mungu. Pia, tunaweza kujitoa kwa vitu vilivyoumbwa badala ya kujitoa kwa muumbaji. Badala ya kumpenda Mungu, tunaweza kupenda vitu vya dunia hii ... viwe ni vitu vizuri au vibaya. Majaribu mengi ya dunia ni ya moja kwa moja na ni ya wazi. Lakini, mengine mengi ni fiche na si ya moja kwa moja. Tunapaswa kukua ili tuzidi kuwa kama Yesu ... lakini tunaishi katika dunia yenye vishawishi viingi vibaya. Watu na vitu vya dunia hii vinaweza kutuathiri moja kwa moja na kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Ni lazima tuwe waangalifu sana ili kuzuia watu na vitu vya dunia hii visituweke chini ya ushawishi wao.

**Kumshinda adui.** Kushinda vita vyetu dhidi ya dunia kunaanza na kule kujua kwamba ushindi wa mwisho tayari umeshapatikana. Yesu alisema, *“Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu,”* Yohana 16:33. Tunaweza kupata ushindi katika vita vyetu vya kila siku dhidi ya ulimwengu. *“Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu. Mwenye kuushinda ulimwengu ni nani, isipokuwa ni yeye aaminiye ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu?”* 1 Yohana 5:4-6. Ushindi wa mwisho dhidi ya ulimwengu umeshapatikana. Tunaweza kupata ushindi wa kila siku ikiwa tutafuata maagizo ya vita ya Mungu kwa ajili ya vita vyetu dhidi ya ulimwengu.

### Maagizo ya Mungu ya vita

*“Ndugu zangu, msistaajabu, ulimwengu ukiwachukia,”* 1 Yohana 3:13. Usifikiri kwamba unapaswa kukubaliwa na ulimwengu. Yesu alisema, *“Iwapo ulimwengu ukiwachukia, mwajua ya kuwa umenichukia mimi kabla ya kuwachukia ninyi. Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda walio wake; lakini kwa kuwa ninyi si wa ulimwengu, bali mimi naliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia,”* Yohana 15:18-19. Ufalme wake si wa ulimwengu huu, Yohana 18:36. Uraia wetu uko Mbinguni, Wafilipi 3:20. Tuko ulimwenguni ... lakini sisi si wa ulimwengu huu, Yohana 17:14-18. Wewe ni mgeni katika ulimwengu huu. Usitarajie kwamba utajihisi uko nyumbani. Bado hujafika nyumbani.

*“Ushiriki taabu pamoja nami, kama askari mwema wa Kristo Yesu. Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia, ili ampendeze yeye aliyemwandika awe askari,”* 2 Timotheo 2:3-4. Usijitie katika shughuli za dunia. Hiyo haimaanishi kuwa hupaswi kuhusika katika maisha. Hata hivyo, inamaanisha kwamba hupaswi kuruhusu shughuli, mali, na mahusiano yako yakuzuie kumtii Mungu. Kujitia katika mambo ya kidunia huwafanya baadhi ya Wakristo wasizae matunda, Marko 4:19. Ikiwa una shughuli nyingi sana kiasi kwamba huna muda wa kugundua na kutekeleza mapenzi ya Mungu ... basi una shughuli nyingi sana katika kufanya mambo yasiyo sahihi. Tumia wakati wako vizuri, Waefeso 5:15-16. Kujitia katika dhambi kutakurudisha nyuma. Na kujitia katika mambo yanayokupendeza kunaweza kukuzuia kufanya kile kilicho bora zaidi ambacho Mungu anataka ufanye. Je, ni upasuaji wa kiasi gani unahitajika katika hali yako ya kujitia katika mambo ya dunia? Je, unahitaji upasuaji mdogo au mkubwa? Usijitie katika mambo ya kidunia. Kuwa tayari kutumiwa na Mungu.

*“Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia,”* 1 Yohana 2:15. Kujitoa kwetu kwa mambo yasiyodumu ya dunia hii kunaweza kutufanya tupuuze mambo ya milele ... Mungu, Neno Lake, na watu. Tathmini nzuri ya jambo hili ni matumizi ya rasilimali, muda, na pesa zetu. Kama Yesu alivyosema, *“Bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi; kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako,”* Mathayo 6:20 21. Kupenda vitu vya dunia ni hatari sana. *“Enyi wazinzi, hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu,”* Yakobo 4:4. Usipende dunia. Mpende Mungu.

*“Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu,”* Warumi 12:2. Usiruhusu dunia ikushawishi kufuata mwenendo wake. Usijitie katika kile ambacho watu wanafanya au hawafanyi. Dunia inafuata tamaa ya mwili, tamaa ya macho, na kiburi cha maisha. Kuwa tofauti na dunia. Tumia muda wako katika Neno la Mungu. Fanya upya akili yako. Weka akili yako katika mambo ya Mungu. Usifuate mambo ya dunia. Badilika.

## VITA VYETU DHIDI YA MWILI

*"Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka."* Wagalatia 5:16-17

**Kumwelewa Adui.** Mwili wetu wenyewe ni adui. Mwili ni sehemu ya ndani ya kila mtu inayompinga Mungu. Mtu anapomwamini Yesu Kristo, asili mpya huzaliwa ndani ya mtu huyo. Hata hivyo, asili ya zamani bado iko ... hiyo ni mwili. Matendo ya mwili yanajumuisha *"uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, mhusuda, ulevi, ulafi,"* Wagalatia 5:19-21. Matendo ya mwili yanatoka kwenye moyo wa mwanadamu. Yesu alisema, *"Kwa maana moyoni hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati; wivi, ushuhuda wa uongo, na matukano,"* Mathayo 15:19. Alisema, *"Kimtokacho mtu ndicho kimtiacho unajisi. Kwa maana ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo mabaya, uasherati, wivi, uuaji, uzinzi, tamaa mbaya, ukorofi, hila, ufisadi, kijicho, matukano, kiburi, upumbavu. Haya yote yaliyo maovu yatoka ndani, nayo yamtia mtu unajisi,"* Marko 7:20-23. Mambo haya yote yanaweza kutoka kwa adui aliye ndani yetu ... kutoka kwenye mwili wetu.

**Kuelewa mbinu za adui.** Mwili ndio adui wetu wa ndani. Mwili wetu ni msaliti katika miili yetu ya nyama. Mwili wetu hupigana dhidi ya asili yetu mpya. *"Ziepukeni tamaa za mwili zipiganazao na roho,"* 1 Petro 2:11. Mwili hupigana vita na Roho iliyo ndani yetu, *"Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka,"* Wagalatia 5:17. Kila moja ya asili zetu mbili, ya zamani na mpya, hutafuta kutawala maisha yetu kutoka ndani yetu, Warumi 7:15-25. Mwili wetu hutujaribu ili tutende dhambi. Asili yetu mpya hutuhimiza kumwishia Mungu.

**Kumshinda adui.** Vita vyetu dhidi ya mwili ni vita ambavyo tayari vimeshashindwa na Kristo. *"Utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena,"* Warumi 6:6. Ushindi huo katika Kristo unaimarishwa na matendo yetu tunapompenda na kumtii Mungu. Mwili wetu umekufa kwa sababu ya dhambi, Warumi 8:10. Kwa namna fulani, vita ni kati ya kile kilichokufa na kile kilicho hai ... mwili wetu uliokufa dhidi ya roho yetu iliyo hai. Katika vita hivi lazima tupande katika Roho … si katika mwili. Tuna ahadi na onyo kwamba tutavuna kile tulichopanda. *"Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele,"* Wagalatia 6:7-8. Ni lazima tupigane kwa dhati dhidi ya adui huyu wa ndani. Mungu ametupatia maagizo yake ya vita kwa ajili ya kupata ushindi dhidi ya mwili kila siku.

### Maagizo ya Mungu ya vita

Mvue utu wa zamani na mvae utu mpya. *“Mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani … na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu; mkavae utu mpya,”* Waefeso 4:22-24. Ni zaidi ya kubomoa. Ni kubomoa *na* kukarabati. Kubomao kile kilicho cha zamani na kujenga upya, Wakolosai 3:9-10.

Weka akili yako kwenye mambo ya Roho wala si kwenye mambo ya mwili. *“Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili; bali wale waifuatao roho huyafikiri mambo ya roho. Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani. Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu,”* Warumi 8:5-8.

Hupaswi kuutumainia mwili ... hupaswi kuutumainia mwili wako wa nyama, umri wako, nguvu zako, ukoo wako, rangi yako, kabila lako, na wala utaifa wako. “*Hatuutumainii mwili,”* Wafilipi 3:3. Tumaini lako linapaswa kuwa katika Mungu, Mithali 3:26.

Acha kukubali kushawishiwa na tamaa ya mwili. Ikimbie tamaa ya mwili. *“Wapenzi, nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho,”* 1 Petro 2:11. *“Lakini zikimbie tamaa za ujanani,”* 2 Timotheo 2:22. Yafisheni matendo ya mwili, Warumi 8:12-13. Sulubisha mwili pamoja na tamaa zake, Wagalatia 5:24.

Usiupatie mwili nafasi. Usimpe msaliti zana za kukupiga vita. Usiilishe asili yako ya zamani. Inyime chakula kabisa. Usiupatie mwili wako nafasi ya kukujaribu. Usiende sehemu zinazoipa nafasi mwili wako kukujaribu. Usifanye mambo yanayosababisha dhambi za mwili. Usijiletee majaribu wewe mwenyewe. *“Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tamaa zake.”* Warumi 13:14. Acheni kutoa miili yenu kwa mambo yasiyo ya haki ... toeni miili yenu kwa mambo ya haki, Warumi 6:11-20.

Jifikirie kuwa uko hai kutoka kwa wafu. Ulikuwa umekufa kabla ya kumwamini Yesu. *“Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu; ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga,”* Waefeso 2:1-2. Mtazamo wetu unapaswa kudhihirisha habari kuu kwamba hapo awali tulikuwa wafu, lakini sasa tuko hai. *“Jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa,”* Warumi 6:13. Uko hai kutoka kwa wafu. Uko hai kwa nguvu ya Roho. *“Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho,”* Wagalatia 5:25.

## VITA VYETU DHIDI YA IBILISI

*"Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho."* Waefeso 6:10-12

**Kumwelewa Adui.** Shetani ni kiumbe halisia. Yeye si kiumbe aliyebuniwa na mawazo ya wanadamu. Yeye si kiumbe wa kubuniwa anayewakilisha uovu. Shetani anatajwa kuwa kiumbe halisia na Yesu, Paulo, Petro, Yohana, waandishi wote wa Agano Jipya, na katika vitabu saba vya Agano la Kale. Shetani si sawa na Mungu wala si kinyume cha Mungu. Shetani si wa milele ... na ana mipaka. Yeye si mwenye uwezo wote, hayuko kila mahali kwa wakati mmoja, wala si mjua yote. Hata hivyo, Shetani ana nguvu. Yeye ni *"mkuu wa ulimwengu huu,"* Yohana 12:31. Yeye ni *"mfalme wa uwezo wa anga,"* Waefeso 2:1-2.

**Kuelewa mbinu za adui.** *"Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo,"* 1 Yohana 3:8. Yeye ni mjaribu, 1 Wathesalonike 3:5 ... mdanganyifu, 2 Wakorintho 11:3 ... na mwenye hila, 2 Wakorintho 2:10-11. *"Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo,"* Yohana 8:44. *"ibilisi … hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa huo,"* Yohana 8:44. Shetani na mawakala wake wanaweza kujipenyeza miongoni mwa viongozi wa kanisa. *"Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru" na "watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa watumishi wa haki,"* 2 Wakorintho 11:13-15. Yeye ni chanzo cha mafundisho ya uwongo, 1 Timotheo 4:1-5. Shetani anapigana dhidi ya Injili. Anapigana kuzuia watu kumwamini Yesu. Shetani amewashika mateka wasioamini, 2 Timotheo 2:24-26 ... anaiba Neno kutoka kwao, Luka 8:12-13 ... na anapofusha macho yao wasiione nuru ya Injili, 2 Wakorintho 4:3-4. Shetani na pepo wake wanaweza kuwamiliki wasioamini, na kuwadhibiti, Luka 22:3, Luka 8:30. Shetani ni adui wa Waumini, 1 Petro 5:8. Yeye hutushtaki mbele za Mungu, Ufunuo 12:10. Yeye huwakandamiza Waumini, Matendo 10:38. Hata hivyo, hakuna chochote katika Biblia kinachoonyesha kwamba Shetani anaweza kumpagaa muumini. Hatuko chini ya udhibiti wake. *"Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake,"* Wakolosai 1:13. Punde unapomwamini Yesu, hauko tena chini ya utawala wa Shetani, Matendo 26:18.

**Kumshinda adui.** Kupitia kifo chake, Yesu alimshinda Shetani, Waebrania 2:14. Mungu hajatuacha bila ulinzi katika vita vyetu vya kila siku dhidi ya Shetani. Amemwekea Shetani mpaka. Ibilisi lazima akimbie tunapompinga, Yakobo 4:7. Na tuna ahadi kuu, *"Yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia,"* 1 Yohana 4:4. Tunaweza kupata ushindi wa kila siku tukifuata maagizo ya Mungu ya vita kwa ajili ya vita vyetu dhidi ya Shetani.

**Maagizo ya Mungu ya vita**

Mpinge ibilisi. Simama imara dhidi yake. *"Nanyi mpingeni huyo, mkiwa thabiti katika imani,"* 1 Petro 5:9. Simama imara dhidi yake, Waefeso 6:11-14.

Omba! Sala ya Bwana inajumuisha, *"Utuokoe na yule mwovu,"* Mathayo 6:13. Neno la Kigiriki la *uovu* katika sala hiyo linamjumuisha Shetani. Neno hilo la Kigiriki liko katika hali ya nomino, ambayo mara nyingi huonyesha cheo. Maagizo ya Kristo kwa ukamilifu ni *utuokoe na yule mwovu.* Vile vile, alimwomba Mungu *"uwalinde na yule mwovu,"* Yohana 17:15.

Kuwa macho. Kuwa mwangalifu. Jihadhari na mashambulizi ya adui. *"Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze,"* 1 Petro 5:8.

Usimpe Shetani nafasi hata kidogo. Usimfungulie milango. Usimpe Shetani nafasi kupitia hasira isiyoshughulikiwa, Waefeso 4:26-27. Usiruhusu roho ya kutosamehe impe nafasi, 2 Wakorintho 2:10-11. Na kunyimana tendo la ndoa katika ndoa humpa Shetani nafasi ya kuleta majaribu ... usimnyime mwanandoa mwenzako, 1 Wakorintho 7:5.

Usijihusishe katika jambo lolote la ushirikina. Jiepushe kabisa na unajimu, uchawi, uaguzi, falaki, watu wanaowasiliana na roho za watu waliokufa, ubao wa Ouija, walozi, watu wanaowasiliana na roho, uchawi unaoaminika kuleta ulinzi na kitu chochote cha kishirikina. Paulo aliandika, *"Nami sipendi ninyi kushirikiana na mashetani. Hamwezi kunywea kikombe cha Bwana na kikombe cha mashetani. Hamwezi kushirikiana katika meza ya Bwana na katika meza ya mashetani,"* 1 Wakorintho 10:20-21.

*"Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani,"* Waefeso 6:11. Kabla ya vita, jifunge kiunoni ukweli wa Yesu na Neno lake ... vaa dirii ya imani, upendo, na haki ... na uvae miguuni mwako utayari wa kushiriki Injili. Katika vita, twaa ngao ya imani ... vaa chepeo cha tumaini la wokovu ... na utumie silaha yako moja ya mashambulizi, upanga wa Roho, yaani Biblia. Vaa silaha zote za Mungu, Waefeso 6:13-17 na 1 Wathesalonike 5:8.

Waambie watu habari za Yesu ... hata kama inamaanisha ni lazima utoe maisha yako kwa ajili ya Injili. Shetani atashindwa kupitia damu ya Yesu na utiifu wako wa Agizo Kuu. *"Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi … mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu … Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa,"* Ufunuo 12:9-11.

## KUPAMBANA NA DHAMBI

*“Basi, dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake; wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki. Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema.”* Warumi 6:12-14

**Mtu anawezaje kuepuka kutenda dhambi?** Ni lazima tuwe watendaji wa Neno na si wasikilizaji tu, Yakobo 1:22-25. Neno la Mungu litatusaidia kuepuka dhambi ... lakini ikiwa tu tutalitii. Jitathmini kwa msingi wa maagizo yaliyoorodheshwa hapa chini. Je, umekuwa ukifanya mambo haya? Kukosa kufuata maagizo yake kunaweza kusababisha kuanguka kimaadili, katika vipindi vya kutenda dhambi fulani kwa njia kubwa, na katika kutenda dhambi za mazoea. Fuata maagizo yake. Unaweza kushinda dhambi.

> Omba. Omba kwamba Mungu aelekeze njia yako mbali na watu, sehemu, na vitu vinavyokutia katika majaribu ya kutenda dhambi. Sala ya Bwana inajumuisha ombi linalosema, *“Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu,”* Mathayo 6:13. Omba kwamba Mungu akuepushe na ushawishi wa Shetani. Omba akukomboe kutokana na vishawishi vyote vyote vibaya.
>
> Lijue Neno lake. Tafakari Neno lake. Jifunze Neno lake. Kariri Neno lake. Muda mwingi katika Biblia hupunguza dhambi. Muda mchache katika Biblia husababisha ongezeko la dhambi. *“Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, Nisije nikakutenda dhambi,”* Zaburi 119:11.
>
> Enenda katika Roho wake. Huwezi kuepuka dhambi kwa kuishi maisha ya kujiongoza mwenyewe. Ni lazima uishi maisha yanayoongozwa na Mungu ili uepuke dhambi. *“Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili,”* Wagalatia 5:16.
>
> Weka akili zako katika yale yaliyo juu … si mambo ya dunia, mwili, na ibilisi. *“Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi,”* Wakolosai 3:1-2. Maisha yako yatafuata lengo na mwelekeo wa akili yako. *“Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo,”* Wafilipi 4:8.
>
> Jihadhari na kujiamini kupita kiasi. Usifikiri kwamba umefikia kiwango cha kuwa na kinga dhidi ya hatari za dhambi na majaribu. *“Kwa hiyo anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke,”* 1 Wakorintho 10:12. Usijiamini kupita kiasi kwamba una uwezo wa kupinga dhambi. *“Kiburi hutangulia uangamivu; Na roho yenye kutakabari hutangulia maanguko,”* Mithali 16:18.

Chukua hatua kali na za haraka dhidi ya dhambi yoyote katika maisha yako. *“Na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu,”* 2 Wakorintho 7:1. *“Wekeeni mbali uchafu wote na ubaya uzidio,”* Yakobo 1:21. Usijihusishe na tabia yoyote ya uasherati. Je, unajihusisha na dhambi fulani ya ngono? Basi iache! *“Mwepukane na uasherati,”* 1 Wathesalonike 4:3. Usikubali kujihusisha na uovu wa aina yoyote. *“Jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema; jitengeni na ubaya wa kila namna,”* 1 Wahesalonike 5:21-22.

Kutoroka kutoka kwenye uwanja wa vita. Kutoroka kutoka kwenye uwanja wa vita mara nyingi ni njia bora ya kushinda dhambi ya ngono. Toroka watu, sehemu, na vitu vinavyokutia katika majaribu. *“Lakini zikimbie tamaa za ujanani,”* 2 Timotheo 2:22. *“Ikimbieni zinaa,”* 1 Wakorintho 6:18. Toroka kutoka kwenye uwanja wa vita vya ibada ya sanamu. Kuna sanamu nyingi katika ulimwengu huu ... vitu ambavyo vinaweza kuwa vitu vya uwongo vinavyoabudiwa. Kuna sanamu za dini ya uwongo. Utajiri na mali vinaweza kuwa vitu vinavyoabudiwa. Hata watu wanaweza kuwa sanamu. Mwabudu Mungu na Mungu pekee. Mungu ameamuru, *“Usiwe na miungu mingine ila mimi,”* Kutoka 20:3. Toroka kutoka uwanja huo. *“Ikimbieni ibada ya sanamu,”* 1 Wakorintho 10:14.

Kumbuka kwamba mwili wako ni hekalu la Roho Mtakatifu. Unapojaribiwa … fikiria Roho akikuambia, *We! Hili ni hekalu langu. Usifanye hivyo katika hekalu langu*. Weka hekalu lake katika hali safi. *“Ikimbieni zinaa. Kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake; ila yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe. Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe,”* 1 Wakorintho 6:18-19.

Kumbuka ulinunuliwa kwa gharama kubwa. Yesu alimwaga damu yake kwa ajili yako. *“Na ikiwa mnamwita Baba, yeye ahukumuye kila mtu pasipo upendeleo, kwa kadiri ya kazi yake, enendeni kwa hofu katika wakati wenu wa kukaa hapa kama wageni. Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo,”* 1 Petro 1:17-19. Unapojaribiwa ... fikiria kwamba unamtazama Yesu kutoka kwenye shina la msalaba. Tazama taswira ya mwili wake uliojeruhiwa na kupigwa. Tazama kichwa chake chenye taji la miba. Fikiria damu inayotiririka kutoka kwenye mikono na miguu yake iliyopigwa misumari. Fikiria kwamba anakutazama machoni mwako. Msikie akisema, *Usifanye hivyo ... Ninamwaga damu yangu kwa ajili yako.* Yesu alikufa kwa ajili yako. Kumbuka gharama aliyokulipia. *“Maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu,”* 1 Wakorintho 6:20.

## KUTAMBUA DHAMBI

**Je, ni dhambi?** *"Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu,"* Warumi 3:23. Dhambi ni jambo lolote lisiloambatana na, au linaloenda kinyume cha tabia, Neno, au mapenzi ya Mungu. Vitendo fulani ni dhambi katika hali fulani ... lakini si katika hali zingine. Mambo mengine ni dhambi kwa watu fulani ... lakini si kwa watu wengine. Mungu ametupatia maagizo kuhusu jinsi ya kutambua dhambi. Biblia inatambua wazi matendo na mitazamo mingi kuwa ni dhambi ... na ina miongozo ya kuamua ikiwa mambo yenye utata ni dhambi au si dhambi.

> Ni dhambi ikiwa ... inamhuzunisha badala ya kumtukuza Mungu. *"Msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu,"* Waefeso 4:30. *"Fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu."* 1 Wakorintho 10:31. Maisha yetu yanapaswa kuendana na nafasi yetu kama watoto wa Mungu. *"Mwenende kama ilivyo wajibu wenu kwa Mungu, mwenye kuwaita ninyi ili mwingie katika ufalme wake na utukufu wake,"* 1 Wathesalonike 2:12.
>
> Ni dhambi ikiwa ... inakiuka Neno la Mungu. *"Wazishike amri zake,"* Zaburi 78:7. *"Wewe umetuamuru mausia yako, Ili sisi tuyatii sana,"* Zaburi 119:4. Ubora wa uhusiano wako na Yesu unafungamana na utiifu wako. Yesu alisema, *"Mkinipenda, mtazishika amri zangu,"* Yohana 14:15. *"Ninyi mmekuwa rafiki zangu, mkitenda niwaamuruyo,"* Yohana 15:14.
>
> Ni dhambi ... ikiwa utakosa kufanya kile kilicho sahihi. Dhambi za kutofanya kile kilicho sahihi pia ni dhambi. Utakatifu ni zaidi ya kutotenda dhambi. *"Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi,"* Yakobo 4:17.
>
> Ni dhambi ... hata kama inatendwa kwa kutojua. Kutojua Biblia si kisingizio cha kutenda dhambi. *"Na kama mtu akifanya dhambi, na kutenda mambo hayo mojawapo ambayo BWANA alizuilia yasifanywe, ajapokuwa hakuyajua, ni mwenye hatia vivyo, naye atachukua uovu wake,"* Mambo ya Walawi 5:17.
>
> Ni dhambi ikiwa ... inaharibu au inadhalilisha hekalu la Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu anakaa ndani yako. *"Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe,"* 1 Wakorintho 6:19.
>
> Ni dhambi ikiwa ... inasababisha utumwa. Tabia ya uraibu na vitu vya uraibu si sahihi. *"Vitu vyote ni halali kwangu, lakini si vyote vifaavyo; vitu vyote ni halali kwangu, lakini mimi sitatiwa chini ya uwezo wa kitu cho chote,"* 1 Wakorintho 6:12.
>
> Ni dhambi ikiwa ... unaitenda akilini mwako. Imesemekana kwamba huwezi kuwazuia ndege kuruka juu ya kichwa chako ... lakini unaweza kuwazuia kujenga viota kwenye nywele zako. Hii inaonyesha tofauti kati ya *majaribu ya mawazo* na *dhambi za mawazo.* Yesu alisema, *"Lakini mimi nawaambia, Kila mtu atazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake,"* Mathayo 5:28.

Ni dhambi ikiwa ... unafikiri ni dhambi. *“Najua, tena nimehakikishwa sana katika Bwana Yesu, ya kuwa hakuna kitu kilicho najisi kwa asili yake, lakini kwake yeye akionaye kitu kuwa najisi, kwake huyo kitu kile ni najisi,”* Warumi 14:14. Ukifanya jambo ambalo unafikiri ni dhambi, hata kama si dhambi kiasili, una hatia ya kumwasi Mungu. Shaka yako inalifanya liwe dhambi. Hata hivyo, kinyume cha hilo si kweli ... kutokuwa na shaka hakufanyi jambo hilo lisiwe dhambi. Dhamiri iliyochomwa inaweza kukuzuia kutambua dhambi, 1 Timotheo 4:2.

Ni dhambi ikiwa ... ni ushawishi mbaya badala ya kuwa ushawishi mzuri. Jenga. Usibomoe. Imarisha. Usidhoofishe. Saidia. Usijeruhi. *“Vitu vyote ni halali; bali si vitu vyote vifaavyo. Vitu vyote ni halali; bali si vitu vyote vijengavyo,”* 1 Wakorintho 10:23. Jiulize, “Je, jambo hili lina manufaa?”

Ni dhambi ikiwa ... inamchukiza mtu asiyeamini. Usiwachukize watu wasioamini. *“Msiwakoseshe Wayahudi wala Wayunani wala kanisa la Mungu, vile vile kama mimi niwapendezavyo watu wote katika mambo yote, nisitake faida yangu mwenyewe, ila faida yao walio wengi, wapate kuokolewa,”* 1 Wakorintho 10:32-33. Ujumbe wa Injili unaweza kumchukiza mtu asiyeamini … lakini mjumbe hapaswi kuwa sababu ya chukizo hilo. Ni vizuri kuwa na ujasiri na Injili, Waefeso 6:19-20 na Mithali 28:1. Hata hivyo, ujasiri usiozingatia hisia za msikilizaji ni dhambi. Ujasiri na kuzingatia hisia za watu zinapaswa kwenda pamoja.

Ni dhambi ikiwa ... inachukiza au ni kikwazo kwa ndugu. Wakati mwingine, lazima tubadilishe tabia zetu kwa faida ya Waumini wengine. *“Lakini angalieni huu uwezo wenu usije ukawakwaza wale walio dhaifu,*” 1 Wakorintho 8:9. *“Bali afadhali toeni hukumu hii, mtu asitie kitu cha kumkwaza ndugu au cha kumwangusha … Na ndugu yako akiingia huzuni kwa sababu ya chakula, umeacha kwenda katika upendo. Kwa chakula chako usimharibu mtu yule ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake … Maana ufalme wa Mungu si kula wala kunywa, bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu … Kwa ajili ya chakula usiiharibu kazi ya Mungu. Kweli, vyote ni safi; bali ni vibaya kwa mtu alaye na kujikwaza,”* Warumi 14:13-21. Tumia uhuru wako wa Kikristo kwa uangalifu. Kama muumini, uhuru wa kula chakula fulani au kunywa kinywaji fulani si uhuru wa kula au kunywa vitu hivyo katika kila hali.

*Si* dhambi ... kubadilisha tabia yako katika hali tofauti na ukiwa miongoni mwa watu tofauti. Kubadilisha tabia yako, bila kutenda dhambi, ili kufanikisha huduma si unafiki. Yesu alichukua mfano tofauti. Akawa mwanadamu. Yesu *“alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu,”* Wafilipi 2:7. Paulo alibadilisha tabia yake ili awashuhudie wasioamini. *“Nalikuwa kama Myahudi kwa Wayahudi, ili niwapate Wayahudi … ili niwapate walio chini ya sheria. Kwa wale wasio na sheria nalikuwa kama sina sheria … ili niwapate hao wasio na sheria. Kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge. Nimekuwa hali zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu,”* 1 Wakorintho 9:20-22.

Ni dhambi ikiwa ... ni kutii mila, kanuni na desturi zinazopingana na Biblia. Desturi na mila zinaweza kuwa sawa ... lakini haziko katika kiwango kimoja na Biblia wala si kuu kuliko Biblia. Yesu alisema, *“Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu,”* Mathayo 15:9. Kuna viongozi wapotovu ambao huwalaghai Waumini wengine kwa kufundisha mafundisho ya wanadamu kama ukweli wa Biblia, Wakolosai 2:18-23, 1 Timotheo 4:1-5. Kumfuata mwalimu wa uwongo, au kufuata mafundisho ya uwongo, hakuwaondolei Waumini uwajibikaji wao kwa ajili ya dhambi, Wakolosai 2:8.

Utiifu haukubaliki ikiwa ... hautoki moyoni. Maombi na ibada za kijuujuu hazina maana. *“Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi,”* Mathayo 6:7. Yesu alisema, *“Enyi wanafiki, ni vema alivyotabiri Isaya kwa habari zenu, akisema, ‘Watu hawa huniheshimu kwa midomo; Ila mioyo yao iko mbali nami,’”* Mathayo 15:7-8. Unaposali Sala ya Bwana mara kwa mara, je, unamaanisha kila neno? Je, unaisali kutoka moyoni mwako? Kuna nyimbo nyingi nzuri za sifa. Je, wewe humaanisha maneno unayoimba? Je, wewe huimba kutoka moyoni mwako?

Utiifu haukubaliki ikiwa … unafanywa ili kuwavutia wengine. Msikilizaji mmoja au zaidi wanaweza kutushawishi kujaribu kuwavutia. *“Angalieni msifanye wema wenu machoni pa watu, kusudi mtazamwe na wao; kwa maana mkifanya kama hayo, hampati thawabu kwa Baba yenu aliye mbinguni,”* Mathayo 6:1. Kushangiliwa kunaweza kuwa thawabu yako ya pekee, Mathayo 6:2, 5, na 16. Usitafute kutambuliwa na wengine unapotoa, Mathayo 6:2-4. Usisali ili kuwavutia wengine unaosali nao, Mathayo 6:5-6. Funga… lakini usijaribu kuwavutia wengine kwa kufunga kwako, Mathayo 6:2-6. Kutenda haki ili uonekane na wengine si kutenda haki hata kidogo.

Utiifu haukubaliki ikiwa ... unajaribu kuficha kutotii. Anania na Safira walitoa sadaka kubwa … lakini haikukubalika kwa sababu ya dhambi yao, Matendo 5:1-11. Kutotii kunaondoa thamani ya shughuli za kidini, Isaya 1:11-16, Amosi 5:21-24. Mafarisayo walificha dhambi zao kubwa zaidi kwa utiifu wa nje wa mambo madogo madogo, Mathayo 23:23-28. Wakristo mara nyingi huwa na orodha zao za dhambi za kuepuka ... zile dhambi tisa mbaya, nane ovu, au zile kumi na mbili mbaya zaidi. Mara nyingi vitu vilivyo kwenye orodha hizo ni dhambi. Lakini, Je, kuhusu dhambi zingine nzito zaidi? Je, kuhusu kutoshuhudia? Je, kuhusu kutofanya wanafunzi? Je, hayo yako kwenye orodha nyingi ya dhambi za kuepuka? Yesu aliwashutumu Mafarisayo kwa kuwaita viongozi vipofu wanaochuja mbu [mdudu mdogo najisi] huku wakimeza ngamia [mnyama mkubwa najisi]. Je, katika utiifu wetu, tunachuja mbu na kumeza ngamia?

## MAJARIBU

Maneno ya Kiebrania na Kigiriki yanayotafsiriwa katika Biblia kama aina mbalimbali za *majaribu* kwa kiasi fulani yanatumiwa kumaanisha jambo lile lile. Maneno hayo yanamaanisha kupima, kuthibitisha thamani, kusafisha, kufichua udhaifu, kuwa chini ya shinikizo na kushawishi kufanya mabaya. Hata hivyo, neno la Kiswahili *kujaribu* kimsingi linaeleweka kumaanisha *kushawishi kufanya uovu*. Vyanzo vitatu vya majaribu ya kufanya maovu ni ulimwengu, 1 Yohana 2:16 ... mwili, Yakobo 1:14-15 ... na ibilisi, Mathayo 4:3, 1 Wakorintho 7:5. Mungu huwa hatujaribu ili tufanye maovu. *“Mtu ajaribiwapo, asiseme, Ninajaribiwa na Mungu; maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu mtu,”* Yakobo 1:13. Hata hivyo, yeye huturuhusu tujaribiwe, Kutoka 16:4, Kumbukumbu la Torati 13:1-3, 1 Petro 1:6-7. Mungu hutusafisha kupitia majaribu, Zaburi 66:10, Isaya 48:10. Majaribu si dhambi ... lakini yanaweza kusababisha dhambi ikiwa hayatashughulikiwa kama Mungu anavyotaka. Yesu alijaribiwa ... lakini hakutenda dhambi. *“Alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi,”* Waebrania 4:15. Neno *majaribu* linatumika kumaanisha jambo lile lile katika maagizo yafuatayo.

> Omba ili usiingie katika majaribu. Yesu alijumuisha ombi hilo, *“Na usitutie majaribuni,”* katika Sala ya Bwana, Mathayo 6:13. Akiwa Gethsemane aliwaambia wanafunzi wake watatu, *“Ombeni kwamba msiingie majaribuni,”* Luka 22:40.
>
> Fahamu kuwa hauko peke yako katika mapambano yako. Yesu anaelewa kile unachopitia. Anaweza kukuhurumia kwa sababu yeye pia alijaribiwa. *“Hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote … Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa,”* Waebrania 2:17-18. *“Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji,”* Waebrania 4:15-16. Waumini wengine wamejaribiwa kwa njia sawa na wewe. Fahamu kwamba jaribu lako si la kipekee. *“Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu,”* 1 Wakorintho 10:13.
>
> Panga kustahimili. Mungu hatakuacha ujaribiwe kupita uwezo wako wa kustahimili. Mungu huwekea majaribu yako mipaka ili uweze kuyastahimili. Hupaswi kushindwa. *“Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili,”* 1 Wakorintho 10:13. Pamoja na lile jaribu, anatoa njia ya kuliepuka. Kwa nini? Anatoa njia ya kuepuka ili uweze *kustahimili* jaribu hilo. Kifungu hiki hakitoi ahadi kwamba utaweza kutoroka mara moja ... lakini kinaahidi kwamba unaweza kustahimili.
>
> Tazamia manufaa ya baadaye. *“Aliyekulisha jangwani kwa mana, wasiyoijua baba zako; apate kukutweza, apate kukujaribu, ili kukutendea mema mwisho wako,”* Kumbukumbu la Torati 8:16.

Tazamia kupata nguvu zaidi. *“Wala si hivyo tu, ila na mfurahi katika dhiki pia; mkijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta saburi; na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo; na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini; na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi,”* Warumi 5:3-5.

Tazamia kuwa mstahimilivu zaidi. Mungu anakuandaa ili uweze kukimbia kwa kasi zaidi, mbali zaidi na kwa muda mrefu zaidi. *“Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno,”* Yakobo 1:2-4.

Tazamia kuwa na uwezo wa kuwasaidia wengine. *“Akasema, Simoni, Simoni, tazama, Shetani amewataka ninyi apate kuwapepeta kama vile ngano; lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitindike; nawe utakapoongoka waimarishe ndugu zako,”* Luka 22:31-32.

Tazamia kubarikiwa. *“Angalieni, twawaita heri wao waliosubiri. Mmesikia habari ya subira yake Ayubu, mmeuona mwisho wa Bwana ya kwamba Bwana ni mwingi wa rehema, mwenye huruma,”* Yakobo 5:11.

Puuza matatizo yoyote ya muda mfupi na utazamie baraka za milele. *“Mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbalimbali; ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo,”* 1 Petro 1:6-7. *“Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele,”* 2 Wakorintho 4:17-18.

Endelea kumtazama Yesu. Tuna mifano mikuu ya imani inayoshinda majaribu katika Waebrania 11:1-40. Zaidi ya hayo, Yesu ndiye mfano wetu mkuu zaidi. Mtazame yeye badala ya majaribu yako. *“Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu. Maana mtafakarini sana yeye aliyeyastahimili mapingamizi makuu namna hii ya watendao dhambi juu ya nafsi zao, msije mkachoka, mkizimia mioyoni mwenu,”* Waebrania 12:1-3.

## UNGAMO NA MSAMAHA

**Msamaha.** Msamaha hutolewa kwa wale ambao wamemwamini Yesu. *"Kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi,"* Matendo 10:43. Tulipomwamini Yesu tuliwekwa huru kutokana na adhabu ya dhambi ... lakini dhambi bado iko katika maisha yetu, 1 Yohana 1:8. Dhambi hiyo ni kikwazo katika uhusiano wetu na Mungu. Tunahitaji kuungama dhambi zetu kwa Mungu.

**Ungamo.** Kuungama ni zaidi ya kuomba tu msamaha. Ni kukubaliana na Mungu kwamba dhambi yako ni dhambi. Ni kukiri kwake kwamba umetenda dhambi fulani mahususi. Ni zaidi ya kukiri kwamba wewe ni mwenye dhambi ... ni kukubali kwamba matendo na mitazamo yako ni dhambi. Kuungama kwa njia hiyo ni sharti la msamaha na utakaso unaotajwa katika 1 Yohana 1:9, *"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."*

**Baraka za msamaha.** *"Heri aliyesamehewa dhambi, Na kusitiriwa makosa yake,"* Zaburi 32:1. Dhambi zilizosamehewa huondolewa. *"Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi,"* Zaburi 103:12. *"Umezitupa dhambi zangu zote nyuma yako,"* Isaya 38:17. *"Mimi, naam, mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe, wala sitazikumbuka dhambi zako,"* Isaya 43:25.

**Matokeo ya dhambi ambayo haijaungamwa.** Mungu anajua kila kitu kutuhusu, Waebrania 4:13. Kuungama ni kukubaliana na kile ambacho Mungu anajua tayari ... kwamba dhambi zetu ni dhambi. Ni kazi bure kujaribu kumficha Mungu dhambi zetu. *"Afichaye dhambi zake hatafanikiwa; Bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema."* Mithali 28:13. Mungu hutuhurumia tunapoungama. Lakini, tusipoungama tunaweza kujawa na wasiwasi, Zaburi 38:18. Tukinyamaza kuhusu dhambi zetu, hiyo inaweza kudhuru afya yetu ... tunaweza kuhisi mkono mzito wa Mungu juu yetu ... nguvu yetu inaweza kupungua ... na hisia ya kuwa na hatia inaweza kutulemea, Zaburi 32:3-5. Hasira ya Mungu na hisia ya kuwa na hatia inaweza kuwa mzigo mkubwa. Dhambi ambayo haijaungamwa inaweza kusababisha magonjwa na uchovu, Zaburi 38:4.

**Kuwasamehe wengine.** Hatupaswi kuwa wanajeshi wanaowapiga risasi wenzao waliojeruhiwa. Shughulikia majeraha ya wengine ... wasamehe na uwarejeshe, Wagalatia 6:1-2. Mungu amekusamehe ... kwa hivyo wasamehe wengine, Waefeso 4:32. Usimnyime msamaha mtu anayetubu, Luka 17:3-4. Petro aliuliza, *"Bwana, ndugu yangu anikose mara ngapi nami nimsamehe? Hata mara saba? Yesu akamwambia, Sikuambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini,"* Mathayo 18:21-22. Msamaha wa Mungu kwako unafungamana na msamaha wako kwa wengine, Mathayo 6:14-15. Tunaomba hivi katika Sala ya Bwana, *"Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu,"* Mathayo 6:12.

Acts One Eight [Matendo Moja Nane] huchapisha tafsiri hii ya Kiswahili ya kozi ya lugha ya Kiingereza ya *Disciplemaking 1 … Abiding in His Word*. Unaweza kunakili kozi hii au sehemu yake yoyote bila malipo au kwa gharama ya usambazaji pekee, bila kubadilisha maudhui yake na ukiwa umeambatanisha kauli hii ya chanzo. Kozi hii inapatikana bila malipo katika lugha ya Kiswahili kutoka katika www.Theolojia.org au katika lugha ya Kiingereza kutoka katika www.VIrtualBibleAcademy.org. Kwenye tovuti hizi, unaweza kusoma mtandaoni, kufundishwa, kupakua, au kuchapisha nakala zako mwenyewe. Nukuu za Biblia ya Kiswahili zimetoka katika Biblia ya Swahili Union Version (SUV) ya 1997.

# Somo la 10 - Katika Vita … ukurasa wa 136 - 150

Sehemu ya kujifunza ni kufanya marudio … kuhifadhi maarifa mapya kwenye kumbukumbu yako ya muda mrefu. Chapisha mtihani huu wa marudio au tumia karatasi tofauti kujibu maswali yafuatayo. Kisha rudia mtihani huu, ukisoma maelezo ya kozi au bila kuyasoma, hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi. *Mitihani hii ya marudio* pamoja na majibu sahihi yanapatikana kwenye www.Theolojia.org.

1. Maadui wetu watatu ni ______________, ______________, na ______________.

2. Tumezaliwa katikati ya _____________________ katika ____________________ iliyoanguka.

3. Tuna _______________ ndani yetu, yetu iliyoanguka ________________.

4. Tunapigana na adui _______________ ambaye ni Shetani, aliyeanguka. _______________.

5. Tayari tumeshinda vita kwa sababu ya kile Yesu alifanya _______________.

6. Ulinzi tuliopewa na Mungu katika vita dhidi ya dunia ni:

   a. Usijitie katika ___________________________________, 2 Timotheo 2:3-4.

   b. Usi _________________ dunia, wala _________________ katika dunia, 1 Yohana 2:15.

   c. Msi ________________________________ ya dunia hii bali ____________________________ kwa ____________________________ nia zenu, Warumi 12:2.

7. Katika vita vyetu dhidi ya mwili, ni lazima:

   a.

   b.

   c.

   d.

   e.

   f.

8. Katika vita vyetu dhidi ya ibilisi, ni lazima:

   a.

   b.

   c.

   d.

   e.

   f.

   g.

9. Weka mviringo au piga mstari chini ya vitu ambavyo Shetani hufanya katika orodha ifuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| Kuua | Kuwashtaki waumini | Ni chanzo cha mafundisho ya uwongo |
| Kudanganya | Kujigeuza | Kupofusha macho ya wasioamini |
| Kujaribu | Kutafuta watu wa kumeza | Kuwashika mateka wasioamini |
| Kufanya hila | Kwa jumla ni mzuri | Kuiba Neno kutoka kwa wasioamini |

10. Katika kupambana na dhambi, ni lazima:

   a.

   b.

   c.

   d.

   e.

   f.

   g.

   h.

   i.

   j.

11. *Kweli au Uwongo*: Mungu ni chanzo cha majaribu. ____________________

12. Pitia orodha [kurasa 148-149] ya njia za kukabiliana na majaribu.

   a. Ni ipi kati ya njia hizo ilikuwa muhimu zaidi katika ushindi wako hapo awali?

   b. Ukosefu wa njia ipi ulikuwa muhimu zaidi katika kushindwa kwako hapo awali?

*Kufanya Wanafunzi - Majibu ya Maswali ya Marudio*

## Somo la 10 - Katika Vita … ukurasa wa 151 - 152

Usitumie karatasi hizi za majibu kupata majibu yako. Tafadhali zitumie tu kukagua majibu yako. Rudi kwenye somo ili kupata taarifa za kurekebisha majibu yako. Rudia mtihani hadi uweze kujibu maswali yote kwa usahihi na kwa urahisi. Masomo yote, mitihani ya marudio, na kurasa za majibu zinapatikana katika www.Theolojia.org.

1. Maadui wetu watatu ni ____*dunia*____ , ____*mwili*____ , na ____*ibilisi*____ .

2. Tumezaliwa katikati ya ____*maadui*____ katika ____*dunia*____ iliyoanguka.

3. Tuna ____*msaliti*____ ndani yetu, ____*asili*____ yetu iliyoanguka.

4. Tunapigana na adui ____*asiyeonekana*____ ambaye ni Shetani, ____*malaika*____ aliyeanguka.

5. Tayari tumeshinda vita kwa sababu ya kile Yesu alifanya ____*msalabani*____ .

6. Ulinzi tuliopewa na Mungu katika vita dhidi ya dunia ni:

   a. Usijitie katika ____*shughuli za dunia*____ , 2 Timotheo 2:3-4.

   b. ____*Msiipende*____ dunia, wala ____*mambo yaliyomo*____ katika dunia, 1 Yohana 2:15.

   c. ____*Msiifuatishe namna*____ ya dunia hii bali ____*mgeuzwe*____ kwa ____*kufanywa upya*____ nia zenu, Warumi 12:2.

7. Katika vita vyetu dhidi ya mwili, ni lazima:

   a. *Tutupilie mbali utu wa kale na tuvae utu mpya.*

   b. *Tuweke akili zetu kwenye mambo ya Roho wala si mambo ya mwili.*

   c. *Tusiutaminie mwili.*

   d. *Tuache kukubali ushawishi wa tamaa ya mwili.*

   e. *Tusiupatie mwili nafasi.*

   f. *fTujifikirie kuwa tuko hai kutoka kwa wafu.*

8. Katika vita vyetu dhidi ya ibilisi, ni lazima:

   a. *Tumpinge.*

   b. *Tusali.*

   c. *Tuwe macho.*

   d. *Tusimpe nafasi yoyote.*

   e. *Tusijihusishe na kitu chochote cha kishirikina.*

   f. *Tuvae silaha zote za Mungu.*

   g. *Tuwaambie watu kuhusu Yesu.*

9. Weka mviringo au piga mstari chini ya vitu ambavyo Shetani hufanya katika orodha ifuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| *Kuua* | *Kuwashtaki waumini* | *Ni chanzo cha mafundisho ya uwongo* |
| *Kudanganya* | *Kujigeuza* | *Kupofusha macho ya wasioamini* |
| *Kujaribu* | *Kutafuta watu wa kumeza* | *Kuwashika mateka wasioamini* |
| *Kufanya hila* | *Kwa jumla ni mzuri* | *Kuiba Neno kutoka kwa wasioamini* |

10. Katika kupambana na dhambi, ni lazima:

   a. *Tuwe watendaji na si wasikiaji tu wa Neno.*

   b. *Tusali.*

   c. *Tufahamu Neno la Mungu.*

   d. *Tuenende katika Roho wake.*

   e. *Tuyatafute yaliyo juu.*

   f. *Tujihadhari na kujiamini kupita kiasi.*

   g. *Tuchukue hatua kali dhidi ya dhambi katika maisha yetu.*

   h. *Tuutoroke uwanja wa vita … kukimbia dhambi na majaribu.*

   i. *Tukumbuke kwamba miili yetu ni Hekalu la Roho Mtakatifu.*

   j. *Tukumbuke kwamba tulinunuliwa kwa damu ya Yesu.*

11. *Kweli au Uwongo:* Mungu ni chanzo cha majaribu. ____*Uwongo*_.

12. Pitia orodha [kurasa 148-149] ya njia za kukabiliana na majaribu.

   a. Ni ipi kati ya njia hizo ilikuwa muhimu zaidi katika ushindi wako hapo awali?

   b. Ukosefu wa njia ipi ulikuwa muhimu zaidi katika kushindwa kwako hapo awali?

## KIAMBATISHO: KUWAFUNDISHA WENGINE

*“Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine.”* 2 Timotheo 2:2

Unapaswa kuwa umeandaliwa vyema zaidi kuwa mwanafunzi kwa vile umemaliza masomo haya kumi ya *Kufanya Wanafunzi 1.* Kama mwanafunzi wa Yesu Kristo, unapaswa kuendelea kukua na kuwa mfanya wanafunzi. Maneno mawili muhimu katika maisha ya mwanafunzi ni *tumia* na *zidisha*. Tumia kile unachojifunza katika maisha yako mwenyewe. Kisha kizidishe katika maisha ya wengine ukiwasaidia kuwa wanafunzi na wafanya wanafunzi. Paulo aliandika juu ya kufanya wanafunzi katika kifungu kilicho hapo juu. Paulo alikuwa amemfundisha Timotheo. Kisha akamhimiza Timotheo awafundishe watu waaminifu mambo yale yale aliyomfundisha ... watu waaminifu watakaowafundisha wengine mambo hayo hayo. Uzidishaji ulitoka kwa Paulo ... hadi kwa Timotheo ... kisha kwa watu waaminifu ... na hatimaye kwa watu wengine. Hilo ndilo lengo la kozi hii ya *Kufanya Wanafunzi 1*.

Mambo ambayo umejifunza kutoka kwangu katika kozi hii, uyakabidhi kwa waumini waaminifu ambao wataweza kuwafundisha wengine pia. Yaani kutoka kwangu hadi kwako ... hadi kwa Waumini waaminifu ... kisha kwa watu wengine pia. Kuwa mfanya wanafunzi kwa kufundisha baadhi ya yale uliojifunza katika *Kufanya Wanafunzi 1*. Kufundisha kozi nzima ni changamoto. Hivyo ni bora ukianza kwa kufundisha sehemu kadhaa tu. Fursa za kufundisha zinaweza kuwa zimekuzunguka ... katika mkutano wa kujifunza Biblia, katika shule ya Jumapili, au ana kwa ana na rafiki. Kufundisha ana kwa ana kunaweza kuwa mahali rahisi pa kuanzia. Unaweza kuwafundisha Waumini wapya, Waumini wachanga, au Waumini waliokomaa ambao wanataka kuwasaidia wengine. Omba. Mwombe Mungu akupe fursa. Mungu atakupa fursa sahihi ikiwa umejiandaa na uko tayari.

Kiambatisho hiki kimeundwa ili kukusaidia kubadilika kutoka kuwa mwanafunzi hadi kuwa mwalimu ... kutoka kuwa mwanafunzi hadi kuwa mfanya mwanafunzi. Ikiwa una lengo sahihi na ufuate miongozo rahisi, unaweza kuwa mwalimu bora zaidi. Na unaweza kufurahia mchakato wa kufundisha. Lengo la kufundisha ni kubadilisha maisha ya watu ... kuongezeka kwa maarifa kunakosababisha kuongezeka kwa utiifu. Kwa ufupi, matokeo ya kufundisha vizuri ni maisha makamilifu, si madaftari yaliyojaa maandishi. Paulo aliandika hivi kuhusu kufundisha kwake kwenyewe, *“Sisi tunamhubiri habari zake* [Yesu] *tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu katika hekima yote, tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo,”* Wakolosai 1:28. Kiambatisho hiki kinatoa miongozo rahisi ya kufundisha. Miongozo hiyo iko katika nyanja nne ... kuelewa kufundisha ni nini ... kumwandaa mwalimu ... kuandaa mpango wa somo ... na kufundisha somo. Fuata miongozo hii na utakuwa mwalimu bora zaidi. Jifunze miongozo hiyo kabla ya kufundisha. Itumie unapofundisha. Zipitie tena baada ya kufundisha.

## KUELEWA MCHAKATO WA KUFUNDISHA

**Kuna tofauti kati ya kuhubiri na kufundisha.** Kuhubiri huwashawishi watu. Kufundisha huwaandaa watu. Lengo la kuhubiri ni kuhamasisha watu kuchukua hatua mara moja. Lengo la kufundisha ni kuongeza maarifa ambayo yatasababisha hatua za haraka na za muda mrefu. Wasikilizaji wa mhubiri si lazima wahifadhi sehemu kubwa ya maudhui ya mahubiri … lakini wanahamasishwa kubadilisha maisha yao. Wanafunzi wa mwalimu hujifunza na kuhifadhi maarifa na hivyo wanabadilisha maisha yao. Nimewahi kuhubiri *Somo la 4 - Agano la Kale* na watu walivutiwa na jinsi ninavyofahamu vyema Agano la Kale. Lakini pia nimewahi kufundisha somo hilo na watu walivutiwa na jinsi walivyojifunza mengi kuhusu Agano la Kale. Kuhubiri vizuri na kufundisha vizuri vyote ni muhimu. Vyote viwili ni vizuri. Lakini vinatofautiana katika malengo na katika mbinu.

**Fafanuzi.** *Kuhubiri* ni kutangaza, kukiri, kushawishi. *Kufundisha* ni kuandaa, kutoa maarifa, kuwezesha kujifunza, na kufunza maarifa na matumizi yake. *Kuhubiri* hushawishi ... hutia moyo, huhimiza, na katika kanisa la leo lililoshawishiwa na mataifa ya Magharibi, pia huwahimiza watu kuamini, kuwa na tabia za aina fulani, na kuwa sehemu ya kanisa. *Kufundisha* huhamisha maarifa kwa wanafunzi … *kukiwandaa* kuamini, kuwa na tabia njema na kuwa sehemu ya kanisa.

**Mifano ya Agano Jipya.** Maneno mawili tofauti yanatumika katika Agano Jipya kwa ajili ya kuhubiri na kufundisha. Maneno hayo mawili si visawe. Yesu alihubiria umati. Lakini aliwafundisha Wanafunzi wake. Paulo alihubiri Injili. Lakini aliwafundisha Waumini kukua katika Kristo. Katika Agano Jipya mahubiri mara nyingi yalifanywa mhubiri akiwa amesimama … wasikilizaji wake wakiwa ni watu wasioamini. Katika Agano Jipya mafundisho mara nyingi yalifanywa mwalimu akiwa ameketi … wasikilizaji wake wakiwa ni Waumini.

**Kufanana.** Mafundisho mazuri yana maudhui mazuri ya kibiblia. Mahubiri mazuri yana maudhui mazuri ya Kibiblia … lakini maudhui mazuri ya kibiblia hayafanyi mahubiri hayo yawe mafundisho mazuri. Kuhubiri bila maudhui mazuri si lingine bali mahubiri mabaya. Unahitaji kuwa mahiri katika mbinu za usemaji za enzi ya Warumi na Wagiriki. Kuhubiri vizuri *na* kufundisha vizuri kunajumuisha vipengele vitatu vya usemaji … logos, ethos, na pathos. Ustadi katika vipengele vyote vitatu unahitaji wasilisho lenye mantiki na maudhui mazuri [logos] … kutoka kwa mwasilishaji anayeaminika na wasilisho linaloaminika [ethos] … lenye ushawishi [pathos]. Mahubiri mazuri ni muhimu. Nimehubiri mara nyingi … na mara kwa mara mimi husikiliza mahubiri mazuri. Na nimefundisha mara nyingi ... wakati mwingine kwa saa 30 au 40 katika wiki moja. Ninajua kuwa mbinu [ujuzi] ni tofauti. Na kufundisha vizuri ni vigumu, labda hata ni vigumu zaidi kuliko kuhubiri vizuri.

**Mbinu tofauti.** Ujuzi na mbinu ni tofauti kabisa.

*Kuhubiri* hakuhitaji wasikilizaji watumie sana kumbukumbu zao za ufahamu wa muda mrefu. *Kufundisha* kunahitaji mwanafunzi akumbuke kile alichohifadhi kwenye kumbukumbu yake ya muda mrefu. Ni jukumu la mwalimu kumwezesha mwanafunzi kufanya hivyo.

*Kuhubiri* hulenga kuwafanya watu wakiri na wakubali … hayo mawili hayahitaji utumizi mkubwa wa akili [uchakataji wa kiakili]. Ni sawa ikiwa wasikilizaji wa mhubiri hawawezi kuhifadhi au kusema tena maudhui na mantiki iliyowashawishi ... mradi tu wawe wameshawishiwa. Kufundisha huhitaji utumizi wa akili [uchakataji wa kiakili] … hulenga kumsaidia mwanafunzi kujumuisha maarifa mapya kutoka kwa mwalimu kwenye maarifa yake aliyohifadhi hapo awali.

*Kuhubiri* hufululiza maudhui katika mfululizo unaoendelea wa maneno na hivyo kunatoa muda mchache kwa wasikilizaji kutumia akili zao katika mchakato huo. *Kufundisha* hutoa taarifa katika vipande vinavyoweza kuchakatwa kiakili. *"Kukusikiliza ni kama kunywa maji kutoka kwenye bomba la maji ya kuzima moto"* inaweza kuwa pongezi kwa mhubiri ... lakini si pongezi kwa mwalimu.

## KUMWANDAA MWALIMU

Kufundisha vizuri huanza na maandalizi ya mwalimu. Ili kujiandaa kama mwalimu unapaswa kuomba ... kusoma ... kufanya mapitio ... na kuwa kielelezo.

**Omba.** Jiombee. Omba kama Musa alivyoomba, *"Mafundisho yangu yatadondoka kama mvua, Maneno yangu yatatona-tona kama umande; Kama manyunyu juu ya majani mabichi; Kama matone ya mvua juu ya mimea,"* Kumbukumbu la Torati 32:2. Omba unapotayarisha kila somo. Omba kwamba utaelewa vyema kila somo. Omba unapotayarisha mpango wa somo. Omba kwamba uweze kufundisha kwa uwazi, usahihi, shauku, ushawishi, na kwa ajili ya kazi ya Roho Mtakatifu. Ombea wanafunzi wako ukitaja majina yao. Omba kwamba wataelewa na watatumia yale watakayojifunza katika maisha yao wenyewe. Ombi la Paulo kwa ajili ya Waumini wa Kolosai ni mfano mzuri sana, *"Kwa sababu hiyo sisi nasi, tangu siku ile tuliposikia, hatuachi kufanya maombi na dua kwa ajili yenu, ili mjazwe maarifa ya mapenzi yake katika hekima yote na ufahamu wa rohoni; mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu; mkiwezeshwa kwa uwezo wote, kwa kadiri ya nguvu ya utukufu wake, mpate kuwa na saburi ya kila namna na uvumilivu pamoja na furaha; mkimshukuru Baba, aliyewastahilisha kupokea sehemu ya urithi wa watakatifu katika nuru,"* Wakolosai 1:9-12.

**Soma.** Kwanza, fahamu maudhui utakayofundisha vizuri. Soma somo husika wewe mwenyewe. Chunguza kila sehemu yake ... litafakari ... likumbuke. Soma kila sehemu, chati, na ramani. Soma na uchunguze marejeo ya vifungu vya Biblia. Fahamu somo husika kwa ujumla. Lifahamu kwa undani. Fahamu somo lote vizuri kabisa. Hatua ya pili ya kusoma inahusisha kuandaa mpango wa somo husika. Kufahamu somo husika wewe mwenyewe ni tofauti na *jinsi* ya kumfundisha mtu mwingine somo hilo. Miongozo ya kuandaa mpango wa kufundisha somo iko kwenye ukurasa unaofuata wa kiambatisho hiki. Kusoma ni kazi ngumu. Inachukua muda. Hakuna njia za mkato. *"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli,"* 2 Timotheo 2:15.

**Fanya Mapitio.** Baada ya kusoma somo husika na kuandaa mpango wa somo hilo, fanya mapitio ya hayo mara nyingi. Kufanya mapitio mara nyingi kunafanya somo husika kuwa lako wewe binafsi ... kukikupatia ufahamu kamili. Ufahamu kamili unakupa ujasiri na urahisi katika kufundisha. Unapofahamu somo husika kwa undani, unaweza kutilia mkazo kuhakikisha kwamba mwanafunzi analielewa kwa usahihi badala ya wewe kufundisha kwa usahihi. Pitia somo husika kila mara kabla ya kulifundisha. Huenda unalifundisha kwa mara ya 5 ... lakini wanafunzi wako huenda wanalisikia kwa mara ya kwanza. Pitio la mwisho dakika chache kabla ya kufundisha linaweza kukusaidia pakubwa.

**Kuwa Kielelezo.** Kuwa kielelezo kizuri wa kile unachofundisha. Kuwa kielelezo cha somo husika. Tumia somo husika kwako kabla ya kulizidisha kwa wengine. Ishi kulingana na somo husika kabla ya kulitoa kwa wengine. Utakuwa mwalimu bora kwa kufanya hivyo. Utaonyesha kwamba inawezekana kujifunza somo hilo na kuishi kulingana nalo. Wanafunzi wako wataamini mafundisho yako kwa sababu wewe ni kielelezo kizuri. Paulo alisema, *"Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo,"* 1 Wakorintho 11:1, na *"Uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi,"* 1 Timotheo 4:12. Unpaswa kuweza kuwaambia wanafunzi wako, *"Twendeni pamoja katika kiwango cha juu zaidi … nimewahi kuwa huko."* Usiseme, *"Nendeni huko ... nimesikia tu ni kuzuri."* Huwezi kuwafundisha wanafunzi wako kuwa wa kiroho zaidi kuliko wewe. Yesu alisema, *"Mwanafunzi hawi mkuu kuliko mwalimu wake, lakini kila mtu ambaye amehitimu hulingana na mwalimu wake,"* Luka 6:40.

## KUANDAA MPANGO WA SOMO

Mpango wa somo ni jibu la swali, *Nitafundishaje somo hili? Jinsi* si sawa na *kile* unachopaswa kufundisha. Mpango wa somo ni maagizo yako kwako mwenyewe kuhusu *jinsi* ya kufundisha maudhui ya somo husika. Andika mpango wako wa somo kwenye kurasa za somo.

**Weka lengo.** Amua lengo lako ni lipi kwa ajili ya kila somo. Fahamu kile unachotaka wanafunzi wajifunze, wakumbuke, na watumie. Unda mpango wako wa somo ili kufikia lengo hilo.

**Maswali ya awali … fundisha … maswali ya baadaye.** Kuuliza maswali ya awali humsaidia mwanafunzi kukumbuka kile anachojua tayari kuhusu somo husika. Kuuliza tu maswali machache kuhusu somo husika kunaweza kufanya hivyo. Ikiwa unafundisha kikundi, waambie *wasitoe* majibu kwa sauti, kwa sababu mara tu mtu mmoja anapojibu kwa sauti, watu wote wengine wataacha kufikiria. Kisha fundisha somo husika au sehemu yake kama ilivyoelezwa hapa chini. Hatimaye, uliza maswali kadhaa [bila majibu kutolewa kwa sauti] ili kuwasaidia wanafunzi wako kukumbuka maudhui ya somo husika.

**Muhtasari ... kwa kina ... na mapitio.** Kufundisha vizuri kunajumuisha mambo haya yote matatu. Yajumuishe katika mpango wako wa somo. Hatua ya kwanza ni muhtasari mfupi wa somo husika au sehemu yake. Hiyo inampa mwanafunzi msingi wa maudhui ya kina ya somo husika. Hatua inayofuata ni maudhui ya kina ya somo. Haya ni maudhui yaliyochapishwa *na* vidokezo vyako ulivyoandika. Hatua ya mwisho ni mapitio ya kila sehemu na somo zima. Waambie kile utakachowaambia ... kisha waambie ... kisha uwaambie ulichowaambia. Fuata utaratibu huu sehemu kwa sehemu katika kila somo.

**Ongeza uwazi.** Kufundisha kuzuri hueleweka. Kufundisha kunahitaji kuwa wazi na kueleweke kwa urahisi. Ongeza fafanuzi na vielelezo [taswira]. Vielelezo vizuri huongeza uwazi ... kueleza yale yasiyojulikana kwa msingi wa yale yanayojulikana. Amua ni maswali gani ungependa kuwauliza wanafunzi wako ambayo yatawafanya wafikirie na waelewe somo.

**Tayarisha vidokezo vyako.** Mahali pazuri pa kuandika vidokezo vyako ni kwenye kurasa za somo. Jiandikie maagizo wewe mwenyewe. Andika maoni kuhusu maudhui ya masomo. Piga mstari au chora miviringo kuonyesha msisitizo. Chora vishale unganishi kuonyesha mwendelezo au sababu na athari. Weka kazi za ziada za wanafunzi wako mwishoni mwa kila somo. Vidokezo vyako viwe vifupi, rahisi, wazi, kamili, na vinavyoweza kusomeka vizuri *kabisa* ... kumbuka utakuwa ukivirejelea unapofundisha.

## KUFUNDISHA SOMO HUSIKA

Kufundisha vizuri ni matokeo ya maandalizi ya mwalimu na maandalizi ya mpango mzuri wa somo. Kufundisha vizuri kwa njia thabiti hakuwezekani bila mambo hayo mawili.

**Chukua muda wa kujiandaa kiakili kabla ya kufundisha.** Katika dakika chache kabla ya kufundisha, chukua muda wa kuelekeza akili na moyo wako kwenye somo husika. Jiombee wewe mwenyewe, wanafunzi wako, kufundisha kwako, na kazi ya Roho Mtakatifu. Fikiria juu ya lengo la somo. Pitia somo kwa ufupi ... hasa mwanzo wake.

**Eleza kusudi la somo.** Waambie wanafunzi wako lengo la somo kwa ufupi. Waambie kusudi la mafundisho yako. Kujua kwao kile wanachopaswa kutarajia kunafanya kufundisha kwako na kujifunza kwao kuwe rahisi zaidi.

**Watie moyo wanafunzi wako kujifunza na kutumia kile wanachojifunza.** Paulo aliwatia moyo wanafunzi wake. *"Vile vile, kama mjuavyo, jinsi tulivyomwonya kila mmoja wenu kama baba awaonyavyo watoto wake mwenyewe, tukiwatia moyo na kushuhudia; ili mwenende kama ilivyo wajibu wenu kwa Mungu, mwenye kuwaita ninyi*

*ili mwingie katika ufalme wake na utukufu wake,"* 1 Wathesalonike 2:11-12. Kuwa kama Paulo. Na ufahamu wako wa kina wa maudhui ya somo husika huonyesha kuwa inawezekana kujifunza somo hilo. Na mifano ya kweli, isiyo na kiburi, na ya kibinafsi kutoka katika maisha yako inaweza kuwatia wanafunzi wako moyo kwa njia kubwa.

**Fundisha kwa uwazi ... kwa njia rahisi ... kwa ufupi.** Ugumu kwa kawaida ni kizuizi katika kuelewa. Maneno mengi, na maneno mengi magumu, huongeza ugumu na mkanganyo katika mafundisho. Hotuba maarufu nchini Marekani, Hotuba ya Rais Abraham Lincoln aliyoitoa huko Gettysburg mnamo mwaka 1863, ilikuwa kielelezo cha urahisi unaoongeza matokeo ya mawasiliano. Lincoln alizungumza kwa takriban dakika mbili. Hotuba yake ilikuwa na maneno 262 pekee ... na 202 yalikuwa maneno yenye silabi moja. Hakikisha masomo yako ni rahisi. Zingatia mada husika. Kuongeza maelezo mengi ya ziada au maudhui ya ziada huwazuia wanafunzi kuelewa somo zima ... na hufanya iwe vigumu kuwafunza wengine somo hilo.

**Muhtasari ... kwa kina ... na mapitio.** Fuata mpango wako wa somo … uliza maswali ya awali … kisha muhtasari, mafundisho ya kina, na mapitio … kisha uliza maswali ya baadaye. Fanya mambo haya kwa kila sehemu ya somo. Usisahau kuuliza maswali ya awali na ya baadaye.

**Wachochee kufikiria.** Kufundisha vizuri huwafanya wanafunzi wahusike kiakili katika somo. Wape jukumu la kugundua. Kuuliza maswali ya awali na ya baadaye husaidia hilo kutokea. Wahimize kupigia mstari na kuandika vidokezo. Wachochee kufikiria ... wape muda wa kufikiria ... na wafanye waendelee kufikria.

**Wape wanafunzi wako nafasi ya kwanza.** Ukuaji wao wa kiroho unapaswa kuwa kipaumbele chako cha juu katika kuwafundisha. Lengo ni kuongezeka kwa ufahamu wao na utiifu wao. Waambie wanafunzi wako wakati hujui jibu ... kisha kuwa na jibu hilo mtakapokutana tena.

**Fundisha tu ikiwa wanafunzi wako makini.** Watu wakiacha kusikiliza, acha kuongea. Huwezi kufundisha wakati wanafunzi hawako makini. Fanya mipango mapema ili kuondoa vikengeushi. Usishangae ukiona vikengeushi. Huwa vinatokea. Nyamaza na usubiri kikengeushi hicho kimalizike. Anza tena wanafunzi watakapokuwa makini tena. Wanafunzi wasumbufu huhujumu mafunzo. Kuwarekebisha kwa upole kwa kawaida hutosha ... lakini ikiwa sivyo, kuwa thabiti zaidi na uwakabili moja kwa moja. Zungumza nao peke yao baadaye ili uwaeleze kwa nini uliwarekebisha. Andika orodha ya maswali yaliyo nje ya mada ya masomo, na uyajibu nje ya muda wa darasa. Tumia wakati wa maswali na majibu, majadiliano ya darasa, na mapumziko kudumisha umakini ... au kurejesha umakini.

**Tathmini kufundisha kwako.** Pitia kiambatanisho hiki na utathmini kufundisha kwako baada ya kufundisha kila somo. Na walimu wanaweza kusaidiana … kutathminiana, kusahihishiana, na kutiana moyo. *"Chuma hunoa chuma; Ndivyo mtu aunoavyo uso wa rafiki yake,"* Mithali 27:17. Usijitetee unaporekebishwa, *"Mkaripie mwenye hekima, naye atakupenda. Mwelimishe mwenye hekima, naye atazidi kuwa na hekima,"* Mithali 9:8-9. Fanya mabadiliko yanayohitajika kwa ajili ya somo linalofuata.

> *"Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine."* 2 Timotheo 2:2

Acts One Eight [Matendo Moja Nane] huchapisha tafsiri hii ya Kiswahili ya kozi ya lugha ya Kiingereza ya *Disciplemaking 1 … Abiding in His Word*. Unaweza kunakili kozi hii au sehemu yake yoyote bila malipo au kwa gharama ya usambazaji pekee, bila kubadilisha maudhui yake na ukiwa umeambatanisha kauli hii ya chanzo. Kozi hii inapatikana bila malipo katika lugha ya Kiswahili kutoka katika www.Theolojia.org au katika lugha ya Kiingereza kutoka katika www.VIrtualBibleAcademy.org. Kwenye tovuti hizi, unaweza kusoma mtandaoni, kufundishwa, kupakua, au kuchapisha nakala zako mwenyewe. Nukuu za Biblia ya Kiswahili zimetoka katika Biblia ya Swahili Union Version (SUV) ya 1997.

## Mahimizo ya Mwisho

Mpendwa Mwanafunzi au Mwalimu,

Vifungu fulani vya Biblia vimeshawishi huduma yangu ya kufanya wanafunzi na uinjilisti. Kwa hivyo nakuacha na baadhi ya vifungu hivyo kama mahimizo yangu ya mwisho kwako. Kifungu cha kwanza kiliandikwa kwenye Biblia yangu siku nilipompokea Yesu Kristo kama Mwokozi wangu.

*"Basi, ndugu zangu wapendwa, mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana sikuzote, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana."*
1 Wakorintho 15:58

*"Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu."*
Warumi 12:1-2

*"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; 17ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."* 2 Timotheo 3:16-17

*"Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, 'Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru.'"* Yohana 8:31-32

*"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli."* 2 Timotheo 2:15

*"Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine."* 2 Timotheo 2:2

*"Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, 'Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.'"* Mathayo 28:18-20

*"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi."* Matendo 1:8

Wenu katika Kumtumikia Mungu,

*John D. Morris III*

Mwanzilishi na Rais, Acts One Eight
John@Theolojia.org